**25 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 25 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuketi.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 *(The Finance Bill, 2025)*.

**MHE. SUBIRA K. MGALU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 *(The Finance Bill, 2025)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 675

**Kujenga Barabara ya Mshangano – Legele – Mletele kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mshangano – Legele hadi Mletele?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara ya Mshangano - Legele hadi Mletele, na tayari imefanya usanifu wa ujenzi kwa kiwango cha lami ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2.513 kinahitajika ili kujenga kilometa tano, na kwa sasa inaendelea kutafuta fedha za kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imekuwa ikiendelea kuifanyia matengenezo barabara hii, ambapo katika mwaka 2022/2023 yalifanyika matengenezo ya kuifungua barabara, kung’oa miti, ujenzi wa mitaro, ujenzi wa makalavati na uwekwaji wa changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023/2024 na 2024/2025 Serikali ilifanya matengenezo ya kawaida katika barabara hiyo ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha tuta la

barabara kwa kuichonga na kuchimba mitaro ya kutolea maji ya mvua kwa gharama ya shilingi milioni 84.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025/2026 Serikali imeweka katika mipango yake matengenezo ya kawaida kwa shilingi milioni 47.5. Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja ya Mji wa Songea kwa kuijenga, kuikarabati na kuifanyia matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana katika kuchagiza uchumi katika Manispaa ya Songea. Wanawake wamekuwa wakipata adha kubwa kupeleka bidhaa zao masokoni.

(a) Je, Serikali ni lini itaanza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

(b) Serikali imeeleza hapo kwamba inatakiwa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kilometa tano. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha na vifaa vya ujenzi, *graders*, *caterpillars* ili ujenzi huu uanze mara moja kwa ajili ya kuchagiza uchumi katika Manispaa ya Songea? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara zetu hizi za Wilaya, barabara zinazosimamiwa na *TARURA* hasa kwa maana barabara hizi zinachangia sana katika shughuli za uchumi na kuwawezesha wananchi kufika katika huduma za msingi kabisa za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona katika Wilaya ya Songea, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, zaidi ya shilingi bilioni 20 zimetumika katika kuimarisha miundombinu ya barabara hizi za Wilaya. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, shilingi bilioni 7.65 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumjibu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kwamba lini ujenzi wa barabara hii utaanza, kama nilivyotangulia kusema, tayari usanifu umefanyika katika barabara hii ya Mshangano – Legele, na imebainika kwamba shilingi bilioni 2.5 zinahitajika kwa ajili ya kuijenga barabara hii kwa kilometa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa, fedha itakapopatikana, ujenzi utaanza, ataona wakandarasi wako *site*, ataona hiyo mitambo anayotaka kuiona, ataiona ipo *site,* kwa ajili ya kuanza kujenga barabara hii, kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, barabara hii ina umuhimu mkubwa sana kiuchumi, lakini inawasidia wananchi kufikia huduma za msingi za kijamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga barabara ya Mtandika – Ikula, Kata ya Ruaha Wilaya ya Kilolo? Hii barabara nimepita mimi Jumapili, haipitiki. Mimi mwenyewe nimekwenda kwa bodaboda tu, hata bodaboda zinapita kwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu moja ambayo inatakiwa itengenezewe mawe ili mwamba uweze kutoka. Wananchi wanapata mateso makubwa sana hasa akina mama wajawazito kwenda kwenye kituo cha afya. Ni mateso makubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba Serikali inaendelea na inafanya uwekezaji mkubwa sana katika eneo la kuimarisha barabara zetu hizi za Wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Barabara hii ya Mtandika anayoitaja Mheshimiwa Mbunge ambayo ipo Kilolo, Serikali itafika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa ili iweze kuwanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kuendelea kumsisitiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa pamoja na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya waendelee kufanya tathmini na kubaini barabara muhimu za msingi kabisa kama hizi ambazo zinahitaji uwekezaji wa Serikali, kwa maana ya kuziimarisha barabara hizi ili sasa fedha iweze kutengwa, iwe kwenye mipango na bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kumhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba Serikali itafika kwa ajili ya kuja kuhakikisha barabara hii inajengwa ili iweze kuwanufaisha wananchi wa Kilolo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu mazuri na ya uhakika anayotupatia, na watu wanasubiri utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, katika Awamu ya Tano wakati wa kampeni, wananchi wa Uru katika Kata ya Uru Magharibi, eneo la Uru Shimbwe waliahidiwa kwamba barabara yao itatengenezwa kuanzia Rau – Uru Shimbwe Kwa Kinyasha, wakati wa kuweka jiwe la msingi Awamu hii ya Sita pia waliahidiwa jambo hilo hilo. Kwa hiyo, viongozi wawili wa juu waliahidi. Je, ni lini sasa barabara hiyo ya Rau – Shimbwe Kwa Kinyasha itajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake, inaweka kipaumbele kikubwa sana kwa ahadi za Viongozi Wakuu. Mheshimiwa Shally Raymond ametoa historia kidogo kueleza kuhusiana na ahadi ya ujenzi wa barabara hii ya Rau – Shimbwe. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Shally Raymond kwamba Serikali tayari imeiweka barabara hii katika mipango yake kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inakuja kuijenga ili iweze kuwanufaisha wananchi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kutoa kauli ya Serikali kwamba Serikali itakuja kuhakikisha inatekeleza ahadi hii muhimu kabisa iliyotolewa na viongozi wetu ili wananchi waweze kupata barabara nzuri ambayo itawasaidia katika majukumu yao, kwa maana ya shughuli za kiuchumi, na pia kufikia huduma za msingi za kijamii.

**MWENYEKITI:** Swali linalofuata, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, aulize swali lake.

Na. 676

**Kukamilisha Miundombinu ya Shule za Igamba na Itaka Sekondari**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya Shule za Igamba na Itaka kwa ajili ya kuanza kidato cha tano na sita?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga na kupandisha hadhi shule za sekondari ili kutoa elimu ya Kidato cha Tano na Sita kwa kuzingatia mpango wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018/2019 na mwaka 2023/2024 Serikali ilitoa shilingi milioni 418 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, matundu sita ya vyoo na mabweni mawili katika Shule ya Sekondari Igamba na vyumba vinne vya madarasa na matundu manne ya vyoo katika Shule ya Sekondari Itaka. Aidha, mwaka 2025 shule ya Sekondari Igamba imepangiwa wanafunzi 57 wa Kidato cha Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita katika shule za Sekondari Igamba na Itaka kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ni kweli Shule ya Sekondari Igamba imepokea wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita, lakini Jimbo la Mbozi ndiyo linaloongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu ndani ya Mkoa wa Songwe. Tupo wakazi laki tatu, lakini tuna shule za sekondari 28 na tuna *high school* moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya msingi ya kupeleka fedha kwa haraka ili hii Shule ya Sekondari ya Itaka ianze nayo kuwa *high school* na kupokea wanafunzi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana kwenye upande huu wa kuimarisha miundombinu ya Sekta ya Elimumsingi, lakini kuhakikisha Sekta ya Elimumsingi kwa ujumla wake inaweza kuendelea kuimarika ili wanafunzi wetu wapate elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa miundombinu, Serikali kama nilivyotangulia kusema katika Jimbo hili la Mbozi,

tayari imefanya uwekezaji wa kujenga miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kupandisha shule moja hii ya Sekondari ya Igamba iweze kuwa shule ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeweka katika mipango ujenzi wa miundombinu muhimu na uimarishaji wa Shule hii ya Sekondari ya Itaka ili na yenyewe iweze kupandishwa hadhi kuwa kidato cha tano na cha sita ili iweze kuwanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kutumia nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wajibu wake wa msingi, kwamba kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri, aweze kuweka katika mipango na kutenga bajeti kwa ajili ya kuanza kujenga miundombinu hii muhimu kabisa itakayohitajika kwa ajili ya kupandisha shule hii ya Sekondari Itaka kuwa na kidato cha tano na cha sita. Serikali Kuu itakuja kuunga mkono jitihada hizi kwa kuongeza nguvu kuhakikisha miundombinu yote inayohitajika inakamilika, na shule hii inapata usajili wa kuweza sasa kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Shule ya Sekondari ya Chamriho na Shule ya Sekondari ya Hunyari zimekamilisha miundombinu yote ya kuanzishwa kwa *high school* kidato cha tano na kidato cha sita. Je, ni lini hizo shule zitafunguliwa; na miundombinu yote, imekamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa shule za sekondari kama hizi, mathalan hii Shule ya Sekondari Chamriho na Hunyari ambazo tayari zimejengewa miundombinu ya msingi zitakazoziwezesha kuwa shule za kidato cha tano na cha sita, ni kwamba, Mkurugenzi anafanya mawasiliano na Wizara ya Elimu ili wadhibiti ubora waweze kufika

kufanya ukaguzi na hatimaye shule hizi ziweze kupata usajili na wanafunzi sasa waweze kuanza kupokelewa katika shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kutumia nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wajibu wake wa msingi, aweze kufanya mawasiliano hayo na Wizara ya Elimu kwa ajili ya kupata usajili wa shule hizi, ziweze sasa kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Na. 677

**Kutenga Bajeti ya Ujenzi wa Barabara za Lami Mitaa ya Namtumbo**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatenga bajeti ya ujenzi wa barabara za lami katika mitaa ya Namtumbo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu hitaji la barabara za lami katika Mji wa Namtumbo ambazo ni takribani kilomita 28.1, na imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo kwa awamu, ambapo katika mwaka 2023/2024 kiasi cha shilingi milioni 890 kilitumika kujenga kilomita 1.6 za tabaka la lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024/2025, Serikali ilijenga barabara yenye urefu wa kilomita 0.5 kwa tabaka la lami kwa gharama ya shilingi milioni 295. Katika mwaka 2025/2026, Serikali imeweka katika mipango yake na bajeti ujenzi wa barabara kwa

tabaka la lami yenye urefu wa kilomita moja kwa shilingi milioni 475.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara kwa tabaka la lami katika Mji wa Namtumbo na Makao Makuu ya Miji ya Wilaya zote hapa nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Vita Kawawa amefurahia na anaishukuru Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya katika Jimbo lake. Pamoja na kufurahia yeye, mimi naomba kupachika hapo swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuishukuru *TARURA* kwa kuweza kuweka taa kwenye Mji wa Himo, taa kama thelathini hivi, nashukuru sana. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba barabara hii ya Uchira – Kisomachi anaifahamu sana, tulikuwa tumeahidiwa kwamba wangekamilisha ujenzi wa kilometa 2.8 kwa kiwango cha lami katika kipindi hiki, lakini juzi nimepita kule bado yule mkandarasi hajafanya chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Naibu Waziri tutegemee nini au una kauli gani kuhusiana na suala hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu kabisa wa barabara hii ya kutokea Uchira yenye urefu wa kilometa 2.8 ambayo ipo katika Mji wa Himo, na tayari tumeshakaa naye. Alifika ofisini; Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tukazungumza na kukubaliana kimsingi kuhusiana na ukamilishaji wa ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itahakikisha barabara hii inajengwa, ila nitumie nafasi hii kumkumbusha Meneja wa *TARURA* wa Mkoa na wa Wilaya waweze kufanya usimamiaji na ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kwamba mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi wa barabara hii anaweza kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ratiba iliyowekwa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara hii iweze kusimamiwa ili barabara hii iweze kukamilika kwa wakati na iweze kuwanufaisha wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge Serikali itafanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha barabara hii inakamilika iweze kuwa na manufaa makubwa kwa ajili ya wananchi wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ni lini Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ambazo zinapita milimani katika Jimbo la Newala, hasa kutoka Mikumbi kwenda Mpanyani, Mkomatuu kwenda Chimemena, na Lihanga kwenda Chikalule? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya na inaendelea kufanya uwekezaji mkubwa sana katika kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Pia, utaona kwamba katika kipindi hiki cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita bajeti ya *TARURA* imeongezeka mara dufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021, bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni shilingi bilioni 275 kwa mwaka, lakini muda huu tunavyozungumza mwaka wa fedha 2025/2026, bajeti ya *TARURA* itakuwa ni shilingi trilioni 1.18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la bajeti linaonekana katika kila wilaya. Kila wilaya imepata ongezeko la bajeti kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu muhimu kabisa ya barabara hizi za wilaya inaendelea kuimarika. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwamba barabara hizi alizozitaja ambazo ni za milimani katika Jimbo la Newala zitafikiwa na Serikali na zitakuja kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Mameneja wa *TARURA* ngazi ya Mkoa na Meneja wa *TARURA* Wilaya waweze kufanya tathmini na waweke katika mipango ili ziweze kujengwa barabara hizi, kwa maana zitengewe bajeti ziweze kujengwa barabara hizi na ziweze kuwanufaisha wananchi wa Newala. Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Serikali inakuja kujenga barabara hizi ulizozitaja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona. Nitaanza na Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza Naibu Waziri ninawashukuru *TARURA* jinsi mnavyofanya kazi. Swali langu la msingi, makao makuu ya Wilaya ya Mbogwe yako Kasosobe Bwerwa pale. Tuna jengo pale la halmashauri, lakini pia hata nyumba za watumishi zipo pale Makao Makuu ya wilaya mpya. Ni lini Serikali itatoa fedha ili angalau tuweke kilometa tatu za lami katika eneo lile? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipokea pongezi za kutoka kwa Mheshimiwa Nicodemas Maganga kuja *TARURA*. Pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipaumbele kikubwa cha Serikali ni kuhakikisha kwamba kwenye makao makuu ya wilaya barabara za lami zinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimhakikishie kwamba, katika makao makuu ya wilaya hii na hasa katika eneo lile la Kasosobe tayari Serikali imeweka katika mipango na bajeti kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi katika eneo hilo kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, eneo hili linakuja kujengwa lami kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Serikali ilitujengea kilometa moja ya lami makao makuu pale Kalumwa, na nimewahi kukuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni lini tutajengewa mitaro kwa sababu ile kilometa moja kuna nyumba pembezoni, inaponyesha mvua, maji yale huwa yanaenda kuharibu mali za watu ndani ya majengo hayo. Ni lini sasa utatoa fedha hizo ili mitaro hiyo iweze kujengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweka kipaumbele kikubwa sana katika kuhakikisha inapojenga barabara, hizi barabara tunazozijenga zijengwe pamoja na mitaro na ziwekewe na taa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la msingi la ujenzi wa mitaro ni kwa sababu maji ni adui namba moja wa barabara zetu hizi. Kwa hiyo, ili barabara zetu ziweze kuishi kwa muda unaokubalika, tunatengeneza mitaro ili ku-*drain* maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Serikali ilifika ikaanza ujenzi wa barabara katika makao makuu ya wilaya kwa kilometa moja, na tayari tumeweka katika mipango na bajeti ujenzi wa mitaro ili kuhakikisha barabara hiyo inakuwa na mitaro, lakini mwisho wa siku pia inakuwa ina taa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Hussein Amar, Serikali itafika kwa ajili ya kuhakikisha inaimarisha miundombinu ya barabara hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalumu, aulize swali lake.

Na. 678

**Kudhibiti Vumbi la Makaa ya Mawe – Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kudhibiti vumbi la makaa ya mawe yanayosafirishwa kupitia Bandari ya Mtwara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Makamu wa Rais imechukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti vumbi la makaa ya mawe yanayosafirishwa kupitia Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizo ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa bandari nyingine nje ya Manispaa ya Mtwara Mikindani katika eneo la Kisiwa Mgao ambapo bandari hiyo itatumika kusafirisha bidhaa chafuzi kwa mazingira, kama vile simenti na makaa ya mawe. Hivyo, magari yote yanayobeba makaa ya mawe yatapita nje ya Manispaa kuelekea bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni pamoja na kutumia mitambo miwili yenye uwezo wa kupakia tani 600 kwa saa ambayo ina mikanda maalum *(Conveyor Belt)* kwa ajili ya kupakia mzigo kwenye meli, kuweka nyavu za kuzuia vumbi,

kuhakikisha magari yote yanayosafirisha makaa ya mawe yanafunikwa ili kuzuia vumbi lisisambae kwenye mazingira, na kunyunyuzia maji mara kawa mara katika eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Ni kwa kiwango gani Serikali imetoa elimu na vifaa stahiki kwa wale vibarua na wafanyakazi ambao wanashughulika pale bandarini ili kuwakinga na athari zitokanazo na vumbi hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa Bandari ile ya Mtwara bado inatumika na siyo kule ambako kunajengwa bandari kwa sababu bado haijakamilika, ni kwa namna gani wafanyakazi wanaofanya kazi pale bandarini wanakingwa ili wasiathirike kutokana na hiyo vumbi ya makaa ya mawe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza na kumshukuru sana kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini kubwa zaidi kwa kutaka kuona namna ambavyo Serikali inatatua changamoto za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hatua mbalimbali ambazo Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na *NEMC*, kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, *OSHA*, bandari na taasisi nyingine ambazo kwa namna moja ama nyingine zinahusika, tumechukua katika kutoa elimu na kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba tunawaelimisha wananchi hasa wafanyakazi wa maeneo hayo juu ya masuala mazima ya matumizi ya vifaakinga

ambavyo vinaweza vikawasaidia kuepukana na athari kubwa ya vumbi linalosababishwa na mkaa ama makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ni elimu ya usalama mahali pa kazi. Tumekuwa tukiwapa elimu mara kwa mara wenzetu wa bandari, hasa na wananchi ambao wanazunguka maeneo hayo. Pia, kubwa zaidi tumekuwa tukiwaelekeza, kuwasimamia na kuwasisitiza kuwa wote wanaomiliki magari yanayopakia mkaa wa mawe kuhakikisha kwamba wanafunika ili mavumbi yasitoke yakaenda kuathiri wananchi. Kikubwa tumekuwa tunatoa elimu ya uchimbaji na namna ambavyo tunaweza tukasimamia sheria za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni kweli kumekuwa kuna changamoto hasa kwenye athari ya bandari. Moja ni kwamba, kama alivyosema na kama tulivyoeleza katika jibu la msingi, sasa hivi bandari imeshaanza kujengwa ingawa haijakamilika, lakini itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari hii itakapokamilika maana yake ni kwamba magari yote ambayo yatabeba mkaa wa mawe na bidhaa nyingine chafuzi za mazingira hayatapita eneo la makazi na yatapita mbali ili wananchi wasiweze kuathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi na tunaendelea kutumia mitambo maalumu ambapo mtambo huo hautafanya magari yaingie baharini au bandarini. Pia mtambo huo ndiyo utakaobeba mizigo kuingiza kwenye bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul Maalim.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Changamoto iliyokuweko Mtwara ndiyo iliyokuweko Zanzibar, ya vumbi la saruji na bidhaa nyingine ambazo zinatumia bahari. Je, Serikali mna mpango gani wa kushughulikia changamoto hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Abdul Maalim, Mbunge na mtumishi wa wananchi wa Jimbo la Amani. Naye nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya, hasa ya kutaka kujua namna ambavyo Serikali tumejipanga katika kutatua changamoto za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zipo hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa. Moja ni kubwa la mwanzo ni la kuendelea kutoa elimu kwa wananchi, kwa sababu ni kweli, kama saruji na kule inashushwa, kama ni *gypsum* kule pia inashushwa, na kama baadhi ya bidhaa nyingine ambazo zinaweza kuwa ni chafuzi nazo zinashushwa kupitia bandari tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumekuwa tukitoa elimu, hasa elimu ya mazingira ya kazi kwa wananchi na hasa wafanyakazi wa hapo. Kikubwa Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya ukarabati wa bandari nyingi sana ambapo bandari nyingi sasa zimeanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Bandari ya Mpigaduri inajengwa, lakini ipo Bandari ya Mwangapwani. Bandari hizi zitapunguza msongamano wa mizigo kushushwa sehemu moja na badala yake ikawa kuna sehemu ya abiria na kuna sehemu ya mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, sasa aulize swali lake.

Na. 679

**Msimamo wa Serikali Kwenye Suala la Nchi za *BRICS* Kujiondoa Kwenye *Dollarisation***

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** auliza: -

Je, nini faida na hasara ya Tanzania kutokana na msimamo wa Nchi za *BRICS* ambazo zimejipanga kujiondoa kwenye Mfumo wa *Dollarisation*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa na ushirikiano wa karibu wa muda mrefu na nchi za *BRICS* (*Brazil*, *Russia*, *India*, *China* na Afrika Kusini) katika nyanja mbalimbali ikijumuisha masuala ya kiuchumi, biashara, na diplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahusiano hayo yanadumishwa kwa kuendelea kuwepo kwa Balozi za nchi hizo hapa nchini na Tanzania kuwa na Balozi katika nchi hizo. Mahusiano hayo yanaendelea kuleta mafanikio chanya kwa Serikali ya Tanzania kwa kutumia fursa za kiuchumi zinazopatikana katika nchi hizo ambazo pia zinaimarisha mahusiano ya uwili baina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Tanzania siyo mwanachama wa *BRICS* ila inashiriki katika mikutano ya *BRICS* kama *observer*. Hivyo, mafanikio au changamoto zozote katika umoja huo zinazoweza kutokea katika sekta ya kiuchumi na fedha hususan ya kujiondoa kwenye *Dollarisation*, Tanzania hatutakuwa na athari za moja kwa moja kwa kuwa sio wanachama wa *BRICS*. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri na ambayo kwa kweli nilitegemea ndivyo yatakavyokuja. Naomba niishauri Serikali baada ya kuuliza swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRICS* ni *Economic Alliance* na duniani sasa tuna kitu tunaita *Economic Intelligence*. Kwa hiyo, ningeiomba na kuishauri sana Serikali, kwa sababu hii vita ni vita kubwa na *real,* ina uwezo wa kutengeneza uchumi na kuuangusha siku moja tu, ninadhani ushahidi wanao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali na hasa wale wataalamu wetu wa mambo ya uchumi na fedha, hebu waende wakakae wafanye tathmini kwa sababu kushiriki kwetu kama washirika tu kwenda kuangalia mikutano, lazima kuwe na tija ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba waangalie kwa sababu kwa kweli hii ni vita ni ya kiuchumi, na sisi kama Tanzania tusije tukaachwa nyuma tujikaona kama ni wasindikizaji. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri unapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Zahor kwa kuwa mara nyingi ushauri wake unakuwa ni wa kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Zahor kwamba, ushauri wake tumeuchukua na Serikali itaufanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini sasa aulize swali lake, na swali hilo litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Daniel Pallangyo.

Na. 680

**Kufufua Viwanda vya *TPI* na *General Tyre***

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO K.n.y. MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Viwanda vya *Tanzania Pharmaceutical Industries (TPI)* na *General Tyre*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kufufua viwanda vyote nchini ambavyo havifanyi kazi kwa sasa ili kujiepusha na gharama kubwa za uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, upotevu wa ajira, na upotevu wa fedha za kigeni za kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industries*, kupitia Serikali, Msajili wa Hazina anashirikiana na mwekezaji kukifufua kiwanda hicho, na kwa sasa kipo hatua za mwisho za kuanza ukarabati wa kiwanda pamoja na mitambo; na baada ya ukarabati huo kukamilika, uzalishaji utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kiwanda cha *General Tyre*, Serikali kupitia Shirika la Mandeleo la *NDC* inatafuta mwekezaji wa kimkakati ili kuanza uzalishaji wa matairi ya magari hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Danielson John Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pia niseme kwamba Mji wa Arusha ulikuwa na viwanda vingi sana. Kwa kifupi, kufa kwa viwanda hivi wananchi wamepoteza ajira na mapato. Kuna viwanda vingine ambavyo vilikufa tu hivi katika mazingira

ambayo hatukujua. Kwa mfano, Kiwanda cha *Kilitex*, Kiwanda cha Kiko, Kiwanda cha Kuchakata Pareto, na vingine vilikufa. Je, Serikali inasemaje kuhusu kufufua hivyo viwanda sasa hivi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, ukiangalia nchi yetu rekodi tulikuwa na viwanda vingi sana vya kihistoria. Baba wa Taifa alitengeneza viwanda vya kimkakati, lakini ilikuwa nia njema ya Serikali ya kufanya ubinafsishaji wa viwanda hivyo, lakini kwa bahati mbaya sana maeneo mengi viwanda hivyo hatukufikia malengo tuliyofikia. Ndiyo maana Serikali sasa hivi tunafanya *analysis* katika mikoa mbalimbali, na tayari timu yetu imeanza katika mikoa mbalimbali ukianzia Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga, lakini inaenda katika mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa ni kuhakikisha tunakamilisha ule mpango mkakati wa viwanda 9,045 tunavyotarajia kutengeneza ndani ya miaka mitano hii, ndani yake ikiwepo kufufua viwanda vyote ambavyo vimetelekezwa na wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba niwahakikishie wananchi wa Kilimanjaro, wananchi wa Arusha na kote Tanzania kwamba, Serikali imeamua kuliweka jambo hili kimkakati, na tushukuru sana Ofisi ya Msajili wa Hazina inatupa ushirikiano wa kutosha kuona jinsi ya kufikia malengo mapana kuhakikisha viwanda hivi vyote vinafufuliwa na hasa wale waliokuwa na nia ovu ya kuchukua viwanda na kuvifanya *Collateral* katika upatikanaji wa fedha. Kwa hakika tumejipanga, hatutakubali katika eneo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Hanang, Kata ya Mogitu ina malighafi ya kutosha kabisa kwa ajili ya utengenezaji wa *cement*. Je, Serikali ina

mkakati gani wa kuleta wawekezaji pamoja na kuwezesha wananchi ili kuanzishwa kiwanda cha *cement*, kwa sababu malighafi hiyo ipo ya kutosha kwa zaidi ya miaka 50? Je, Serikali ina mpango gani kuja kuwekeza sasa ili kuona *cement* hiyo na malighafi hiyo inaleta tija kwa wananchi wa Hanang, na pia kwa Taifa letu la Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kushukuru na nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Asia kwa sababu amekuwa Mbunge machachari sana na wananchi wa Mkoa wa Manyara wanajivunia yeye, kijana machachari na shupavu sana. Hongera sana dada yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la malighafi inayopatikana Mkoa wa Manyara, *especially* eneo la Hanang. Ni kweli, nchi yetu hivi sasa katika mpango wa viwanda, tumejielekeza kwanza kuangalia malighafi tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara una fursa kubwa sana kwa ajili ya kuzalisha madini ya *Iron Ore,* ambayo yanatumika katika uzalishaji wa *cement*. Hivi karibuni, bahati nzuri juzi tu, nilikuwa na mwekezaji ambaye anakuja kuangalia eneo la kimkakati kati ya Manyara na Dodoma kutengeneza kiwanda kikubwa cha *cement* kwa lengo la kutumia malighafi iliyopo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutachagiza eneo hili, hasa kuwahamasisha wawekezaji fursa hiyo iweze kutumika vizuri kwa maslahi mapana ya uchumi wa mtu mmoja mmoja katika eneo la Hanang na Mkoa wa Manyara, Dodoma na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yetu kubwa, kama nilivyosema hapa juzi kwamba nchi yetu sasa hivi *production* ya *cement* imeenda vizuri, sasa tunazalisha tani milioni 10 na *demand* yetu ni tani milioni saba. Tunataka tu-*expand* kabisa

eneo hilo la sekta, ili tuweze ku-*export* katika nchi nyingine tupate fedha za kigeni. Hiyo ndiyo *target* yetu kama nchi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa wote nimeshawaona, mnaweza kuketi. Tutaanza na Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kufufua kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa za kilimo cha *Twiga Chemical* kilichopo Mjini Moshi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Profesa, watu wa Kilimanjaro wanajivunia yeye, kwani amekuwa mbobezi mahiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki, kama *target* yetu, tumeanza kufanya *mapping* katika Mkoa wa Kilimanjaro kubainisha viwanda vyote. Kwa mfano, hapa utasikia Kiwanda cha Kibo, Kilimanjaro ilikuwa na utajiri mkubwa sana wa viwanda. Hii ndiyo miongoni mwa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika eneo ambalo tunataka tulifanyie kazi na hasa ukiangalia katika kipindi cha sasa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kufanya *investment* kubwa sana katika upande wa sekta ya Kilimo. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima twende tufikie muda tusi-*import,* baadhi ya dawa tuzalishe hapa nchini. Kwa hiyo, hilo ni miongoni mwa maeneo ambayo naomba nikuhakikishie katika mpango wetu mkakati ule wa viwanda 9,045 ikiwa ni pamoja na kufufua vile viwanda ambavyo mwanzo vilikuwa vinafanya kazi, lakini sasa hivi havifanyi kazi, na eneo hilo la *Twiga Chemical Limited* tutalifanyia kazi kwa nguvu zote. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnaweza mkaketi nimeshawaona. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tunajua lengo la Serikali kutenga hivyo viwanda zaidi ya 900, naamini ni pamoja na kuendeleza yale maeneo ambayo wananchi walitenga ya *EPZA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo anajua, nilisema, kwetu Jimbo la Bunda Mjini, Kata ya Guta, eneo la Tailo, ni zaidi ya miaka 17 wananchi wamelipwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ambavyo vitachangia ajira katika Jimbo la Bunda Mjini, Halmashauri pamoja na Wilaya nzima ya Bunda na Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, ni lini sasa watajenga viwanda kutokana na malighafi zinazopatikana Mkoa wa Mara na Jimbo la Bunda Mjini? Kuna wafugaji, kuna wavuvi, tunalima pamba na mambo mengine. Ni lini sasa watatujengea viwanda, ili akinamama na vijana waweze kupata ajira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze UVCCM mwenzangu, dada yangu, Mheshimiwa Ester Bulaya alikuwa Lumumba pale, amefanya kazi kubwa sana katika Redio Uhuru na maeneo mengine. Ni miongoni mwa vijana waliokuwa shupavu sana wakati ule, *comrade* Masauni akiwa Mwenyekiti. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo kwanza *target* yetu ni kweli, tuna maeneo mengi tuliyatenga kwa ajili ya kuhakikisha tunawekeza viwanda, siyo Mara peke yake, hata katika Mkoa wa Tanga na maeneo mengine. Kwa hiyo, nakuhakikishia kwamba, mpango huu Serikali tunaondokanao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tutabainisha yale maeneo ambayo Serikali tuliyatenga kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, na

inawezekana tulilipa fidia, lakini sehemu nyingine fidia haijalipwa. Hivyo, mpango mkakati ni wa kujenga *industrial parks* na *clusters* mbalimbali, tunaenda kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie wananchi wa Mkoa wa Mara, kama Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ilivyojipanga kimkakati, tutashughulikia maeneo yote kwa kipaumbele kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanaleta tija kwa vijana wetu ambao ni wengi. Sasa hivi ni *graduates,* wanamaliza vyuo vikuu waweze kupata ajira kupitia Sekta ya Viwanda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *issue* ya fidia, maeneo ya Yombo katika Wilaya ya Bagamoyo, wamekaa kwa muda mrefu sana pasipokulipwa fidia. Ni lini watu hawa watalipwa fidia ikiwa maeneo haya yamechukuliwa na Serikali kwa muda mrefu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mchungahela, kwa kuuliza eneo la Bagamoyo. Kubwa zaidi naomba nikuhakikishie kwamba, ni mpango wa Serikali kuhakikisha eneo la Bagamoyo linaenda kuwa nyeti kwa Taifa letu katika mpango mkakati wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni katika mpango huo kuna maeneo mengine yamelipwa fidia na maeneo mengine hayajalipwa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi amesikia Waziri wa Mipango alikuja na mpango mkakati mkubwa sana wa suala zima la ujenzi wa viwanda na hasa upande wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie wale ambao hawajalipwa fidia, *provided* kwamba wapo katika

taratibu zile ambazo zimeainishwa na Serikali, kila mtu atapata haki yake ile inayostahili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Ilemela Eneo la Nyamanoro, ilitenga eneo kwa ajili ya *industrial park* na andiko tayari lilishakuja Wizarani, na mwaka juzi liliingia kwenye utaratibu wa mchakato, lakini mpaka sasa ni kimya. Napenda kujua ni lini *industrial park* hiyo itajengwa; kwa sababu, miundombinu yote ya umeme na barabara ipo vizuri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze mtani wangu, bibi yangu, Mheshimiwa Angeline Mabula, kutoka Wilaya ya Ilemela. Ni kweli, nashukuru eneo hilo la Ilemela, mimi na yeye kipindi kile tulienda pamoja, wakati ile timu ya Mawaziri, hasa upande wa karibuni na uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie kwamba, katika mipango ambayo tumeweka ya kuainisha maeneo ya ujenzi wa *industrial park* na tunafahamu kwamba, Kanda ya Ziwa tunatumia bidhaa nyingi kutoka nchi jirani, tuna kila sababu ku-*establish hub* kubwa ya viwanda eneo hilo. Lengo ni kupunguza *importation* ya bidhaa kutoka nchi za jirani na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia dada yangu, bibi yangu, Mheshimiwa Angeline Mabula, tutalifanyia kazi eneo hili na hasa, mahususi, eneo la Mkoa wa Mwanza katika Wilaya ya Ilemela. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Wakili Msomi, Edward Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amesema kuna

mwekezaji anataka kuja Manyara na sisi Kiteto tupo tayari kumpokea, lini atamleta Kiteto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Wakili Msomi, kaka yangu, Mheshimiwa Olelekaita na ninamombea sana watu wa Kiteto wamrudishe, amefanya kazi kubwa sana, amelielimisha Bunge hili sana. Elimu yake ya usomi wa sheria imetusaidia sana kama Bunge la Tanzania, na watu wa Manyara wasikie kwamba tuna Mbunge makini kutoka katika Wilaya ya Kiteto. Hongera sana ndugu yangu Mheshimiwa Olelekaita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili maana yake ni watu wanafanya *needs assessment* katika maeneo haya. Tutahakikisha maeneo yote wanayapitia na ninaamini katika kanda hii tutapata kiwanda kimoja kikubwa, *provided* kokote kitakapojengwa kitasaidia wananchi wa kanda hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imani yetu kama Serikali ni tutachagiza kuwapata watu hawa wafike, wabainishe maeneo, waweze kuwekeza. Kwa hiyo, naomba niwawahakikishie watu wa Manyara na Dodoma, tunahangaikia ujenzi wa kiwanda kikubwa cha *cement* hapa, lengo kubwa ni kutumia *Iron Ore* iliyopo, kuzalisha malighafi ya *cement,* hasa kuzalisha *cement for export* katika maeneo mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, nakushukuru. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, sasa aulize swali lake.

Na. 681

**Ukarabati wa Gereza la Keko**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya ukarabati au kuliongeza Gereza la Keko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Mahabusu Keko ni miongoni mwa Magereza yaliyojengwa katika kipindi cha ukoloni, mwaka 1957. Serikali kupitia Jeshi la Magereza imepokea fedha kiasi cha shilingi 988,125,000.00 kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Jeshi la Magereza linaendelea na hatua mbalimbali za manunuzi kwa ajili ya kuanza kazi ya ukarabati wa gereza hilo, ahsante.

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Dorothy George Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nishukuru sana kwa jinsi ambavyo fedha hizi zimeweza kushushwa. Sina swali la nyongeza, lakini napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo hakika tumeweza kuomba na fedha hizi na zimeshuka. Muhimu ni kwamba, tunaomba sasa Jeshi la Magereza lifanye kazi kwa udhibiti, ili gereza lile lipate kuwa na usafi na usalama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kupokea ushauri na maombi ya Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Temeke, kwa ufuatiliaji wake. Pia, namshukuru sana kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ukarabati wa magereza mbalimbali hapa nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Gereza la Wilaya ya Mbulu limejengwa toka enzi za koloni. Kwa Bahati nzuri na Serikali imekuwa na mipango mizuri ya kukarabati magereza haya kongwe nchini. Mpango ukoje kwa magereza yote nchini, likiwemo Gereza la Wilaya ya Mbulu, katika ukarabati na ujenzi wa makazi ya Askari na jengo la magereza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kila mwaka wa fedha tunatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa magereza mbalimbali. Kwa *Mwaka wa Fedha* 2024/2025 tulitenga shilingi bilioni 6.272, kwa ajili ya ukarabati wa magereza haya. Tumeanza na Gereza la Keko, Ukonga, Segerea pamoja na Gereza la Lilungu liliopo Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge pia, kama nilivyosema, tunatenga fedha kila mwaka. La Mbulu pia, tutalichukua tuliingize kwenye mpango, tayari kwa ajili ya kutengewa fedha ya ukarabati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Omar Said.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali isiyoridhisha ya makazi ya Askari wa Finya, Basara pamoja na Wetelaini, ni lini Serikali ifanya ukarabati mkubwa wa makazi hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka na kufanya ukarabati wa makazi ya Askari wetu. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pia maeneo aliyoyataja ya Finya pamoja na Wete wataalamu wetu wataenda kufanya tathmini, ili kuona kiasi kinachotakiwa na kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati.

Askari wetu wakae katika mazingira salama kwa ajili ya kulinda raia na mali zao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, uwepo wa magereza katika maeneo mbalimbali umesaidia sana kuongeza nguvukazi, hasa katika masuala ya usafi na mambo mengine, maeneo ya miji. Je, ni lini Gereza la Wilaya ya Nyasa, ambalo tayari Wizara imeshalipa fidia, litaanza kujengwa ili pia, Nyasa inufaike na uwepo wa magereza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya kwa ufuatiliaji wake wa Gereza la Nyasa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tayari kama ambavyo Serikali imelipa fidia, ndiyo hiyo hatua ya kwanza. Kulipia fidia ni kuwaondoa wananchi katika eneo hilo na sasa hatua inayofuata ni kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Gereza la Nyasa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 682

**Ujenzi wa Barabara ya Kasulu Hadi Uvinza**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Kasulu hadi Uvinza kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa sehemu ya Kasulu – Kanyani, kilometa 10. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Sehemu ya Kanyani hadi Uvinza Kibaoni, kilometa 60 umekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa ujenzi wa barabara unaoendelea ndani ya Mkoa wa Kigoma. Swali langu la kwanza, je, ni lini sasa ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Ni lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Simbo mpaka Kalya kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Uvinza kwenda Kanyani ni muhimu, ni kati ya barabara kuu. Tayari tumeshakamilisha usanifu, na ndiyo kipande pekee kitakachokuwa kimebaki katika Mkoa wa Kigoma, barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mambo mawili ambayo tunayafanya. Moja ni kutafuta fedha za ndani kujenga hicho kipande cha kilometa 60, lakini pia, yapo mazungumzo ambayo yanaendelea na Benki ya Maendeleo ya Afrika, ambao wameonesha uwezekano wa kuweza kutoa fedha, ili tuweze kuijenga hiyo barabara kwa mkopo nafuu. Kwa hiyo, Serikali inaifanyia kazi kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara ya Simbo kwenda Kalya. Barabara hii najua ina changamoto kubwa, na Serikali baada ya kuona ina changamoto kubwa, hasa kwenye Mto

Malagarasi, tunachofanya mwaka huu, 2025, ni kufanya ujenzi wa Daraja la Mto Malagarasi, ambapo kuna kivuko. Ndiyo imekuwa changamoto kubwa, na tayari usanifu umekamilika, tupo kwenye hatua za mwisho na wenzetu wa *World Bank* kulijenga hilo daraja wakati tukifanya maandalizi ya kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami kutoka Simbo hadi Kalya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kutupatia barabara ya kutoka Tarime Mjini mpaka kule Serengeti, Mugumu na imeanza kujengwa kilometa 25. Tayari kilometa 10 wananchi wanatumia barabara ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, Mkandarasi kipande ambacho kimebaki aliingia *site,* halafu ameondoka, mvua inanyesha, magari hayapiti. Nini kauli ya Serikali kwa sasa, ya dharura, ili wananchi waweze kutoka Nyamongo kwenda mjini na Mugumu, Serengeti, bila ya usumbufu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Mara kuhakikisha kwamba, Mkandarasi huyu anarudi *site* kuhakikisha zile njia za mchepuko, kwa maana ya *diversion,* anazitengeneza, ili watu wa Tarime, Nyamwaga hadi Nyamongo waweze kufanya shughuli zao za kimaendeleo na kijamii bila matatizo, kwa sababu, mkataba unamwambia mkandarasi aliyeko *site* ni lazima ahakikishe barabara ambayo anaifanyia kazi inapitika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa, barabara ya kutoka Kibena - Lupembe hadi Madeke, Mbunge wa eneo hilo Mheshimiwa Swalle, amekuwa akiulizia kila wakati. Ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara ambayo inatoka Njombe, kwa maana ya Kibena *Junction*, Madeke, Mlimba hadi Ifakara, tumeshaanza kuijenga kwa upande wa Ifakara. Kwa upande wa kutoka Njombe - Kibena - Lupembe hadi Kidigembe, yalikuwa pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Kilometa 40 tayari ipo kwenye hatua za manunuzi, ili ianze kujengwa kwa awamu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, hali ya barabara ya Makofia, - Mlandizi - Nzenga mpaka Vikumburu kwa sasa kutokana na mvua zilizonyesha ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, tuna matumaini ya kwamba, barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami, je, Serikali inatupa matumaini gani mapya ya barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami pamoja na kuhuisha fidia ya maeneo ya Makofia - Mlandizi na Nzenga? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Makofia hadi Mlandizi, barabara ilishafanyiwa usanifu, na tayari tunasubiri wenzetu wa Hazina kuweza kutoa fidia, ili kazi ya ujenzi ianze kujengwa. Kutoka Mlandizi – Mzenga kwenda Vikumburu, kwanza ipo kwenye bajeti kwa maana ya kuanza ujenzi, lakini kipande ambacho kinakwenda kutoka Mlandizi hadi kwenye Reli tayari tumeshatangaza zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelekeza tu Meneja wa Mkoa wa Pwani kwamba, kama mvua imeshakatika, ahakikishe kwamba, barabara hiyo inatengenezwa ili iweze kupitika wakati tunasubiri kuanza kwa ujenzi wa lami kwa vipande ambavyo tutaanza mwaka huu wa fedha, 2025/2026, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 683

**Barabara ya Igauri – Ilongero Hadi Haydom**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Igauri Km 11.5 – Ilongero hadi Haydom Km 80 kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Igauri – Ilongero hadi Haydom ni barabara ya mkoa inayojulikana kwa jina la Singida *Urban* – Ilongero – Haydom (kilometa 93.8). Ujenzi wa Barabara hii kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa jumla ya kilometa 12.5 kutoka Singida eneo la Njuki hadi Igauri zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ipo katika hatua za mwisho za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya Igauri – Ilongero (kilometa 18.5). Kwa sehemu iliyobaki ya kutoka Ilongero hadi Haydom (kilometa 69.8), Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhani Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninashukuru kwa maelezo hayo yanayotia moyo ya kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningependa kujua; kwanza, mchakato huu kidogo umekwishakuwa wa muda mrefu, Je, Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kwa *TANROADS*

na kwa Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa, kuhakikisha kwamba huu mchakato unaharakishwa uende haraka ili ujenzi uweze kuanza haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika mwaka wa fedha 2022/2023 tukiwa hapa Bungeni niliwahi kuuliza kuhusu ujenzi wa kiwango cha lami wa kipande cha barabara ya Ilongero - Ikhanoda hadi Ngamu kwa kiwango cha lami, ambacho nacho kinatuunganisha sisi na Manyara, nataka kujua, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hiyo sasa na yenyewe ujenzi unaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, suala la manunuzi linaweza likachukua muda mfupi ama muda mrefu kulingana na wale walioomba kazi. Wakati fulani wanaweza wakaomba wakandarasi ambao hawana sifa, kwa hiyo, unaweza ukatangaza upya. Ama wakaomba, lakini kukawa na bei kubwa, ambayo kwa utaratibu uliopo haiwezi ikakubalika. Kwa hiyo, lazima itachukua muda kukaa nao ili kuweza kupunguza bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kazi iliyopo sasa hivi, tuko kwenye majadiliano na wakandarasi ambao wameomba. Mimi nitoe maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Singida na Makao Makuu *TANROADS* kuhakikisha kwamba suala hili linafanyiwa uharaka ili ujenzi uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, la Ilongero – Ngamu barabara ambayo ina takribani kilometa kama 27, kitu tutakachokifanya ni kuweka kwenye mpango ili kwanza iweze kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mwaka wa fedha unaokuja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekamilisha kufanya upembuzi yakinifu wa barabara ya

kutoka Bariadi – Itilima – Kisesa – Mwandoya – Mwanhuzi – Bukundi – Mkalama – Iguguno hadi Singida, je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipande alichataka cha kuanzia Iguguno hadi Itilima viko vipande ambavyo viko tayari kwenye hatua za kuanza ujenzi, kwa maana ya manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kuwa ndiyo kwanza tumekamilisha upembuzi yakinifu, na sasa Serikali katika mwaka wa fedha unaokuja itabidi ipange, tutakuwa sasa tunaipangia kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Isingekuwa rahisi kuipanga wakati usanifu bado haujakamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, kabisa ninaishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara ya kuanzia Dumila mpaka Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninatambua kuwa kuna ujenzi unaoendelea kwenye kipande cha barabara pale Ulaya kwa kiwango cha lami. Je, ni lini kipande kilichobaki kuanzia Kilosa mpaka Mikumi kitajengwa kwa kiwango cha lami, kwani wakati wa mvua hii barabara ni mbovu sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwa kuwa mvua imekatika, nimwelekeze Meneja wa Mkoa ahakikishe mkandarasi aliyepangiwa kazi aende akarekebishe maeneo yote yaliyokuwa korofi ama yaliyoharibika ili magari yaweze kupita katika hali ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuikamilisha hii barabara, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kuna barabara ambayo sasa ni kipaumbele cha Serikali ni Kilosa - Mikumi kwa sababu ndiyo inayounganisha karibu ukanda huu wa Njombe kama tutakamilisha kutoka Ruvuma ili watu wasiende Morogoro wakishafika Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inatafuta chanzo madhubuti ama chanzo kizuri, ikiwa ni pamoja na kuangalia fedha za wahisani ili tuweze kuijenga hiyo barabara ya kuunganisha Mikumi – Kilosa hadi hapa Dumila kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi. Barabara ya Kiranjeranje - Nanjirinji mpaka Ruangwa imekamilika kufanyiwa upembuzi na usanifu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami angalau kutoka Kiranjeranje mpaka Makangaga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumekamilisha kuifanyia usanifu barabara hiyo, lakini Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nao kwamba barabara hiyo ina madaraja kama matatu ambayo ni korofi, ambayo mvua ikinyesha hayapitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika katika Awamu hii ya Sita ni kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa fedha kujenga Daraja la Mbwemkuru. Ukishamaliza hili Daraja la Nakiu kwenda Kiranjeranje imekuwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza tunahakikisha kwanza tunayajenga hayo madaraja yote matatu wakati tunatafuta fedha sasa za kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, aulize swali lake.

Na. 684

**Barabara ya Handeni – Kiteto – Chemba hadi Singida**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto – Mrijo – Chemba – Kwamtoro hadi Singida kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kiteto – Mrijo – Chemba hadi Singida yenye urefu wa kilometa 461 kwa awamu ambapo kwa sehemu ya kwanza Handeni – Mafuleta (kilometa 20) ujenzi umefikia asilimia 46.06.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sehemu ya pili ya Mafuleta – Kileguru (Km 30) na Kibaya – Kisima (kilometa 50) makandarasi wapo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* na Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)* wako kwenye majadiliano ya awali ya kuijenga kwa utaratibu wa *PPP*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara ambayo inaunganisha mikoa mitatu, kwa maana ya Singida, Dodoma na Manyara. Barabara hiyo inatoka Manyoni inaingia Mpendo -

Sanzawa – Kwa Mtoro – Lahoda hadi Hanang. Mpaka leo hii, pamoja na kuwa ni barabara inayounganisha mikoa mitatu, bado inahudumiwa na *TARURA*. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa barabara hiyo inapandishwa hadhi na ijengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Monni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu uliopo, ili barabara iweze kupandishwa hadhi, Wakala wa Barabara ama Wizara ya Ujenzi huwa inapokea maombi kutoka kwenye mikoa husika, na hasa baada ya kuwa imejadiliwa kwenye vikao vya *Road Board* na *RCC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimshawishi Mheshimiwa Mbunge kwamba wenzetu wa Mkoa wa Singida, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyoni, kwa maana inaunganisha mikoa hiyo, basi waweze kuleta hayo maombi Wizara ya Ujenzi, nasi tutaifanyia tathmini na ikikidhi vigezo itapandishwa hadhi ili iweze kuhudumia na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya *interchange* kutokea Zamahelo hadi Donsee ili kusudi iweze kuja kuungana na ile barabara ambayo ni ya Chemba hadi Singida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii barabara sina uhakika kama itakuwa ni *interchange,* lakini ukitoka Zamahelo kwenda Donsee ndiyo barabara ambayo inakutana na ile barabara ndefu ya kutoka Kibirashi kwenda Kwa Mtoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya kwenye hii barabara ni kuanza kuifanyia usanifu ili wananchi watakaokuwa wanatoka Chemba kama wanakwenda Singida wasilazimike kwenda huko. Kwa hiyo, wana uwezo wa kutokea hapa Zamahelo kwenda Donsee, halafu baada ya kukamilisha usanifu itakuwa ni kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Barabara ya Kibirashi – Kwa Mtoro mpaka Singida ilikuwa inaambatana pamoja na ulipaji wa fidia kwa wananchi waliokuwa wanaathirika na barabara hiyo. Ametuambia hapa kwamba *TPA* pamoja na *TANROADS* wako kwenye michakato. Je, Serikali inawaambia nini Watanzania ambao wamepitiwa na barabara hiyo kwa ajili ya ulipaji wa fidia ili mchakato utakapokamilika barabara hiyo isilete tena kikwazo kwa ajili ya fidia kwa wananchi wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, pale ambapo fidia inahitajika, Serikali haianzi ujenzi mpaka iwe imekamilisha usanifu. Tunachofanya sasa hivi ni kwamba watu watafanyia tathmini, na ukishafanyiwa tathmini watalipwa ndipo ujenzi utakapoanza; lakini wakati tunafanya hizi shughuli, hazizuii kuendelea na taratibu nyingine za *TPA* na *TANROADS* kufanya kuingia kwenye mazungumzo ili tuanze kuijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi watakaoathirika na barabara hiyo kwamba watalipwa mafao yao kwa maana ya fidia kabla hatujaanza ujenzi wa hiyo barabara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linafuatwa. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, sasa aulize swali lake.

Na. 685

**Ujenzi wa Barabara ya Usalimwani – Ikuwo – Nkenja – Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Usalimwani - Ikuwo hadi Nkenja kwa kiwango cha changarawe utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Usalimwani – Ikuwo – Nkenja yenye urefu wa klometa 42.7 ni barabara ya Wilaya iliyokasimiwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* mwaka 2023. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 jumla ya shilingi milioni 865.14 zimetumika kufanya matengenezo ya barabara hii ikiwa ni pamoja na kuongeza upana wa barabara, kuweka changarawe, kujenga makalavati pamoja na kuweka zege katika maeneo korofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026 jumla ya shilingi milioni 488.8 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na matengenezo ya barabara hiyo, ikiwa ni pamoja na kuweka changarawe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makete, hususan wananchi wa Kata hii ya Ikuwo pamoja na Kata ya Mfumbi kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kujenga barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ilikuwa ni barabara yenye changamoto kubwa sana, lakini tulipoomba kuipandisha isimamiwe na *TANROADS,* wakapokea na wakaitengea fedha kwa ajili ya kuijenga na imejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii barabara hii imetumika kama mbadala. Unajua changamoto ya barabara kutoka Makete kwenda Mbeya, barabara hii ndiyo imetumika mbadala sasa hivi kuisaidia Wanamakete. Kwa niaba ya wananchi wa Makete na kwa niaba ya Serikali ya Makete nichukue nafasi hii kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu kwa Mheshimiwa Waziri. Barabara kutoka Lupila – Kipengele kilometa 42 tuliwaomba waipandishe kwenda *TANROADS,* na ninashukuru waliipandisha kwenda *TANROADS*. Tangu tarehe 12 mwezi wa Saba mwaka 2024 leo hii tunaizungumza ni tarehe 25 barabara hii haijaanza kujenga. Je, ni lini barabara hii itajengwa ili iwasaidie wananchi wa Lupila, Kipengele katika shughuli zao za kiuchumi kwa sababu ni barabara ya kimkakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya barabara hii kupandishwa hadhi, sasa tumepata bajeti ya kuijenga. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Makete kwamba mwaka huu wa fedha, barabara hiyo kwanza baada ya kupandishwa hadhi itaongezwa upana, itakarabatiwa madaraja na pia itajengwa kwa kiwango cha changarawe, kwa maana ya *standard* ya barabara zetu za *TANROADS*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Nimesimama kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu alinifuata mara kadhaa ofisini kufuatilia fedha za barabara ile ya kwanza ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri

amejibu pamoja na hii, nimhakikishie kwamba, hata baada ya Bunge kuvunjwa, maombi yake aliyoyaleta kwa ajili ya wananchi wa Kata hizi alizozisema yataendelea kutekelezwa kwa fedha kwenda kwenye miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema jana wakati nahitimisha, kwamba Waheshimiwa Wabunge ambao wameleta maombi yao kwa ajili ya miradi iliyoko majimboni mwao itaendelea kutekelezwa hata wakati uchaguzi inaendelea; na *inshallah* watakapomrudisha tena wakati anaapa atapita kwenye barabara hiyo ikiwa imeshatengenezwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru. Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Charles Mwijage.

Na. 686

**Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria kwa Kata za Muleba**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE K.n.y. MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza: -

Je, lini mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya Kata za Gwanseli, Magata, Muleba, Bureza, Kikuku na Kagoma – Muleba utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Kata Sita za Muleba, Magata/Kurutanga, Gwanseli, Bureza, Kikuku na Kagoma Wilayani Muleba Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo unaokadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 42. Aidha, katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya majisafi na salama katika kata hizo, Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi ya maji minne ya Ilemela, Magata/Kurutanga, Butembo na Kagoma inayohudumia wananchi 22,279 waishio kwenye Vijiji nane vya Ilemela, Gwanseli, Bureza, Butembo, Makarwa, Kikuku, Kagoma na sehemu ya Kijiji cha Nsisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, Serikali imekamilisha mradi wa upanuzi wa skimu za maji ya Kurutanga na Butembo kwenda Kijiji cha Magata na Kitongoji cha Omdangara, Muleba Mjini ambapo huduma ya maji inawafikia wananchi wapatao 11,340, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa sera yake ya kuhakikisha kuwa maji ya Ziwa Victoria yanakwenda kwenye mikoa au miji iliyolizunguka, hususan Muleba. Swali dogo la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri anakumbuka ombi letu la Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria pale Kasharunga kwenda Muleba Magharibi? Je, ni lini upembuzi na usanifu wa kina kwa ajili ya kutoa maji Kasharunga - Mubunda - Nyakatanga - Mushabago, kwenda Ngenge na Rutoro utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ambaye anaendelea kushirikiana vizuri sana na wananchi wake kutatua changamoto za maji kwa kuwasemea katika Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ambao ni wa kimkakati ambao Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiusemea mara kwa mara na sisi Serikali tumeona ni vyema sasa tukauingiza katika

hatua za utekelezaji. Nimtoe hofu kwamba mwaka wa fedha 2025/2026 mradi huo utaanza kufanyiwa upembuzi yakinifu katika hatua za awali za na baadaye tutafanya *detail design* kwa ajili ya kujua kwamba sasa gharama gani zitahitajika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huo unatekelezwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Wizara imeshatekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba maji safi na salama ya mradi wa shilingi bilioni 500 wa Arusha unapelekwa Kata za Mererani na Endiamtu, kwa sasa bado Kata ya Shambarai, Naisinya na Oljoro namba tano ambapo Mheshimiwa Rais alielekeza maji yale yafike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itatekeleza mradi huo ikiwa ni pamoja na Kata ya Msitu wa Tembo ambayo madini ya *flouride* yanaharibu meno ya watu na pia kupindisha watoto miguu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Ole-Sendeka na kwa kutambua uwekezaji mkubwa sana uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kuwekeza shilingi bilioni 500, pia, ninafahamu kabisa kwamba kuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuendelea kutekeleza mradi katika maeneo ya Mererani, Msitu wa Tembo na pia utekelezaji upo chini ya Wizara ya Maji tu umeshaanza na utekelezaji huu unaenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, maeneo yote ambayo Mheshimiwa Rais ameshaelekeza na maeneo mengine ambayo ni mpango wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tutahakikisha kwamba tunawapelekea huduma ya maji ili waweze kuondokana na madini ya *flouride* ambayo yamekuwa yakiwatesa sana wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayoendelea ya kutoa maji kutoka *Lake Victoria* kwenda Urambo, je, ni lini sasa Serikali itaanza kuweka miundombinu ya maji itakayowezesha kufikisha maji katika tanki litakalokusanya maji hadi kuwafikia wananchi kutokana na shida kubwa ya maji tuliyonayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana mama yangu Margaret Simwanza Sitta kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kwa wananchi wake wa Urambo. Tunatambua kabisa kwamba Serikali iliwekeza zaidi ya shilingi bilioni 680 kuyatoa maji kutoka ziwa victoria mpaka Tabora, lakini pia Serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 143 kwa ajili ya Kaliua, Urambo pamoja na Sikonge. Tunatambua kwamba mradi huu umefikia asilimia nzuri sana za utekelezaji zaidi ya 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mradi huu wakati unatekelezwa, pia kulikuwa na mtandao wa zamani ambao ulikuwa unawahudumia wananchi wa Urambo. Sasa kazi ambayo tunaifanya kwa sasa, kwa sababu tanki limeshakamilika, ni kuanza kupeleka maji kwenye mtandao wa zamani, wakati mradi ukiwa unaendelea wa kuondoa mtandao wa zamani na kuweka mtandao mpya, lakini wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikutoe hofu, lengo letu ni kuhakikisha kwamba maji yawe yanapatikana kwa wingi kwa kupitia mtandao wa zamani ambapo tunajua pia mtandao wa zamani una changamoto zake, lakini tutaendelea kujenga ule mtandao mpya, baadaye mpya utakapokamilika, mtandao wa

zamani tunauondoa ili wananchi muda wote waweze kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Lusanga kina changamoto kubwa sana ya maji hasa Kitongoji cha Lusanga A, Kilingeni na Mkuyuni. Tunamshuruku Mheshimiwa Rais, tumepata mradi wa maji wa shilingi milioni 400, lakini mkandarasi toka amekabidhiwa *site,* ni miezi miwili hajarudi tena. Nini kauli ya Serikali juu ya huyu mkandarasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jonas, Mbunge wa Mvomero na hakika sisi Wizara ya Maji tunaendelea kumshukuru kwa kutupatia ushirikiano mkubwa sana, pale ambapo kunapotokea changamoto ndani ya jimbo lake, amekuwa akituwasilishia kwa haraka sana na Wizara ya Maji imekuwa ikichukuwa hatua. Pia tunamshukuru kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwa kuwasemea wananchi wake wa Mvomero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tumeshapata mkandarasi baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuridhia kutoa kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya kupeleka katika kijiji kile, na kweli mkandarasi ameshapatikana, lakini kulikuwa na changamoto hapa, lakini zimeshakamilika, zimeshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Maji kumwelekeza *RM* - Mkoa wa Morogoro ahakikishe mkandarasi huyu anafika *site* na kuanza kufanya kazi mara moja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaishukuru Serikali kwa kutupatia Mradi wa Maji wa Miji 28 wa shilingi bilioni 41. Je, Serikali haioni umuhimu sasa, kwa kuwa tunakwenda kuvunja Bunge la kuwatuma ama kuwaelekeza watendaji wakuu wa Wizara kama vile Katibu Mkuu kumtembelea mkandarasi yule ili kuhakikisha anamaliza mradi kwa wakati kwa maana ya kum-*push?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Asenga kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya wananchi wake wa Ifakara. Pia, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, kama Wizara, watendaji wetu wataenda kutembelea na kuona namna gani mkandarasi anaendana na makubaliano yaliyopo kwenye mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kuna mkataba lazima uheshimiwe. Wakati wa kuhitimisha mkataba ni lazima sisi kama Serikali tujue kabisa kwamba haendi nje ya mkataba ambao tunakubaliana. Kwa hiyo, nimtoe hofu kuwa watendaji wetu wa Wizara akiwemo Katibu Mkuu, wataenda kuhakikisha kwamba mkandarasi huyo anaharakisha aweze kukamilisha kwa wakati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chanzo cha maji ambacho kipo maeneo ya Magamba na wataalamu wakiongozana na Mkurugenzi wa *RUWASA* walienda kuona chanzo kile; na chanzo kile mradi wake ukitekelezeka utahudumia zaidi ya kata 15. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanza kujenga mradi huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuna hiki chanzo, na kati ya vitu ambavyo ni vya muhimu

sana kupata huduma ya maji safi na salama ni chanzo cha uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujiridhisha kwamba chanzo hiki kitaweza kuhudumia maeneo ambayo tumeyatarajia au tumeyaweka kwenye *scope* yetu ya kazi, basi hatua za kufanya upembuzi yakinifu huanza, na baada ya hapo tutafanya *detail design* na baada ya hapo tutajua gharama ya mradi na baada ya hapo tutafanya kazi ya kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kutoka Mwanza kwenye Mikoa ya Tabora na maeneo mbalimbali ni mradi ambao ni wa kupongezwa sana, Serikali imefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inaonaje iweze kuhakikisha wakati maji haya yanapotoka kule Ziwa Victoria Mwanza, kabla ya kwenda kwenye maeneo mengine; Tabora ni kwa ndugu zetu tunawapenda, lakini walau yaweze kupita na kufika kwenye maeneo ya karibu hasa Mkoa wa Shinyanga kwenye Jimbo la Kishapu kwa sababu kumekuwa kuna miradi ya maji, lakini ni kama ya kudokoadokoa? Wananchi wanalalamika sana kuhusu ukosefu wa maji katika Wilaya ya Kishapu na hasa Jimbo la Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaiomba Serikali ije na mradi mkubwa ambao utagusa maeneo mengi katika wilaya hii ambayo ni kame.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhudumia Watanzania wote ambao wanatoka kwenye vyanzo

vya maji na maeneo ambayo yamepakana na Ziwa victoria ikiwemo Shinyanga, Simiyu, Bariadi, Itilima pamoja na Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais maelekezo yake yapo wazi kabisa. Kwa upande wa maji kwa bomba ambalo linapeleka Kahama pamoja na Tabora, tayari; Shinyanga hivi tunavyoongea tayari wanatumia maji ya kutoka Ziwa Victoria; vilevile katika Wilaya ya Kishapum tayari wanatumia maji ya kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichobaki kwa upande wa Kishapu kuna vijiji 11 ambavyo bado havijafikiwa na huduma hii ya maji ya kutoka Ziwa Victoria wanatumia visima. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali ni kufanya *extension* kutoka bomba kuu la kutoka Ziwa Victoria kuhakikisha kwamba tunawasambazia wananchi waliopo katika Wilaya ya Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu dada yangu Mheshimiwa Lucy Mayenga, pia ninampongeza kwa kuendelea kuwasemea wananchi na wakina mama wa Kishapu. Pia, nimtoe hofu kuwa Serikali imelitazama kwa umakini sana na tayari kuna mradi ambao unaenda kuanza hivi karibuni kuhakikisha kwamba tunafanya *extension* kwa ajili ya vijiji hivyo 11 vya Jimbo la Kishapu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea swali linalofuata, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, aulize swali lake.

Na. 687

**Kusambaza Maji Vijiji vya Hatete, Ihowa Weluli, Luanda na Moyovizi – Vwawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kusambaza maji katika Vijiji vya Hatete, Ihowa, Welu II, Ruanda na Myovizi – Vwawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Hatete - Ruanda uliopo Wilaya ya Mbozi Mkoani Songwe. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 200,000, ujenzi wa dakio *(intake),* ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 25 sanjari na ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 55% na unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2025 na kunufaisha wananchi 6,628 waishio kwenye vijiji vitano vya Hatete, Ruanda, Ihowa, Myovizi na Welu II.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa kuanza kutekeleza mradi huu. Kwa kweli Serikali imefanya vizuri sana, hongereni sana. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa katika eneo la *intake* pale pana malalamiko ya baadhi ya wananchi, lakini pia wamevamia katika maeneo yale ambapo pana *intake*. Je, upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wanajenga wigo kwa ajili ya kulinda ile *intake* pamoja na kupanda miti katika maeneo yale kusudi maji yasije yakapungua siku za usoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tanki moja la lita 2,000 ni dogo sana ukilinganisha na ukubwa wa vijiji na umbali wa vijiji vilivyopo, je, upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba mnajenga matanki mengine katika kila kijiji kusudi wawe na uhakika wa upatikanaji wa maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Hasunga. Kwanza kwa niaba ya Serikali ninapokea pongezi zako na hizi maana yake ni pongezi za wananchi wake. Tunampongeza pia Mheshimiwa Hasunga kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wake na tunampongeza kwa kuendelea kushirikiana na Wizara ya Maji ili kuendelea kutatua changamoto za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria namba Tano ya Mwaka 2019 inawapatia mabonde. Kuna Bodi za Mabonde ambazo majukumu yake ni kulinda vyanzo vya maji, na pia kuendeleza kuhakikisha kwamba hatuwi na changamoto katika vyanzo vyetu vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *intake* kama kuna malalamiko ya wananchi na kuvamia, sisi kupitia mabonde tutahakikisha kwamba kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya tunajenga ili kuhakikisha kwamba kusiwe na changamoto wakati wa kutatua changamoto nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lengo ni kwamba, vyanzo vilindwe, lakini na wananchi wasikilizwe kuangalia malalamiko yao yapo na *base* ipi ili kuleta maridhiano ambayo hayatakuwa na changamoto katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa tanki hili la lita 200,000, ni kwamba, tunapofanya usanifu wa miradi tunaangalia mahitaji ya wananchi katika eneo husika; na tunapoona kwamba mahitaji, hatuwezi kujenga tanki kubwa wakati tunajua kabisa mahitaji yanahitajika kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaendelea kupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Kulingana na sensa ya watu na makazi na ongezeko la watu, tutajaribu kuwa *proactive* kuangalia ongezeko hilo kama litaathiri upatikanaji wa maji kulingana na tanki ambalo tulikuwa tunalijenga. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, hilo tutalizingatia sana na tunaupokea ushauri wako kama Serikali. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Kinjumbi Kata ya Kinjumbi, Jimboni Kilwa Kaskazini Serikali ilianza kutekeleza mradi wa maji wa kisima kirefu tangu mwaka 2021. Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huu wa kimkakati katika Kata ya Kinjumbi ili kuwatua wakina mama ndoo kichwani na kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanaweza kupatikana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu, kwa kweli amekuwa akiusemea sana mradi huu. Nimtoe hofu, na ninaomba nilipokee kwa ajili ya kulifuatilia na ili tutoe majibu ya uhakika kwa wananchi wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa shilingi 1,800,000,000.00 kujenga mradi wa maji katika Kata ya Mbangamao iliyopo katika Mji wa Mbinga. Mradi ule ulikamilika na ukaanza kutoa maji, lakini una changamoto kubwa sana. Wananchi bado hawapati maji safi na salama kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wale wanapata maji na mradi ule unarekebishwa ili wananchi waendelee kupata maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Jonas Mbunda na ninamshukuru pia kwa kutambua uwekezaji mkubwa sana wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika eneo la Mbangamao ndani la Jimbo lake la Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatuma timu ya wataalamu. Sisi Wizara ya Maji tunayo taasisi ambayo inashughulika na kupima ubora wa maji na usalama wa maji. Lengo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tutatuma timu yetu ya wataalamu wakachunguze na kujiridhisha kama hayo maji yana changamoto ya kiusalama, basi tutachukua hatua stahiki. Lengo ni kwamba wananchi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na wananchi wa Mheshimiwa Jonas Mbunda wapate huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mbunge wa Viti Maalum sasa ulize swali lake.

Na. 688

**Kuongeza Fedha za Mkopo kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum**

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza fedha za mkopo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu wenye mahitaji maalumu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Daktari, ninaomba nichukue nafasi hii kipekee kabisa kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, na kuwashukuru Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge lako hili Tukufu kwa malezi yenu katika kipindi chote cha miaka mitano. Ushauri wenu kwa Serikali, maoni na miongozo yenu ambayo mara kwa

mara mmekuwa mkitupatia sisi kama Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa upande wa Wizara ya Elimu, hili ni swali letu la mwisho kwenye Bunge hili, na niwaombee heri Wabunge wote tuje kuonana tena hapa mwezi wa Kumi na Moja tukiwa na afya njema, Mwenyezi Mungu akatuvushe huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba kujibu swali la Dkt. Nahato, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu mwaka hadi mwaka ili kuwawezesha wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu ambao ni wahitaji na wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo wa kiuchumi ili kuwawezesha kumudu gharama za masomo ya Elimu ya Juu na kufikia ndoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za mikopo zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 464 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 787 mwaka 2024/2025 na idadi ya wanufaika imeongezeka pia kutoka wanafunzi 145,000 mwaka 2020/2021 hadi 235,799 mwaka 2024/2025 wakiwemo wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, utoaji mikopo unawapa ahueni wanafunzi wenye mahitaji maalumu au wenye wazazi wenye ulemavu kwa kuwapatia kipaumbele katika upangaji wa mikopo ili kuwawezesha kumudu mazingira ya chuo katika kipindi cha masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wanafunzi 2,398 wamenufaika na mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka 2024/2025 kupitia kigezo cha mahitaji maalumu. Serikali inaendelea kupokea ushauri na maoni ya wadau kwa ajili ya kuyafanyia kazi kwa kushirikiana na wadau ili kubainisha aina ya uhitaji unaostahili kupewa kipaumbele bila kuathiri dhana ya uhitaji inayotamkwa na sheria. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Nahato.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kusema mambo mawili. Jambo la kwanza, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia na Serikali yake kwa jinsi ambavyo amewawekea mazingira mazuri sana wanafunzi, wahadhiri na wafanyakazi wa Vyuo Vikuu vya Umma Tanzania. Kama mwakilishi wao, naomba salamu zangu zimfikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, napenda sana kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na Naibu Waziri kwa umakini na umahiri wa kujibu maswali ya vyuo vikuu ambavyo kimsingi yameshatekelezwa na vingine vinatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mara yangu ya mwisho leo kuwa Mbunge wa Viti Maalum nikiwakilisha vyuo vikuu, nawapongeza Mawaziri wote mlioongezea kuchangia suala la vyuo vikuu, akiwepo Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni *Ph.D* mwezangu kutokea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuweza kuweka bajeti nzuri kwa vyuo vyetu vikuu nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Paulina tafadhali, Kanuni zinakutaka uulize swali la nyongeza, kama huna tunakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu ya swali hilo. Tunaendelea na swali linalofuata, kama linakuhusu unaweza ukabaki. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake swali litaulizwa na Mheshimiwa Felista Njau.

Na. 689

**Huduma za Afya kwa Wazee**

**MHE. FELISTA D. NJAU K.n.y. MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Wazee wanapata huduma za afya bila kikwazo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ambapo mara utekelezaji wake utakapoanza, utakuwa suluhisho katika kuwezesha makundi yote wakiwemo wazee kupata huduma pasipo kikwazo cha gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wazee bado wanatozwa fedha wanapokwenda kupata huduma za afya licha ya Sera ya Afya kutamka kwamba wazee wapate huduma hii bure, hasa Jimbo la Moshi Vijijini na nchi nzima. Serikali haioni haja sasa ni wakati wa kutengeneza bima za dharura kwa ajili ya wazee hawa wakati wanasubiri Bima ya Afya kwa Wote kwa nchi nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kumekuwa na gharama kubwa na mzunguko mkubwa kwa wazee kuelekea kwenye vituo vya afya kwa ajili ya kupata huduma, ikizingatiwa wazee wengi wamepata magonjwa mengi yasiyoambukizwa, hivyo kuwa na mzunguko mkubwa katika vituo vya afya na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa sana. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuweka dirisha maalum kwa ajili ya wazee na wahudumu wake ili waweze kupata huduma hii kirahisi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kumpongeza dada yangu kwa maswali yake mazuri

sana, lakini michango yake mizuri sana kwa sekta yetu ya afya kwa kipindi chote ambacho amekuwa hapa Bungeni na anayo maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kuhusu suala hili la wazee. Ni kweli tunazungumzia wazee wasiojiweza, lakini kuna mtu kwa mfano, baba yake Mheshimiwa Dkt. Mollel au mwenye uwezo hata kuliko Mheshimiwa Dkt. Mollel, ambaye ni mzee wa miaka 60, huyo kwa sababu ya suala zima la bajeti, pia ukiangalia shilingi bilioni 200 tunayopitisha, tukisema tuwahudumie watu wote wasiojiweza, fedha hiyo inaweza isitoshe. Kwa hiyo, tunatumia hekima kuhakikisha wale wanaoweza kuchangia, wanachangia lakini wale wasioweza, basi wanahudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo tu kwa *group* la wazee, ni pamoja na akina mama wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na wengine ambao hawako kwenye makundi hayo lakini hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *checks and balance,* basi yule anayeweza, tunamwomba achangie, kwa sababu hata ukiangalia gharama za bei za afya kwenye nchi yetu iko chini ukilinganisha na nchi zilizotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Serikali inachangia kwa ulipiaji, huwa ni watu wanachangia *percent* wakati tayari Serikali imeshachangia kiasi kikubwa, ndiyo maana gharama zetu ni ndogo ukilinganisha na wenzetu waliotuzunguka. Kwa hiyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kweli tunahitaji kuongeza nguvu kwenye eneo hilo, pia baadaye kuongeza bajeti kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu suala la kwamba wazee wasizunguke sana kwenye hospitali zetu kwenda maeneo mbalimbali; nitumie fursa hii kumtaarifu kuwa, kwa kweli tumeanza. Kwenye hospitali zetu zote tayari limeshatolewa maelekezo, na baadhi ya hospitali zetu za Mikoa, hospitali za Taifa na baadhi ya hospitali za Wilaya wanalo dirisha la wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kupitia swali hili kuagiza vituo vyote vya afya nchini, kuanzia zahanati mpaka Hospitali ya Taifa, pawepo na dirisha la wazee na kutengenezwa *mechanism* ambayo wazee hawatakiwi kuzunguka sana wakati wanapata huduma. Siyo wazee tu, na wengine wenye ulemavu mbalimbali na wengine wenye matatizo mbalimbali ambayo hayawahitaji kuzunguka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Bananga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Vifurushi vya Bima ya Afya bado vinaonesha vina gharama kubwa sana kwa wazee kuanzia miaka 60 na kuendelea. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wazee hawa angalau wanapunguziwa gharama za matibabu ili waweze kupata matibabu inavyostahili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimjibu shemeji yangu Mheshimiwa Hawa Mwifunga, na nimshukuru kwa mchango wake mkubwa kwenye eneo hili kwa kipindi chake chote alichokuwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kwanza moja kuna vifurushi ambavyo ni *optional,* kwa maana mtu unachagua, tusichanganye. Tunapozungumzia Bima ya Afya kwa Wote, vifurushi vilivyowekwa siyo kwa ajili ya Bima ya Afya kwa Wote, kwa hiyo, ni *optional.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusisahau kwamba bima ya afya siyo mfuko wa kusaidia wasiojiweza, ni watu wanachangia fedha zao halafu ziwatibu wakati watakapokutana na matatizo ya kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukigeuza bima ya afya kwamba ni mfuko wa kusaidia wasiojiweza, mwisho wa siku wewe Mbunge na wafanyakazi wa umma ambao wanachangia kwenye ule mfuko siku wanakuja kuugua wao watakuta fedha hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kuna *options* hizi ambazo nimezungumzia hapa ambazo zimetajwa na Sera yetu ya Mwaka 2027 ya kusaidia wasiojiweza waweze kupata huduma, lakini kumbuka magonjwa haya ya kuambukiza ni gharama sana. Kwa hiyo, tunachosema alipie yule kwenye bima ambaye anaweza kulipia, asiyeweza, atapitia kwenye hili dirisha lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, huyo wa bima atakayelipia kifurushi kidogo ambacho ana uwezo nacho, lakini ikifika mahali anatumia bima yake, anatakiwa aongeze fedha na hana fedha, bado kuna dirisha Serikali imeweka asaidiwe asiongeze fedha, bima yake ichangie kile kilichochangiwa, lakini zifuatwe *procedures* nyingine ili aweze kusaidiwa hizo fedha ambazo zimeongezeka pale juu. Kwa hiyo, kuna namna mbalimbali za kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema bima, wasipige hesabu sahihi ambayo itafanya mfuko uweze kuwa *sustainable,* tutarudi hapa Bungeni kwamba Mfuko wa Bima ya Afya umeingia kwenye matatizo. Bado wewe Mbunge utalaumu kwa nini mmeua bima ya afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliohudhuria Shughuli za Bunge leo. Kwanza tunao wageni wa Mheshimiwa Spika. Mgeni mmoja wa Mheshimiwa Spika ambaye ni Ndugu Mussa Athuman, Dereva wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Tunaye kwanza Mgeni wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge, ambaye ni Shekhi Mohamed Hamis kutoka Lushoto Mkoa wa Tanga. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge ambao ni familia yake kutoka Kilombero Mkoani Morogoro ambao ni Ndugu Anna Mushi ambaye ni mama mzazi wa Mheshimiwa Mbunge. Karibu sana mama yetu.

Tunaye Mwalimu Amina Athuman, mke wa Mheshimiwa Mbunge. Karibu sana shemeji yetu. Yuko wapi sijui? Amesimama wapi? *Okay*.

Wapo watoto wa Mheshimiwa Mbunge ambao ni Ndugu Amani Abubakari, Ndugu Alphan Abubakari na Ndugu Anaya Abubakari, wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Haji Amour Haji, ambao ni familia yake kutoka Mjini Zanzibar. Kwanza ni Ndugu Salma Almad ambaye ni mke wa Mheshimiwa Mbunge, asimame. Karibu sana. Pia, tunaye Ndugu Atka Haji, mtoto wa Mheshimiwa Mbunge. Karibuni sana Bungeni. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni Saba wa Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge, ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Shinyanga na Morogoro wakiongozwa na Mama yake mzazi, Ndugu Suzana Sabuni. Karibu sana Mama Mzazi. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni Nane wa Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Tunao wageni wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Ndugu Francis Kapinga, Meneja wa Uzalishaji wa Vipindi *TV3* na *ST Bongo TV* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 29 wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ambao ni wachungaji na wainjilisti kutoka Babati Vijijini, Mkoani Manyara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao ni wapigakura wake kutoka Kwela Mkoani Rukwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni familia yake kutoka Mkoani Katavi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Prof. Alois Ndakidemi, Mbunge, ambaye ni Ndugu Moses Peter, rafiki yake kutoka Mkoani Morogoro. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, ambaye ni Ndugu Hamis Jumbe, Mpiganaji wake kutoka Songea Mkoani Ruvuma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge na Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge ambao ni Ndugu zao kutoka Zanzibar, wageni wote hao wa makundi mawili, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge, ambaye ni Ndugu Shalon Nashon, mtoto wake kutoka Mkoani Kigoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, ambaye ni Mwalimu Hamis Kassinge, Mdogo wake kutoka Kilwa Mkoani Lindi. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni Sita wa Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge, ambao ni watoto wa rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge kutoka Kasulu Mkoa wa Kigoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mbunge ambao ni jamaa zake kutoka Bukoba Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wananchi kutoka Jijini Dar es Salaam ambao ni Ndugu Kajula, Ndugu Varian Nchimbi na Ndugu Valence Nchimbi. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wananchi wawili kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Juma Mashango na Ndugu Modrick Juma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wawili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 52 na Walimu Sita wa Shule ya Awali ya Msingi Elizabeth, kutoka Halmashauri ya Ubungo Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi 12 wa Chama cha Madereva wa Serikali. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 47, Wanachama wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kutoka Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Walimu Sita na Wanafunzi 106 wa Shule ya Awali na Msingi *Fountain of Joy* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninampisha Mheshimiwa Spika aendelee na majukumu.

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025
### *(The Finance Bill, 2025)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, aje awasilishe hoja inayohusu Muswada huu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, leo ni Jumatano, tarehe 25 mwezi wa Sita, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha Mwaka 2025 *(The Finance Act 2025)* pamoja na marekebisho yake usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoka shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini pamoja na Makamu wake na Kamati nzima kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoka ushauri kwa ajili ya maboresho.

Mheshimiwa Spika, majadiliano yamefanyika ya kina sana. Jana tumemaliza saa nane usiku; juzi ilikuwa saa saba na siku kabla ya hapo, jana jioni binti yangu alinitumia meseji, "Baba utarudi nyumbani?" Akidhani siku mbili hizi sikurudi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, kwa mara nyingine, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao wamechangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni jana, tarehe 24 Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi wa Sheria, Wataalam wa Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Aidha, ninawashukuru wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi wa ujumla ambao kwa nyakati tofauti wametoa ushauri wao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi za pekee kwa Mnadhimu Mkuu wa Serikali kwa uratibu wake mzuri aliofanya katika zoezi zima hili la uandaaji wa Muswada huu na hadi kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 12 Juni, 2025 na kupitishwa hapa Bungeni jana tarehe 24 Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho unakusudia kufanyia marekebisho sheria 33 ili kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umelenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi, uchukuzi na usafirishaji pamoja na sekta za elimu na afya ili kuboresha uzalishaji na kukuza uchumi wa jumla, kukuza ajira na hatimaye kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zinalenga pia kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Spika, Sheria zifuatazo ni Sheria ninazopendekeza kuzifanyia marekebisho: -

(i) Sheria ya Tozo za Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365;

(ii) Sheria ya Benki Kuu na Taasisi za Fedha, Sura ya 342;

(iii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;

(iv) Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 101;

(v) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439;

(vi) Sheria ya Korosho, Sura ya 203;

(vii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;

(viii) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;

(ix) Sheria ya Ushindani, Sura ya 285;

(x) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;

(xi) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;

(xii) Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276;

(xiii) Sheria ya Bima, Sura ya 394;

(xiv) Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025;

(xv) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;

(xvi) Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85;

(xvii) Sheria ya Madini, Sura ya 123;

(xviii) Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124;

(xix) Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282;

(xx) Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127;

(xxi) Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284;

(xxii) Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari, Sura ya 264;

(xxiii) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348;

(xxiv) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371;

(xxv) Sheria ya Tume ya UKIMWI, Sura ya 379;

(xxvi) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;

(xxvii) Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161;

(xxviii) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;

(xxix) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370;

(xxx) Sheria ya Reli, Sura ya 170;

(xxxi) Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220;

(xxxii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na

(xxxiii) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maudhui ya Muswada, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 34 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza, yenye ibara ya kwanza na ya pili inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, ambapo sheria itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2025 isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili yenye ibara za tatu hadi tano, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365 kama ifuatavyo: -

(i) Ibara ya nne, inapendekeza kurekebisha kifungu cha tatu ili kuongeza Shilingi za Kitanzania 1000 katika tozo inayotozwa kwa kila abiria anayesafiri kwa ndege; na

(ii) Ibara ya tano, inapendekeza kurekebisha kifungu cha saba ili kuwianisha tarehe ya kulipa ada ya huduma za bandari na tarehe ya kuwasilisha *return* kuwa siku ya 20 ya mwezi baada ya kukusanywa kwa ada hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha ulipaji na kuboresha usimamizi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu yenye ibara ya sita na saba kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 39(A) katika Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 ili kuiongezea majukumu Bodi ya Bima ya Amana *(Deposit Insurance Board - DIB)* ya kuweza kuongeza ukwasi kwa njia ya mikopo kwa benki au taasisi ya fedha yenye changamoto ya ukwasi. Aidha, kupitia utaratibu huo, benki au taasisi ya fedha iliyoongezewa ukwasi itakuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuipa *DIB* nguvu na uhalali wa kisheria wa kushiriki kikamilifu, kwa kushirikiana na Benki Kuu, katika kutathmini na kuamua hatua muafaka ambayo inapaswa kuchukuliwa pindi benki au taasisi ya fedha inapokuwa katika hatari ya kufilisika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne yenye ibara za nane hadi 18, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya

marekebisho katika Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 kama ifuatavyo: -

(i) Ibara ya tisa inapendekeza kurekebisha kifungu cha tano ili kuipa Benki Kuu jukumu la kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha na kuongeza masharti ya kuiwezesha Benki Kuu kutekeleza majukumu yake kwa uhuru;

(ii) Ibara ya 10 inapendekeza kurekebisha kifungu cha tisa ili kubainisha majukumu ya Bodi ya Benki katika usimamizi wa Benki Kuu, kuongeza idadi ya Wakurugenzi wasio watendaji katika Bodi ya Benki, kuongeza muda wa kuhudumu wa wajumbe wa Bodi ya Benki na kuweka utaratibu wa kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi kwa vipindi tofauti. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Benki Kuu;

(iii) Ibara ya 11 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 12 kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kubainisha muundo, ukomo wa muda na majukumu ya Kamati ya Sera ya Fedha na Kamati ya Ukaguzi. Lengo la marekebisho haya ni kubainisha masharti kuhusu Kamati ya Sera ya Fedha na Kamati ya Ukaguzi ili kuchochea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati husika;

(iv) Ibara ya 12 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 12(A) ili kuipa Bodi ya Benki Kuu mamlaka ya kuanzisha kamati nyingine kwa ajili ya kuiwezesha kutekeleza majukumu yake;

(v) Ibara ya 13 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 19 ili kubainisha muda ambao Waziri wa Fedha anaweza kutoa dhamana ili kurejesha mtaji wa Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ulinzi wa kisheria wa uhuru wa kifedha wa Benki Kuu na kuweka muda ambao Waziri wa Fedha anaweza kutoa dhamana za Benki ili kuongeza mtaji wa Benki pale inapobidi;

(vi) Ibara ya 14 inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 20 ili kubainisha sifa za maafisa walio katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, uteuzi na muda wa utumishi wa Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

(vii) Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 38 ili kuwezesha shughuli za uondoaji na uhamishaji wa fedha kati ya Taasisi za Kifedha, wakiwemo watoa huduma za fedha kwa njia ya kielektroniki, waunganishaji wa malipo, pamoja na kampuni za teknolojia ya kifedha. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha kusomana kwa mifumo ya malipo katika mfumo mzima wa kifedha;

(viii) Ibara ya 16 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 40 ili kuongeza wigo wa mikopo ya dharura inayotolewa na Benki kwa taasisi za fedha au mabenki kama mkopeshaji wa mwisho; na

(ix) Ibara ya 17 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 60 ili kuainisha wajibu wa Benki Kuu katika uandaaji wa bajeti ya Serikali, Sheria ya Fedha na mambo mengine yanayoathiri kazi, mamlaka na wajibu wa Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ushiriki wa Benki Kuu katika nyanja zote zinazohusiana na majukumu ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano yenye ibara ya 19 hadi 20 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 60 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 ili kuweka sharti la mashauriano baina ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha na Wizara, Taasisi za Serikali, Wakala au Mamlaka za Serikali kabla ya Wizara au Taasisi hizo kuanzisha tozo, ada mpya au wakati wa kufanya mabadiliko yoyote ya viwango vya ada na tozo.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuipa Wizara ya Fedha nguvu za kisheria ili kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa mapato ya Serikali ikiwemo kufanya tathmini ya athari au faida ya viwango vya ada na tozo vinavyopendekezwa. Hatua hii haitahusisha utaratibu wa uanzishaji au marekebisho ya tozo na ada kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita yenye ibara za 21 hadi 23, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 101 kama ifuatavyo: -

(i) Kubainisha kwenye kifungu cha tatu tafsiri ya maneno "*Noncitizens*" ndani ya Sheria hiyo;

(ii) Ibara ya 22 inapendekeza kurekebisha kifungu cha nne ili kuziondolea mamlaka za utoaji leseni uwezo wa kufunga biashara pale mfanyabiashara amekiuka masharti ya leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mazingira bora ya kibiashara; na

(iii) Ibara ya 23 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 14 ili kwanza, kuweka sharti kwa mamlaka za utoaji leseni kutoa leseni za biashara kwa raia wa kigeni kwa biashara zinazoruhusiwa kufanywa na raia hao; pili, kumpa Waziri mwenye dhamana na biashara mamlaka ya kuainisha biashara ambazo hazipaswi kufanywa na raia wa kigeni.

Lengo la marekebisho haya ni kulinda ajira za Watanzania na kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara baina ya Watanzania na raia wa kigeni. Aidha, utaratibu wa utekelezaji wa mapendekezo haya, utafanywa kupitia amri itakayotolewa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya biashara ili kubainisha orodha ya shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba yenye Ibara ya 24 na 25 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 18 cha Sheria ya Korosho, Sura ya 203 ili kumwezesha Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuweka mapato yatokanayo na tozo ya korosho kwa kipindi cha miaka minne. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Bodi ya Korosho kupata mapato haya kwa wakati ili kuchochea maendeleo ya sekta ya korosho.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane yenye Ibara za 26 hadi 34 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha pili ili kubainisha ndani ya Sheria tafsiri ya maneno "*Financial Institution*";

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 10 ili ukomo wa leseni kwa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kuwa miezi 12 tangu tarehe ya kutolewa badala ya leseni kufika ukomo kila mwisho wa mwaka. Hatua hii inatoa nafuu kwa wazalishaji na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 29 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 126 ili:-

(i) Kwanza, kufuta pendekezo la kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka 17% hadi 17.5%. Tunafuta pendekezo hilo la kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye mawasiliano;

(ii) Kuboresha tafsiri ya maneno "*dutiable value*" kwa ajili ya ushuru wa bidhaa katika mawasiliano ya kielektroniki;

(iii) Kuongeza katika wigo wa kodi watoa huduma za fedha na malipo kwa kutumia mifumo binafsi;

(iv) Kuongeza ushuru wa bidhaa katika malipo ya kutazama vipindi vya televisheni vinavyolipiwa kutoka 5% hadi 7%; na

(v) Kutoza ushuru wa bidhaa wa 20% kwenye vyombo vya nyumbani vilivyotumika na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza utumiaji wa bidhaa hizi ambao una madhara kiafya, kulinda viwanda vya ndani na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninapendekeza kufuta pendekezo la kutoza ushuru kwa kiwango cha shilingi 22,000.00 kwa kila tani ya hewa ukaa inayozalishwa kwenye makaa ya mawe na gesi

asilia lililobainishwa kwenye Ibara ya 29*(e)* ya Muswada, kama ambavyo Bunge lilishauri.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kupunguza gharama za makaa ya mawe na gesi asilia ili kuendana na azma ya Serikali na Agenda ya Kimataifa kuhusu matumizi ya nishati safi. Serikali sikivu imesikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, hatua hii inalenga kupunguza gharama za uzalishaji kwa viwanda vinavyotumia makaa ya mawe kama chanzo cha nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara za 30 na 31 kama zilivyorekebishwa, zinapendekeza kurekebisha vifungu vya 128 na 129 ili kubadilisha tarehe ya ukomo wa kufanya malipo ya ushuru wa bidhaa na ukomo wa ahirisho la kulipa ushuru kutoka siku ya mwisho wa mwezi hadi tarehe ya 25 ya mwezi unaofuata kwa lengo la kuwianisha na tarehe ya uwasilishaji wa *return* pamoja na kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 132 ili kujumuisha mvinyo unaotambulika kwa *Heading* 22.05 kwenye wigo wa bidhaa za mwisho ambazo hutumia pombe kali yenye kilevi zaidi ya 80% *(ethane),* ambapo wazalishaji wa bidhaa hiyo wataruhusiwa kujirejeshea ushuru wa bidhaa *(duty offset)* uliolipwa wakati wa ununuzi wa malighafi hiyo inayotumika katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuzuia ulipaji wa ushuru wa bidhaa mara mbili kwa bidhaa moja na hivyo, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 33 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 146(A) ili kuweka msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye *Un-denatured Ethyl Alcohol* inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi, mathalani uzalishaji wa ladha za vyakula *(Food Flavours)* kama vile *cocoa*, *vanilla*, na kahawa.

Mheshimiwa Spika, bidhaa hiyo inatambulika kwa *HS Code* 2207.10.00. Msamaha husika utatolewa baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala husika ili kuhakikisha msamaha unatumika kama ilivyokusudiwa na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza ushindani wa viwanda hivyo, pamoja na kuongeza fedha za kigeni kwa kuwa bidhaa husika kwa kiasi kikubwa zinauzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 34 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha jedwali la nne ili: -

(i) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 500.00 kwa kila kilo ya siagi/majarini inayoingizwa nchini inayotambulika kwa *Heading* 15.17. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani wa siagi ya karanga kwa kuwa bidhaa hiyo hutumika kama mbadala wa majarini;

(ii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 5% kwa soseji na bidhaa nyingine zinazofanana na hizo zinazozalishwa nchini, na 10% kwa zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa *HS Code* 1601.00.00. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali, kuvutia uwekezaji nchini na kulinda wazalishaji wa ndani;

(iii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 50.00 kwa kilo ya *crips* zinazozalishwa nchini, na shilingi 100.00 kwa kilo ya *crips* zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa *HS Codes* 1905.90.90, 2005.20.00 na 2008.99.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya ikiwemo ongezeko la uzito *(obesity)* zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(iv) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 5% kwenye *ice cream* zinazotengenezwa nchini kwa kutumia kakao au malighafi nyingine, na 10% kwa zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa *HS Code* 2105.00.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya zinazotokana na matumizi

ya bidhaa hizi, kuongeza mapato ya Serikali, na kulinda wazalishaji wa ndani;

(v) Kuanzisha ushuru wa bidhaa wa shilingi 134.2 kwa kila lita kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu *(energy drinks)* vyenye *caffein* isiyozidi kiwango cha 300 *parts per million* vinavyozalishwa ndani ya nchi. Hivi sasa vinywaji hivi havitozwi ushuru wa bidhaa. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizi, na kuongeza mapato ya Serikali;

(vi) Kuongeza ushuru wa bidhaa kwa shilingi 10.00, shilingi 15.00 na shilingi 25.00 kwenye lita ya bia, mvinyo na vinywaji vikali mtawalia. Lengo la marekebisho haya ni kupata mapato kwa ajili ya kugharamia huduma za afya ikiwemo udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI na kuongeza vyanzo vya kugharamia bima ya afya kwa wote;

(vii) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye *Undenatured Ethyl Alcohol* yenye kilevi cha 80% au zaidi inayotoka nje ya nchi kutoka shilingi 7,000.00 hadi shilingi 5,000.00 kwa kila lita na kutoka shilingi 5,000.00 hadi shilingi 4,000.00 kwa kila lita kwa *Alcohol* yenye kilevi cha 80% au zaidi inayozalishwa ndani ya nchi. Bidhaa hiyo inatambulika kwa *HS Code* 2207.10.00.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuweka unafuu katika ulipaji wa ushuru wa bidhaa wa awali kwa viwanda na kuendelea kulinda viwanda vya ndani;

(viii) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye gesi asilia kutoka shilingi 0.45 kwa kila futi za ujazo *(cubic feet)* hadi shilingi 0.55 kwa kila futi za ujazo. Lengo la hatua hii ni kulinda thamani ya fedha kwa kuwa kiwango cha sasa hakijabadilishwa kwa takribani miaka nane na hakiendani na hali ya uchumi katika kipindi hicho;

(ix) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 10% kwenye sabuni zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika kwa *HS Codes* 3301.11.00; 3401.19.00; 3402.50.00; na 3402.90.00.

Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani na kuongeza ajira;

(x) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 25% kwenye baruti *(fireworks)* zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika kwa *HS Code* 3604.10.00. Lengo la hatua hili ni kupunguza athari za kimazingira ikiwemo uchafuzi wa hali ya hewa zinazotokana na matumizi ya baruti hizo wakati wa sherehe mbalimbali;

(xi) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 400.00 kwa kila kilo ya viberiti vinavyoingizwa nchini vinavyotambuliwa kwenye *HS Code* 3605.00.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

(xii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 10% kwenye vito bandia vinavyotengenezwa au vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi vinavyotambulika kwa *Heading* 71.17. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali;

(xiii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 30% kwenye vifaa vya sigara za kielektroniki *(parts of electronic cigarettes)* vinavyotambulika kwa *HS Code* 8543.90.00 na vimiminika vya sigara za kielektroniki *(Electronic Cigarettes consumable liquids)* vinavyotambulika kwa *HS Code* 2404.12.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo na kuongeza wigo wa kodi; na

(xiv) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye samani *(furniture)* zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa *Heading* 94.01 na 94.03 kutoka 20% hadi 25%. Lengo la hatua hii ni kulinda watengenezaji wa samani nchini na kuvutia uwekezaji nchini ili kuendelea kukuza sekta zinazofungamana na uzalishaji husika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa yenye Ibara ya 35 hadi 37, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika

Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196, kama ifuatavyo:-

a) Ibara ya 36 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha Pili kwenye tafsiri ya neno "kamishna", ili kumtambua Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambaye ni mkusanyaji wa kodi hiyo; na

b) Ibara ya 37, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha jedwali, ili kuweka tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha 30% au shilingi 150 kwa kilo moja kutegemea na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye vinia (mbao laini) inayotambulika kwa *Heading 44.08*. Lengo la marekebisho haya ni kulinda viwanda vya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya ndani vya bidhaa za *plywood* na *marine board* inapatikana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi yenye Ibara ya 38 na 39, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 79 cha Sheria ya Ushindani, Sura ya 285, ili kubainisha kuwa, mapato ya Tume ya Ushindani yanapaswa kujumuisha asilimia 1.5 ya ada zinazotokana na leseni ya biashara badala ya utaratibu wa sasa uliopo ambapo mapato yanapaswa kuwa siyo zaidi ya asilimia 2.5.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu hicho kinarekebishwa kwa kubainisha kuwa, asilimia moja ya mapato ghafi ya Mamlaka za Udhibiti, ikiwemo *EWURA, LATRA, TCRA* na *TCAA* yatawasilishwa kwa Tume ya Ushindani. Lengo la marekebisho haya ni kuweka bayana vyanzo vya mapato na taasisi zinazopaswa kuwasilisha sehemu ya mapato yake Tume ya Ushindani.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 11 yenye Ibara ya 40 na 41, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 34 cha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41, ili kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye zawadi ya ushindi kwenye michezo ya kubashiri matokeo kutoka 10% hadi 12% na michezo ya *Casino* ya ardhini kutoka 12% hadi 13%, ambapo kiwango kilichoongezeka kitaelekezwa kwenye

Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 12 yenye Ibara za 42 na 45, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276, kama ifuatavyo:-

a) Ibara ya 43, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha kifungu cha pili, ili kuweka tafsiri ya maneno "Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania";

b) Ibara ya 44 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 18, ili kwanza; kujumuisha bidhaa zinazotoka kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye wigo wa tozo ya maendeleo ya viwanda, kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani na kuongeza mapato ya Serikali. Pili, kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kusamehe tozo ya maendeleo ya viwanda pale anapoona kuna maslahi ya umma,

c) Ibara ya 45 inapendekeza kurekebisha jedwali, ili kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwenye bidhaa za sabuni, karatasi *starch, liquid glucose, optical fibres*, tambi, misumari, vichwa vya kuvuta matrela, samani, marumaru, nondo, mabati, vyombo vya jikoni na mezani vya plastiki, mahema ya chuma na vioo ambavyo vinaingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwekezaji na uzalishaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa, bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini. Aidha, marekebisho yaliyofanyika yameondoa klinka kwenye wigo wa bidhaa zinazotozwa tozo ya maendeleo ya viwanda. Hatua hii inalenga kupunguza gharama kwa viwanda vya uzalishaji wa saruji nchini. Aidha, tozo hii kwa *optical fibres, spaghetti na starch* itaanza kutozwa kuanzia tarehe 1 Januari, 2026.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 13 yenye Ibara za 46 hadi 56, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kama ifuatavyo:-

a) Ibara ya 47 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha Tatu, ili kuboresha tafsiri ya maneno "*permanent establishment*";

b) Ibara ya 48 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 12, ili kujumuisha faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa kwenye tafsiri ya neno "*equity*", ili kuwezesha ukokotoaji wa riba itakayoruhusiwa kwenye kutoza kodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho haya yatawezesha kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha 10% kwenye faida ambayo haitakuwa imegawanywa katika kipindi cha miezi 12. Lengo la hatua hii ni kuchochea uingizaji wa mitaji katika shughuli za uchumi na kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali;

c) Ibara ya 49 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 44, ili kubainisha mapato na gharama zinazopaswa kujumuishwa wakati wa ukokotoaji wa kodi ya ongezeko la mtaji wakati wa uhamishaji wa umiliki wa mali. Lengo la marekebisho haya ni kutambua gharama zote zilizotumika kwenye umiliki wa mali husika katika ukokotoaji wa ziada au hasara ya mtaji;

d) Aidha, inapendekezwa kuongeza Kifungu Kipya cha 33A, ili kutoza kodi ya zuio kwenye gawio ambalo halijagawanywa kwa wanahisa. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

e) Ibara za 50 hadi 53 zinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 71, 75, 80, na 84 kupunguza kiwango cha hasara mlimbikizo kinachoruhusiwa kupunguza mapato katika sekta za madini, petroli, mafuta na gesi kutoka 70% hadi 60%. Lengo la marekebisho haya ni kulinda wigo wa kodi dhidi ya hasara mlimbikizo na kuongeza mapato ya Serikali;

f) Ibara ya 54 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 105, ili kuwezesha utozaji wa 10% kwenye huduma ya ukodishaji magari;

g) Ibara za 55 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 106, ili kwanza, kutoza kodi ya zuio ya asilimia mbili kwenye malipo yanayotokana na ununuzi wa chumvi ghafi kutoka kwa wamiliki wa leseni ya uchimbaji mdogo wa madini au wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wazalishaji hao, ili kuondoa changamoto zilizopo kwenye ukusanyaji wa kodi kwenye sekta hiyo. Pili, kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha 10% kwenye malipo ya kamisheni yatokanayo na matangazo ya michezo ya kubahatisha. Lengo la hatua hii ni kuwiana na kanuni za usawa wa utozaji kodi pamoja na kupanua wigo wa kodi;

h) Ibara za 56 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 115, ili kuongeza kiwango cha kodi ya ongezeko la mtaji kwa mtu asiye mkazi kutoka 20% hadi 30%. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza misingi ya usawa wa kikodi na kupanua wigo wa kodi;

i) Ibara ya 57 inapendekeza kuongeza Kifungu Kipya cha 116A, ili kuanzisha utaratibu wa kulipa kodi ya mapato kwa mkupuo mmoja *(single instalment tax)* kwa kila thamani ya mzigo kwa kiwango cha asilimia mbili ya mapato yatokanayo na uuzaji wa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa pendekezo hili utaanza Januari 1, 2026 na vilevile katika utekelezaji wa pendekezo husika, Waziri amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni, kwa ajili ya utekelezaji wa pendekezo hili. Lengo la marekebisho haya ni kurasimisha sekta ndogo ya misitu na kupanua wigo wa kodi;

j) Ibara ya 58 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 117, ili kuweka sharti la ritani za watu binafsi wenye mauzo yanayozidi shilingi milioni 500 na kampuni yenye mapato

yanayozidi shilingi milioni 100 kuandaliwa au kuthibitishwa na wahasibu wa umma walioidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara kwa watu binafsi na kampuni zenye mauzo chini ya viwango husika;

k) Ibara ya 59 inapendekeza kurekebisha kedwali la Kwanza kwa kuongeza kiwango cha kodi kwa mapato mbadala *(Alternative Minimum Tax)* inayolipwa na kampuni inayotengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kutoka asilimia 0.5% hadi asilimia moja, kuongeza kiwango cha kodi ya zuio kwenye malipo ya bima na bima mtawanyo yanayofanywa kwa kampuni za nje kutoka asilimia tano hadi 10%, pamoja na kuongeza kodi ya zuio kwenye malipo ya huduma za kitaalamu na kiusimamizi zinazotolewa na walipakodi wa ndani *(resident persons)* kwenye sekta ya uziduaji kutoka asilimia tano hadi 10%. Lengo la marekebisho hayo ni kupanua wigo wa kodi;

l) Ibara ya 60 inapendekeza kurekebisha jedwali la pili kwa kufuta msamaha wa kodi ya mapato uliokuwa unatolewa kwa kipindi cha awali cha miaka 10 kwa wawekezaji waliosajiliwa katika maeneo maalum ya kiuchumi pale bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa ndani ya maeneo hayo zinapouzwa kwenye soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuweka usawa wa kikodi kwa wazalishaji wanaouza bidhaa au huduma katika soko la ndani na wazalishaji wengine walio nje ya *EPZ,* ambapo wanauza bidhaa zao nje ya nchi ambao wanauza kwenye soko moja na wafanyabiashara waliopo kwenye *EPZ*.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 14 yenye Ibara ya 61 na 62, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwa kuongeza Kifungu cha 134A katika Sheria ya Bima, Sura ya 394, ili kuanzisha bima ya usafiri kwa wageni wanaoingia nchini kwa kiwango cha Dola za Marekani 44.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaowezesha kuwalinda wageni wanapokuwa nchini dhidi ya dharura za kiafya, kupotea kwa mizigo yao na kugharamia wageni wanapoondoshwa. Hatua hii haitahusisha wakaazi wanaotoka nchi za Afrika Mashariki na zile za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 15 yenye Ibara za 63 hadi 66, kama ilivyorekebishwa, inaleta mapendekezo ya kufuta pendekezo lililopo katika Ibara za 64 na 66 lililokuwa limekusudia kurekebisha vifungu vya 2 - 21 kuhusu kutambua mwekezaji aliyesaini mkataba wa kimsingi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 65 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19, ili kuweza kubainisha bidhaa ambazo hazipaswi kupata msamaha wa kodi. Ibara za 67 na 68 zinapendekeza kurekebisha Vifungu vya 65 na 67 kwa kufuta orodha ya bidhaa ambazo hazikidhi kupata msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 16 yenye Ibara ya 69 hadi 73, kama ilivyorekebishwa, zinapendekeza marekebisho katika vifungu vya sita, saba na nane pamoja na jedwali katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, ili kupunguza kiwango cha ada ya ushuru wa hoteli *(Hotel Levy)* kutoka 10% hadi asilimia mbili na kuweka kiwango mfuto cha ushuru wa huduma cha asilimia 0.25. Aidha, jedwali linapendekezwa kurekebishwa pia kwa kuweka zuio la kutoza ada za upakiaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 17 yenye Ibara ya 74 hadi 76, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85, kama ambavyo nimebainisha katika kipengele A kuongeza Kifungu cha 11A kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu. Ibara ya 76 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 25, ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri kutengeneza Kanuni zitakazobainisha utaratibu wa utunzaji kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 18 yenye Ibara ya 77 hadi 79, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123, kama ifuatavyo:-

a) Ibara ya 78 inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 69 ya kuweka masharti ya lazima kwa kampuni za madini zenye mikataba ya Serikali kutenga dhahabu kwa kiwango kisichopungua asilimia 20 ya uzalishaji, kwa ajili ya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na kuuzwa ndani ya nchi;

b) Ibara ya 79 inapendekeza kuongeza Kifungu Kipya cha 113A, ili kuanzisha tozo ya kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI kwa kiwango cha asilimia 0.1.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 19 yenye Ibara ya 80 hadi 83, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124, kama ambavyo nimebainisha:-

a) Ibara za 81 na 83 zinapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 5A na jedwali la tatu, ili kuanzisha tozo ya kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI. Ibara ya 83 inapendekeza kurekebisha jedwali la kwanza kuainisha madaraja mbalimbali ya magari ya umeme yanayotozwa ada ya usajili.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 20 yenye Ibara ya 84 na 85, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha Tisa cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, kwa kuweka mgawanyo wa 91% ya mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na *TANAPA*, ambapo 51% itawekwa katika akaunti ya taasisi husika zilizopo Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 21 yenye Ibara ya 86 na 87, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 22 cha Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127, ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri kutengeneza kanuni zitakazobainisha vigezo vya kuzingatiwa wakati wa kufanya tathmini ya miradi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 22 yenye Ibara ya 88 na 89, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kuweka mgawanyo wa 91% ya mapato

yatokanayo na huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, ambapo 51% itawekwa katika akaunti ya Mamlaka hiyo iliyopo Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 23 yenye Ibara ya 90 na 91, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha Saba cha Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari, Sura ya 264, ili kuwianisha tarehe ya kulipa ada ya huduma za bandari na tarehe ya kuwasilisha *return* kuwa siku ya 20 ya mwezi baada ya kukusanywa kwa ada hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 24 yenye Ibara za 92 hadi 96 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348. Kama ambavyo nimebainisha, Ibara ya 93 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha Tano, ili kuweka sharti la kwa Wizara na Taasisi za Serikali kupata ridhaa ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kabla ya kuanzisha tozo, ada, ushuru na tozo mbalimbali, kama nilivyoelezea awali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 94 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 13, ili kuweka masharti yatakayowezesha kuweka viwango tofauti kwa Wakala wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma vya kuchangia kati ya 15% hadi 60% ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 95 inapendekeza kurekebisha Jina la Sehemu ya Nne ya Sheria lililokuwa linasomeka "*Preparation and Examination of Accounts*", ili lisomeke "*Preparation of Financial Reports*". Ibara ya 96 inapendekeza kufuta na kuandika upya Kifungu cha 31, ili kuweka sharti la maandalizi ya hesabu za majumuisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 25 yenye Ibara ya 97 na 97, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 80 cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuongeza masharti yanayotambua wastaafu wanaolipwa mafao ya pensheni kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 26 yenye Ibara ya 99 hadi 100, marekebisho katika Kifungu cha 18 cha Sheria ya Tume ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 27 nimeweka marekebisho A na B. Naomba yasomeke, yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi, kama ambavyo nimeyaandika kwenye wasilisho hili.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 29 ina A, B na C, kama ambavyo inaenda mpaka Ukurasa wa 33. Ukurasa wa 34 mpaka wa 39 nimebainisha maeneo mengine ambayo tumeleta mapendekezo. Ukurasa wa 39 mpaka wa 40 tumeelezea maeneo mengine na utumiaji wa sheria mpya ambayo tunaipendekeza.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, kama nilivyoeleza hapo awali, sheria tunazopendekeza ni utekelezaji wa Sheria ya Mapendekezo ya Serikali kuhusu Bajeti ya Mwaka 2025/2026. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha ili kuiwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, miradi yote ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeiombea itaendelea kutekelezwa hata baada ya ninyi kuwa kwenye mchakato wa kuwaomba Watanzania wawarejeshe upya hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2025 (THE FINANCE BILL, 2025) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 **(The Finance Act, 2025)** pamoja na marekebisho yake sasa **usomwe kwa mara ya pili.**

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya

Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini** kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri kwa ajili ya kuuboresha.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni jana tarehe 24 Juni, 2025. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waandishi wa Sheria na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Aidha, nawashukuru wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao kuhusu Muswada huu.

4. **Mheshimiwa Spika**, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 12 Juni, 2025 na kupitishwa Bungeni jana tarehe 24 Juni, 2025.

5. **Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho** unakusudia kufanyia marekebisho **Sheria Thelathini na Tatu** ili kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Muswada huu umelenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, hususan katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi, uchukuzi na usafirishaji pamoja na sekta za elimu na afya ili kuboresha uzalishaji na kukuza uchumi wa jumla, kukuza ajira na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi. Hatua hizi zinalenga pia kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuboresha mazingira ya biashara.

6. **Mheshimiwa Spika,** zifuatazo ni Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho: -

(i) Sheria ya Tozo za Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365;
(ii) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342;
(iii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;
(iv) Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 101;
(v) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439;
(vi) Sheria ya Korosho, Sura ya 203;
(vii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
(viii) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;
(ix) Sheria ya Ushindani, Sura ya 285;
(x) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
(xi) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
(xii) Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276;
(xiii) Sheria ya Bima, Sura ya 394;
(xiv) Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025;
(xv) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
(xvi) Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85;
(xvii) Sheria ya Madini, Sura ya 123;
(xviii) Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124;
(xix) Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282;
(xx) Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127;
(xxi) Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284;
(xxii) Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari, Sura ya 264;
(xxiii) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348;
(xxiv) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371;
(xxv) Sheria ya Tume ya UKIMWI, Sura ya 379;
(xxvi) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
(xxvii) Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161;
(xxviii) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;

(xxix) Sheria ya Mamlaka na Majukumu na Msajili wa Hazina, Sura ya 370;
(xxx) Sheria ya Reli, Sura ya 170;
(xxxi) Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
(xxxii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na
(xxxiii) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

**MAUDHUI YA MUSWADA:**

7. **Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika sehemu **Thelathini na Nne** kama ifuatavyo: -

8. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza,** yenye Ibara ya 1 na 2 inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo Sheria itaanza kutumika tarehe 1, Julai 2025 isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo.

9. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili** yenye Ibara za 3 hadi 5, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365** kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 4 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 3 ili kuongeza Shilingi za Kitanzania 1000 katika tozo inayotozwa kwa kila abiria anayesafiri kwa ndege; na

(b) Ibara ya 5 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 7 ili kuwianisha tarehe ya kulipa ada ya huduma za bandari na tarehe ya kuwasilisha ritani kuwa siku ya 20 ya mwezi baada ya kukusanywa kwa ada hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha ulipaji na kuboresha usimamizi wa kodi.

10. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu** yenye Ibara ya 6 na 7 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwa kuongeza Kifungu kipya cha 39A katika **Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342** ili kuiongezea majukumu Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board - DIB) ya kuweza kuongeza

ukwasi kwa njia ya mkopo kwa benki au taasisi ya fedha yenye changamoto ya ukwasi. Aidha, kupitia utaratibu huo, benki au taasisi ya fedha iliyoongezewa ukwasi itakuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuipa DIB nguvu na uhalali wa kisheria wa kushiriki kikamilifu, kwa kushirikiana na Benki Kuu, katika kutathmini na kuamua hatua muafaka ambayo inapaswa kuchukuliwa pindi benki au taasisi ya fedha inapokuwa katika hatari ya kufilisika.

11. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne** yenye Ibara za 8 hadi 18, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197** kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 9 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 ili kuipa Benki Kuu jukumu la kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha na kuongeza masharti ya kuiwezesha Benki Kuu kutekeleza majukumu yake kwa uhuru;

(b) Ibara ya 10 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 9 ili kubainisha majukumu ya Bodi ya Benki katika usimamizi wa Benki Kuu, kuongeza idadi ya wakurugenzi wasio watendaji katika Bodi ya Benki, kuongeza muda wa kuhudumu wa wajumbe wa Bodi ya Benki na kuweka utaratibu wa kufanya uteuzi wa wajumbe wa Bodi kwa vipindi tofauti. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika utendaji wa Bodi ya Benki Kuu;

(c) Ibara ya 11 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 12 kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kubainisha muundo, ukomo wa muda na majukumu ya Kamati ya Sera ya Fedha na Kamati ya Ukaguzi. Lengo la marekebisho haya ni kubainisha masharti kuhusu Kamati ya Sera ya Fedha na Kamati ya Ukaguzi ili kuchochea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati husika;

(d) Ibara ya 12 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 12A ili kuipa Bodi ya Benki Kuu mamlaka ya kuanzisha kamati nyingine kwa ajili ya kuiwezesha kutekeleza majukumu yake;

(e) Ibara ya 13 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19 ili kubainisha muda ambao Waziri wa Fedha anaweza kutoa dhamana ili kurejesha mtaji wa Benki. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ulinzi wa kisheria wa uhuru wa kifedha wa Benki kwa kuweka muda ambao Waziri anaweza kutoa dhamana za Benki ili kuongeza mtaji wa Benki pale inapobidi;

(f) Ibara ya 14 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 20 ili kubainisha sifa za maafisa walio katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, uteuzi na muda wa utumishi wa mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.;

(g) Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 38 ili kuwezesha shughuli za uondoaji na uhamishaji wa fedha (clearing and inter-Financial Institutions transfers) kati ya Taasisi za Kifedha, wakiwemo watoa huduma za fedha kwa njia ya kielektroniki (EMIs), waunganishaji wa malipo (payment aggregators), pamoja na kampuni za teknolojia ya kifedha (FinTechs). Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha kusomana kwa mifumo ya malipo katika mfumo mzima wa kifedha;

(h) Ibara ya 16 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 40 ili kuongeza wigo wa mikopo ya dharura inayotolewa na Benki kwa taasisi za fedha au mabenki kama mkopeshaji wa mwisho; na

(i) Ibara ya 17 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 60 ili kuainisha wajibu wa Benki Kuu katika uandaaji wa bajeti ya serikali, sheria ya fedha na mambo mengine yanayoathiri kazi, mamlaka na wajibu wa Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ushiriki wa

Benki Kuu katika nyanja zote zinazohusiana na majukumu ya Benki Kuu.

12. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano** yenye Ibara ya 19 na 20 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwenye Kifungu cha 60 cha **Sheria ya Bajeti, Sura ya 439** ili kuweka sharti la mashauriano baina ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha na Wizara, Taasisi za Serikali, Wakala au Mamlaka za Serikali kabla ya Wizara au Taasisi hizo kuanzisha tozo, ada mpya au wakati wa kufanya mabadiliko yoyote ya viwango vya ada na tozo. Lengo la marekebisho haya ni kuipa Wizara ya Fedha nguvu za kisheria ili kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa mapato ya Serikali ikiwemo kufanya tathmini ya athari au faida ya viwango vya ada na tozo vinavyopendekezwa. Hatua hii haitahusisha utaratibu wa uanzishaji au marekebisho ya tozo na ada kwa Halmashauri.

13. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita** yenye Ibara za 21 hadi 23, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 101** kama ifuatavyo:

(a) Kubainisha kwenye Kifungu cha 3 tafsiri ya maneno "noncitizen" ndani ya Sheria hiyo;

(b) Ibara ya 22 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 4 ili kuziondolea mamlaka za utoaji leseni uwezo wa kufunga biashara pale ambapo mfanyabiashara amekiuka masharti ya leseni. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mazingira bora ya kibiashara; na

(c) Ibara ya 23 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 14 ili Kwanza, kuweka sharti kwa mamlaka za utoaji leseni kutoa leseni za biashara kwa rai a wa kigeni kwa biashara zinazoruhusiwa kufanywa na raia hao; Pili,kumpa Waziri mwenye dhamana na biashara mamlaka ya kuainisha biashara ambazo hazipaswi kufanywa na raia wa kigeni. Lengo la marekebisho haya ni kulinda ajira za watanzania na kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara baina ya

watanzania na raia wa kigeni. Aidha, utaratibu wa utekelezaji wa mapendekezo haya utafanywa kupitia Amri itakayotolewa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya biashara ili kubainisha orodha ya shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni.

14. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba** yenye Ibara ya 24 na 25 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 18 cha **Sheria ya Korosho, Sura ya 203** ili kumwezesha Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuweka mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi kwenye Akaunti ya Bodi ya Korosho kwa kipindi cha miaka minne. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Bodi ya Korosho kupata mapato haya kwa wakati ili kuchochea maendeleo ya sekta ya korosho nchini.

15. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane** yenye Ibara za 26 hadi 34 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 27 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 2 ili kubainisha ndani ya Sheria tafsiri ya maneno "financial institution";

(b) Ibara ya 28 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 10 ili ukomo wa leseni kwa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kuwa miezi kumi na mbili tangu tarehe ya kutolewa badala ya leseni kufika ukomo kila mwisho wa mwaka. Hatua hii inatoa nafuu kwa Wazalishaji na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini;

(c) Ibara ya 29 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 126 ili; **Kwanza**, kufuta pendekezo la kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka asilimia 17 hadi asilimia 17.5; **Pili**, kuboresha tafsiri ya maneno "dutiable value" kwa ajili ya ushuru wa bidhaa katika mawasiliano ya kielektroniki; **Tatu,** kuongeza katika

wigo wa kodi watoa huduma za fedha na malipo kwa kutumia mifumo binafsi, **Nne**, kuongeza ushuru wa bidhaa katika malipo ya kutazama vipindi vya televisheni vinavyolipiwa kutoka asilimia 5 hadi asilimia 7; **Tano**, kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 20 kwenye vyombo vya nyumbani vilivyotumika na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza utumiaji wa bidhaa hizi ambao una madhara kiafya, kulinda viwanda vya ndani na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, napendekeza kufuta pendekezo la kutoza ushuru kwa kiwango cha shilingi 22,000 kwa kila tani ya hewa ukaa inayozalishwa kwenye makaa ya mawe na gesi asilia lililobainishwa kwenye Ibara ya 29(e) ya Muswada. Lengo ni kupunguza gharama za makaa ya mawe na gesi asilia ili kuendana na azma ya Serikali na Agenda ya Kimataifa kuhusu matumizi ya nishati safi. Vilevile, hatua hii inalenga kupunguza gharama za uzalishaji kwa viwanda vinavyotumia makaa ya mawe kama chanzo cha nishati;

(d) Ibara za 30 na 31 kama zilivyorekebishwa, zinapendekeza kurekebisha vifungu vya 128 na 129 ili kubadilisha tarehe ya ukomo wa kufanya malipo ya ushuru wa bidhaa na ukomo wa ahirisho la kulipa ushuru kutoka siku ya mwisho wa mwezi hadi tarehe ya 25 ya mwezi unaofuata kwa lengo la kuwianisha na tarehe ya uwasilishaji wa ritani pamoja na kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa wakati;

(e) Ibara ya 32 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 132 ili kujumuisha mvinyo unaotambulika kwa Heading 22.05 kwenye wigo wa bidhaa za mwisho ambazo hutumia pombe kali yenye kilevi zaidi ya asilimia 80 (yaani ethane); ambapo wazalishaji wa bidhaa hiyo wataruhusiwa kujirejeshea ushuru wa bidhaa (duty offset) uliolipwa wakati wa ununuzi wa malighafi hiyo inayotumika katika uzalishaji. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia ulipaji wa ushuru

wa bidhaa mara mbili kwa bidhaa moja na hivyo, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini;

(f) Ibara ya 33 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 146A ili kuweka msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye Un-denatured Ethyl Alcohol inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi mathalani uzalishaji wa ladha za vyakula (Food Flavors) kama vile cocoa, vanila, na kahawa. Bidhaa hiyo inatambulika kwa HS Code 2207.10.00. Msamaha husika utatolewa baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala husika ili kuhakikisha msamaha unatumika kama ilivyokusudiwa na si vinginevyo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza ushindani wa viwanda hivyo, pamoja na kuongeza fedha za kigeni kwa kuwa bidhaa husika kwa kiasi kikubwa zinauzwa nje ya nchi;

(g) Ibara ya 34 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Jedwali la Nne ili:

(i) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 500 kwa kila kilo ya siagi/majarini (margarine) inayoingizwa nchini inayotambulika kwa Heading 15.17. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani wa siagi ya karanga (peanut butter) kwa kuwa bidhaa hiyo hutumika kama mbadala wa majarini;

(ii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwa soseji na bidhaa zingine zinazofanana na hizo zinazozalishwa nchini, na asilimia 10 kwa zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa HS Code 1601.00.00. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali, kuvutia uwekezaji nchini na kulinda wazalishaji wa ndani;

(iii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha Shilingi 50 kwa kilo ya crips zinazozalishwa nchini, na shilingi 100 kwa kilo ya crips zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa HS Codes 1905.90.90, 2005.20.00 na 2008.99.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya ikiwemo ongezeko la uzito (obesity) zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(iv) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye aisikrimu (ice cream) zinazotengezwa nchini kwa kutumia kakao au malighafi nyingine, na asilimia 10 kwa zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Bidhaa hizo zinatambulika kwa HS Code 2105.00.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizi, kuongeza mapato ya Serikali, na kulinda wazalishaji wa ndani;

(v) Kuanzisha ushuru wa bidhaa wa shilingi 134.2 kwa kila lita kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu (energy drinks) vyenye caffein isiyozidi kiwango cha 300 parts
per million vinavyozalishwa ndani ya nchi. Hivi sasa vinywaji hivi havitozwi ushuru wa bidhaa. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizi, na kuongeza mapato ya
Serikali;

(vi) kuongeza ushuru wa bidhaa kwa shilingi 10, 15 na 25 kwenye lita ya bia, mvinyo na vinywaji vikali mtawalia. Lengo la marekebisho haya ni kupata mapato kwa ajili ya kugharamia huduma za afya ikiwemo udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI na kuongeza vyanzo vya kugharamia bima ya afya kwa wote;

(vii) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye Undenatured Ethyl Alcohol yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayotoka nje ya nchi kutoka shilingi 7,000 hadi shilingi 5,000 kwa kila lita na kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 4,000 kwa kila lita ya Un-denatured Ethyl Alcohol yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayozalishwa ndani ya nchi. Bidhaa hiyo inatambulika kwa HS Code 2207.10.00. Lengo la hatua hii ni kuweka unafuu katika ulipaji wa ushuru wa bidhaa wa awali kwa viwanda na kuendelea kulinda viwanda vya ndani;

(viii) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye gesi asilia kutoka shilingi 0.45 kwa kila futi za ujazo (cubic feet) hadi shilingi 0.55 kwa kila futi za ujazo. Lengo la hatua hii ni kulinda thamani ya fedha kwa kuwa kiwango cha sasa hakijabadilishwa kwa takriban miaka 8 na hakiendani na hali ya uchumi katika kipindi hicho;

(ix) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye sabuni zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika kwa HS Codes 3401.11.00, 3401.19.00, 3402.50.00 na 3402.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa ndani na kuongeza ajira;

(x) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 25 kwenye baruti (fireworks) zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika kwa HS Code 3604.10.00. Lengo la hatua hili ni kupunguza athari za kimazingira ikiwemo uchafuzi wa hali ya hewa zinazotokana na matumizi ya baruti hizo wakati wa sherehe mbalimbali;

(xi) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 400 kwa kila kilo ya viberiti (safety match) vinavyoingizwa nchini vinavyotambuliwa kwenye HS Code 3605.00.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

(xii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye vito bandia (imitation jewellery) vinavyotengenezwa au vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi vinavyotambulika kwa Heading 71.17. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali;

(xiii) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 30 kwenye vifaa vya sigara za kielektroniki (parts of electronic cigarettes) vinavyotambulika kwa HS Code 8543.90.00 na vimiminika vya sigara za kielektroniki (Electronic Cigarettes consumable liquids) vinavyotambulika kwa HS Code 2404.12.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza athari zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo na kuongeza wigo wa kodi; na

(xiv) Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye samani (furniture) zinazoingizwa nchini zinazotambulika kwa Heading 94.01 na 94.03 kutoka asilimia 20 kwenda asilimia 25. Lengo la hatua hii ni kulinda watengenezaji wa samani nchini na kuvutia uwekezaji nchini ili kuendelea kukuza sekta zinazofungamana na uzalishaji husika.

16. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa** yenye Ibara ya 35 hadi 37 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika

**Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 36 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 2 kwenye tafsiri ya neno "kamishna" ili kumtambua Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ambaye ni mkusanyaji wa kodi hiyo; na

(b) Ibara ya 37 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Jedwali ili kuweka tozo ya usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya Nchi kwa kiwango cha asilimia 30 au shilingi 150 kwa kilo moja kutegemea na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye vinia (Mbao laini) inayotambulika kwa Heading 44.08. Lengo la marekebisho haya ni kulinda viwanda vya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya ndani vya bidhaa za plywood na marine board.

17. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi** yenye Ibara ya 38 na 39 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 79 cha **Sheria ya Ushindani, Sura ya 285** ili kubainisha kuwa, mapato ya Tume ya Ushindani yanapaswa kujumuisha asilimia 1.5 ya ada zinazotokana na leseni ya biashara badala ya utaratibu wa sasa uliopo ambapo mapato yanapaswa kuwa si zaidi ya asilimia 2.5. Aidha Kifungu hicho kinarekebishwa kwa kubainisha kuwa asilimia moja ya mapato ghafi ya Mamlaka za Udhibiti ikiwemo EWURA, LATRA, TCRA na TCAA yatawasilishwa kwa Tume ya Ushindani. Lengo la marekebisho haya ni kuweka bayana vyanzo vya mapato na taasisi zinazopaswa kuwasilisha sehemu ya mapato yake Tume ya Ushindani.

18. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja** yenye Ibara ya 40 na 41 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 34 cha **Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41** ili kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye zawadi ya ushindi kwenye michezo ya kubashiri matokeo kutoka asilimia 10 hadi 12, na michezo ya kasino ya ardhini kutoka asilimia 12 hadi 13, ambapo kiwango

kilichoongezeka kitaelekezwa kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

19. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili** yenye Ibara za 42 hadi 45 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 43 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 2 ili kuweka tafsiri ya maneno "Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania";

(b) Ibara ya 44 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 18A ili **Kwanza**; kujumuisha bidhaa zinazotoka kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye wigo wa tozo ya maendeleo ya viwanda kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani na kuongeza mapato ya Serikali. **Pili**, kumpa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kusamehe tozo ya maendeleo ya viwanda pale anapoona kuna maslahi ya umma; na

(c) Ibara ya 45 inapendekeza kurekebisha Jedwali ili kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwenye bidhaa za sabuni, karatasi (unbleached papers), starch, liquid glucose, optical fibres, tambi (spaghetti), misumari, vichwa vya kuvuta matrela, samani, marumaru, nondo, mabati, vyombo vya jikoni na mezani vya plastiki, hema za chuma na vioo ambavyo vinaingizwa nchini. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwekezaji na uzalishaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini. Aidha, marekebisho yaliyofanyika yameondoa klinka kwenye wigo wa bidhaa zinazotozwa tozo ya maendeleo ya viwanda. Hatua hii inalenga kupunguza gharama kwa viwanda vya uzalishaji wa saruji nchini. Aidha, tozo hii kwa optical fibres, spaghetti na starch itaanza kutozwa kuanzia tarehe 1 Januari, 2026.

20. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu** yenye Ibara za 46 hadi 56 kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 47 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 3 ili kuboresha tafsiri ya maneno "permanent establishment";

(b) Ibara ya 48 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 12 ili kujumuisha faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa kwenye tafsiri ya neno "equity" ili kuwezesha ukokotoaji wa riba itakayoruhusiwa kwenye kutoza kodi. Aidha, marekebisho haya yatawezesha kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye faida ambayo haitakuwa imegawanywa katika kipindi cha miezi 12. Lengo la hatua hii ni kuchochea uingizaji wa mitaji katika shughuli za Uchumi na kuongeza wigo wa kodi na mapato ya Serikali;

(c) Ibara ya 49 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 44 ili kubainisha mapato na gharama zinazopaswa kujumuishwa wakati wa ukokotoaji wa kodi ya ongezeko la mtaji wakati wa uhamishaji wa umiliki wa mali. Lengo la marekebisho haya ni kutambua gharama zote zilizotumika kwenye umiliki wa mali husika katika ukokotoaji wa ziada au hasara ya mtaji;

(d) Aidha, inapendekezwa kuongeza Kifungu kipya cha 33A ili kutoza kodi ya zuio kwenye gawio ambalo halijagawanywa kwa wanahisa. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

(e) Ibara za 50 hadi 53 zinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 71, 75, 80, na 84 ili kupunguza kiwango cha hasara mlimbikizo kinachoruhusiwa kupunguza mapato katika sekta za madini, petroli, mafuta na gesi kutoka asilimia 70 hadi asilimia 60. Lengo la marekebisho haya ni

kulinda wigo wa kodi dhidi ya hasara mlimbikizo na kuongeza mapato ya Serikali;

(f) Ibara ya 54 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 105 ili kuwezesha utozaji wa asilimia 10 kwenye huduma ya ukodishaji magari;

(g) Ibara za 55 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 106 ili: **Kwanza**, kutoza kodi ya zuio ya asilimia 2 kwenye malipo yanayotokana na ununuzi wa chumvi ghafi kutoka kwa wamiliki wa leseni ya uchimbaji mdogo wa madini au wachimbaji wadogo wa madini. Lengo la hatua hii ni kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wazalishaji hao ili kuondoa changamoto zilizopo kwenye ukusanyaji wa kodi kwenye sekta hiyo. **Pili**, kutoza kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye malipo ya kamisheni yatokanayo na matangazo ya michezo ya kubahatisha. Lengo la hatua hii ni kuwiana na kanuni za usawa wa utozaji kodi pamoja na kupanua wigo wa kodi;

(h) Ibara za 56 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 115 ili kuongeza kiwango cha kodi ya ongezeko la mtaji kwa mtu asiye mkazi kutoka asilimia ishirini hadi asilimia thelathini.
Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza misingi ya usawa wa kikodi na kupanua wigo wa kodi;

(i) Ibara ya 57 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 116A ili kuanzisha utaratibu wa kulipa kodi ya mapato kwa mkupuo mmoja (single instalment tax) kwa kila thamani ya mzigo kwa kiwango cha asilimia 2 ya mapato yatokanayo na uuzaji wa mazao ya misitu. Aidha, utekelezaji wa pendekezo hili utaanza Januari 1, 2026 na vilevile katika utekelezaji wa pendekezo husika, Waziri amepewa mamlaka ya kutengeneza Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa pendekezo hili. Lengo la marekebisho haya ni kurasimisha sekta ndogo ya misitu na kupanua wigo wa kodi;

(j) Ibara ya 58 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 117 ili kuweka sharti la ritani za watu binafsi wenye mauzo yanayozidi shilingi milioni mia tano na kampuni yenye mapato yanayozidi milioni mia moja kuandaliwa au kuthibitishwa na wahasibu wa umma walioidhinishwa. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara kwa watu binafsi na kampuni zenye mauzo chini ya viwango husika;

(k) Ibara ya 59 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Kwanza kwa kuongeza kiwango cha kodi kwa mapato mbadala (Alternative Minimum Tax) inayolipwa na kampuni inayotengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kutoka asilimia 0.5 hadi asilimia 1, kuongeza kiwango cha kodi ya zuio kwenye malipo ya bima na bima mtawanyo yanayofanywa kwa kampuni za nje kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10, pamoja na kuongeza kodi ya zuio kwenye malipo ya huduma za kitaalamu na kiusimamizi zinazotolewa na walipakodi wa ndani "resident persons" kwenye sekta ya uziduaji (extractive sector) kutoka asilimia 5 hadi asilimia 10. Lengo la marekebisho hayo ni kupanua wigo wa kodi; na

(l) Ibara ya 60 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Pili kwa kufuta msamaha wa kodi ya mapato uliokuwa unatolewa kwa kipindi cha awali cha miaka 10 kwa wawekezaji waliosajiliwa katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi pale bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa ndani ya maeneo hayo zinapouzwa kwenye soko la ndani. Lengo la hatua hii ni kuweka usawa wa kikodi kwa wazalishaji wanaouza bidhaa au huduma katika soko la ndani, na wazalishaji wengine walio nje ya EPZ ambao wanauza bidhaa zao nje ya nchi ambao wanauza kwenye soko moja na wafanyabiashara waliosajiliwa EPZ.

21. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne** yenye Ibara ya 61 na 62 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwa

kuongeza Kifungu kipya cha 134A katika **Sheria ya Bima, Sura ya 394** ili kuanzisha bima ya usafiri kwa wageni wanaoingia nchini kwa kiwango cha dola za Marekani 44. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaowezesha kuwalinda wageni wanapokuwa nchini dhidi ya dharura za kiafya, kupotea kwa mizigo yao, na kugharamia wageni wanapoondoshwa kwa lazima au panapokuwepo na hatari yenye kulazimu uondoshwaji. Hatua hii haitahusisha wakaazi wanaotoka nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

22. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano** yenye Ibara za 63 hadi 66 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025** kama ifuatavyo;

(a) Kufuta pendekezo lililopo katika Ibara za 64 na 66 lililokuwa limekusudia kurekebisha vifungu vya 2 na 21 kuhusu kumtambua mwekezaji aliyesaini mkataba wa msingi na Serikali kama mwekezaji wa kimkakati;

(b) Ibara ya 65 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 19 ili kuweka kubainisha bidhaa ambazo hazipaswi kupata msamaha wa kodi. Lengo la marekebisho haya ni kulinda viwanda vya ndani, ajira na mapato ya Serikali. Kifungu hicho kinarekebishwa pia kwa kujumuisha masharti kuhusu msamaha wa ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 75 kwenye bidhaa za mtaji zisizo za asili zinazoingizwa na wawekezaji waliosajiliwa chini ya Sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kuendelea kuweka unafuu kwa wawekezaji nchini na kuhakikisha bidhaa mtaji zisizo za asili zinapatikana kwa bei nafuu; na

(c) Ibara za 67 na 68 zinapendekeza kurekebisha vifungu vya 65 na 67 kwa kufuta orodha ya bidhaa ambazo hazikidhi kupata msamaha wa kodi kwa kuwa orodha hiyo imebainishwa katika Kifungu cha 19 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho.

23. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita** yenye Ibara ya 69 hadi 73 kama ilivyorekebishwa, zinapendekeza marekebisho katika vifungu vya 6, 7, 8 na Jedwali katika **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290** ili kupunguza kiwango cha ada ya ushuru wa hoteli (hotel levy) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 2 na kuweka kiwango mfuto cha ushuru wa huduma cha asilimia 0.25. Aidha, Jedwali linapendekezwa kurekebishwa pia kwa kuweka zuio la kutoza ada za upakiaji (loading) na upakuaji (offloading) wa mizigo zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini pamoja na kuendana na masharti ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI).

24. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba** yenye Ibara ya 74 hadi 76 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 75 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 11A ili kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za alama za biashara kwa bidhaa zinazoingizwa nchini. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti bidhaa bandia zinazozalishwa na kuingizwa nchini kutoka nje ya nchi; na

(b) Ibara ya 76 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 25 ili kumwezesha Waziri kutengeneza Kanuni zitakazobainisha utaratibu wa utunzaji kumbukumbu za alama za biashara kwa bidhaa.

25. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane** yenye Ibara ya 77 hadi 79 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Madini, Sura ya 123** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 78 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 69 ili kuweka masharti ya lazima kwa kampuni za madini zenye mikataba na Serikali kutenga dhahabu kwa kiwango kisichopungua asilimia 20 ya uzalishaji kwa ajili

ya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na kuuzwa ndani ya nchi; na

(b) Ibara ya 79 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 113A ili kuanzisha tozo ya kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI kwa kiwango cha asilimia 0.1 ya thamani ya madini. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza juhudi za kuimarisha huduma za afya ikiwemo kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI na kuongeza vyanzo vya kugharimia bima ya afya kwa wote.

26. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tisa** yenye Ibara ya 80 hadi 83 kama ilivyorekebishwa, zinapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124** kama ifuatavyo;

(a) Ibara za 81 na 83 zinapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 5A na Jedwali la Tatu ili kuanzisha tozo ya kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI kwenye usajili wa kwanza wa vyombo vya moto. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza juhudi za kuimarisha huduma za afya ikiwemo kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI na kuongeza vyanzo vya mapato ya kugharamia bima ya afya kwa wote. Aidha, inapendekezwa kuwa asilimia 70 ipelekewe katika Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI na asilimia 30 kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote; na

(b) Ibara ya 82 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Kwanza ili kuainisha madaraja mbalimbali ya magari ya umeme yanayotozwa ada ya usajili wa magari ili kuwezesha utozaji wenye ufanisi wa chanzo hicho cha mapato.

27. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini** yenye Ibara ya 84 na 85 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 9 cha **Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282** kwa kuweka mgawanyo wa asilimia 91 ya mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na TANAPA, ambapo asilimia 51

itawekwa katika akaunti ya taasisi hiyo iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na asilimia 40 itawekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, inapendekezwa kuongeza sharti la kuomba kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kabla ya matumizi ya fedha zinazowekwa katika akaunti ya TANAPA.

28. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Moja** yenye Ibara ya 86 na 87 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 22 cha **Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127** ili kumwezesha Waziri kutengeneza kanuni zitakazobainisha vigezo vya kuzingatiwa wakati wa kufanya tathmini ya miradi ya uwekezaji wa umma. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Tume kuzingatia vigezo mtambuka vinavyotambuliwa ndani ya nchi, kikanda na kimataifa wakati wa ufanyaji wa tathmini na kuwezesha kuweka mikakati itakayosaidia katika kuhimili athari za miradi husika.

29. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili** yenye Ibara ya 88 na 89 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 12 cha **Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284** kwa kuweka mgawanyo wa asilimia 91 ya mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, ambapo asilimia 51 itawekwa katika akaunti ya Mamlaka hiyo iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na asilimia 40 itawekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, inapendekezwa kuongeza sharti la kuomba kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kabla ya matumizi ya fedha zinazowekwa katika akaunti za Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

30. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tatu** yenye Ibara ya 90 na 91 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 7 cha **Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari, Sura ya 264** ili kuwianisha tarehe ya kulipa ada ya huduma za bandari na tarehe ya kuwasilisha ritani kuwa siku ya 20 ya mwezi baada ya kukusanywa kwa ada hiyo. Lengo la marekebisho ni kurahisisha ulipaji wa kodi.

31. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Nne** yenye Ibara za 92 hadi 96 inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348** kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 93 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 ili kuweka sharti la kwa Wizara na Taasisi za Serikali kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kabla ya kutoza au kubadili ada, ushuru na tozo mbalimbali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ada, tozo na ushuru zina ufanisi, tija na zinaendana na malengo ya sera za fedha, kuzuia utozaji usiozingatia utaratibu na kuhamasisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa mapato. Hatua hii haitahusisha tozo na ada zinazosimamiwa na Halmashauri;

(b) Ibara ya 94 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 13 ili kuweka masharti yatakayowezesha kuweka viwango tofauti kwa Wakala wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma vya kuchangia kati ya asilimia 15 hadi 60 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi;

(c) Ibara ya 95 inapendekeza kurekebisha Jina la Sehemu ya Nne ya Sheria lililokuwa linasomeka “PREPARATION AND EXAMINATION OF ACCOUNTS” ili lisomeke “PREPARATION OF FINANCIAL REPORTS”; na

(d) Ibara ya 96 inapendekeza kufuta na kukiandika upya Kifungu cha 31 ili kuweka sharti la maandalizi ya hesabu za majumuisho kwa kutumia hesabu za taasisi za umma zilizokaguliwa, kupunguza muda unaotumiwa na maafisa masuuli kuandaa hesabu kutoka miezi mitatu hadi miwili baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha na kuweka bayana sharti kwa maafisa masuuli kuandaa hesabu kwa kutumia Viwango vya kimataifa vya Uhasibu (International Public Sector Accounting Standards- IPSAS) katika sekta ya umma na ridhaa ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kutumia Viwango vya

Kimataifa vya Kihasibu (International Financial Reporting Standards – IFRS) iwapo kuna ulazima wa kutumia viwango hivyo.

32. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tano** yenye Ibara ya 97 na 97 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 80 cha **Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371** ili kuongeza masharti yanayotambua wastaafu wanaolipwa mafao na pensheni kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na kuweka utaratibu wa kubadili kima cha chini cha mafao na pensheni kwa wastaafu hao.

33. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Sita** yenye Ibara ya 99 na 100 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 18 cha **Sheria ya Tume ya UKIMWI, Sura ya 379** ili kutambua vyanzo vipya vya mapato katika Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI kwa ajili ya kugharamia jitihada za kukabiliana na UKIMWI. Kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa, vyanzo hivyo vinajumuisha mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kilevi, tozo ya kukabiliana na UKIMWI katika madini, tiketi za treni na ndege.

34. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Saba** yenye Ibara za 101 hadi 102 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 102 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 ili; Kwanza, kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania mamlaka ya kuanzisha chuo cha mafunzo ya kodi kwa watumishi wake, wataalam wa kodi au watu wengine wanaotekeleza majukumu ya kikodi. Lengo la marekebisho haya ni kukitambua Chuo cha Kodi kinachosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; Pili, kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzisha maabara ili kuwezesha usimamizi na utekelezaji wa Sheria za kodi; na

(b) Ibara ya 103 inapendekeza kufuta Kifungu cha 37 kwa kuwa maudhui ya Kifungu hicho yapo katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438.

35. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Nane** yenye Ibara ya 104 na 105 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 25 cha **Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161** ili kutambua vyanzo vipya vya mapato katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote kwa ajili ya kugharamia huduma mbalimbali za afya. Kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa, vyanzo hivyo vinajumuisha mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kilevi, tozo ya kukabiliana na UKIMWI katika madini, tiketi za treni na ndege.

36. **Mheshimiwa Spika**, **Sehemu ya Ishirini na Tisa** yenye Ibara za 106 hadi 114 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438** kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 107 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 11 ili kumwezesha Kamishna Mkuu kutambua hadhi ya ukaazi na kutoa cheti kwa madhumuni ya kodi;

(b) Ibara ya 108 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 23 kwa kuweka sharti kwa Kamishna Mkuu kutambua usajili wa wafanyabishara wadogo katika sekta isiyokuwa rasmi ambao wamesajiliwa na mamlaka husika. Aidha, Kifungu hicho kinaweka sharti kwa mamlaka husika ya usajili kujumuisha Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi katika vigezo vya kuwasajili wafanyabiashara wadogo wenye kipato chini ya kiwango cha ukomo wa kodi ya mapato. Lengo la marekebisho haya ni kurasimisha sekta ya wafanyabiashara wadogo na kuongeza wigo wa utozaji kodi;

(c) Ibara ya 109 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 42 ili kumwezesha Kamishna Mkuu kuanzisha mfumo wa kodi wa kielektroniki, kuunganisha mfumo huo na

mifumo ya walipa kodi, kuweka utaratibu wa matumizi sahihi ya mfumo huo kwa madhumuni ya usimamizi wa kodi pamoja na kubainisha adhabu kwa watakaokiuka matumizi ya mfumo huo. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea uzingatiaji wa sheria za kodi;

(d) Ibara ya 110 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 54 ili kuweka sharti la kuzitaka pande zinazohusika na mikataba ya ujenzi na uziduaji (extractive) kutoa taarifa kwa Kamishna Mkuu kuhusu mikataba yao na maelezo mengine ndani ya muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kuanza kwa kazi chini ya mikataba hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati na kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali;

(e) Ibara za 111 na 112 zinapendekeza kurekebisha vifungu vya 62 na 63 kuweka sharti la kutambua tarehe itakayohesabika kuwa pingamizi limepokelewa na Kamishna Mkuu. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata wa tarehe ya kupokelewa kwa notisi ya mapingamizi ya kodi;

(f) Ibara ya 113 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 75 ili kuweka ukomo wa miezi mitatu kwa Kamishna Mkuu kuzuia mali iliyokamatwa kabla ya kuuzwa au kuondolewa kwa madhumuni ya kukomboa kodi; na

(g) Ibara za ya 114 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 90 ili kuweka adhabu ya asilimia thelathini ya mapato yaliyorekebishwa kwa mlipa kodi aliyetoa taarifa za udanganyifu kuhusu hasara. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia udanganyifu na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria za kodi.

37. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini** yenye Ibara ya 115 na 116 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 9 cha **Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370** ili kumpa Msajili wa Hazina jukumu la

kuzitaka taasisi na mashirika ya umma kuchangia viwango kati ya asilimia 15 hadi 60 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kila mwezi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348. Utekelezaji wa hatua hii utafanyika baada ya uchambuzi utakaofanywa na Msajili wa Hazina na baada ya mashauriano na Waziri wa Fedha.

38. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Moja** yenye Ibara ya 117 na 118 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho kwa kuongeza Kifungu cha 73A katika **Sheria ya Reli, Sura ya 170** ili kuanzisha tozo ya udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI kwa kiwango cha shilingi mia tano kwa kila tiketi ya usafiri wa reli. Aidha, inapendekezwa kuwa mapato yatakayotokana na tozo hiyo yatagawanywa kwa uwiano wa asilimia 70 katika Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na asilimia 30 katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza juhudi za kuimarisha huduma za afya ikiwemo kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI na bima ya afya kwa wote;

39. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Mbili** yenye Ibara za 119 hadi 122 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220** kama ifuatavyo:

(a) Ibara za 120 na 122 zinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 4 na Jedwali la Pili ili kuanzisha tozo ya shilingi 10 kwa kila lita ya mafuta ya taa. Inapendekezwa kuwa mapato yatakayotokana na tozo hizo kugawanywa kwa uwiano wa asilimia 70 katika Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na asilimia 30 katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza juhudi za kuimarisha huduma za afya ikiwemo kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI na bima ya afya kwa wote; na

(b) Ibara ya 121 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 ili kuongeza shilingi 10 katika tozo inayotozwa kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli.

40. **Mheshimiwa Spika**, **Sehemu ya Thelathini na Tatu** yenye Ibara za 123 hadi 137 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148** kama ifuatavyo;

(a) Ibara ya 124 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 2 ili kuweka tafsiri ya misamiati "assisted Government entity" na "withholding agent" na kuboresha tafsiri ya msamiati "resident" ili kujumuisha kampuni zilizosajiliwa Tanzania Bara kwenye tafsiri hiyo;

(b) Ibara ya 125 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 ili kuanzisha utaratibu wa kodi ya zuio ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia tatu na kuanzisha utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 16 kwa malipo yanayofanyika kupitia benki au mfumo wa malipo ya kielektroniki. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya ongezeko la thamani na kuchochea ulipaji kodi wa hiyari;

(c) Ibara ya 127 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 27A ili kutambua kodi ya mauzo iliyolipwa kwa taasisi ya serikali na kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kama kodi ya mauzo iliyolipwa mapema na taasisi hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa changamoto ya kuhasibu kodi ya VAT kwa Mamlaka za Ngorongoro, TANAPA na TAWA kutokana na huduma wanazotoa ambapo makusanyo yake ikijumuisha kodi yanakusanywa na TRA;

(d) Ibara ya 128 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 29 ili kuweka utaratibu wa kuzingatiwa pale ambapo mtu aliyesajiliwa kabla ya kufikia kiwango cha usajili anapokiuka masharti ya usajili. Lengo la marekebisho haya ni kutoa nafasi ya kusikilizwa kwa mlipakodi;

(e) Ibara ya 129 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 46 ili kuwianisha na misingi ya utozaji wa kodi ya ongezeko

la thamani kwenye mali zisizohamishika ambapo muamala utahesabika umefanyika ndani ya Tanzania Bara na kodi itapaswa kutozwa endapo mali husika ipo ndani ya Tanzania bara na si vinginevyo;

(f) Ibara ya 130 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 51 ili kujumuisha katika tafsiri ya msamiati "electronic services" huduma za malipo kwa njia ya mtandao zinazotolewa na mtu asiye mkaazi wa Tanzania Bara. Lengo la marekebisho ni kupanua wigo wa kodi;

(g) Ibara za 131 na 132 zinapendekeza kurekebisha vifungu vya 56 na 57 ili kutoza kodi kwa kiwango cha asilimia sifuri katika mauzo ya mbolea iliyozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu na kwenye mauzo ya bidhaa za nguo zilizotengenezwa ndani ya nchi kwa kutumia pamba iliyolimwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la marekebisho haya ni kuvutia uwekezaji kwa kupunguza gharama ya uzalishaji na kuhamasisha uzalishaji wa nguo kwa kutumia pamba inayozalishwa nchini;

(h) Ibara ya 133 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 70 ili kuweka sharti la kuambatisha cheti cha kodi ya zuio au cheti cha kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa wakati wa kuwasilisha ritani;

(i) Ibara ya 134 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 71 ili kutoa mwongozo na utaratibu wa namna kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa mapema na kodi ya ongezeko la thamani iliyozuiliwa zitakavyohasibiwa wakati wa ukokotoaji wa kodi itakayopaswa kulipwa na wakala wa kuzuia kodi au taasisi ya serikali;

(j) Ibara ya 135 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 72 ili kuweka masharti ya kutoruhusu mtu kudai kurejeshewa kodi ya ongezeko la thamani ambayo haikulipwa wakati wa uingizaji wa bidhaa Tanzania

Bara. Lengo la marekebisho haya ni kulinda mapato ya Serikali;

(k) Ibara ya 136 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 90A na 90B ili kuweka takwa la kutoa cheti cha kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa mapema na cheti cha kodi ya zuio. Lengo la marekebisho haya ni kubainisha nyaraka zinazohitajika na namna ya kuhasibu kodi ya ongezeko la thamani iliyolipwa mapema na kodi ya ongezeko la thamani iliyozuiliwa;

(l) Ibara ya 137 inapendekeza kurekebisha Jedwali kwa:

(i) kuweka masharti kuwa msamaha wa kodi kwenye zana za kilimo utatolewa baada ya idhini ya Wizara yenye dhamana ya masuala ya kilimo kwa lengo la kuhakikisha kuwa msamaha husika unatolewa kwa walengwa;

(ii) kufuta msamaha kwenye magazeti yanayoingizwa nchini, lami kwa lengo la kupunguza wigo wa misamaha isiyo na tija na kulinda mapato ya Serikali;

(iii) kusamehe kodi kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yanayosafishwa mara mbili kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini ili kutoa nafuu kwa mlaji;

(iv) kusamehe kodi kwenye bima mtawanyo ili kupunguza gharama na kuweka usawa kwa kampuni za ndani na nje;

(v) kusamehe kodi kwenye gesi ya petroli, mitungi na matenki ya kuhifadhia gesi kwa ajili ya kupikia, gesi asilia na gesi asilia iliyogandamizwa kwa ajili ya matumizi ya magari na mitambo ya kuondoa gesi ukaa katika utengenezaji wa mkaa mbadala.

Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu na kuhamasisha matumizi ya nishati safi kwenye kupikia na magari;

(vi) kuongeza kwenye orodha ya msamaha nyuzi za katani na viuatilifu. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo;

(vii) kufanya maboresho katika msamaha wa kodi kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha nishati ya jua na katika huduma za ndani za matengenezo ya ndege, uunganishaji na utengenezaji wa ndege pamoja na vipuri vitakavyonunuliwa au kuingizwa kutoka nje ya nchi na wazalishaji wa ndani.
Lengo la marekebisho haya ni kuweka ufafanuzi wa msamaha huu na kuzuia matumizi mabaya ya msamaha uliotolewa.

41. **Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Nne** yenye Ibara ya 138 na 139 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 8 cha **Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283** ili kuweka mgawanyo wa mapato yanayotokana na shughuli za utalii katika maeneo ya uhifadhi kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), halmashauri za wilaya na vijiji na Serikali kuu. Aidha, Kifungu kinarekebishwa ili kuweka sharti kuwa mapato yaliyokusudiwa kwa ajili ya halmashauri za wilaya na vijiji vinavyopakana na maeneo ya uhifadhi yatawekwa katika akaunti ya TAWA. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha uhifadhi na kutoa motisha kwa halmashauri za wilaya na vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi.

42. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya hatua nyingine za mapato zilizopo katika Hotuba ya Bajeti na ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada huu, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali (Government Notices) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika.

**HITIMISHO:**

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji **kisheria** wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2025/26. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**MLNM**
**WF**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti. Namwona Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe akija kusoma kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 *(The Finance Bill, 2025)*. Naomba taarifa hii yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa kuzingatia Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 96 (1) na 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni tarehe 16 Juni, 2025 na kuelekezwa kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti, kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kama taratibu za Kamati zilivyo, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha aliwasilisha rasmi Muswada huo kwenye Kamati tarehe 17 Juni, 2025 kwa niaba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 unakusudia kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali, ili kuwezesha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 12 Juni, 2025. Kupitia Muswada huo, jumla ya Sheria 33 zilipendekezwa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho hayo yanajumuisha marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali na kuendelea kutoa misamaha ya kodi kwa baadhi ya bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kwa ujumla umelenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kulinda viwanda vya ndani, kuweka utaratibu rafiki wa uanzishwaji wa kodi, tozo na ada, kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali pamoja na kuanzisha vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI *(AIDS Trust Fund)* na Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada; Kamati imefanya uchambuzi wa Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa ajili ya kujiridhisha na maudhui yaliyopo yanayokusudiwa na kufanyia marekebisho pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilikutana na wadau *(Public Hearing)* kuanzia tarehe 17 hadi 20

Juni, 2025. Vilevile Kamati ilipokea maoni kwa njia ya barua pepe kwa lengo la kuboresha Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue wadau hao kama ifuatavyo: *Tanzania Private Sector Foundation, Legal Human Rights Centre, Steel Industries, Java Glass Limited, Lodhia Industries, Simba Cement, Dangote Cement, Twiga Cement, Tanzania Portland Cement Public Limited Company,* Shirika la Viwanda Tanzania*, Tanzania Sports Betting Association, Tanzania Bankers Association,* Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kariakoo, *Tanzania Mobile Network Operators, Salebhai Glass Industries LTD,* na Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, wadau wengine ni *PHARMA Africa, NACOPHA, Deloitte, Barrick Gold Mine, TAMSOA, TAFFA, TASAA, Tanzania Human Rights Centre, East African Starch Limited, Raddy Fibre,* Wafanyabiashara kutoka Mwanza*, Motor Vehicles Assemblers, Mufindi Paper Mill, NYP, Serengeti Breweries Limited, Tanzania Breweries Limited,* Wadau wa Afua ya Afya, *Tanzania Cigarette Company, KPMG, TAYOA, Maweni Limestone Limited, Tanzania Commercial Poultry Association, ALAF*, Wazalishaji wa vinywaji baridi, *Faraja Human Development Tanzania, Pay TV service providers* wakiwemo *Azam TV, DSTV, Startimes na Zuku), Agricultural Non State Actors Forum, Kick start international* na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea na kuchambua maoni ya wadau, iliandaa bangokitita lenye maoni ya Kamati kuhusu Muswada na kuliwasilisha Serikalini kwa lengo la kupata ufafanuzi. Mashauriano kati ya Kamati na Serikali yalifanyika kuanzia tarehe 21 hadi 25 Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri walioshiriki vikao hivyo ni Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge na Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo, Mbunge na Waziri wa Viwanda; na Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge na Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge na

Naibu Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii; na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa mrejesho wa mashauriano hayo kati ya Kamati na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha Mwaka 2025, jumla ya Sheria 33 zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ambazo Kamati ilikubaliana na Mapendekezo ya Serikali, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali katika sheria na baadhi ya maeneo ya sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya Tume ya UKIMWI, Sura ya 379 na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161;
(ii) Sheria ya Reli, Sura ya 170;
(iii) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
(iv) Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
(v) Sheria ya Madini, Sura ya 123; na
(vi) Sheria ya Kodi ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya maboresho ya sheria tajwa hapo juu kwa lengo la kuanzisha vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kugharamia afua za afya na kuendeleza Mfuko wa Udhamini na Udhibiti wa UKIMWI pamoja na Mfuko wa Bima ya Afya kwa wote.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mabadiliko ya kisera ya Washirika wa Maendeleo ambao walikuwa wanagharamia sehemu kubwa ya bajeti ya Serikali kwenye afua mbalimbali za afya na hasa UKIMWI, Serikali imechukua hatua za kukusudia ili kutafuta vyanzo mbadala kwa ajili ya kugharamia afua hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali chini ya mwongozo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi huo thabiti na makini ambao unaandaa kuondoa utegemezi na ushirika wa maendeleo kwa kuhudumia programu mbalimbali zikiwemo afua za afya.

Mheshimiwa Spika, huyu ndiye Rais ambaye anakwenda kuandika historia kwa kuifanya Tanzania ianze kujitegemea katika bajeti yake yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria ya Korosho, Sura ya 203, maboresho katika sheria hii, yalilenga kumpa jukumu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kupeleka mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi moja kwa moja kwenye Akaunti ya Bodi ya Korosho kwa kipindi cha miaka minne. Kamati inaipongeza Serikali kwa maboresho hayo kwa kuwa awali fedha hizo zilikuwa zikipelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu huo ulikuwa unachelewesha Bodi kupata fedha kwa wakati. Hivyo, hatua hii itasaidia kuondoa changamoto hii ili kuchochea maendeleo ya tasnia ya korosho nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371; Kamati inakubaliana na marekebisho ya Serikali katika sheria hii ambayo yanalenga masuala yafuatayo: -

(i) Kuwatambua wastaafu wanaolipwa mafao kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali; na

(ii) Kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kurejea viwango vya pensheni vya wastaafu hao baada ya kupata idhini ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa marekebisho hayo; na huu ni ukweli usiyopingika, huyu ndiye Rais ambaye anatambua

mchango mkubwa wa wastaafu katika kulijenga Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali katika sheria hii ambapo Serikali inakusudia kumwezesha Kamishina Mkuu kufanya yafuatayo: -

(i) Kutambua hadhi ya ukazi na kutoa cheti kwa madhumuni ya kodi;

(ii) Kutambua usajili wa wafanyabishara wadogo katika sekta isiyo rasmi ambao wamesajiliwa na mamlaka husika. Aidha, maboresho hayo yanaweka sharti kwa mamlaka husika ya usajili kujumuisha namba ya utambulisho kwa mlipakodi kama kigezo cha kuwasajili wafanyabiashara wadogo wenye kipato cha chini ya kiwango cha ukomo wa kodi ya mapato;

(iii) Kuanzisha mfumo wa kodi wa kielektroniki na kuunganisha mifumo hiyo na mifumo ya walipa kodi;

(iv) Kuweka utaratibu wa matumizi sahihi ya mifumo kwa madhumuni ya usimamizi wa kodi pamoja na kubainisha adhabu kwa watakaokiuka matumizi ya mifumo;

(v) Kuzitaka pande zinazohusika na mikataba ya ujenzi na uziduaji *(extractive)* kutoa taarifa kwa Kamishina Mkuu kuhusu mikataba yao na maelezo mengine ndani ya muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kuanza kwa kazi chini ya mikataba hiyo;

(vi) Kutambua tarehe itakayohesabika kuwa pingamizi la kodi limepokelewa na Kamishina Mkuu;

(vii) Kuweka ukomo wa miezi mitatu kwa Kamishina Mkuu kuzuia mali iliyokamatwa kabla ya kuuzwa au kuondolewa kwa madhumuni ya kukomboa kodi; na

(viii) Kuweka adhabu ya 30% ya mapato yaliyorekebishwa kwa mlipa kodi aliyetoa taarifa za udanganyifu kuhusu hasara.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo yanalenga: -

(i) Kuboresha usimamizi wa kodi kwa kutambua sekta isiyo rasmi na kuongeza wigo wa kodi;
(ii) Kuhamasisha matumizi ya mifumo;
(iii) Ushughulikiaji wa malalamiko ya kodi; na
(iv) Kutoa utaratibu wa uandaaji wa hesabu za kikodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hizo zitakazosaidia ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85; Serikali inapendekeza kufanya maboresho katika sheria hii ili kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za alama za biashara kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na hivyo kudhibiti bidhaa bandia zinazozalishwa na kuingia nchini. Vilevile, marekebisho hayo yanalenga kumpa Mamlaka Waziri wa Viwanda na Biashara kutengeneza Kanuni zitakazobainisha utaratibu wa utunzaji kumbukumbu za alama za biashara na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo, kwani kwa mara ya kwanza yanaenda kutambua dhana ya usajili wa alama za bidhaa kwa ajili ya ulinzi *(trademarks recordation)* yaliyokasimiwa na Tume ya Ushindani kupitia Sheria ya Alama za Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Maboresho hayo yanatoa fursa kwa mmiliki wa alama ya bidhaa kuwasilisha Tume nyaraka hizo kwa usajili kwa lengo la kuweka kumbukumbu za usajili unaoonyesha taarifa zote muhimu ili kudhibiti matumizi ya nembo yake kwenye bidhaa bandia. Kamati ilikubaliana na mapendekezo hayo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* Sura ya 148; Kamati ilifanya uchambuzi wa

mapendekezo ya Serikali katika sheria hii na kubaini kuwa marekebisho hayo yana lengo la kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwenye malipo, kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza mauzo nje pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati safi. Muhtasari wa hatua hizo ni kama unavyoonekana hapa chini.

(i) Kurekebisha Kifungu cha Tano ili kuanzisha utaratibu wa kodi ya zuio ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia tatu;

(ii) Kuanzisha utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha 16% kwa malipo yanayofanyika kupitia benki au mfumo wa malipo ya kielektroniki;

(iii) Kurekebisha Kifungu cha 56 na 57 ili kuendelea kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri katika mauzo ya mbolea iliyozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu na kwenye mauzo ya bidhaa za nguo zinazotengenezwa nchini kwa kutumia pamba iliyozalishwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuvutia uwekezaji kwa kupunguza gharama ya uzalishaji na kuhamasisha uzalishaji wa nguo kwa kutumia pamba inayozalishwa ndani ya nchini; na

(iv) Kusamehe kodi hii kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yanayosafishwa mara mbili kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini ili kutoa nafuu kwa mlaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290; Serikali inakusudia kurekebisha vifungu vya sita, saba, na nane vya sheria hii pamoja na jedwali ili kupunguza kiwango cha ada ya ushuru wa hoteli *(Hotel Levy)* kutoka 10%

hadi asilimia mbili na kuweka kiwango mfuto cha ushuru wa huduma cha asilimia 0.25 ya mapato ghafi.

Mheshimiwa Spika, aidha, inapendekezwa kurekebisha jedwali ili kutoa msamaha wa ada za upakiaji *(loading)* na upakuaji *(offloading)* wa mizigo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini, kuongeza hamasa ya ulipaji wa kodi kwa hiari pamoja na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Ibara ya 27, 28, 30, 31, 32, 33, na 34 ambapo Serikali inakusudia kufanya yafuatayo: -

(i) Kurekebisha Kifungu cha 10 ili ukomo wa leseni kwa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kuwa miezi 12 tangu tarehe ambayo leseni imetolewa badala ya utaratibu uliokuwepo wa leseni utakapofika ukomo wake tarehe 30 Desemba;

(ii) Kurekebisha Kifungu cha 146A ili kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa inayotambulika kwa *HS Code 2207.10.00* kwenye *Un-denatured Ethyl Alcohol* inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi mathalani uzalishaji wa ladha za vyakula *(Food Flavors)* kama vile *cocoa, vanila*, na kahawa; na

(iii) Kufanya marekebisho ya kutoza kodi katika jedwali la nne lenye bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282; Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha Tisa ili kugawa 91% ya mapato ya *TANAPA* ambapo 51% itawekwa kwenye akaunti ya *TANAPA* iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na 70% katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vilevile, inapendekezwa matumizi ya fedha kutoka akaunti ya TANAPA yawe yanatolewa kwa kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikubaliana na pendekezo hili la Serikali baada ya kuthibitishiwa kwamba 51% ya mapato yanayobakizwa yanalingana na mahitaji ya fedha ya *TANAPA*. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali kufanya uchambuzi zaidi katika mwaka wa fedha 2026/2027 kwa sababu kiasi cha 51% hakitoshi kuendeleza kwenye miundombinu ya utalii.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Muswada ambayo yana marekebisho ya Kamati na Serikali imeridhia mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Serikali ilikuwa imekusudia kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka 17% hadi 17.5%. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba ushuru wa bidhaa kwenye mawasiliano Tanzania ni mkubwa kuliko nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Kenya ni 15%, Uganda 12%, Rwanda 10%, Malawi 10%, Botwana na Afrika kusini hawatozi kabisa. Hivyo, kuongeza kiwango hicho kingeleta madhara kwenye kuchochea kasi ya kuelekea uchumi wa kidijitali. Aidha, hatua hiyo ni kinzani kwa maendeleo yaliyofikiwa na Serikali katika kuchochea matumizi ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kuacha kuongeza kiwango cha asilimia 0.5 na hivyo itaendelea kutoza kiwango cha sasa cha 17% kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo kazi kubwa ya Kamati yako ya Bajeti inayoifanya katika kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika sheria hii Serikali imefanya marejeo ya viwango vilivyokuwa vimebainishwa katika *headings* zenye *HS. Code 23.03, 22.04, 22.05, 22.06* na 22.08. Lengo la marekebisho hayo ni kwa sababu awali ilitakiwa marekebisho yafanyike baada ya miaka mitatu; yaani ifikapo mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kutokana na changamoto za mapato, Serikali iliamua kubadili viwango hivyo ili kutanua wigo wa mapato, na hivyo ilikuwa ni vyema kuweka viwango ambavyo sekta ingeweza kuvibeba. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kama yanavyoonekana kwenye marekebisho ya Jedwali la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276; katika Sheria hii Serikali ilikusudia kufanya yafuatayo: -

(i) Kujumuisha bidhaa zinazotoka ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye wigo wa tozo ya maendeleo ya viwanda kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani na kuongeza mapato ya Serikali; na

(ii) Kurekebisha Jedwali ili kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwenye bidhaa za misumari, vichwa vya kuvuta matrela, samani, marumaru, nondo, mabati, vyombo vya plastiki, hema za chuma na vioo ambavyo vinaingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuongeza uwekezaji na uzalishaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani kwa kuwa bidhaa hizo zinazalishwa kwa wingi nchini. Hata hivyo pendekezo hili lilikuwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Mapendekezo ya kujumuisha bidhaa zinazotoka ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye wigo wa tozo ya maendeleo ya viwanda yanakinzana na Ibara ya 19 ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ya mwaka 2009 *(East Africa Common Market Protocol 2009)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua hiyo itasababisha vita ya kibiashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki hususan maeneo ya Kanda ya Ziwa kutokana na shughuli za kibiashara zinazofanywa na nchi wanachama katika ukanda huo. Vilevile, hatua hiyo ingechochea uingizwaji wa bidhaa kimagendo nchini na hivyo

kuikosesha Serikali mapato stahiki. Kutokana na sababu hizo, Kamati ilipendekeza Ibara ya 44 (b) ya Muswada ifutwe; na

(ii) Kamati ilipendekeza kuongeza bidhaa nne katika jedwali ambazo ni *starch* inayotambulika kwa *HS. Code 17.02; liquid glucose* inayotambulika kwa *HS. Code 11.08*; karatasi zinazotambulika kwa *HS. Code* 4804.11.00, 4804.21.00, 4804.31.00, 4804.41.00 na 4804.51.00 pamoja na nyaya za mkongo zinazotambulika kwa *HS. Code* 8544.70.00. Pendekezo hili lilizingatia kwamba viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo navyo vinahitaji ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliridhia mapendekezo ya Kamati ambapo bidhaa kutoka nchi wanachama wa Afrika Mashariki zitakuwa zikipewa msamaha na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la taarifa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342; Serikali imefanya marekebisho katika sheria hii kwa kuongeza Kifungu kipya cha 39(a) chenye lengo la kuongeza jukumu kwa Bodi ya Bima ya Amana *(DIB)* la kuongeza ukwasi kwa njia ya mkopo kwa benki au taasisi ya fedha yenye changamoto ya ukwasi na ipo hatarini kufilisika. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha *DIB* kwa kushirikiana na Benki Kuu kunusuru taasisi za fedha zenye changamoto ya ukwasi na zilizo hatarini kufilisika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Kifungu hiki na kuona kwamba ili kuhakikisha benki zilizopokea fedha kutoka *DIB* zinaimarika, ni vyema benki hizo zikawekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu mara baada ya kupokea fedha kutoka kwa *DIB*.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati iliitaka Serikali kuongeza kifungu kidogo kipya kinachozitaka benki zilizopokea msaada wa ukwasi kuwekwa chini ya usimamizi wa karibu wa Benki Kuu ya Tanzania. Serikali ilikubali mapendekezo hayo kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, Serikali ilipendekeza kufanya maboresho kwenye Sheria ya Bajeti kwa kuongeza kifungu kipya cha 60(a) kinachoweka sharti la kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kabla ya kutoza au kubadili ada, tozo, faini na ushuru mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lengo la mabadiliko haya ni kuongeza tija, ufanisi na kuhakikisha yanaenda sambamba na malengo ya sera za fedha pamoja na kuzuia utozaji usiozingatia utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kifungu hiki hakikuweka muda maalumu ambao Taasisi, Wizara na Mamlaka zinaweza kufanya maboresho ya ada, tozo, faini na ushuru. Hivyo, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kwa kuongeza kifungu kidogo kipya kinachompa mamlaka Waziri kuomba ushauri kwenye Kamati ya Ushauri ya Masuala ya Kikodi kwa mujibu wa Kifungu cha 19 cha Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilipendekeza Serikali kutoa tafsiri ya Wizara ili kuondoa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye masharti ya kifungu hicho. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima, Sura ya 394; katika Sheria hii Serikali inakusudia kuanzisha bima ya usafiri kwa wageni wanaoingia nchini kwa kiwango cha Dola za Marekani 44. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaowezesha kuwalinda wageni wanapokuwa nchini dhidi ya dharura za kiafya, kupotea kwa mizigo yao, na kugharamia wageni wanapoondoshwa kwa lazima au inapotokea hatari yenye kulazimu uondoshwaji.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Serikali yanalenga kutoa msamaha kwa wakazi wanaotoka nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba hatua hii inaenda kuongeza gharama kwa watalii na

wafanyabiashara wanaoingia nchini. Hivyo, Kamati ilikubaliana na Serikali kwamba utekelezaji wa vifungu vinavyopendekezwa uanze mwezi Januari, 2026 ili kutoa fursa ya kufanya majadiliano na sekta zinazoweza kuathirika na sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura namba 332; Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha tatu kwa kurekebisha tafsiri ya msamiati '*permanent establishment*' na '*capitalization of profits.*'

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini maneno hayo hayajaorodheswa kwa mpangilio wa irabu. Hivyo, Kamati ilishauri kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya namba ya kifungu kwa kuzingatia mpangilio wa irabu. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 12 ili kutambua faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa *(retained earning)* kuwa sehemu ya mtaji.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo kwa ujumla yatapelekea faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa kutozwa kodi ya zuio kwa kiwango cha 10% baada ya miezi sita. Lengo la Serikali lilikuwa ni kuchochea uingizaji wa mitaji katika shughuli za uchumi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua suala hili kwa kina kwa kuangalia nia ya Serikali ya kuzuia ukwepaji wa kodi na kuleta usawa katika utozaji wa kodi ya mapato. Masuala mengine yaliyoangaliwa ni:-

(i) Kutovutia mitaji na uwekekezaji nchini kwa kuhofia kwamba pale wanapotaka kuongeza mitaji yao kupitia faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa itatozwa kodi;

(ii) Tafsiri ya maneno '*capitalization by profit*' yanajumuisha sekta bila kuzingatia namna sekta hiyo inavyoendeshwa na madhara yanayoweza kujitokeza mfano sekta ya benki; na

(iii) Endapo lengo la Serikali haliwezi kuzuia ukwepaji wa kodi ya mapato kupitia Kifungu cha Nane cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 ambacho kinampa Mamlaka Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kuchunguza na kubaini endapo kuna ukwepaji wa kodi na kukusanya kodi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi huo Kamati ilibaini kwamba kifungu hiki siyo kipya kilikuwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 1973. Aidha, Kamati ilibaini Taifa jirani la Kenya lina kifungu kama hicho. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufanya marejeo ya kifungu hicho na kuondoa utata uliopo. Serikali ilikubali na marekebisho yalifanyika kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Namba Sita ya Mwaka 2025. Sheria hii inarekebishwa katika Kifungu cha Pili na 21 ili kuwatambua wawekezaji waliosaini mikataba na Serikali katika sekta ya madini kuwa ni wawekezaji wa mahiri. Aidha, Kifungu cha 19 kinarekebishwa ili kuweka masharti yanayobainisha bidhaa ambazo hazikidhi kupata msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kifungu hicho kinatoa msamaha wa ushuru wa forodha kwa kiwango cha 75% kwa mwekezaji atakayeagiza bidhaa za mtaji usio wa asili na atalazimika kulipa ushuru wa forodha wa 25%.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa madhara yanayoweza kutokea kwenye mapato ya Serikali kwa sekta ya madini kujumuishwa katika miradi inayoweza kupewa vivutio vya ziada. Kamati iliishauri Serikali kuiondoa sekta hiyo na kuacha utaratibu ulivyo hivi sasa ili kulinda mapato ya Serikali. Serikali ilikubaliana na kufanya marekebisho ya kufuta Ibara ya 64 na 66 ya Muswada kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ambayo Kamati Haijakubaliana na Serikali. Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura namba 370 pamoja na Sheria ya Fedha za Umma, Sura

namba 348. Serikali ilikusudia kurekebisha Kifungu cha 9(1)(f) cha Sheria ya Msajili wa Hazina na Kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Fedha za Umma ili kuongeza kiwango kinachotakiwa kuchangiwa na Taasisi na Mashirika ya umma kati ya 15% hadi 60% ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejadiliana kwa kina sana na Serikali na masuala yafuatayo yaligundulika:-

(i) Hakuna vigezo vilivyowekwa kisheria vitakavyotumika kubainisha ni Taasisi gani au shirika gani lichangie kwa 15% au zaidi;

(ii) Serikali haikuwasilisha mbele ya Kamati uchambuzi wa kitaalamu uliosababisha kufikia mapendekezo hayo;

(iii) Mapendekezo haya yanaenda kinyume na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akipokea gawio la mashirika ya umma ambapo aliagiza yalelewe ili yachangie zaidi;

(iv) Kuna udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya mashirika na hivyo badala ya Serikali kushughulikia udhaifu huo, imekuja na pendekezo hili;

(v) Hivi sasa kuna baadhi ya mashirika na taasisi za umma zinashindwa kuchangia 15% ya mapato ghafi, hivyo kupanua wigo ni kuleta changamoto kubwa kwenye taasisi na mashirika ya umma;

(vi) Mchango huo unatokana na mapato ghafi ya taasisi bila kutoa gharama zozote za uendeshaji. Hivyo, kuongeza kiwango kati ya 15% hadi 60% kutaleta madhara makubwa katika utendaji kazi wa taasisi hizo; na

(vii) Utaratibu huu unaathiri mtiririko wa fedha kwa baadhi ya mashirika ambayo yanatumia mtiririko wake kukopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo Kamati haikukubaliana na Serikali na imewasilisha Jedwali la Marekebisho ili Bunge lako Tukufu lifanye maamuzi sahihi kwa maslahi mapana ya kiuchumi ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Ninapenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Kwanza Mwanamke wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*; na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika, kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu kwa hekima na uongozi mahiri.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Madelu, Mbunge na Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge, na Naibu Waziri wa Fedha na Mbunge wa Kamati Kuu ya Fedha ya Chama cha Mapinduzi kwa ushirikiano wao wa karibu na mchango wao mkubwa wakati wa kuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninapenda kuwashukuru, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali; Ndugu Elijah Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Ndugu Yusuph Juma Mwenda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; na Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, pia, ninawashukuru Makamishna wa Taasisi na Wataalamu wote wa Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme umepata Mwenyekiti mahiri mwenye uwezo mkubwa, na sisi tunajivunia kuwa na Mheshimiwa Njeza kama Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bajeti. Ni imani yangu wananchi wa Mbeya Vijijini wanakwenda kumrudisha baba huyu mwezi wa 11 aje kuapa hapa ili aweze kuendelea kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, pia, ninawashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umakini waliouonesha wakati wa kujadili Muswada huu. Ninaomba niwatambue kama majina yao yanavyoonekana katika Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kipekee zaidi, ninaomba niwashukuru wananchi wangu na Wapigakura wangu wa Jimbo la Kibiti kwa heshima kubwa waliyonipatia kuweza kuwaongoza katika kipindi cha miaka mitano. Ninaomba tu niseme ni imani yangu mwezi wa 11 nitarudi hapa.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie wananchi wa Jimbo la Kibiti, Mpembenwe ndiyo yule yule, Kibiti ndiyo ile ile, na adhima yetu ya Kibiti kwa maendeleo inawezekana tunakwenda kuikamilisha tena.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ila siyo kwa umuhimu, nimshukuru Bwana Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba tu niseme Watumishi wa Bunge wa Kamati ya Bajeti wanafanya kazi kubwa na sisi kama Wabunge tunajivunia kuwa na watumishi hawa. Jana tumetoka hapa saa 8.30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na kwa heshima na taadhima ninaunga mkono hoja.

**25 JUNI, 2025**

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2025 (THE FINANCE BILL, 2025) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

### 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa kuzingatia kifungu cha 9 (1) cha Sheria ya Bajeti Sura 439, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 96 (1) na 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2025 ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni tarehe 16 Juni, 2025 na kuelekezwa kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kama taratibu za Kamati zilivyo, Mhe. Hamad Hassan Chande, (Mb), Naibu Waziri wa Fedha aliwasilisha rasmi Muswada huo kwenye Kamati tarehe 17 Juni, 2025 kwa niaba ya Waziri wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 unakusudia kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26 iliyowasilishwa Bungeni tarehe **12 Juni, 2025**. Kupitia Muswada huo, jumla ya **Sheria 33** zilipendekezwa kufanyiwa marekebisho. Aidha, marekebisho hayo yanajumuisha marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali na kuendelea kutoa misamaha ya kodi kwa baadhi ya bidhaa.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu kwa ujumla umelenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kulinda viwanda vya ndani, kuweka utaratibu rafiki wa uanzishwaji wa kodi, tozo na ada, kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali pamoja na

kuanzisha vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko wa udhamini wa UKIMWI (AIDS Trust Fund) na Bima ya Afya kwa wote.

**2.0. UCHAMBUZI WA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa ajili ya kujiridhisha na maudhui yaliyokuwa yanakusudiwa na kuufanyia marekebisho pale ilipobidi. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ilikutana na Wadau (Public Hearing) kuanzia tarehe 17 hadi 20 Juni, 2025, vilevile Kamati ilipokea maoni kwa njia ya barua pepe kwa lengo la kuboresha Muswada huo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba niwatambue Wadau hao kama ifuatavyo:- Tanzania Private Sector Foundation (TPSF), Legal Human Rights Centre (LHRC), Steel Industries, Java Glass Limited, Lodhia Industries, Simba Cement, Dangote Cement, Twiga Cement, Tanzania Portland Cement Public Limited Company, Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), Tanzania Sports Betting Association (TSBA), Tanzania Bankers Association (TBA), Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kariakoo, Tanzania Mobile Network Operators (TAMNOA), Salebhai Glass Industries LTD, Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA), PHARMA Africa, NACOPHA, Deloitte, Barrick Gold Mine, TAMSOA, TAFFA, TASAA, Tanzania Human Rights Centre (THRC), East African Starch Limited, Raddy Fibre, Wafanyabiashara kutoka Mwanza, Motor Vehicles Assemblers, Mufindi Paper Mill, NYP, Serengeti Breweries Limited (SBL), Tanzania Breweries Limited (TBL), Wadau wa Afua za Afya, Tanzania Cigarette Company (TCC), KPMG, TAYOA, Maweni Limestone Limited, Tanzania Commercial Poultry Association, ALAF, Wazalishaji wa vinywaji baridi, Faraja human development Tanzania, Pay TV service providers (Azam tv, Dstv, Startimes na Zuku), Agricultural non state actors Forum, Kick start international na watu binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kupokea na kuchambua maoni ya wadau, iliandaa bangokitita lenye maoni ya Kamati kuhusu Muswada na kuliwasilisha kwa Serikali kwa lengo la

kupata ufafanuzi. Mashauriano kati ya Kamati na Serikali yalifanyika kuanzia tarehe 21 hadi 25 Juni, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Mawaziri walioshiriki vikao hivyo ni Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb) Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Selemani Said Jafo, (Mb) Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, (Mb) Waziri, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mhe. Hamad Hassan Chande, (Mb) Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Dunstan Luka Kitandula, (Mb) Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb) Naibu Waziri Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa mrejesho wa mashauriano hayo kati ya Kamati na Serikali.

## 3.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2025

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya Sheria 33 zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Tozo za Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365;
(ii) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342;
(iii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;
(iv) Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 101;
(v) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439;
(vi) Sheria ya Korosho, Sura ya 203;
(vii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
(viii) Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;
(ix) Sheria ya Ushindani, Sura ya 285;
(x) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
(xi) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
(xii) Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276;
(xiii) Sheria ya Bima, Sura ya 394;
(xiv) Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025;

(xv) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
(xvi) Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85;
(xvii) Sheria ya Madini, Sura ya 123;
(xviii) Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124;
(xix) Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282;
(xx) Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127;
(xxi) Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura ya 284;
(xxii) Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari, Sura ya 264;
(xxiii) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348;
(xxiv) Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371;
(xxv) Sheria ya Tume ya UKIMWI, Sura ya 379;
(xxvi) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
(xxvii) Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161;
(xxviii) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
(xxix) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370;
(xxx) Sheria ya Reli, Sura ya 170;
(xxxi) Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
(xxxii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na
(xxxiii) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

### 3.1. Sheria ambazo Kamati ilikubaliana na Mapendekezo ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Sheria na baadhi ya maeneo ya Sheria zifuatazo:-

### 3.1.1. Sheria ya Korosho, Sura ya 203

**Mheshimiwa Spika,** maboresho katika Sheria hii yalilenga kumpa jukumu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kupeleka mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi moja kwa moja kwenye Akaunti ya Bodi ya Korosho kwa kipindi cha miaka minne. Kamati inaipongeza Serikali kwa maboresho hayo kwa kuwa awali fedha hizo zilikuwa zikipelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu huo ulikuwa unachelewesha Bodi kupata fedha kwa wakati. Hivyo, hatua hii

itasaidia kuondoa changamoto hiyo ili kuchochea maendeleo ya tasnia ya korosho nchini.

**3.1.2. Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196**
**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya maboresho katika sheria hii ili kuanzisha kodi ya usafirishaji wa mbao laini kwenda nje ya nchi kwa kiwango cha **asilimia 30** au **shilingi 150** kwa kilo moja kutegemea na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye vinia (mbao laini) inayotambulika kwa **Heading 44.08**. Lengo la marekebisho haya ni kulinda viwanda vya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za kutengeneza bidhaa za *plywood* na *marine board*.

**3.1.3. Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127**
**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Serikali inakusudia kuongeza kifungu kidogo cha 22(2)(d) ili kumwezesha Waziri kutengeneza kanuni zitakazobainisha vigezo vya kuzingatiwa wakati wa kufanya tathmini ya miradi ya uwekezaji wa umma. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Tume ya Mipango kuzingatia vigezo mtambuka vinavyotambuliwa ndani na nje ya nchi katika kufanya tathmini ya miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuwa vigezo hivyo vitumiwe na Wizara na Taasisi zote za Umma ili kuweka usawa katika ufanyaji wa tathmini na ufuatiliaji wa miradi.

**3.1.4. Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari, Sura ya 264**
**Mheshimiwa Spika,** maboresho katika sheria hii yanalenga kuweka uwiano wa tarehe ya kulipa ada ya huduma za bandari na tarehe ya kuwasilisha ritani kuwa siku ya 20 ya mwezi baada ya kukusanywa kwa ada hiyo. Aidha, maboresho kama hayo pia yamefanyika katika **Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege, Sura ya 365.** Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha ulipaji kodi na usimamizi wake pamoja na Serikali kukusanya mapato yake kwa wakati. Awali ritani hizi zilikuwa zinawasilishwa siku ya mwisho ya kazi ya mwezi.

**3.1.5. Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Sura ya 371**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na marekebisho ya Serikali katika sheria hii ambayo yana lenga masuala yafuatayo:-

i. Kuwatambua wastaafu wanaolipwa mafao kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali; na

ii. Kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kurejea viwango vya pensheni vya wastaafu hao baada ya kupata idhini ya Mheshimiwa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa marekebisho hayo.

**3.1.6. Sheria ya Tume ya UKIMWI, Sura ya 379 na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mabadiliko ya kisera ya Washirika wa Maendeleo ambao walikuwa wanagharamia sehemu kubwa ya bajeti ya Serikali kwenye afua mbalimbali za afya na hasa UKIMWI, Serikali imechukua hatua za makusudi ili kutafuta vyanzo mbadala kwa ajili ya kugharamia afua hizo. Aidha, utakumbuka kuwa mwaka 2023/24 Bunge lilipitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa wote hata hivyo, sheria hiyo haikuanza kutekelezwa kutokana na kuipa Serikali muda wa kufanya maandalizi ya utekelezaji wa mpango huo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kugharamia bima ya afya kwa wote na afua za UKIMWI, Serikali inapendekeza vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kugharamia huduma hizo kama ifuatavyo: -

i. Mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kilevi;
ii. Tozo kwenye madini;
iii. Tozo kwenye tiketi za treni na ndege;
iv. Ada ya usajili wa vyombo vya moto; na
v. Michezo ya kubahatisha.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba hatua hii inaenda kuongeza wigo wa mapato ya Serikali ili kugharamia afua za UKIMWI na afya. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutafuta vyanzo vipya ili kutunisha Mfuko wa Udhibiti wa Ukimwi pamoja na Bima ya Afya kwa Wote.

**3.1.7. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali katika sheria hii ambapo Serikali inakusudia kumwezesha Kamshna Mkuu kufanya yafuatayo:-

i. kutambua hadhi ya ukaazi na kutoa cheti kwa madhumuni ya kodi;

ii. kutambua usajili wa wafanyabishara wadogo katika sekta isiyokuwa rasmi ambao wamesajiliwa na mamlaka husika. Aidha, maboresho hayo yanaweka sharti kwa mamlaka husika ya usajili kujumuisha namba ya utambulisho wa mlipakodi kama kigezo cha kuwasajili wafanyabiashara wadogo wenye kipato cha chini ya kiwango cha ukomo wa kodi ya mapato;

iii. kuanzisha mfumo wa kodi wa kielektroniki na kuunganisha mifumo hiyo na mifumo ya walipa kodi;

iv. kuweka utaratibu wa matumizi sahihi ya mifumo kwa madhumuni ya usimamizi wa kodi pamoja na kubainisha adhabu kwa watakaokiuka matumizi ya mifumo;

v. kuzitaka pande zinazohusika na mikataba ya ujenzi na uziduaji (extractive) kutoa taarifa kwa Kamishna Mkuu kuhusu mikataba yao na maelezo mengine ndani ya muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kuanza kwa kazi chini ya mikataba hiyo;

vi. kutambua tarehe itakayohesabika kuwa pingamizi la kodi limepokelewa na Kamishna Mkuu;

vii. kuweka ukomo wa miezi mitatu kwa Kamishna Mkuu kuzuia mali iliyokamatwa kabla ya kuuzwa au kuondolewa kwa madhumuni ya kukomboa kodi; na

viii. kuweka adhabu ya **asilimia 30** ya mapato yaliyorekebishwa kwa mlipa kodi aliyetoa taarifa za udanganyifu kuhusu hasara.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho hayo yanalenga: -

i. kuboresha usimamizi wa kodi kwa kutambua sekta isiyo rasmi na kuongeza wigo wa kodi;

ii. kuhamasisha matumizi ya mifumo; iii. ushughulikiaji wa malalamiko ya kodi; na iv. kutoa utaratibu wa uandaaji wa hesabu za kikodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hizo zitakazosaidia ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

**3.1.8. Sheria ya Reli, Sura ya 170**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria hii ili kuanzisha tozo ya udhibiti wa maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa kiwango cha **shilingi 500** kwa kila tiketi ya usafiri wa reli. Mapato yatakayotokana na tozo hiyo yatagawanywa kwa uwiano ufuatao **asilimia 70** yataelekezwa katika Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na **asilimia 30** yataelekezwa katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

**3.1.9. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283**

**Mheshimiwa Spika,** maboresho katika Sheria hii yanalenga kuweka mgawanyo wa mapato yatokanayo na shughuli za utalii katika maeneo ya uhifadhi kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Halmashauri za wilaya, vijiji na Serikali kuu. Aidha, maboresho yanaweka masharti ili mapato ya Halmashauri za wilaya na vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi kuwekwa katika akaunti ya TAWA. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha uhifadhi na kutoa motisha kwa Halmashauri za wilaya na vijiji vilivyotenga maeneo yao kwa ajili ya uhifadhi.

**3.1.10. Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220;**
**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kuanzisha tozo ya **shilingi 10** kwa kila lita ya mafuta ya taa na kuongeza **shilingi 10** katika tozo inayotozwa kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli. Mapato yatakayopatikana kutokana na tozo hiyo, **asilimia 70** yataelekezwa katika Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI na **asilimia 30** yataelekezwa katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Sheria hii inalenga kuimarisha huduma za afya ikiwemo kukabiliana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuhakikisha kuwa Sheria ya bima ya afya kwa wote inatekelezwa.

**3.1.11. Sheria ya Ushindani, Sura ya 285;**
**Mheshimiwa Spika,** maboresho katika Sheria hii yanalenga kuweka bayana vyanzo vya mapato vya Tume ya Ushindani pamoja na kubainisha kiwango kinachopaswa kuwasilishwa kwa Tume kutoka kwenye Mamlaka tano za udhibiti za TCRA, EWURA, LATRA, TASAC na TCAA. Lengo la maboresho ni kuondoa changamoto ya Mamlaka hizo kuwasilisha michango yao chini ya kiwango kilichowekwa kikanuni chini ya Sheria hii na hivyo kuathiri utendaji kazi wa Tume.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Serikali ni kupunguza ada ya leseni kutoka wigo wa **asilimia 0** hadi **2.5** na kuweka kiwango kimoja cha **asilimia 1.5.** Aidha, mamlaka za udhibiti zilizolengwa zitatakiwa kuchangia **asilimia 1** ya mapato ghafi kwa Tume ya Ushindani. Lengo la maboresho haya ni kuhakikisha Tume inakuwa na mapato ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kamati ilikubaliana na pendekezo hili la Serikali.

**3.1.12. Sheria ya Alama za Bidhaa, Sura ya 85;**
**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya maboresho katika sheria hii ili kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za alama za biashara kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na hivyo kudhibiti bidhaa bandia zinazozalishwa na kuingia nchini. Vilevile, marekebisho hayo yanalenga kumpa Mamlaka Waziri wa Viwanda na Biashara kutengeneza Kanuni zitakazobainisha

utaratibu wa utunzaji kumbukumbu za alama za biashara na bidhaa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwani kwa mara ya kwanza yanaenda kutambua dhana ya usajili wa alama za bidhaa kwa ajili ya ulinzi (trademarks recordation) yaliyokasimiwa kwa Tume ya Ushindani kupitia Sheria ya Alama za Bidhaa. Maboresho hayo yanatoa fursa kwa mmiliki wa alama ya bidhaa kuwasilisha Tume nyaraka hizo za usajili kwa lengo la kuweka kumbukumbu za usajili unaoonyesha taarifa zote muhimu ili kudhibiti matumizi ya nembo yake kwenye bidhaa bandia. Kamati ilikubaliana na pendekezo hilo la Serikali.

**3.1.13. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura ya 148**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali katika Sheria hii na kubaini marekebisho hayo yana lengo la kuhamasisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwenye malipo, kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza mauzo nje pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati safi. Muhtasari wa hatua hizo ni:-

i. Kurekebisha Kifungu cha 5 ili kuanzisha utaratibu wa kodi ya zuio ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha **asilimia 3;**

ii. kuanzisha utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha **asilimia 16** kwa malipo yanayofanyika kupitia benki au mfumo wa malipo ya kielektroniki;

iii. kurekebisha kifungu cha 56 na 57 ili kuendelea kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha **asilimia 0** katika mauzo ya mbolea iliyozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu na kwenye mauzo ya bidhaa za nguo zilizotengenezwa nchini kwa kutumia pamba iliyozalishwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la marekebisho haya ni kuvutia uwekezaji kwa kupunguza gharama ya uzalishaji na kuhamasisha

uzalishaji wa nguo kwa kutumia pamba inayozalishwa nchini;

iv. kufuta msamaha kwenye magazeti yanayoingizwa nchini na lami kwa lengo la kupunguza wigo wa misamaha isiyo na tija na kulinda mapato ya Serikali;

v. kusamehe kodi hii kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyosafishwa mara mbili kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini ili kutoa nafuu kwa mlaji; na

vi. kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi ya petroli (LPG), mitungi ya kuhifadhia gesi (LPG) na gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) kwa ajili ya matumizi ya magari na mitambo ya kuondoa gesi ukaa katika utengenezaji wa mkaa mbadala. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu na kuhamasisha matumizi ya nishati safi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu mapendekezo hayo.

**3.1.14. Sheria ya Madini, Sura ya 123**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 69 cha sheria hii kinarekebishwa ili kuweka masharti kwa makampuni ya madini yenye mikataba na Serikali kutenga si chini ya **asilimia 20** ya madini yaliyochimbwa ili yaongezewe thamani nchini. Aidha, inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 113A ili kuanzisha tozo ya kukabiliana na maambukizi ya UKIMWI kwa kiwango cha **asilimia 0.1** ya thamani ya madini. Lengo la marekebisho haya ni kuendeleza juhudi za kuimarisha huduma za afya ikiwemo kukabiliana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na bima ya afya kwa wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kusimamia uamuzi huo wa kuyataka makampuni ya madini kuongeza thamani nchini. Uamuzi huo ni wa kizalendo na ni wa kupongeza.

**3.1.15. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kurekebisha vifungu vya 6, 7 na 8 vya Sheria hii pamoja na Jedwali ili kupunguza kiwango cha ada ya ushuru wa hoteli (hotel levy) kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 2** na kuweka kiwango mfuto cha ushuru wa huduma cha **asilimia 0.25** ya mapato ghafi. Aidha, inapendekezwa kurekebisha Jedwali ili kutoa msamaha wa ada za upakiaji (loading) na upakuaji (offloading) wa mizigo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini, kuongeza hamasa ya ulipaji wa kodi kwa hiari pamoja na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI).

**3.1.16. Sheria ya Kodi ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124**

**Mheshimiwa Spika,** katika sheria hii Serikali inakusudia kuongeza kifungu kipya cha 5A na Jedwali la Tatu ili kuanzisha tozo ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwenye usajili wa vyombo vya moto vinapoingizwa nchini. Aidha, Jedwali la Kwanza linarekebishwa ili kuyatambua magari yanayotumia umeme. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza vyanzo vya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

**3.1.17. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali katika ibara ya 27, 28, 30, 31, 32, 33, na 34 ambapo Serikali inakusudia kufanya yafuatayo:-

i. kurekebisha Kifungu cha 2 ili kubainisha tafsiri ya maneno "financial institution" ili kufafanua maana ya msamiati huo katika muktadha wa Sheria hiyo;

ii. kurekebisha Kifungu cha 10 ili ukomo wa leseni kwa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kuwa miezi kumi na mbili tangu tarehe ambayo leseni imetolewa badala ya utaratibu uliokuwepo wa leseni kufika ukomo kila tarehe 31 ya mwezi Desemba;

iii. kurekebisha vifungu vya 128 na 129 ili kubadilisha tarehe ya ukomo wa kufanya malipo ya ushuru wa bidhaa na ukomo wa ahirisho la kulipa ushuru kutoka siku ya mwisho wa mwezi hadi tarehe 25 ya kila mwezi unaofuata. Madhumuni ya mabadiliko haya ni kuwianisha na tarehe ya uwasilishaji wa kodi pamoja na kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa wakati;

iv. kurekebisha Kifungu cha 132 ili kujumuisha mvinyo unaotambulika kwa *Heading* 22.05 kwenye wigo wa bidhaa zinazotumia pombe kali zenye kilevi zaidi ya **asilimia 80** (ethane) ambapo wazalishaji wa bidhaa hiyo wataruhusiwa kujirejeshea ushuru wa bidhaa (duty offset) uliolipwa wakati wa ununuzi wa malighafi hiyo;

v. kurekebisha Kifungu cha 146A ili kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa inayotambulika kwa **HS Code 2207.10.00** kwenye *Un-denatured Ethyl Alcohol* inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi mathalani uzalishaji wa ladha za vyakula (Food Flavors) kama vile cocoa, vanila, na kahawa; na

vi. kufanya marekebisho ya kutoza kodi katika Jedwali la Nne lenye bidhaa mbalimbali.

**3.1.18. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 kwa kuongeza kifungu (b) ili kuanzisha chuo cha mafunzo ya kodi kwa watumishi wake, wataalam wa kodi na watu wengine wanaotekeleza majukumu ya kodi. Lengo la maboresho hayo ni kutambua kisheria Chuo cha Kodi kilichopo. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu suala hili.

**3.1.19. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Ibara za 8,9,10,11,13,14,16,17 na 18 za sheria hii ambapo Serikali inakusudia kufanya yafuatayo:-

i. kurekebisha kifungu cha 5 ili kuipa Benki Kuu jukumu la kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha na kuongeza masharti ya kuiwezesha Benki Kuu kutekeleza majukumu yake kwa uhuru;

ii. kurekebisha kifungu cha 9 ili kubainisha majukumu ya Bodi ya Benki katika usimamizi wa Benki Kuu, kuongeza idadi ya Wakurugenzi wasio watendaji katika Bodi ya Benki pamoja na kuongeza muda wa wajumbe wa Bodi ya Benki kutoka muda wa miaka mitatu hadi minne na kuweka utaratibu wa kufanya uteuzi wa wajumbe; iii. kufuta na kuandika upya kifungu cha 12 ili kubainisha muundo, ukomo wa muda na majukumu ya Kamati ya Sera ya Fedha na Kamati ya Ukaguzi;

iv. kurekebisha kifungu cha 19 ili kubainisha muda ambao Bodi ya dhamana ya Amana kuweza kutoa dhamana ili kurejesha mtaji wa Benki;

v. kurekebisha kifungu cha 20 ili kubainisha sifa za maafisa walio katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, uteuzi na muda wa utumishi wa Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani; vi. kurekebisha Kifungu cha 38 ili kuwezesha shughuli za uondoaji na uhamishaji wa fedha kati ya Taasisi za kifedha, wakiwemo watoa huduma za fedha kwa njia ya kielektroniki (EMIs), waunganishaji wa malipo (payment aggregators) pamoja na kampuni za teknolojia ya kifedha (FinTechs);

vii. kurekebisha kifungu cha 40 ili kuongeza wigo wa mikopo ya dharura inayotolewa na Benki kwa Taasisi za fedha au mabenki kama mkopeshaji wa mwisho; viii. kurekebisha kifungu cha 60 ili kuainisha wajibu wa Benki Kuu katika uandaaji wa bajeti ya Serikali, Sheria ya fedha na mambo mengine yanayoathiri kazi, majukumu ya Benki Kuu; na ix. kufuta na kuandika upya kifungu cha 69 ili kubainisha vigezo ambavyo Benki inaweza kuruhusu mikopo ya muda mfupi kwa Serikali endapo kutatokea matukio yasiyotabirika au yasiyozuilika na kubainisha

masuala yatakayochukuliwa kuwa matukio yasiyotabirika au yasiyozuilika.

**3.1.20. Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 9 ili kugawa **asilimia 91** ya mapato ya TANAPA ambapo **asilimia 51** itawekwa kwenye akaunti ya TANAPA iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na **asilimia 40** katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vilevile, inapendekezwa matumizi ya fedha kutoka akaunti ya TANAPA yawe yanatolewa kwa kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na pendekezo hili la Serikali baada ya kuthibitishiwa kwamba **asilimia 51** ya mapato yanayobakizwa yanalingana na mahitaji ya fedha ya TANAPA. Hata hivyo, Kamati imeishauri Serikali kufanya uchambuzi zaidi katika mwaka wa fedha 2026/27 kwa sababu kiasi cha **asilimia 51** hakitoshi kuendeleza kwenye miundombinu ya utalii.

**3.1.21. Sheria ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Sura ya 284**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 12 kwa lengo la kuweka mgawanyo wa mapato ya Ngorongoro yanayokusanywa na TRA kama ifuatavyo:-

i. **asilimia 9** itawekwa kwenye akaunti maalum iliyofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania, ambapo **asilimia 3** itakuwa kwa ajili ya Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania; na **asilimia 6** itakuwa kwa ajili ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii;

ii. **asilimia 51** itawekwa kwenye akaunti ya Mamlaka iliyofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania; na

iii. **asilimia 40** itawekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa spika**, marekebisho hayo pia yameweka sharti kwamba, matumizi ya fedha zilizotajwa yatafanyika baada ya kupata kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

## 4.0. MAPENDEKEZO YA MUSWADA AMBAYO YANA MAREKEBISHO YA KAMATI NA SERIKALI IMERIDHIA MAPENDEKEZO HAYO

### 4.1. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikuwa imekusudia kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka **asilimia 17** hadi **asilimia 17.5.** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba ushuru wa bidhaa kwenye mawasiliano Tanzania ni mkubwa kuliko nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki mfano Kenya ni **asilimia 15,** Uganda **asilimia 12**, Rwanda **asilimia 10,** Malawi **asilimia 10,** Botwana na Afrika kusini hawatozi kabisa. Hivyo, kuongeza kiwango hicho kingeleta madhara kwenye kuchochea kasi ya kuelekea uchumi wa kidijitali. Aidha hatua hiyo ni kinzani kwa maendeleo yaliyofikiwa na Serikali katika kuchochea matumizi ya teknolojia.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati ya kuacha kuongeza kiwango kwa **asilimia 0.5** na hivyo itaendelea kutoza kiwango cha sasa cha **asilimia 17** kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, katika sheria hii Serikali imefanya marejeo ya viwango vilivyokuwa vimebainishwa katika Heading zenye **HS. Code 23.03, 22.04, 22.05, 22.06** na **22.08**. Lengo la marekebisho hayo ni kwa sababu awali ilitakiwa marekebisho yafanyike baada ya miaka mitatu yaani ifikapo mwaka 2026/27. Hata hivyo kutokana na changamoto za mapato, Serikali iliamua kubadili viwango hivyo ili kutanua wigo wa mapato na hivyo ilikuwa ni vyema kuweka viwango ambavyo sekta ingeweza kuvibeba. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

### 4.2. Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276;

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Serikali ilikusudia kufanya yafuatayo:-

i. kujumuisha bidhaa zinazotoka ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye wigo wa tozo ya maendeleo ya viwanda kwa ajili ya

kulinda viwanda vya ndani na kuongeza mapato ya Serikali; na

ii. kurekebisha Jedwali ili kutoza tozo ya maendeleo ya viwanda kwenye bidhaa za misumari, vichwa vya kuvuta matrela, samani, marumaru, nondo, mabati, vyombo vya plastiki, hema za chuma na vioo ambavyo vinaingizwa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwekezaji na uzalishaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani kwa kuwa bidhaa hizo zinazalishwa kwa wingi nchini. Hata hivyo pendekezo hili lilikuwa na changamoto zifuatazo:-

i. Mapendekezo ya kujumuisha bidhaa zinazotoka ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye wigo wa tozo ya maendeleo ya viwanda yanakinzana na Ibara ya 19 ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ya mwaka 2009 (East Africa Common Market Protocol 2009). Aidha, hatua hiyo itasababisha vita ya kibiashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki hususan maeneo ya Kanda ya Ziwa kutokana na shughuli za kibiashara zinazofanywa na nchi wanachama katika ukanda huo. Vilevile, hatua hiyo ingechochea uingizwaji wa bidhaa kimagendo nchini na hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki. Kutokana na sababu hizo, Kamati ilipendekeza Ibara ya 44 (b) ya Muswada kufutwa; na

ii. Kamati ilipendekeza kuongeza bidhaa nne katika jedwali ambazo ni *starch* inayotambulika kwa **HS. Code 17.02**; *liquid glucose* inayotambulika kwa **HS. Code 11.08;** karatasi zinazotambulika kwa **HS. Code 4804.11.00, 4804.21.00, 4804.31.00**, **4804.41.00** na **4804.51.00** pamoja na nyaya za mkongo zinazotambulika kwa **HS. Code 8544.70.00**. Pendekezo hili lilizingatia kwamba viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo navyo vinahitaji ulinzi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iliridhia mapendekezo ya Kamati ambapo bidhaa kutoka nchi mwanachama wa Afrika Mashariki zitakuwa zikipewa msamaha na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho la Serikali.

**4.3. *Sheria* ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya marekebisho katika Sheria hii kwa kuongeza kifungu kipya cha 39A chenye lengo la kuongeza jukumu kwa Bodi ya Bima ya Amana (DIB) la kuongeza ukwasi kwa njia ya mkopo kwa benki au taasisi ya fedha yenye changamoto ya ukwasi na ipo hatarini kufilisika. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha DIB kwa kushirikiana na Benki Kuu kunusuru taasisi za fedha zenye changamoto ya ukwasi na zilizopo hatarini kufilisika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kifungu hiki na kuona kwamba ili kuhakikisha benki zilizopokea fedha kutoka DIB zinaimarika, ni vema benki hizo zikawekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu mara baada ya kupokea fedha kutoka kwa DIB. Hivyo, Kamati iliitaka Serikali kuongeza kifungu kidogo kipya kinachozitaka benki zilizopokea msaada wa ukwasi kuwekwa chini ya usimamizi wa karibu wa Benki Kuu ya Tanzania. Serikali ilikubali mapendekezo hayo kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

**4.4. Sheria ya Tozo za Huduma za viwanja vya Ndege, Sura ya 365**

**Mheshimiwa Spika**, maboresho katika Sheria hii yalilenga kuongeza kiasi cha **shilingi 1000** katika tozo inayotozwa kwa kila abiria anayesafiri kwa ndege ili kuendeleza juhudi za kuimarisha huduma ya afya nchini ikiwemo kukabiliana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Vilevile, katika kifungu cha 7 (2) inapendekezwa kuongezwa ili kubainisha mgawanyo wa fedha kutoka chanzo hiki ambapo **asilimia 70** itaelekezwa kwenda Mfuko wa udhamini wa kudhibiti UKIMWI na **asilimia 30** itaelekezwa kwenda kwenye Mfuko wa bima ya Afya kwa wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kwamba kwa mujibu wa Sera za Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), mapato yote yatokanayo na tozo za huduma za viwanja vya ndege yanapaswa kutumika kwa ajili ya kugharamia huduma na kazi zinazohusiana na usafiri wa anga na si vinginevyo. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufuta ibara hiyo na Serikali iliridhia pendekezo la Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

**4.5. Sheria ya Leseni ya Biashara, Sura ya 101**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipendekeza kufanya maboresho katika sheria hii kwa kuongeza kifungu kipya cha 14A ili kumpa Waziri mamlaka ya kuainisha biashara ambazo hazipaswi kufanywa na raia wa kigeni. Lengo la marekebisho haya ni kulinda fursa za ajira za watanzania na kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara kati ya ya watanzania na wageni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na maboresho hayo, hata hivyo uchambuzi wa Kamati ulibaini Sheria hiyo haijatoa tafsiri ya raia wa Tanzania na raia wa kigeni. Kutokuwepo kwa tafsiri hiyo kungesababisha changamoto katika utekelezaji wa Sheria hii. Hivyo, Kamati ilipendekeza Serikali kutumia tafsiri ya neno raia kutoka kwenye Sheria ya Uraia, Sura ya 357. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

**4.6. Sheria ya Bajeti, Sura ya 439**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilipendekeza kufanya maboresho kwenye Sheria ya Bajeti kwa kuongeza kifungu kipya cha 60A kinachoweka sharti la kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha kabla ya kutoza au kubadili ada, tozo, faini na ushuru mbalimbali. Lengo la mabadiliko haya ni kuongeza tija, ufanisi na kuhakikisha yanaenda sambamba na malengo ya sera za fedha pamoja na kuzuia utozaji usiozingatia utaratibu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa kifungu hiki hakikuweka muda maalum ambao Taasisi, Wizara na Mamlaka zinaweza kufanya maboresho ya ada, tozo, faini na ushuru. Hivyo, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati kwa kuongeza kifungu

kidogo kipya kinachompa mamlaka Waziri kuomba ushauri kwenye Kamati ya ushauri wa masuala ya kikodi kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria ya Bajeti. Aidha, Kamati ilipendekeza Serikali kutoa tafsiri ya Wizara ili kuondoa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye masharti ya kifungu hicho. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

**4.7. *Sheria ya Bima, Sura ya 394***

**Mheshimiwa Spika**, katika sheria hii Serikali inakusudia kuanzisha bima ya usafiri kwa wageni wanaoingia nchini kwa kiwango cha **dola za Marekani 44**. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaowezesha kuwalinda wageni wanapokuwa nchini dhidi ya dharura za kiafya, kupotea kwa mizigo yao, na kugharamia wageni wanapoondoshwa kwa lazima au inapotokea na hatari yenye kulazimu uondoshwaji. Mapendekezo ya Serikali yanalenga kutoa msamaha kwa wakaazi wanaotoka nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba hatua hii inaenda kuongeza gharama kwa Watalii na Wafanyabiashara wanaoingia nchini. Hivyo, Kamati ilikubaliana na Serikali kwamba utekelezaji wa vifungu vinavyopendekezwa uanze mwezi Januari 2026 ili kutoa fursa ya kufanya majadiliano na sekta zinazoweza kuathirika kabla ya kuanza kutekelezwa.

**4.8. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 3 kwa kuboresha tafsiri ya msamiati "*permanent establishment*" na "capitalization of profits". Uchambuzi wa Kamati ulibaini maneno hayo hayajaorodheswa kwa mpangilio wa irabu. Hivyo, Kamati ilishauri kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya namba ya kifungu kwa kuzingatia mpangilio wa irabu. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 12 ili kutambua faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa (retained earning) kuwa sehemu ya mtaji. Marekebisho hayo kwa ujumla yatapelekea faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa kutozwa kodi ya zuio kwa kiwango

cha **asilimia 10** baada ya miezi sita. Lengo la Serikali ilikuwa ni kuchochea uingizaji wa mitaji katika shughuli za uchumi na kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua suala hili kwa kina kwa kuangalia nia ya Serikali ya kuzuia ukwepaji wa kodi na kuleta usawa katika utozaji wa kodi ya mapato. Masuala mengine yaliyoangaliwa ni:-

i. kutovutia mitaji na uwekekezaji nchini kwa kuhofia kwamba pale wanapotaka kuongeza mitaji yao kupitia faida ambayo haijagawanywa kwa wanahisa itatozwa kodi;

ii. tafsiri ya maneno *capitalization by profit* yanajumuisha sekta zote bila kuzingatia namna sekta hiyo inavyoendeshwa na madhara yanayoweza kujitokeza mfano sekta ya benki; na iii. endapo lengo la Serikali haiwezi kuzuia ukwepaji wa kodi ya mapato kupitia kifungu cha 8 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 ambacho kinampa Mamlaka Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kuchunguza na kubaini endapo kuna ukwepaji wa kodi na kukusanya kodi ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi huo Kamati ilibaini kwamba kifungu hiki si kipya kilikuwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973. Aidha, Kamati ilibaini Taifa jirani la Kenya lina kifungu kama hicho. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufanya marejeo ya kifungu hicho na kuondoa utata uliopo. Serikali ilikubali na marekebisho yalifanyika kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 4.9. Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi, Na. 6 ya mwaka 2025

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii inarekebishwa katika kifungu cha 2 na 21 ili kuwatambua wawekezaji waliosaini mikataba na Serikali katika sekta ya madini kuwa ni wawekezaji wa mahiri. Aidha, kifungu cha 19 kinarekebishwa ili kuweka masharti yanayobainisha bidhaa ambazo hazikidhi kupata msamaha wa

kodi. Vilevile, kifungu hicho kinatoa msamaha wa ushuru wa forodha kwa kiwango cha **asilimia 75** kwa mwekezaji atakayeagiza bidhaa za mtaji usio asili na atalazimika kulipa ushuru wa forodha wa **asilimia 25**.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina wa madhara yanayoweza kutokea kwenye mapato ya Serikali kwa Sekta ya madini kujumuishwa katika miradi inayoweza kupewa vivutio vya ziada. Kamati iliishauri Serikali kuondoa sekta hiyo na kuacha utaratibu ulivyo hivi sasa ili kulinda mapato ya Serikali. Serikali ilikubali na kufanya marekebisho ya kufuta ibara ya 64 na 66 ya muswada kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

## 5.0. SHERIA AMBAYO KAMATI HAIJAKUBALIANA NA SERIKALI

### 5.1. Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 pamoja na Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikusudia kurekebisha kifungu cha 9(1)(f) cha Sheria ya Msajili wa Hazina na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Fedha za Umma ili kuongeza kiwango kinachotakiwa kuchangiwa na Taasisi na Mashirika ya umma kati ya **asilimia 15 hadi 60** ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kila mwezi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejadiliana kwa kina na Serikali kuhusu suala hili na ikabaini masuala yafuatayo:-

i. hakuna vigezo vilivyowekwa kisheria vitakavyotumika kubainisha ni Taasisi gani au shirika gani lichangie kwa **asilimia 15** au zaidi;

ii. Serikali haikuwasilisha mbele ya Kamati uchambuzi wa kitaalamu uliosababisha kufikia mapendekezo hayo;

iii. mapendekezo haya yanaenda kinyume na maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akipokea gawio la mashirika ya umma ambapo aliagiza yalelewe ili yachangie zaidi;

iv. kuna udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya mashirika na hivyo badala ya Serikali kushughulikia udhaifu huo imekuja na pendekezo hili;

v. hivi sasa kuna baadhi ya Mashirika na Taasisi za umma zinashindwa kuchangia **asilimia 15** ya mapato ghafi hivyo, kupanua wigo ni kuleta changamoto kubwa kwenye Taasisi na mashirika ya Umma;

vi. mchango huo unatokana na mapato ghafi ya Taasisi bila kutoa gharama zozote za uendeshaji. Hivyo, kuongeza kiwango kati ya **asilimia 15** hadi **60** kutaleta madhara makubwa katika utendaji kazi wa Taasisi hizo; na

vii. utaratibu huu unaathiri mtiririko wa fedha kwa baadhi ya mashirika ambayo yanatumia mtiririko wake kukopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na sababu hizo Kamati haikukubaliana na Serikali na imewasilisha jedwali la marekebisho ili Bunge lako lifanye maamuzi sahihi.

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa kwanza Mwanamke wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika, kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu tukufu kwa hekima na uongozi mahiri. Vilevile, nawashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba Madelu (Mb), Waziri wa Fedha na Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wa karibu na mchango wao mkubwa wakati wa kuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, napenda kuwashukuru, Dkt. Natu ElMaamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Ndg. Elijah Mwandumbya Naibu Katibu Mkuu

Wizara ya Fedha, Ndg. Yusuph Juma Mwenda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Dkt. Fred Msemwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango. Pia niwashukuru Makamishna, Wakuu wa Taasisi na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru kwa dhati Mhe. Oran Manase Njeza (Mb), Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati kwa uongozi wake makini. Niwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umakini waliouonesha wakati wa kujadili Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Omar Ali Omar, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe.Yahya Ally Mhata Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho ila si kwa umuhimu, nimshukuru Bw. Baraka Ildefonce Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
25 Juni, 2025

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti kwa wasilisho hilo la maoni ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia, lakini kabla sijaanza kuruhusu hiyo michango, basi wapo wageni ambao wameingia Bungeni baada ya tangazo la awali la wageni.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Yupo mgeni wa Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambaye ni Dkt. Taus Kida, Katibu Mkuu Wizara ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Waziri wa Fedha; Dkt. Natu Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Ndugu Elaija Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Nehemia Mchechu, Msajili wa Hazina; Ndugu Yusuph Mwenda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni wa Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, huyu ni Ndugu Damas Leli, ndugu yake kutoka Bukene mkoani Tabora, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni, ah, hili jina linafanana na Mbunge wa zamani sasa sijajua ndio yeye Mbunge wa zamani au vipi.

Haya, wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 90 na walimu nane wa Shule ya Awali na *Msingi Better Tomorrow* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa heshima uliyonipa ya kuwa mchangiaji wa mwanzo wa kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Ninaomba niseme mambo manne ya jumla.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Serikali imefanya uamuzi wa busara sana kwa kuanzisha vyanzo mahususi ya kukusanya fedha kwa ajili ya kupata mapato kwa ajili ya kugharamia Mfuko Maalum wa UKIMWI na Mfuko wa Bima ya Afya, hili ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka yako mataifa wafadhili, hivi karibuni wamesitisha misaada yao kwa wagonjwa wa UKIMWI na wa Kifua Kikuu. Jambo hili kwa jicho la kibinadamu tunaweza tukaliona kwamba ni jambo baya sana, lakini kifalsafa na mantiki kwangu ninaliona ni jambo ambalo linatujengea moyo wa kujitegemea siku zinazokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mshairi mmoja wa Kiarabu aliwahi kusema, '*Al-khauiru twibat shafii.*' Maana yake ni kwamba matatizo ndiyo chanzo cha mafanikio, lakini Waingereza wana msemo unaofanana na huo wanasema *necessity is the mother of invention*. Mambo au mahitaji ya lazima ndiyo chanzo cha uvumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ninataka kusema nini? Ninachokisema, mwanadamu ana kawaida anapopata matatizo hutafuta njia ya kupata suluhu ya matatizo hayo yanayomkabili.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu unaturudisha zama za Mwasisi wa Taifa letu Mwalimu Nyerere kuwa na Taifa linalojitegemea. Tunapozungumza umuhimu wa kujitegemea, baadhi ya Watanzania wanapata kigugumizi kulizungumza jambo hili. Mimi kwa maoni yangu ninadhani tatizo lao wanashindwa kutofautisha kati ya *self-reliance na self-sufficiency*. Mimi hoja yangu ni *self-reliance* (kujitegemea). Utatumia nguvu za watu wako na rasilimali zako kuleta maendeleo ya Taifa lako na pale ambapo unapungukiwa hutasita kutafuta msaada wa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *self-sufficiency* maana yake utajitosheleza kwa kila kitu na kusema kweli, Taifa la namna hiyo duniani halijaumbwa. Hili ni funzo kwa siku zinazokuja kwamba Afrika haina mjomba tujenge uwezo wetu wa ndani tujitegemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ninaipongeza sana Serikali kwa kutokuongeza kodi ya matumizi ya mawasiliano ya simu. Uamuzi huu unaendana sambamba na dhamira ya Serikali ya kukuza matumizi ya uchumi wa kidigiti, matibabu ya kimtandao, elimu ya mtandao pamoja na malipo ya kutumia mifumo ya kisasa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka tumekuwa tukiitaka Serikali kuwa umefikia wakati matumizi yote yafanyike kwa mifumo ya kisasa badala ya kutumia fedha taslimu. Kwa maana hiyo, uamuzi huu unatufikisha kwenye dhamira hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ninaipongeza Serikali kwa kutokuongeza kodi katika matumizi ya makaa ya mawe pamoja na gesi asilia. Dhamira hii inaenda sambamba na uamuzi wa Serikali ambao tunasisitiza juu ya matumizi ya kupata nishati bora ili kulinda afya za watu wetu, kukuza uzalishaji wa viwandani na pia na kunusuru misitu ili isikatwe hovyo.

Mheshimiwa Spika, jambo langu la mwisho labda ninukuu hapa kabla sijalisema jambo la mwisho, nitanukuu kwa kimombo

ili muktadha wa ninachokisema pengine niwasilishe vizuri hiyo hoja. *There is a delicate balance between our desire to maximize revenue collection and desire to protect local industries and state-owned enterprises.* Kwa tafsiri ya moja kwa moja, kuna uhusiano mwembamba sana kati ya dhamira ya kukusanya mapato, kulinda viwanda vya ndani na kulinda mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, ninataka kusema nini? Uamuzi wa Serikali wa kutaka kila shirika la umma litoe mchango au gawio kati ya 15% mpaka 60% jambo hili mimi ninadhani tuliangalie kwa hekima na busara. Kwa nini ninasema hivyo? Ni kwa sababu nataka tuangalie ni busara gani itatumika au kigezo gani kitatumika ili kitumike kiwango cha chini cha 15% badala ya 60%? Hapa ninaona kama hakuna uwazi.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Wachina mashirika yao ya umma wanayalinda kwa uchu mkubwa. Tunaona mashirika mengi ya reli ya Uchina ni ya umma, mashirika mengi ya umeme ni ya umma, ujenzi ni ya umma, kutafuta gesi na mafuta ni ya umma. Huwezi katika dunia ya leo ya ukoloni mamboleo kama huyalindi mashirika yako ili uweze kuhodhi maslahi ya Kitaifa ya ndani na kupambana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, sasa ninafikiri Serikali hapa itumie busara. Tunataka nini? Nilisema tunataka mapato au tunataka kulinda maslahi mapana ya Taifa hili? Kwa maoni yangu, maamuzi yetu kama Wabunge na kama viongozi, siku zote tuyafanye katika kulinda maslahi mapana ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji ajiandae.

**MHE. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niseme kwamba tunakushukuru sana kwa jinsi ulivyotuwezesha

kufika hapa. Ninaona kama tunafikia mwisho mwisho. Kwa hiyo, ninakushukuru sana na mimi pia nijiunge na wenzangu kukuombea Mungu kule Uyole upite bila tatizo. Tunaamini itakuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba huu Muswada ulikuja kwenye Kamati yetu na mimi ni mmojawapo wa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, na kwa ujumla tu huu Muswada ni mzuri. Tulipoupokea, tulisema ni mzuri japokuwa tumekuwa na mambo ambayo tumelazimika kuyajadili kutokana na mapana yake na *impact* yake kwenye uchumi huu.

Mheshimiwa Spika, pia tulielewa kwamba Mheshimiwa Rais kweli anafanya kazi, ana dira na *vision* kweli ya kusaidia jamii yetu kwa kuona kwamba kusema kweli kuna jambo ambalo limetokea. Suala hili la wabia wetu wa maendeleo kuanza kupunguza au kuondoa kabisa misaada ambayo ilikuwa inakwenda kwenye maeneo haya ya jamii, *particularly* kwenye afya hata kwenye elimu atapunguza na ninaona wanapunguza sana, kwa hiyo, ni pengo kubwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, ni pengo kwa sababu hata kama ilikuwa haiingii moja kwa moja, ilikuja kupitia njia nyingine, lakini ni ukweli kwamba Serikali imefanya uchambuzi wake na imegundua kwamba *impact* inaweza ikawa ni kubwa sana kama Serikali isipotafuta fedha ya kuziba pengo lile.

Mheshimiwa Spika, pengo hilo tulifikiri ni dogo lakini wanazungumza kati 80 *hundred billion* mpaka *even two trillion*. Kwa hiyo, ni pengo kubwa. Tulipopokea hivyo tukaona kwamba kwa namna ya kawaida ingekuwa siyo rahisi tu kama Waziri mwaka uliopita alivyofanya mapendekezo ya kurekebisha sheria chache sana, lakini bahati nzuri amekuja wakati huu amerekebisha sheria nyingi 23.

Mheshimiwa Spika, tumeona nia yake ni kwamba kila mtu achangie mzigo huu ambao sasa ni lazima tuubebe wenyewe. Kila Mtanzania achangie kidogo kidogo, na kweli ukiangalia zile *rates* alivyozileta ongezeko ni kiduchu, kiduchu 0.5% ambayo ni

kidogo au *five percent which is very little compare to what the burden should have been.* Kwa hiyo, ninaamini kwamba Muswada huu ulilenga kweli kila mtu abebe kidogo, tusikaze sana pale ambapo tayari tumekuwa tunapategemea sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, Mfuko huu tukasema kwamba kuwe na vyanzo maalum kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Sasa sisi mwanzoni tukaona kwamba katika pendekezo sehemu kubwa ya fedha ambayo ilikuwa inatafutwa inapelekwa kwenye UKIMWI, tukasema haiwezekani, kwamba mbona huu UKIMWI unaisha lakini sasa tukasema sehemu kubwa iende kwenye Bima ya Afya, lakini sasa walivyokuja watu wa UKIMWI pale wakatuambia kwamba kuna watu wanaoishi na UKIMWI milioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia kuwabeba wale kwa sababu kunahitajika mambo mengi, lishe na nini ni fedha nyingi na tukaambiwa kwamba hela ambayo walikuwa wana *minimum* ni kama *800,000 billion,* na hapa kwenye hivi vyanzo pengine kama ikipatikana kwa bahati *Commissioner General* wa *TRA* akifanya kazi sana pengine atapata angalau hata *five, seventy or six hundred billion.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado siyo kwamba inatosha, lakini ndiyo hapo kwamba hata Kamati ilipokuwa ina-*push* kwamba hiki ondoa na hiki ondoa, tulisema kwamba kwa mfano kwenye ile *issue* ya *withholding tax* kwenye *retained earnings* tulisema hii inaenda kudhoofisha kabisa uwekezaji kwa sababu watu wanaona kwamba sasa *capital is not valued.*

Mheshimiwa Spika, ni kwamba ukipata faida ile faida unatakiwa uirudishe kwenye mtaji, lakini sasa unaambiwa kwamba kutakuwa na *withholding tax* tuka-*push,* lakini baadaye tukaangalia chanzo hicho kilikuwa kinatakiwa kitoe kama shilingi bilioni 130, yaani ukusanyaji kwenye chanzo hicho tu wanaweza wanakadiriwa hivyo, lakini *of course* itategemea sasa kwamba *commissioner general* ataenda kutoa kanuni ya namna gani kwamba huu mtaji, hii *retained earnings* haijatumika, kwa sababu *retained earnings* haipo *in cash or deposit. Retained earnings*

inakuwa tayari imekuwa *invested* kwenye *working capital* na kwenye vitu vingi tu ambavyo inakuwa ni sehemu ya *capital anyway.*

Mheshimiwa Spika, inakuwa ni ngumu sana, lakini ninatumaini wanajua jinsi ya kufanya wataalam wa kodi, jinsi ya kukokotoa, lakini tumefurahi kwamba angalau Serikali imekubali kwamba *okay,* sasa tuseme kwamba ni miezi 12 siyo miezi sita. Kwa hiyo, inatoa unafuu wa namna fulani.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwamba waliweza kuona hilo jambo na wakakubali pendekezo, lakini ninasema kwamba pengine watakapoenda ku-*implement,* wataanza kuona *complication* yake lakini wanaweza wakatumia mbinu hata kama ikilazimika wakatumia *AI* wakaweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo sisi tumefurahia huu Muswada, ni kwamba utaona kilichofanyika kwenye marekebisho ya kodi hizi, kinalenga kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo na hamasa ya kuwekeza, na wale ambao wamewekeza ndani waweze kupata faida kwa kiasi fulani. Pia inahamasisha watu wa ndani kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sasa unaona kwamba wameweza kuweka kuingiza kwenye Muswada huu umuhimu wa Waziri anayehusika kutangaza ni maeneo yapi ambayo watu wa nje wanaweza wakawekeza na ni wapi ambapo hawawezi na ninaamini kwamba hiyo itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, pia tumekuwa tunalia hapa sana kuhusiana na tozo zilizokuwa zinatozwa na mamlaka zinazosimamia sekta mbalimbali na ile tozo utaona kwamba sasa imesemekana kwamba Waziri ameeleza vizuri kwamba sasa kutakuwa na zile tozo zisibadilishwe kiholela lazima zipate idhini ya Waziri anayehusika na masuala ya fedha. Kwa hilo ni jambo zuri sana na ninaamini linaenda kuondoa kero nyingi ambazo tumekuwa tunazizungumza hapa na ninaamini watu wataichukulia vizuri.

Mheshimiwa Spika, utaona pia kwamba kwa mfano kwenye *issue* ile ya vilevi ambavyo vina zaidi ya 80% ya kilevi pale wameamua kupunguza. Mwaka 2024 tulizungumza sana kuhusu hilo ongezeko la kutoka shilingi 2,500.00 mpaka shilingi 7,000.00, sasa hivi wameona walipunguze kwa sababu ninaambiwa kwamba ile hatua haikusaidia sana kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupunguza sasa kunahamasisha uzalishaji wa hii hena kwenye viwanda vyetu na vile viwanda vyetu vitaweza kushindana sasa na *elicit samples* za vilevi vikali hivi na hilo ni jambo linasaidia kwenye upande wa afya na ninaamini hilo ni jambo zuri limefanyika.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba ukiangalia kwa undani zaidi, tulizungumza sana kuhusu dola 44 kama bima kwa mgeni anayeingia Tanzania, tuka-*discourage* sana tukasema hii kusema kweli, hususan kutokana na maelezo kwamba hii bima haiendi kwenye mapato ya Serikali inaenda kwenye mapato ya mashirika ya bima hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, sasa kama haichangii na tunaweka vitu vingi sana, kwa nini tuweke dola 44, ni fedha nyingi. Watu wanafikiri kwamba ni fedha ndogo lakini watalii wetu sio matajiri, wanakuja tu wengine ni wanafunzi, kwa hiyo, ukiongeza dola 44 ni hela nyingi.

Mheshimiwa Spika, japokuwa walisema Zanzibar imefanya vizuri, lakini mimi ninafikiria Zanzibar ni tofauti na Tanzania Bara kwa sababu Zanzibar haishindani, haina ushindani kwa sababu *is a very exclusive* na *it has very different type of environment* ya watalii.

Mheshimiwa Spika, huku kwetu mbuga zetu tunashindana na majirani zetu wote Kenya, Uganda, na Rwanda, wote wana hizi mbuga na wana wanyama walewale. Kwa hiyo, mtalii anapokuja anachagua ni wapi *cheap?* Sasa kama utamwambia uje na bima, na ile bima sisi tukisema kwamba haitasaidia sana au siyo jambo la ajabu sana kwa sababu wale watalii wakija ndani hapa, hata kama kutatokea jambo gumu sana ni kwamba

wanashughulikiwa pia na Mabalozi wao, nao wanakuja na bima zao ambazo ziko kwenye mashirika ya nchi zao.

Mheshimiwa Spika, ninaona kwamba pengine wangeangalia, lakini ninaona bado hili limebaki na tulikubaliana kwenye Kamati kwamba tuliachie tu tuone itakuwaje, lakini baadaye ninatumaini wataacha, lakini wamesogeza utekelezaji wake mpaka Januari, 2026, hiyo nayo itatupa mwanya wa kuangalia zaidi *what is happening*?

Mheshimiwa Spika, kwa kusema zaidi, ni kwamba uhifadhi ambao tunashukuru sana, kule kwenye majimbo yetu, kila mtu na kila Mbunge; mimi ninafuatwa kila siku, watu wengi wanakuja kusema hebu tusemeeni kuhusiana na uhifadhi wa jamii hususan wale wanaolipwa na Hazina. Sasa ninashukuru kwamba wakati huu wamekubali kubadilisha na kuongeza au kuboresha viwango vya pensheni kwa wastaafu ambao wamekuwa wakipata pensheni ndogo sana, kwa mishahara ya miaka ile ya nyuma ilikuwa ni midogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa kama hii imetokea ninashukuru kwamba Waziri atachukua hatua ya kuangalia sasa na ku-*review* na kuona wapate kitu gani kwa sababu hata mishahara ya chini imepandishwa. Kwa hiyo, ninaamini nao watafurahia sana wakiona jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pia tunaunga mkono suala zima ambalo Kamati imeleta marekebisho kwenye jedwali kuhusiana na suala hili ambalo tumefikiri halijakaa sawa. Kwanza kuna maswali mawili kwanza ni hilo la mashirika ya umma kutozwa au ku-*remit between 15% and 60%* ya mapato yao, tukasema kwamba itaharibu sana mtiririko wa fedha kwenye mashirika yale na inaweza ikafanya yakawa na hasara kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa muda ulionipa nami ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya niweze kusimama leo. Ninakushukuru kwa kazi yote ambayo nimeifanya katika kipindi cha miaka mitano, ni kwa rehema za Mwenyezi Mungu ndiyo maana leo niko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti ambao tumefanya kazi nzuri. Ninaomba niishukuru Serikali, wameonesha ushirikiano katika kipindi changu ambacho nimekuwepo Bungeni sijawahi kuona kipindi ambacho Muswada wa fedha umekuja na mapendekezo mengi kama kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuja na mapendekezo mengi, Serikali ilikuwa tayari kukubaliana na ushauri wa Kamati na kuachia baadhi ya mambo mengi, laiti wangekuja wakaweka mguu chini kama ambavyo kwa siku za nyuma ilikuwa Serikali ikija ina uamuzi wake kuja kubadilisha uamuzi ninaamini kazi ingekuwa nzito sana.

Mheshimiwa Spika, pia ni vizuri nikarejea ambayo nimekuwa nikishauri kwamba Bunge tumekuwa tukitumia muda mwingi sana kujadili matumizi lakini tumekuwa tunatumia muda mchache sana kujadili vyanzo vya mapato, inakuwa ni muda mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, unajua tumelazimika kuondoka jana saa saba usiku, na katika hali ya kawaida pale ambapo mnaongelea juu ya chanzo cha mapato kukianzisha au kukiondoa Serikali huwa lazima waseme wafanye utafiti juu ya hicho chanzo ambacho kinapendekezwa au pale mnaposema kiondolewe chanzo hiki kwa sababu wametumia muda mwingi kufanya utafiti,

wanauliza je, tukiondoa hiki wapi tutapata kwa ajili ya kuziba pengo?

Mheshimiwa Spika, bajeti kama inavyojulikana lazima kuwe na *balance* kati ya mapato na matumizi. Kwa hiyo, ninaendelea kushauri kwa siku za usoni muda wa kujadili *finance bill* sisi kama Bunge tuhakikishe kwamba unapatikana muda wa kutosha. Pia suala hili linahusu Wabunge wote, kwa hiyo, ni vizuri kukawa na semina mahususi kwa Wabunge ili kujua *essence,* tunapokuwa tunajadili suala zima la kuhusu tozo na kodi kwa sababu moja kwa moja inaenda kugusa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nijielekeze katika Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini Sura 276. Tulijadiliana na Serikali, na mawazo ya Serikali ni mazuri sana. Kwanza, tunataka kulinda viwanda vyetu. Ni jambo jema, lakini pia sisi kama Taifa, Mwenyezi Mungu ametujalia nchi kubwa.

Mheshimiwa Spika, ukisema kwamba utalinda kiwanda kwa mfuko wa saruji ambao unazalishwa Dar es Salaam, halafu mfuko huo wa saruji unataka ukatumike katika shughuli za ujenzi Mwanza, ambapo ukisafirisha mfuko wa saruji kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza ni shilingi 12,000.00, maana yake ni kwamba unataka mtumiaji wa Mwanza agharamie hizo gharama za usafiri ili ajenge nyumba yake.

Mheshimiwa Spika, sasa kama mfuko wa saruji unauzwa Dar es Salaam shilingi 15,000.00 ukiongeza gharama za usafiri shilingi 12,000.00 maana yake unataka mtu wa Mwanza anunue kwa shilingi 27,000.00 *if I am not mistaken,* lakini bado hata mfanyabiashara hakuna mtu ambaye anafanya kazi bila kuweka *profit margin,* akiweka na faida yake je, mwananchi wa Mwanza ataweza kujenga kwa kutumia saruji ambayo imezalishwa Dar es Salaam? Hesabu zinakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ni ukweli usiopingika kwamba hii mipaka na majirani zetu *these are just colonial boundaries,* lakini mwananchi aliyepo Mwanza na mwananchi aliyepo Musoma hana tofauti na mwananchi aliyepo upande wa pili wa majirani

zetu. Kama hesabu zote zipo sahihi, hii mipaka ambayo tumewekewa ni kwa ajili ya utawala lakini linapokuja suala la maendeleo, hakuna mwananchi ambaye atakuwa tayari auziwe bidhaa kwa tofauti kubwa hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri ni nini? Pamoja na kwamba Serikali wana-*take measures* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wana-*curb* hilo, namna pekee ya kuweza kuhakikisha kwamba jiografia ya nchi yetu tunafaidika nayo, ni kwa ajili ya kutoa *incentives* kwa wale ambao wanataka kwenda kuanzisha viwanda maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kama mtu anataka kwenda kuanzisha kiwanda cha saruji Mwanza, mpeni kivutio ili asilazimike kuanzisha kiwanda Mkuranga, asilazimike kuanzisha kiwanda Pwani kwa sababu anajua kwamba kwanza ana *advantage* ya bandari.

Mheshimiwa Spika, sasa huyu ambaye anajitosa leo kwenda kuanzisha kiwanda Mara huko, Mwanza au Kagera lazima kuwe na kivutio maalum ambacho kitamsukuma aweze kwenda kuanzisha kiwanda kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine nitatoa na tulipata wazalishaji wa saruji. Kwa mwananchi kwa kiwanda ambacho kiko *Mbeya Cement* ambacho kinategemea kupata *clinker* kutoka Dangote Mtwara huko au kutoka Tanga. Ile *Clinker* ikisafirishwa mpaka kufika Mbeya kwa vyovyote vile gharama ya uzalishaji wa mfuko mmoja wa saruji itakuwa ni kubwa hivyo viwanda hivi haviwezi kushindana. Kwa hiyo, *scenario* kama hizo kama Taifa lazima tuweke pamoja tutazame huyu ambaye anaanzisha kiwanda sehemu ambayo mali ghafi ziko mbali tunamlindaje ili aweze kushindana katika hali ya usawa?

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa ambazo inasemekana sasa hivi jirani zangu wa Kigoma hawapo hapa, lakini nimeambiwa sasa hivi saruji inaingia kutoka *DRC* inakuja Kigoma. Kwa nini? Kwa sababu kiwanda kimeenda kimeanzishwa *DRC* mpakani kule kwa hiyo inakuwa ni rahisi kuingiza saruji, kupeleka Kigoma na ukauza

kwa bei nafuu, lakini siku za nyuma saruji ilikuwa inauzwa Kigoma kwa bei kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri Serikali waka-*balance* hizi hesabu ili tusije tukawaumiza watu wetu. Watu wetu wanataka kujenga haijalishi hiyo *raw material* ambayo anaitumia imezalishwa ndani ya nchi na itakuwa ni rahisi. Kwa mipaka ilivyo tukisema kwamba tutatumia *measure* zingine kuzuia ni jambo ambalo siyo rahisi. Ukanda wa ziwa jinsi ulivyokuwa na mipaka yetu ilivyo *porous* si rahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali hizi *measures* ambazo wanazichukua ni za muda, lakini ili tuwe na uhakika juu ya jiografia yetu na jinsi ambavyo mtawanyo wa rasilimali unakuwepo lazima kuwe na *incentive* katika wale ambao wanaenda kuanzisha viwanda maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pia, bidhaa ziko nyingi. Huwezi ukamlazimisha mtu wa Kagera aache kununua bidhaa ambayo inatoka Uganda na wananchi wetu wanapiga hesabu analinganisha kipi ambacho kinampa nafuu kwake anaenda huko. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali tuhakikishe kwamba, tunanufaika na *geographical position* ya nchi yetu na kwamba tunapakana na mipaka mingi na pia tuhakikishe kwamba, bidhaa zetu zinaendelea kuwa na ushindano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia itifaki, kwa busara zaidi ukiona mwenzako hafuati itifaki unamshtua kwamba hicho unachofanya sicho; tumekubaliana ukatekeleze hili, mwenzangu hukutekeleza. Vipi unataka mimi vya kwako niweze kuvilinda wakati wewe vya kwangu hutaki kuvilinda?

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano, Serikali imekubaliana kwamba, katika hali ya kawaida inampa mamlaka Kamishna kwa kuangalia *case by case,* lakini bado *essence* ya kulinda viwanda vyetu iko pale pale. Ni vizuri tukatumia cha kwetu lakini iwe *relative,* iwe kwamba; je, ninapotumia cha kwangu ninapata fursa ipi ambayo ninaona kama ni *advantage*

kwa kutumia cha kwangu, lakini si kwamba ni uzalendo uwe wa kuumizana tu, haiwezi ikawa sawa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo kama Kamati tulipata fursa ya kujadiliana na Serikali ni suala zima la bima na ametoka kulisema Mheshimiwa Dkt. Kimei hapa. Ni jambo jema kuwa na bima na hasa ambayo inalenga hawa watalii, lakini sisi kama Kamati katika majadiliano tuliwaambia Serikali katika hali ya kawaida mtalii anapokuja, *booking* zinafanywa *in advance* siyo kwamba eti ni kama mtu unaanza safari ya kwenda Dar es Salaam leo unasema unapanga kesho unaondoka; hapana. Hizi safari zinakuwa zimeuzwa mapema.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru Serikali kwa kukubaliana kwamba, ni vizuri kwa kushirikiana na wadau wajadiliane ili tusije tukapoteza fursa na kazi kubwa nzuri ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais katika *Royal Tour.* Unajua sasa hivi utalii unaanza kuongezeka kwa kasi kubwa sana. Sasa tusije tukaanzisha mambo ambayo yatahakikisha tena tunaanza kurudi nyuma. Si vizuri kama Serikali kuja kufanya makosa hayo, lakini ninaamini kwa mapendekezo ambayo tumekubaliana kwamba yanaenda mpaka mwezi Juni 2026, tayari watakuwa wamefanya *consultation* na wadau na kushirikishana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa usikivu wa Serikali hii ninaamini tutakuja na *trade off* kuhakikisha kwamba kile ambacho tunakusudia kama Taifa tunapata na vilevile hatuumizi *industry* hii.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida niombe nirudie tena, kama Wabunge tupate fursa ya kutosha na tushirikishane. Hatuwezi kwenda kama majirani ambao wanatoa Muswada wa Fedha miezi mitatu, lakini tuone ni muda gani ambao utatosha. Hii habari ya mchakamchaka haina afya sana.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Jambo la pili, ninaomba niwashukuru wenzetu wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli kazi hii inahitaji muda mrefu sana. Kaka yangu hapa amesema kwamba tunatumia muda mfupi sana kwenye kujadili vyanzo, lakini tunatumia muda mrefu sana kujadili matumizi, *he is very right*.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nianzie pale alipoanza kaka yangu kwamba, siku zote tunapojaribu kutafuta vyanzo vipya vya mapato maana yake ni lazima tunapima faida na hasara hasa kwa mwananchi wa kawaida. Sasa ninaomba niungane na mwenzangu hapa kwamba, jambo hili linahitajika lifanyiwe kazi kwa muda mrefu sana siyo tu kama hivi Mheshimiwa Waziri amekuja kusoma pamoja na kwamba Kamati imekaa, lakini hata Kamati wenyewe wamesema hapa wamekaa mpaka saa nane za usiku jana, wamekubaliana ku-*compromise* baadhi ya mambo, lakini hii yote ni nini maana yake? Tumefanya kwa sababu tumetenga muda mfupi sana wa kujadili vyanzo vyetu hivi. Kwa hiyo ningeomba hili tuliangalie vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili sasa niende kwenye Muswada huo ningependa tuanze kwenye ukurasa wa tisa kwenye Ibara ile ya 22 wanasema inapendekeza kurekebisha kifungu cha nne ili kuziondolea mamlaka ya utozaji leseni uwezo wa kufunga biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninaomba niwapongeze sana Wizara ya Fedha kwa sababu sisi kama Bunge, lakini sisi kama Serikali tulitakiwa kujua kwamba wafanyabiashara wanapofanya biashara kuna suala la kupata na kukosa. Pia, liko suala la kupeana muda ili tuone mfanyabiashara ana-*take time* lakini ana-*comply* na sheria ili kuja kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa zamani kule miaka kama nane mpaka tisa iliyopita tulikuwa tunatumia nguvu sana bila ya kujua

kwamba, hawa wanaolipa kodi wanajenga Taifa kwa hiari yao. Wafanyabiashara hao wanapotozwa kodi wanalijenga Taifa kwa nguvu zao kwa sababu kwa asilimia kubwa sisi kama Serikali hatuwasaidii moja kwa moja wafanyabiashara hawa, lakini wanajitoa kwenda kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hili walilolifanya Wizara ya Fedha la kwamba eti kwa sababu mtu hakufanikiwa kulipa kodi unakwenda kumfungia duka anayekosa ni Serikali inayokosa ni Taifa siyo yule. Kwa hiyo, hapa Mheshimiwa Waziri kwa kweli ninataka nimpongeze sana kwani wanafungua macho sana kuweza sasa kutekeleza sheria hii kwa sababu wenzetu hawa wanadhani kwamba kufunga biashara ni kumkomoa mfanyabiashara, *it is not;* ni kulikomoa Taifa. Kwa hiyo, ninaomba hapa akodolee macho sana ili tuweze kufikia azma hii kwa sababu hawa ndiyo kwa kweli wanaojenga Taifa kwa kutoa damu na jasho lao ili Taifa liweze kusonga mbele; ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo ningependa twende kwenye ukurasa wa 10 pale kwenye Ibara (c) inasema Ibara ya 29 kama ilivyorekebishwa inarekebisha kifungu cha 126 ili kwanza kufuta pendekezo la kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye huduma hizo zote hizo. Sasa Mheshimiwa Waziri hii ni baada ya tathmini yenu kubwa sana kwa sababu siyo Serikali inapata kwenye kuongeza tu hata inapopunguza inasaidia ku-*activate* watu wengine wengi waweze ku-*comply* na sheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninaomba nimpongeze na timu yako kwa kweli hapa wamefikiri; hii inaitwa ni *big brains.* Kwa hiyo, kwenye hili wamefanya kazi kubwa sana kwa sababu Serikali haipati kwenye kuongeza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwenye ukurasa wa 14(4) kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia tano kwenye *ice cream* zinazotengenezwa chini ya kutumia kakao au malighafi nyingine. Ninadhani hapa tumekwenda haraka sana kwa sababu *ice cream* hiyo hiyo inapoletwa kutoka nje kwa *component* hizo hizo za kutumia *vanilla* tumeongeza kodi, lakini kwa ya ndani tumepunguza kodi. Sasa, kinachoniumiza huku chini

anasema sababu pale ukienda kifungu cha 8 anasema ushuru wa bidhaa kwenye hili anasema sababu kubwa ni kwamba, inaleta madhara.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninauliza hivi? Hivi madhara yanaletwa kwa kutumia vanilla inayotoka nje tu, hii ya ndani siyo madhara? Labda waje watusaidie maana hii nimeshindwa kuelewa, watusaidie baadaye. Inawezekana *vanilla* ya ndani haina madhara, lakini *vanilla* ya nje ina madhara; hili watusaidie nitapata kujifunza maana yake inawezekana ni vitu tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye ukurasa wa 15 kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye gesi. Sasa wametaja pale 0.45 mpaka 0.55. Sasa hiyo sina tatizo nalo, tatizo langu liko hivi; lengo la hatua hii ni kulinda thamani ya fedha kwa kuwa kiwango cha sasa hakijabadilishwa kwa takribani miaka nane na hakiendani na hali ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na hili lakini hoja ya kwamba eti hatujabadilisha bado hawajajenga hoja. Kuweka nyongeza ya kodi eti kwa sababu hatujabadilisha miaka nane halafu na kitu chenyewe sasa ni kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye gesi asilia huku tunahamasisha ili wananchi watumie gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaongeza ushuru lakini huku wanasema kwa sababu hatujabadilisha zaidi ya miaka nane. *I don't see the logic.* Inawezekana sikuelewa vizuri lakini wenzetu watusaidie *logic* hasa ya hapa ni nini? Kwa sababu huku tunataka watu watumie gesi kwa sababu mama anapambana kuhamasisha na amegawa mitungi ya gesi mingi sana hapa. Lengo ni kuhamasisha wananchi watumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningefurahi kama tungepunguza ili kuhamasisha badala ya kuongeza halafu ukasema sababu hatujaongeza zaidi ya miaka nane. Ninadhani watusaidie wenzetu hapa, inawezekana sababu haikuwa hii watuambie sababu. Kama iko sababu nyingine *fine,* lakini kwa sababu hii ina-

*contradict* na mawazo ya Mheshimiwa Rais kwamba, kuhamasisha wananchi wajitokeze zaidi badala ya kutumia miti watumie gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba twende kwenye *page number* 14, kwenye *page* hii; ok ninadhani hiyo ndio nimeizungumza. Twende kwenye *page number* 15, kutoza ushuru kwenye kiwango cha 10% kwenye sabuni. Sasa, hapa hoja yangu siyo kuongeza kodi ni kweli lengo letu ni kuvilinda viwanda vyetu vya ndani, lakini tusisahau kwamba, kuna vitu viwili au vitatu vinasaidia. Kwanza, tuna bidhaa zinazotoka kwenye *community* yetu ya *East Africa* na kwenye *SADC,* lakini kuna bidhaa zinatoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu hapa siyo tunalinda tu, tuangalie na *quality* zinaendana? Kwa sababu lengo letu ni kumlinda pia *consumer.* Kwa mfano, utakapotumia bidhaa ya kupiga mswaki (sitaki kuitaja jina) iliyotengenezwa na sisi na ukatumia bidhaa nyingine iliyotoka nje unagundua kuna tofauti. Kwa mfano, kuna madini mle ambayo ukiyatumia kwa asilimia ndogo *end of the time* unaweza ukapata maradhi na kuna *ISO,* ninadhani wenzetu wanatumia wanaelewa wataalam kwamba, *quality* hizi zinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninadhani tuangalie *quality* ya bidhaa, lakini tuangalie na madhara yanayoweza kupatikana. Kwa hiyo, tusilinde tu viwanda vyetu lakini tuangalie; je, hizi athari zinalingana? Kwa hiyo, watusaidie tuvilinde, lakini viwe vinaweza kushindana na viwanda vingine kwa ubora wa bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba niendelee kidogo, pamoja na kwamba lengo lengo letu ni kulinda, pamoja na kwamba lengo letu ni kusaidiana; nimeona hapa wenzetu wameweka kodi maalum kwa ajili ya kupambana na maradhi ya UKIMWI. Ninawashukuru na kuwapongeza sana, lakini sijaona na tumezungumza kama miaka miwili, mitatu nyuma kule; je, athari ya mazingira tunatafutaje hela?

Mheshimiwa Spika, ningedhani na hili waliangalie wenzetu kwa sababu mazingira yanatuathiri, hatujatafuta hiyo hela kwa

sababu wenzetu duniani kule wanaondoa hela hii kuja kwetu. Sasa sisi tutaipata wapi? Kwa hiyo, ninadhani hapa wangetafuta *time* vizuri wakaona je, mazingira tunayapatia pesa gani ukiacha kusaidiwa kule nje? Kwa sababu ni wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho nimeona hapa wenzetu wameongeza kodi kwenye bidhaa za tumbaku hasa kwenye vifaa vya eletroniki ambavyo vinasababisha athari. Ninadhani wenzetu wanaelewa, *issue* siyo vifaa tu vile hata hii sigara ya kawaida bado inatupa madhara na tuliwahi kusema anayetumia tumbaku, anayezalisha na hata yule anaye-*process* tu. Hebu na hili tuone tunasaidiaje wananchi kuwapunguzia madhara ambayo yanasababishwa na tumbaku. Inawezekana lazima Serikali inatengeneza hela, lakini kwa upande wa pili Serikali inasababisha watu watumie tumbaku na yenyewe inaleta madhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninadhani na hiki kiwe chanzo cha kusaidia ili angalau kuwafanya wananchi wapunguze matumizi ya tumbaku kwa kuongeza kodi japo asilimia ndogo itusaidie kupunguza maradhi kwenye hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kuna Mjumbe yeyote wa Kamati ya Nishati na Madini hapa Bungeni? Kuna tofauti gani kati ya ile gesi tunayotumia majumbani (nishati safi ya kupikia) na hii gesi asilia iliyoongezewa ushuru?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, tofauti yake ni kwamba, gesi asilia kwanza inazalishwa Tanzania, lakini shida yake kubwa ni nini? Ni usafiri ndio tunachoona ni kama vile wanataka kuongeza mzigo kwa sababu ile gesi asilia ni kwamba, lazima isafiri kwa bomba na ikisafirishwa kwa gari halafu bado ikawekewa gharama kubwa za kodi hatari yake ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, hii gesi asilia kwa mfano Mheshimiwa; samahani kidogo. Gesi hii ambayo ni *LPG* kodi yake kwanza ni kubwa na gharama inayouzwa hapa sasa hivi ni kubwa pia.

**SPIKA:** Ngoja tujishughulishe na hii kwanza; sasa ukituchanganya wewe Mjumbe wa Kamati. Hoja iliyopo mezani ni kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye gesi asilia.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, hilo ndiyo tatizo.

**SPIKA:** Je, hii gesi asilia ndiyo ile tunayopikia au ni tofauti?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, hapana ni tofauti.

**SPIKA:** Haya basi umeshajibu swali, ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete. *(Makofi)*

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata hii fursa kuweza kutoa mchango kidogo. Kabla ya mchango nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika ambaye baada ya siku chache Bunge litavunjwa na tutarudi majimboni na wewe utarudi katika lile Jimbo jipya la Uyole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba, hakuna mashaka hata kidogo utashinda zaidi ya 100% kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya kwenye Bunge letu kwa miaka hii mitano lakini ni zaidi ya mitano kabla ya kuwa Spika, ulikuwa Naibu Spika. Umefanya kazi yako vizuri na ulipokuwa Spika umefanya kazi yako vizuri sana sana tena sana na kazi nzuri hiyo ndio iliyokuhakikishia kupata Uspika wa Mabunge ya Dunia. Tunawataka wana Uyole wasikupoteze na wamesema hawawezi kukupoteza; hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nilikuwa nisichangie, lakini nikasema ngoja niombe nafasi kuchangia. Kikubwa zaidi kilichonishawishi kuchangia kwanza, ni kuipongeza sana Serikali

kwa usikivu wake mkubwa. Pale ambapo pamestahili kuongezwa kodi imeongezwa na pale ambapo pamestahili kupunguza kodi vilevile wamepunguza kwa maslahi mapana ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kimenishawishi, tunatambua na tunajua Taifa lolote ulimwenguni haliwezi kuwa na ustawi uliokuwa bora kama afya zake haziko barabara. Afya hizi zinakuwa si bora kutokana na mambo kadhaa ukiachia magonjwa, lakini kuna vitu vingine vinaweza vikaachika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, matumizi ya sigara na matumizi ya vinywaji. Hivi vyote vinaweza kuachika. Kitu kikubwa kwenye hili nilisikia kuna kitu ambacho walizungumzia kuhusiana na hivi vinywaji vya kuongeza nguvu kwa sababu kabla ya hapo viwanda vyetu vya ndani vilikuwa havitozwi kodi, lakini leo wameweka eneo la kuwatoza kodi na msingi wa kutoza kodi hiyo ni kuleta manusura kwa ajili ya vijana wetu wa Tanzania na watu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini wamefanya hivyo? Kwa sababu Serikali ni sikivu wanataka tuwe na Taifa lililokuwa bora, wanataka tuwe na Taifa lililokuwa imara, wanataka tuwe na vizazi ambavyo vitaishi miaka mingi na siyo miaka michache, vijana wa miaka 13, 28 na katikati hapa kabla ya miaka 35 vijana wanapoteza maisha yao. Kwa hiyo, nimesimama kupongeza hilo kwa ajili ya kuangalia vijana wa Taifa la Tanzania kutokana na madhara yanayotokana na *energy drink. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaipongeza sana Serikali na ninaishukuru sana Serikali. Pia, ninakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, ninakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza vilevile Wabunge wenzangu na vilevile kwa sababu ninaamini leo ni siku yangu ya mwisho kuzungumza nikiwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; sidhani kama nitapata nafasi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena kuwapongeza Wanalindi wote, Wabunge wa Lindi wote ninawapongeza kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya na hasa ninawapongeza Wanamchinga kwa kuniamini kusimamia shughuli zao na Wanamchinga wanasema hawana wasiwasi hata kidogo na Salma Rashid Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka tu kama hakutatokea lolote wanasema Mama Samia Suluhu Hassan mitano tenaaa; Mama Salma Rashid Kikwete, wanasema mpaka aache mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza, Mwenyezi Mungu awabariki. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sijajua ni wangapi majimboni wanaambiwa mpaka waache wenyewe, lakini tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu yetu ya kwanza kukutana kwa siku ya leo, mchana tutakuwa na wachangiaji wafuatao:-

Ataanza Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu akifuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Rashid Abdallah Rashid, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Ali Hassan King na Mheshimiwa Simon Songe. Kwa hiyo, hao wote watachangia tutakaporejea hapa Bungeni jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni leo.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025**
***(The Finance Bill, 2025)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Reuben Nhamanilo atafuatia, Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo ya kuchangia huu Muswada wa Fedha wa mwaka 2025. Kwa kuwa, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ambayo ilishughulikia Muswada huu ninapenda niseme kwa haraka na kwa mara moja kwamba, ninaunga mkono huu Muswada wa Fedha wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia nichukue fursa hii kukushukuru sana Mheshimiwa Spika wetu kwa namna ambavyo umetuongoza. Tangu Bunge hili limeanza tumeweza kupitia *Finance Bill* mbalimbali, lakini kupitia mwongozo wako tumeenda vizuri na Serikali na kama nilivyopata kusema kwa kweli, Serikali yetu ya Awamu ya Sita ni Serikali sikivu.

Mheshimiwa Spika, licha ya kwamba, kwenye Kamati tunakuwa na majadiliano ya muda mrefu na kubishana kwa hoja, lakini mwisho wa siku tunakubaliana kwa maslahi ya Taifa na inakuwa inasikiliza. Kwa hiyo, hongera sana kwa Serikali chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri. Nikupongeze

sana Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, nimpongeze Naibu wako, Mheshimiwa Chande, nimpongeze Katibu Mkuu, Dkt. Natu, Katibu Mkuu wa kwanza kabisa mwanamke ndani ya hii Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, amefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Manaibu wake wote akiwemo Naibu tunayekuwa naye, Mwandumbya, kwa kazi nzuri ya kufafanua kifungu kwa kifungu. Ninapongeza taasisi zote za fedha chini ya hii Wizara ya Fedha ikiwemo Mamlaka ya Mapato *(TRA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwa kweli, tunapojadili *Finance Bill* hii, tukitoka kupitisha bajeti yetu ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa kishindo kwa zaidi ya 98%, ninaamini ni rekodi ya juu kabisa tangu mfumo wa vyama vingi na tangu Serikali yetu ya Awamu ya Sita imeingia madarakani. Tumekuwa tukipitisha bajeti kwa 95%, 92%, lakini mwaka huu 2025 ni 98%; sababu ni tumeona licha ya kwamba, ni jambo la Kikatiba, lakini Wabunge tumeridhika Serikali yetu inaleta bajeti ambazo zinatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka tulipoanza mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti ilikuwa ni shilingi trilioni 36.66, lakini mwaka huu 2025 tumepitisha bajeti shilingi trilioni 56.49 ongezeko la zaidi ya shilingi trilioni 19. Jambo hili linahitaji pongezi za dhati na kwa kweli, tuna Rais ambaye amejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo za awali nilitaka kusema tozo zote ambazo zimeainishwa katika Sheria mbalimbali za Fedha na ambazo zimeainishwa kwenye Muswada huu, mabadiliko yaliyowasilishwa yalizingatia kuwezesha biashara kutekelezeka vizuri, ili kuwezesha mapato kuongezeka. Kwa hiyo, nianze kwa kushukuru na ninaunga mkono, lakini ninataka niseme tu kwa mfano Sheria ya Korosho, Sura ya 203; niishukuru Serikali kwa kuwezesha mapato yatayokusanywa kutokana na tozo ya kuuza korosho ghafi nje ya nchi *TRA* ikikusanya iyapeleke moja kwa moja kwenye akaunti ya Bodi ya Korosho.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni nzuri, itakuja kuisaidia tasnia ya korosho. Hapa nitoe tu shukrani kwamba, licha ya tozo hii

ambayo itakuja kusaidia, lakini Serikali imekuwa ikisaidia kulima korosho kwa kutoa pembejeo bure, tunaishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tupongeze mabadiliko kwenye Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 371, kwa namna ambavyo Serikali imeleta pendekezo la kumpa dhamana Waziri wa Fedha kuhuisha masuala ya viwango vya pensheni wakati muafaka kwa idhini ya Mheshimiwa Rais. Tumeona hii ni baada ya muda mrefu kupita, lakini kipekee kwa namna ambavyo Serikali, kupitia bajeti hii imeongeza pensheni kutoka laki moja mpaka laki mbili na nusu ya wazee wetu wastaafu, hongereni sana na imekuwa kipindi kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze ubunifu wa Serikali yetu, tumepata changamoto ya namna ambavyo Sera zimebadilika kwa wabia wetu wa maendeleo. Baadhi wamepunguza misaada kwenye afua mbalimbali za afya ikiwemo ugonjwa wa UKIMWI, lakini Serikali hii imejitanabaisha, inaendelea kupambana na adui maradhi kwa kuleta vyanzo vipya, kwa ajili ya kuchangia huu Mfuko wa UKIMWI na pia, kuchangia bima yetu ya afya.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako tulipata fursa pia ya kuwasikiliza wenzetu wa *TACAIDS* namna gani wana nakisi kubwa kutokana na mabadiliko hayo, lakini kwa namna ambavyo Serikali imeendelea kuwa *stable*. Imeendelea kujipanga na kuhakikisha kwamba, inawezekana tukapambana na janga hili kwa kutumia mapato ya ndani, bado tatizo ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vyanzo vilivyoainishwa ninataka niwaombe Watanzania wenzangu kuendelea kuvipokea ikiwemo tozo kwenye tiketi zetu za ndege, tozo kwenye tiketi zetu za treni na tozo kwenye masuala ya mafuta. Ni tozo ndogo, lakini zinaweza kutusaidia. Kwa kuwa tunaenda kuanza jambo la bima ya afya kwa mara ya kwanza kwa kupitia nyongeza ya vyanzo hivi, nina imani Watanzania, hasa zile kaya ambazo ni maskini ambazo tayari zimebainishwa zaidi ya milioni moja na laki mbili zinaenda kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa namna ambavyo Serikali tumekubaliananayo kwenye hii Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Tulikuwa na mjadala mzito wa *retained earnings*, lakini ninataka niseme Serikali kwa kuja pia na pendekezo la kuruhusu kampuni kudai riba yote, kama gharama ya biashara, jambo ambalo linawasaidia kupanua mitaji yao. Kwamba, watakapokuwa wanakokotoa faida Serikali imewaruhusu kuingiza riba yote. Kwa hiyo, kwa kupitia kipengele hiki ambacho Serikali ime-*forgone* zaidi ya shilingi bilioni 200 niishukuru sana na mabadiliko aliyofanya kwenye *written earning* hii nahisi kwamba, Serikali imekuwa sikivu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ninapenda pia, kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imesaidia kuhakikisha huu mpango mkakati wa nishati safi ya kupikia unawafikia Watanzania wengi kwa kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi ya *petrol, LPG,* ambayo kwa kweli, tumeiona, kasi ya mitungi tunaiona. Kwa hiyo, kwa hatua hii ninaamini akinamama wa Tanzania ambao nimepata kuwawakilisha Bungeni kwa vipindi vitatu, akinamama wa Mkoa wa Pwani, watafikiwa na hiyo mitungi kama ambavyo Serikali imejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru pia Serikali kwa kuwa sikivu kwa kuhakikisha kwamba, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, inabaki *rate* ile ile 17%, kama ambavyo tumeishauri Kamati kwa niaba ya Bunge. Sambamba na hilo niombe sasa, mwishoni ninapokaribia kumaliza kwamba, Serikali wamewasilisha bajeti ya shilingi trilioni 56, ni hela nyingi, lakini kati ya hizo mapato ya ndani ni zaidi ya shilingi trilioni 40 na kati ya hizo Mamlaka ya Mapato *(TRA)* mmeipa zaidi ya 80% ikusanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni tumeshuhudia jitihada kubwa za kuiwezesha *TRA* kwa kazi nzuri; Mheshimiwa Spika mwenyewe umemsifia Kamishna Mkuu, Bwana Yusuph Mwenda, Waziri wa Fedha umemsifia. Pia, tumeona hata juzi Mheshimiwa Rais alipofungua ofisi ile ya Simiyu, tunaona ndiyo ofisi zinazojengwa mikoa yote; ombi langu ni Wizara ya Fedha kushirikiana na Wizara nyingine katika utekelezaji wa shughuli zao ili kufungamanisha masuala mazima ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Wizara ya TAMISEMI ina nafasi, mimi nimewahi kutembelea mipaka mbalimbali ya nchi hii ambako kuna fursa za biashara. Niliwahi kwenda Buhigwe, tukatembelea Kata ya Kilelema, lakini kuna changamoto ya barabara, kilomita 15 tu, ambayo inaunganisha na Nchi ya Burundi ambako wananchi pale walikuwa wamehitaji ile barabara ili waweze kufanya biashara na watu wa Burundi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaamini kwa mikakati ya namna hiyo ambayo Serikali inaiweka ya kuwezesha masuala ya mipaka na maeneo ambayo yanapakana na Bahari ya Hindi, maeneo ambayo yanapakana na Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, Serikali ikiwezesha sekta zingine kufanya kazi iliyokusudiwa, miradi ikatekelezeka itaiwezesha hii Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya mapato kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru Watanzania kwa kulipa kodi. Tumeona kodi yetu imetumika vizuri na ndiyo maana tunasema kwamba, hatuna deni na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na tumejipanga kumpa kura anazostahili kwa kazi nzuri aliyoifanya kupitia bajeti mbalimbali zinazopitishwa ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwako nikutakie kila la kheri kwa michakato inayoendelea kwenye Jimbo lako jipya la Uyole. Wewe utaingia kwenye rekodi kuwa Spika wa Bunge hili la Kumi na Mbili lililofanya kazi nzuri zaidi ambayo imevunja rekodi na kwa Bunge ambalo lilikuwa Spika wa Kwanza Mwanamke kutoka Bara la Afrika kuwa Rais wa Mabunge ya Dunia, umetuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wanawake wa Mkoa wa Pwani ninawashukuru kwa kunipa fursa ya kuwatumikia ndani ya Bunge hili, nimewawakilisha vizuri. Ninaamini nimefanya mrejesho kwa namna ambavyo Serikali imetutendea haki, lakini pia, ninaamini kwa namna ambavyo watanitakia baraka katika michakato inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hiyo hoja. Hongera sana Serikali kwa kazi nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, atafutia Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nijumuike na Wabunge wenzangu kuchangia hoja iliyopo mbeleni yetu. Hoja ya Muswada wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo kwa kipindi chote cha miaka minne amekuwa akileta bajeti hapa Bungeni kwa maana ya Miswada hii tunayoijadili. Miswada ambayo imelenga kuwainua wananchi wa chini, kulinda uchumi wetu na kuyajali makundi maalum kwa kuyapa nafasi za upendeleo kupitia sheria hizi za Kikodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano miwili iliyopo ndani ya sheria hii ambayo nikielelezo thabiti juu ya haya ambayo yamekuwa yakifanywa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuyajali makundi ndani ya jamii yetu na kuyapa nafasi ya upendeleo kupitia Sheria zetu za Kodi. Ukisoma Ukurasa wa 35 wa Muswada wa Fedha uliokuwa umewasilishwa na Serikali, unaofanya marekebisho kwenye *Income Tax Act Cap.* 332, Ibara ya 59C, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia Muswada huu na Sheria hii ninayoitaja inayofanyiwa marekebisho anafuta kodi ya mapato kwa Maafisa Usafirishaji, maarufu kama bodaboda. Anafuta kodi ya mapato tofauti na awali ilivyokuwa, ambapo kwa mwaka mmoja kila bodaboda, kwa maana ya kila pikipiki, ilitakiwa kulipiwa kodi ya mapato shilingi 65,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajaji walitakiwa walipie kodi ya mapato shilingi 120,000 kwa mwaka. Kwa kawaida fedha hizi walikuwa wakilipa kwa awamu, kila baada ya miezi mitatu wanalipa *installment,* baada ya miezi sita wanalipa *installment,* baada ya miezi tisa wanalipa *installment* na mwezi Desemba

wanalipa *installment.* Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali kundi kubwa la vijana ambao ndiyo wamejiajiri kwenye maeneo haya, kama Maafisa Usafirishaji maarufu kama bodaboda na kwenye bajaji, amefuta kodi hii ya mapato, ili vijana wetu waimarike katika ajira hizo kujipatia vipato wao wenyewe. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria hii sisi kule Handeni vijana wangu, wananchi wenzangu, wa Kata ya Mabanda kwenye Kijiwe cha Bodaboda pale Mganduni watanufaika na hii. Ukija Njiapanda kwa Baya vijana wa bodaboda ambao wamejiajiri kwenye sekta hii wananufaika na msamaha huu wa kodi ya mapato ambao Dkt. Rais Samia Suluhu Hassan ameutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo ukienda kwenye Kijiwe cha Chogo pale stendi ndani ya Jimbo la Handeni Mjini, vijana wa bodaboda wananufaika na msamaha huu au na eneo hili la kodi ya mapato. Hivyo hivyo ukienda kwenye kijiwe maarufu pale kwa Nyeti, kijiwe maarufu pale kwa John Shayo pale kona, mpaka Stendi ya Nguu kwa ujumla vijana wote Jimbo la Handeni Mjini ambao wamejiajiri kwenye bodaboda na bajaji na pia, vijana wote wa Tanzania katika mikoa na wilaya zote wanakwenda kunufaika na Sheria hii ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta hapa Bungeni sisi tuiridhie, ili wananchi hawa wapate kunufaika.

Mheshimiwa Spika, hizi ni kazi za Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi za Chama Cha Mapinduzi, chama dola, chama kinachoongozwa na Serikali. Chama chenye Ilani yenye kujali makundi ndani ya jamii, kama ambavyo Sheria inathibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni sheria ya pili ambayo inaonesha umakini wa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuyajali makundi maalum, makundi ambayo yana uhitaji ndani ya jamii yetu. Amekuwa akifanya hivyo kwa miaka minne kupitia Sheria za Kodi anazoleta hapa, ni Sheria ambayo inafanyiwa marekebisho, *amendment of the Tanzania Commission for Aids Act cap. 379.*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuanzisha vyanzo vya mapato, kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania wenzetu. Watanzania wenzetu ambao wameathirika na ugonjwa wa UKIMWI kwenye eneo hili tunakwenda, kama nchi, kukusanya shilingi bilioni 576 na maeneo ambayo yanakwenda kuguswa umeyaelezea vizuri Mheshimiwa Subira.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kugusa kidogo tu maeneo ya madini, usafiri wa anga, mawasiliano, vilevi, usafirishaji, shughuli za viwanja vya ndege, michezo ya kubahatisha, kwenye nishati pamoja na eneo la mafuta. Ni muhimu sana Watanzania popote ambapo watakutana na ongezeko la bei kwa hakika wajue tunafanya jambo hili, kama sehemu ya uzalendo wa kuwahudumia wenzetu ambao wana tatizo hili kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu eneo hili la UKIMWI tunao Watanzania milioni moja na nusu ambao wanatumia dawa za UKIMWI. Hiyo ndiyo kusema katika Watanzania milioni 61 ni dhahiri ukitafuta uwiano unaongelea habari ya Mtanzania mmoja kwa kila watu 40, huu ni uwiano ambao nimeufanya hapa. Sasa kama nchi ni muhimu sana, ndiyo maana Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja na wazo hili na sisi hapa ni lazima tuliunge mkono sheria hii lazima tuipitishe, ili tukawahudumie wenzetu ambao wamekumbwa na tatizo hili. Wenzetu ambao ni baba zetu ndani ya familia, ni watoto wetu tunaowapenda, ni waume zetu, ni wenza wetu, tukawahudumie kupitia Sheria hii ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ameileta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizopo Mfuko huu unaoitwa *Aids Trust Fund* umekuwepo toka zamani, *actually* toka mwaka 2001, wakati *TACAIDS* ikianzishwa ndiyo Mfuko huu pia, ulianzishwa, lakini 95% ya fedha ambazo zimekuwa zikienda kwenye Mfuko huu zimekuwa zikitoka kwa nchi ama mashirika wahisani. Sasa kutokana na kubadilika kwa Sera ndiyo maana tunalazimika kuwa na Mfuko wetu huu, kwa maana ya kuweka fedha kutoka kwenye vyanzo vyetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka tunatekeleza Mpango wa Kitaifa, Mpango wa Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI. Kwenye huu mpango wa miaka mitano, huu mwaka tulionao ndiyo wa mwisho wa mpango huu. Mpango kwa ujumla ulihitaji karibu Dola za Kimarekani milioni 986, mpaka sasa tumeshapeleka karibu shilingi trilioni 1.1 ya Kitanzania kwenye mpango huu na bado tuna *gape* kidogo, kwa ajili ya kukamilisha huu mwaka. Ndiyo maana Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja na mapendekezo haya ili Watanzania wenzetu wasiende wakakosa huduma hii ambayo ni muhimu kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni nini Mfuko unafanya? Nini Mfuko huu unafanya kwa fedha hizi tunazokwenda kuzikusanya? Tunakwenda kununua dawa kwa ajili ya wagonjwa ili zikahudumie wagonjwa wenye upungufu wa kinga mwilini (UKIMWI). Ukiangalia gharama za sasa, kila Mtanzania katika wale 1,500,000 wanaotumia dawa hizi, tunagharimu dola 178 kwa kila mtu. Ni fedha nyingi kwa mwaka mzima. Vile vile tunakwenda kupitia Mfuko huu ili kununua dawa kwa ajili ya magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu kwa sasa, Mfuko huu ulikuwa unatumia bilioni 5.1 kwa ajili ya dawa ya magonjwa nyemelezi kama ilivyo Kifua Kikuu. Tunakwenda kufanya nini na makusanyo haya? Tunakwenda kuendeleza huduma za upimaji afya kwa ajili ya kubaini maambukizi ya *virus* vya UKIMWI. Kwa hiyo, ni shughuli za muhimu ambazo zinakwenda kufanyika. Ndiyo maana nikasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mtu muungwana, mtu rahim, kiongozi anayejali watu na kiongozi mwenye kuziishi shida za Watanzania na mwenye kuhakikisha anamjali kila Mtanzania ambaye ana matatizo na ambaye anaguswa na jambo lolote ndani ya jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Mfuko huu tunakwenda kuhakikisha kwamba tunaendelea kukusanya takwimu. Licha ya wafadhili kusitisha kutupa fedha, bado Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuhakikisha tunakwenda kuendelea na kukusanya takwimu na kufanya tafiti kwa ajili ya magonjwa nyemelezi pamoja na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, tunakwenda kuendelea na ununuzi wa kinga kama ilivyo mipira ile inayotumika kwa ajili ya kujikinga, lakini vilevile tunakwenda kuendelea na kuhudumia vituo karibu 33 vya madereva wa masafa marefu kwenye eneo hili kwa kuwapatia huduma hizi za kujikinga au kuendelea kutumia dawa kwa ajili ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike? Kwamba bajeti ya wafadhili imeondoka na sisi tumependekeza vyanzo vyetu ambavyo vinatuletea bilioni 576; kwamba zinaweza zisitoshe. Ni nini tufanye ili fedha hizi zitoshe, au hata kama zinapelea zipelee kidogo?

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni lazima tupitie upya muundo na shughuli za Mfuko huu. Yale mambo ambayo tunayaona kwamba tunaweza tukayaacha na kuyaweka pembeni, tupitie upya ili tubaki na yale mambo ya msingi, tuweze kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Rashid Abdallah Rashid ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hii *Finance Bill* iliyoko mbele yetu. Ninaungana na wenzangu kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika hiki kipindi chake cha miaka minne. Ameweza kufanya kazi nzuri, fedha nyingi sana zimekuja katika miradi yetu hata zimepunguza kwa kiasi kikubwa zile changamoto ambazo zimekuwa zikiwasumbua Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nitazungumzia tu mambo kama matatu hivi ambayo yanahusiana na huu Muswada. Suala la kwanza ni pale ambapo tumekuwa

tukiiambia Serikali, tukiiomba kwamba katika haya mashirika yetu tumeona na tumeomba kwamba ikiwezekana yawe yana-*retain* kama 60% kwa ajili ya shughuli zao. Serikali inaendelea kusema kwamba basi ikiwezekana kiasi hicho kipungue na huo ndiyo msimamo wao.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu mfano mdogo, nilikuwa ninaangalia hapa kwenye takwimu tu za *TANAPA*. Yaani *TANAPA* nimeangalia kwa mwaka huu peke yake, katika bajeti waliokuwa nayo kufikia sasa ya bilioni 49, ni bilioni tisa peke yake ndizo walizopewa. Kwa maneno mengine ni kwamba, katika hiki kipindi kifupi wamepewa chini ya 20%.

Mheshimiwa Spika, sasa matokeo yake ni kwamba, leo ukienda pale *TANAPA* ni kati ya mashirika ambayo yanadaiwa sana na watu mbalimbali; wawe wazabuni, wawe ma-*supplier*; lakini hata shughuli zao zenyewe wanashindwa kuzifanya. Kwa hiyo, ninadhani hili Serikali ni vizuri ingeliangalia, kwamba wakati mwingine sisi wenyewe tunaua mashirika yetu ambayo tumeyatengeneza kwa muda na kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na msimamo wa Serikali, basi ni vizuri Waziri angeangalia kama kuna namna ya kurekebisha aweze kukubaliana na yale mapendekezo ili tuendelee kunusuru hizi taasisi zetu.

Mheshimiwa Spika, la pili ni hili suala hili la Sheria ya Udhibiti na Uingizwaji wa Bidhaa Nchini ya Sura ya 276, ambako Serikali ime-*introduce* Tozo ya Maendeleo ya Viwanda. Imesema vizuri, na Mheshimiwa Waziri amesema vizuri kwamba lengo kubwa lilikuwa ni pamoja na kulinda viwanda, kwa maana kwamba kulinda viwanda vyetu; ambalo sisi wote tunakubaliana. Kwamba, ili tuweze kuendelea watu wetu wapate ajira, ni pale ambapo tunapoweza kufika mahali tukalinda viwanda vyetu. Kwa maana ya kwamba tunaponunua bidhaa nyingi kutoka nje tafsiri yake ni kwamba ajira tunapeleka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na lengo hilo zuri wakati mwingine kuna *measures* ambazo tunazichukua badala ya

kulinda ndiyo tunaendelea kuwapa watu wengine *burden* kutokana na huu ulinzi wenyewe. Kwa mfano, leo ukiangalia viwanda vingi kama kule Kanda ya Ziwa havipo. Kwa sababu viwanda vingi kule Kanda ya Ziwa havipo maana yake ni kwamba, leo bidhaa nyingi sasa, takriban zote, zinatoka huku Dar es Salaam, zinatoka Pwani, zinatoka Tanga, Morogoro kuelekea kule Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni haya; kwamba leo kama *cement* Dar es Salaam utakuta inauzwa shilingi 13,000 hadi 15,000, lakini ukienda Musoma bei ya *cement* ni shilingi 27,000; maana yake una-*double*. Kutokana na sababu kwamba Serikali inaendelea kuvilinda viwanda, maana yake ni kwamba wale wawekezaji waliowekeza huku ambapo ni karibu na bandari hawawezi kuwa na *appetite* ya kuweza kupeleka viwanda *Lake Zone* kwa sababu moja tu. Anajua kuwa Serikali itamlinda; na kwamba, hata lile soko la kule nalo ataendelea kulipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na hali hiyo maana yake ni kwamba tukubaliane kimsingi; tunalinda viwanda vyetu vichache kwa *expense* ya Watanzania wengi ambao wanaendelea kupata kule tabu. Kwa hiyo na hili nalo; kwa mfano, bidhaa kama nondo na misumari, ukikuta bei ya huku na bei ya kule inakaribia mara mbili. Bei yake ni kama nilivyosema; kwamba tunashindwa kuwashawishi au kuchochea; kwamba mtu anashindwa kuwa na hamu ya kuwekeza kule kwa sababu anajua kwamba lile soko lake liko pale, ni *limited* na ataendelea kulifaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukubaliane basi, kwamba leo tunapochukua hii hatua ambayo tunadhani kwamba ni ya kulinda viwanda, ni lazima tukubali kwamba tunachochea ile biashara ya magendo kule nayo iendelee kufanyika. Kwa sababu mtu akiangalia tu na akilinganisha; kwa mfano mtu aliyeko pale Tarime na aliyeko pale Musoma; akilinganisha bei za Musoma akalinganisha na bei pale mpakani ni dhahiri kwamba lazima bidhaa nyingi *smuggling* itakuwa inafanyika. Kwa hiyo, Serikali badala ya kupata mapato basi ndivyo itakavyokuwa inaendelea kupoteza mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaendelea kuishauri Serikali kwamba, pamoja na kwamba Waziri alifika mahala au Serikali imekubali ikasema inampa mamlaka Kamishna wa *TRA* ili aweze kutumia busara. Kwamba, aangalie, pale panapokuwa na maslahi ya umma aweze kuruhusu. Sasa, maana yake ni kuwa hii ni *optional*. Kwamba akiamua anaweza kusema aweze ku-*exempt* lakini asipoamua maana yake ni kwamba wale watu wataendelea kula gharama kwa ajili ya *expense* ya kuvilinda hivi viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninadhani Serikali yetu na Mheshimiwa Waziri wangetumia busara sana ili watu wetu wawe huru katika kufanya shughuli zao kuliko huu utaratibu ambao wameutumia. Yawezekana leo Kamishna huyu yupo anaweza kuwa na nia nzuri, lakini kesho mwingine akilala vibaya basi maana yake ni kwamba wale watu wetu wataendelea kuwa kupata *burden*, lakini na hivi viwanda haviwezi kuhangaika kuhakikisha kwamba vina-*invest* kule. Kwa hiyo na hilo nalo ninadhani waliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ninataka kulichangia, hili Mheshimiwa Waziri alilizungumza wakati wa hotuba yake. Lile suala pale kwenye kipengele cha uvuvi. Aliweza kusema hivi, kwamba Serikali imeweza kupunguza ushuru wa uingizaji wa samaki kutoka dola 2.5 mpaka 1,300. Ukisema dola 2.5 unazungumzia kama shilingi 7,000 hivi na kitu. Sasa, umepungua kutoka 7,000 mpaka 1,300, maana yake ni kwamba, anayeingiza samaki hizi aina ya vibua hizi amepata *discount* zaidi ya shilingi 5,000.

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni nini? Kwanza wale samaki wanaovuliwa kule bahari kuu unakuta ni zile meli kubwa zinakwenda kule, zinatafuta wale samaki wao wanaowataka wa gharama kubwa kama wale *tuna* na wengine, kwa hiyo hawa wengien wanavuliwa kama *byproduct.* Sasa wakishavua, leo tunapopunguza zaidi ya shilingi 5,000 maana yake ni kwamba wale samaki sasa watakuja humu. Wakija humu watasambaa mpaka hata huko Musoma kwa sababu gharama zao zitakuwa chini. Sasa matokeo yake ni kuanzia tu mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameweka fedha nyingi sana kwenye vizimba kule Ziwa Victoria na vijana wetu wanapata ajira. Kwa kufanya hivyo matokeo yake tukubaliane tu kimsingi; kwamba zile ajira ambazo vijana wetu walikuwa wanazipata kule ziwani sasa zile ajira nazo tunakwenda kuziua. Kwa sababu hizo ajira tunakwenda kuziua sasa hata zile fedha ambazo Serikali imewakopesha wale wananchi au wale watu wetu kule vizimba, zitakuwa si kazi rahisi sana kuzilipa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ninakumbuka kwamba kabla ya vizimba kwenda bei ya samaki kule kanda ya ziwa ilikuwa shilingi 12,000 kwa kilo kwa sababu samaki walikuwa wachache sana. Kutokana na hivyo vizimba vichache ambavyo tumevi-*introduce*; kwa mfano, pale kwangu nimepata vizimba visivyopungua 33; na kwa baada ya hivyo na maeneo mengine ya Mwanza, Geita na Bukoba kule nao wamepata; matokeo yake ni kwamba, kwa muda mfupi sana vimeongeza uzalishaji. Leo ukienda pale Musoma samaki unapata mpaka kwa shilingi 7,000 kwa kilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tafsiri yake ni nini? Kama kweli lengo kama walivyosema hapa kwamba kuna upungufu wa samaki, tulichopaswa kufanya ni kitu kidogo sana. Serikali ilipaswa tu iongeze fedha ili vizimba vingi vipatikane. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri mwenyewe alisema kuwa mpaka hivi sasa tunatumia asilimia mbili tu ya maji. Kumbe kama tungeongeza vizimba vingi kwa muda mfupi ni kwamba tungeweza kupata samaki wa kutosha na hili tatizo tulilonalo lingeweza kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninadhani, ni vizuri na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri jana ameniambia kwamba wamepunguza mpaka 1.25. Ni jambo jema kama wangeweza kuondoa na hiyo ingechochea watu wengi zaidi kuwekeza kule ili watu wetu wengi waendelee kupata ajira kuliko ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya. Mheshimiwa Rashid Abdallah Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. RASHID ABDALLAH RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii, nafasi ambayo kwa Bunge hili nami ninasema inawezekana kwamba ni ya mwisho, tutasubiri kuanzia Novemba ambapo tutarudi na inawezekana kiti changu kikawa hiki hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na anayoendelea kuifanya. Ni imani yangu kwamba kwenye Tanzania hii hakuna jimbo hata moja wala kata hata moja ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hajaweza kufika na kutekeleza kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, naye kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuijenga Zanzibar. Kule tumeona juzi pale kwenye mkutano mkuu taarifa iliyotoka ya utekelezaji kwamba Ilani imepitilizwa. Kwa hiyo, ni jambo la kumpongeza sana sana sana Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika tumpongeze naye Waziri wetu wa Fedha hapa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa kazi kubwa ya usimamizi wa Wizara hii na kuhakikisha kwamba kila mwaka na tunaona, bajeti yetu inakua na hairudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumpongeze Kamishna Mwenda naye kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Kamishna huyu ni kamishna wa mfano na nimwambie Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwamba hapa amepata Kamishna. Kamishna huyu tulikuwa naye Zanzibar alikuwa anafanya kazi kubwa sana na alikwenda kunyanyua mapato kwa kiwango kikubwa mno na ni Kamishna ambaye alikuwa hana ugomvi na wafanyabiashara. Wafanyabiashara wote walikuwa ni marafiki zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna wilaya hata moja katika wilaya 11 za Zanzibar ambazo hakwenda na kukaa na wafanyabiashara na kuwasikiliza shida zao ni nini. Matokeo yake baada ya kazi kubwa aliyoifanya, sasa kuja kuwa Kamishna Mkuu wa *TRA* Tanzania. Kwa kweli na yeye anastahiki sana maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba Muswada huu wa Sheria ya Fedha wa 2025/2026 ambao tunataka kuupitisha leo, kwa usimamizi wa Waziri wetu wa Fedha chini ya kiongozi huyu Kamishna wa *TRA*, Muswada huu sasa utafanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Kufanikiwa kwa Muswada huu ni sisi Wabunge katika maeneo yetu na sisi tuwe na utayari wa kuhakikisha kwamba kodi zinalipwa, kodi zinasimamiwa vizuri. Kwa sababu tunasema kwamba kidole kimoja hakibanji chawa. Kwa pamoja tukishirikiana basi kodi zinaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nianze na jambo lingine, hili la suala la leseni hizi za biashara. Kwenye Muswada huu kwenye Ibara ya 23(14) kuna sheria hizi za usimamizi wa leseni za biashara. Kwenye usimamizi wa leseni za biashara ninashukuru sana na ninaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli jambo hili likienda kutekelezwa litaweza kuleta tija kubwa na litaweza kuleta ajira kwa watu wetu. Kwa sababu kama ambavyo wadau wengi walikuja kwenye Kamati na kuomba; ziainishwe biashara ambazo zinaweza kufanywa na wawekezaji na biashara ambazo zinaweza kufanywa na wazalendo wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, tunaona Kariakoo Wachina wamecharukwa sana. Pamefikia hadi Wachina hata dawa za kunguni wanauza wao. Kwa kweli haistahiki kabisa kufanya jambo lile. Sasa, Muswada huu kupitia Waziri anayeshughulika na biashara tunaomba aende akalisimamie vizuri jambo hili ili Watanzania walio wengi waweze kufanya biashara na kuchukua mizigo hiyo huko kwa wafanyabiashara hao ambao na wao wanajifanya kama ni wafanyabiashara wa rejareja ili kutokomeza jambo hilo na wao wawe wamewekewa misingi ambayo

wataweza kufanya biashara kwa mujibu wa uwekezaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka nilizungumzie ni suala hili la *energy drink* ambalo limezungumzwa hapa; kwamba kuna shilingi 132 ambazo zitakatwa kwa lita moja ya *energy drink* kwa hizi za ndani. Sasa, hapa niiombe sana Serikali na nimwombe Waziri wa Fedha, jambo hili bado tuendelee kuliangalia kwa kipindi kichajo, kwamba wazalishaji hawa wa ndani wa hizi *energy* ni vyema tukapunguza kidogo, lakini zile za nje zikiwemo *Red Bull*, zile zinaweza zikapandishwa kwa sababu, *ingredients* ndani ya *Red Bull na energy drink* siyo sawa. Uboreshwaji wao wa kutengenezwa kwa kopo na sisi kwa kutumia plastiki haijawa sababu ya hizi kuziongeza na zile tukaziacha katika ile bei yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivi tutakuwa tunavizorotesha viwanda vyetu. Kwa hiyo, niombe sana hapa kwamba suala hili kwa kipindi kinachokuja basi tulirekebishe wazalishaji hawa wa ndani waweze kufanya kazi kwa uhakika na kuona kwamba wana tija na ajira kuongezeka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika suala hili kitaalam tunawasikia wataalam mbalimbali wakizungumzia suala la *energy drink* na athari zake kiafya. Kwa hiyo hilo siwezi kulisemea sana, lakini ninachoomba kama kuna maneno hayo na kama kuna sababu au kuna tatizo lolote la kiafya ni vyema sasa kwa wasimamizi wa biashara hizi basi kukawa na tangazo kama lilivyowekwa la sigara linalosema "Uvutaji wa sigara ni hatari kwa afya yako."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na hii ni vyema kwamba *energy drink* nayo kukawa kuna *sticker* ambayo imesema unywaji wa *drink* mbali na kukusaidia kwenye nguvu, lakini ni hatari kwa afya yako. Kwa hiyo, baada ya maneno hayo niunge mkono hoja na ninakushukuru sana na wewe pia nikuombee dua katika Jimbo lako la Uyole uende kupita kwa kishindo kikubwa. Juzi tulikuona pale ulikuwa na *function* ambayo ilikuwa hawa vijana wa leo

wanasema ni *function* ya kibabe kabisa, Uyole yote uliikusanya pale ninakutakia kila la heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini sijawakosea wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani. Ninaamini na wewe huko unapofanya sala zako niombee nirudi hapa uje uniapishe niwe Mbunge kwa awamu nyingine ili mambo haya yasonge mbele, kwa hayo machache ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Wiki iliyopita wakati tunachangia bajeti hii na leo tunachangia Muswada *(bill)* ni lazima tuwe wa kweli namna ya kuwapongeza wenzetu kwa majukumu makubwa ambayo wanafanya na mazuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu kaleta bajeti hii ya shilingi trilioni 56.4 kwa ajili ya Watanzania, amefanya kazi kubwa kwa kipindi kilichopita kwenye majimbo yetu yote yamefanyiwa kazi kubwa sana na tunamwombea sana. Kubwa ambalo nilisema kipindi kilichopita na leo ninalisema ni hawa watu ambao wamekuwa wakimchora mara hivi, mara hivi, Watanzania tunatakiwa tuungane kuwalaani sana kwa namna wanavyofanya. Ni Rais anayeheshimika Tanzania na nje ya nchi anaheshimika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nilisema Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na timu yake Naibu Mawaziri wote wa Mpango pamoja na yeye na Profesa pamoja na vitengo vyake vyote vikiwepo Kamishna na Hazina kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana. Jambo ambalo linaonesha hapa kulikuwa kuna hoja mbalimbali za wafanyabiashara ambazo Serikali leo zinaonesha zimejibiwa baadhi na nyingine ninadhani wataendelea. Jambo hili ni lazima tupongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na timu yake kwa kuitikia lile jambo ambalo wafanyabiashara walikuwa wanalalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninataka nichangie mambo mawili tu leo; moja ni hili la Misitu *plot No*.57. Kamati ya Bajeti imefanya kazi nzuri sana sana kuishauri Serikali, sasa hapa kulikuwa kuna mkulima wa kawaida yaani huyu ambaye amelima misitu yake, ameitunza kwa miaka 10 mpaka 15 kulikuwa kuna 3.5% ambayo alikuwa anatakiwa kulipa. Baada ya Kamati ya Bajeti kulizungumza hili, Serikali imekubali kupunguza na kuwa asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu ni nini? Mkulima huyu ni mtu wa kawaida kabisa ambaye misitu yake ameitunza kwa miaka 10 mpaka 15 na anapovuna kuna kodi hapa za *TFS* na za halmashauri, ninadhani wakati wanaendelea kulitafakari hili kwa wakulima wetu litaleta malalamiko makubwa sana na sisi ndiyo wawakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba aidha pamoja na kushukuru kupunguza kuwa asilimia mbili, basi tuwe na asilimia moja au iondoke kwanza tukatoe elimu halafu ndiyo iingizwe kodi hii. Vinginevyo huyu ni mtu wa kawaida kabisa ambaye ana eka zake moja, mbili, tatu. Niombe wenzetu watusikilize hili na wakulima wakubwa wa misitu wapo Nyanda za Juu Kusini (Njombe, Songea, Mbeya, Rukwa, Morogoro na Iringa) ndipo ambapo wakulima hawa wa kawaida mwenye eka mbili, tatu na kadhalika na nini. Ninaomba jambo hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tunaishukuru Serikali kulinda viwanda vya wawekezaji wa ndani ambao wamewekeza na wa nje ambao wamewekeza viwanda hivi hapa, lakini vipo vitu vingine vigumu, kwa mfano, kuna viwanda ambavyo vimeanza kuzalisha magari hapa nchini, sasa tunasema magari (*truck)* hizi kubwa, malori kuagiza kutoka Uingereza na mahali pengine bei iko juu, sasa wenye uwezo wa kununua magari mapya ni wa ngapi?

Mheshimiwa Spika, hawa wanakwenda kununua kwenye hivyo viwanda Watanzania walio wengi hata Wabunge humu ndani wapo ambao wana uwezo wa kununua magari haya ambayo yanatoka Uingereza ambayo yana bei ndogo? Viwanda

hivi ambavyo vinazalisha hapa, vinazalisha magari ya aina moja, ni magari ya Kichina peke yake. Zipo *Scania* hazizalishwi hapa, zipo *IVECO* hazizalishwi hapa, zipo *DAF-MAN* hazizalishwi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipenda roho mwingine imani yake anataka *Scania,* sasa huyu ndiyo unamwekea bei juu na uwezo wake watu wengine wanaagiza gari moja, gari mbili. Kununua gari moja hapa kwa hizi zinazotengenezwa hapa pamoja na *trailer* ni sawa na kuagiza gari karibu mbili, tatu za kutoka Uingereza. Ninadhani jambo hili Serikali iliangalie kwa upana na kwa makini ili watu wote wa Tanzania watendewe haki waweze kuagiza magari kwa haya ambayo hayatengenezwi hapa nchini. Kwa yale ambayo yanatengenezwa nje huko aina ya haya ambayo watu wamewekeza hapa hayo sawa, hayo mtu akiagiza sawasawa kodi iwe tofauti, lakini haya ambayo hapa Tanzania hayatengenezwi ninadhani hilo liangaliwe sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wakati tunachangia hapa kwenye bajeti ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwamba tuna maboma ambayo wananchi waliyajenga kule katika maeneo yetu, yakiwepo ya afya, shule za msingi na sekondari na kumbi mbalimbali za sekondari kwa ajili ya chakula, niombe Serikali ihakikishe fedha hizi zinapofika mwezi Julai ziende ili zikafanye kazi kama ambavyo wananchi tulishawaahidi kule; kwamba baada ya kufika kwenye *lintel* Serikali itapokea kuhakikisha maboma haya yanamaliziwa, yakiwepo ya Jimbo la Makambako, Jimbo mwanana kabisa ambalo mwenyewe mzungumzaji nipo hapa. Niombe sana fedha ziende ili zikafanye kazi hiyo ikiwemo vituo vya afya nivyovitaja siku ile na leo kwa sababu nafasi bado ninayo.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya pale Kivavi, ambacho tunaomba fedha iende ikaweze kujenga kituo hicho, lakini kuna Kituo cha Afya Kitandililo ambacho kinafanya kazi kuna fedha ambazo zinatakiwa kwenda kwa ajili ya kwenda kumalizia. Kuna Kituo cha Afya pale Ikelu tunaomba fedha iende kinafanya kazi iende zikamaliziwe, lakini tuna Kituo cha Afya Usetule, Kata ya Mahongole na mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nilisemee, bajeti iliyopita ya mwaka wa fedha 2024/2025 ilikuwa shilingi trilioni 50 na ushee, bajeti hii ya leo ina shilingi trilioni 56 na mabii (mabilioni). Sasa hapa ndipo unapoona, tunaposema Rais wetu ametupa fedha nyingi, sasa hapa ndiyo tunapotamka, mabii (mabilioni) na mabii (mabilioni) na matii (matrilioni) siyo kitu kidogo.

Mheshimiwa Spika, lazima tumpongeze sana Rais na watu wanaobeza wakati fulani wanasema, tunasema fedha ametoa Rais, kila kitu ametoa Rais, sasa nani anayetoa au anayeidhinisha? Hii *bill* hapa tukishapitisha nani anakwenda kuidhinisha kule? Si ndiyo yeye. Watu wasibeze vitu ambavyo vina ukweli. Sisi kwenye maeneo yetu tunasema Mheshimiwa Rais, kila kijiji kila kata amefika kwa sababu ya utambulisho wa miradi ambayo ipo kule, ni lazima tupongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamekuombea, siku ile nimesema kurudia si vibaya kwa sababu dua inasemwa kila wakati. Unajua na wewe unaheshimika unatupa heshima ya Tanzania, unatupa heshima duniani kwamba kutoka Afrika (Tanzania) tuna Spika wetu. Sasa ombi letu Watu wa Uyole (Mbeya) tunawaomba huyu mtu ametupa heshima, heshima hii ni pamoja na Uyole, Mbeya ni pamoja na Watanzania wote na nje ya nchi. Kwa hiyo, tunakuombea sana kwa dhati kabisa Wabunge kama unavyoona wamekuwa wakikuombea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na timu yako umepata Makamishna wote katika vitengo vyote vya kukusanya kodi, kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Mwigulu katika jimbo lako pamoja na Mpango, Profesa na Naibu Mawaziri wake hapa kwa kweli hawa ni timu moja, tunawaombea sana ili waweze kurudi waweze kuwatekelezea Watanzania kwa mambo mbalimbali wanayofanya. Kwa sababu haya wanayoyafanya ni ya manufaa na faida kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Ali Hassan King, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, pamoja na Waziri kwa hatua kubwa sana ya kuona umuhimu wa kuwapunguzia tozo watu wa bodaboda. Kwa kweli umefanya kazi kubwa sana, kwa sababu hawa ni matajiri wetu wa baadaye tunawalea ili wakue, watoke kwenye bodaboda baadaye waendeshe magari.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia kwenye suala la bidhaa zinazotoka nje. Wenzangu wamechangia kwa kirefu nimemsikia Mheshimiwa Manyinyi anachangia vizuri. Ninatoka kijijini na tunatoka mbali sana na sehemu ambapo hizi bidhaa nyingi tunazozitumia zinatengenezwa hususan Dar es Salaam na Pwani kama walivyosema wenzangu na tofauti ni kubwa sana, lakini pia Mwenyezi Mungu pengine naye alipanga kuna wengine wawe mbali, kuna wengine wawe karibu. Sisi tumepata bahati ya kuwa na ujirani mwema kule Kanda ya Ziwa nchi zinazotuzunguka kama Uganda, Burundi, Rwanda na Kenya. Tunategemeana vitu vingi sana, watu wa Tunduma, watu wengine hawa wanaokaa mipakani.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuzungumza suala moja la bati, mfano kwenye bati. Mwaka 2019 haya mambo tuliyaondoa ambayo leo tunataka kuyarudisha ya kuongeza 10%. Tuliyaondoa na sababu maalum wanafahamu sisi hatuna kipato kikubwa sana kwa watu wetu tunaowaongoza, kwa sababu ya bei watu walikuwa wanakimbilia kuezeka nyumba zao na majani, tulikaa humu mwaka 2019 tukakubaliana, tukaondoa hayo mambo ya usumbufu kule mipakani. Hivi vitu vinakuja tunapata kwa kweli bei rahisi.

Mheshimiwa Spika, leo nilikuwa ninajaribu kuangalia ukiongeza hizi asilimia walizoziweka hapa tunaenda kurudisha bando la bati ambalo sisi tunatumia kwa kijijini tunaezeka nyumba

zetu na *gauge* 32 litaenda kuuzwa shilingi 500,000 na zaidi kutoka kwenye 320,000. Hii ni kuhamasisha tena turudi kujenga kwa manyasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni mwenzangu na kule kwake ana tembe nyingi kweli lakini juzi tunapita na *helicopter* tunaona watu wameanza kuondoa zile nyumba za kizamani za majani na matembe wanaenda kwenye mabati angalau kwenye hiyo *gauge* 32. Kwa hiyo, ninaomba sana kwa sisi tuliopata bahati ya kuwa karibu na nchi zingine tuangalie wapi ambapo kuna hizi bidhaa tulizozipitisha hapa kama kuna unafuu watupe uhuru.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunajenga meli ya tani 400 kule Mwanza ambayo tunategemea iende nchi za jirani Kenya na Uganda. Hizo tani 400 kama wanaanza kuweka haya masharti tunabeba vitu gani kwenye hiyo meli? Maana yake tunatengeneza hasara kwenye hiyo meli, hatuna abiria atakayeenda labda Kenya au Uganda kwa sababu tukienda kule tunaenda kuchukua bidhaa kwa ajili ya kuja kuuza Tanzania na wao wanachukua bidhaa kwetu kwa ajili ya kupeleka kwao.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ninamwomba Mheshimiwa Waziri, amefanya vizuri sana na sasa hivi tunampongeza anajaribu kuangalia hali halisi ya Watanzania. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, wameweka kipengele cha kwamba Kamishna atatoa msamaha, sisemi kwa ubaya na Kamishna Mwenda ni rafiki yangu sana na bahati nzuri na yeye amepita humu ndani kwenye siasa, amepikwa vizuri baadaye ndiyo amekwenda kuwa Kamishna. Nimwombe Mheshimiwa siyo wote hata kabla yake anajua aliyoyakuta mle ndani kwa roho yake ilivyo tukirudisha haya mamlaka tena kwamba unapoingiza bidhaa mpaka Kamishna aone kama inawezekana, tunatengeneza rushwa kule mipakani itakuwa kama kuwaabudu watu Makanisani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama itakubalika nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam, ninajua siyo wataalam wote wana roho hizo, lakini kule ambapo utataka msamaha…;

halafu Mheshimiwa bidhaa zinazoingia ni nyingi mno hata zilizotajwa hapa. Sasa Kamishna atashinda anatoa msamaha toka asubuhi mpaka jioni kwa sababu ni maisha yetu haya. Nimwombe sana Waziri kwa sisi wazawa na wafanyabiashara wenu wazawa kwa sababu wanakusanya kodi, hatuna shida na kodi.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri na timu yake kwamba kwa wazawa wanaoingiza mizigo kutoka kwenye hizo nchi jirani, niwaombe wasiwe na masharti. Kwa mgeni waweweke masharti lakini hawa wanawatengeneza ili baadaye waje kuwakamua kwenye kodi zingine baada ya kuwa amekua.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimwombe Mheshimiwa Waziri sana pendekezo langu japokuwa tumechelewa kupeleka *amendment,* lakini ningeomba hili suala wazawa wote wafanyabiashara waliopo kanda ya ziwa na mipakani wanaofanya biashara tuwape uhuru wa kuendelea na biashara kama ilivyokuwa kwa sababu chochote utakachokifanya unaenda kutuumiza sisi watumiaji.

Mheshimiwa Spika, leo tunapata *cement* labda ya nchi jirani kwa bei nafuu na bati kwa bei nafuu. Bati ya Dar es Salaam ina bei kubwa, utakapomwongezea chochote sisi watumiaji tena tuanze kurudi kwenye majani. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa ninategemea jibu lake atakuwa ameshajadili na wataalam kutuambia kwamba kwa wale wafanyabiashara wetu wazawa na tayari wengine wameshawekeza sasa hivi biashara ipo wazi ili mtu akupe bidhaa zake hata huko nchi jirani lazima ukaweke labda hela kama shilingi bilioni mbili, bilioni kadhaa tayari sheria inaanza tarehe Moja haiwezekani tunaenda kuwaingizia wafanyabiashara wetu hasara. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, akija hapa pengine aone jinsi ya kuliweka kwa sababu huko nje kwa kweli ametengeneza taharuki sana.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna miji kama Musoma, Tarime na Katoro tunategemea hizo biashara, ukitaka bidhaa rahisi ipo na inatoka sehemu fulani. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri inawezekana wamekaa kwenye vikao vyenu vya *East Africa*

wakaweka hivyo, lakini watatuumiza sana sisi watumiaji wa hali ya chini.

Mheshimiwa Spika, suala la pili la *energy,* ninataka kufahamu nimesoma *energy* inawekewa ushuru wa 134 kwa lita *point* mbili ni sawa, ni jambo jema, lakini ukisoma kwenye kile kipengele kwa chini inaeleza hii ni kulinda afya ya mtumiaji. Sasa ninajiuliza yaani afya yetu sisi inawekwa rehani kwa ajili ya kodi ya shilingi 134, Hapana. Kama wataalam wameshachunguza na nimesikia mchangiaji Mama Salma alisema *energy* ni tatizo, ni kweli sisi wote humu ndani ukichoka ukishtua ka-*energy* kidogo nguvu zinarudi sasa kwa watoto? Kwa watoto wenye miaka 10, miaka nane, saba na wenyewe wanabugia *energy* tena mpaka tatu, tunataka kutengeneza watu gani sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niombe kama mmeshaona hili ni tatizo tusiende kuweka kodi ni afadhali tuweke kama kilevi kwamba inaruhusiwa kunywewa na mtu wa kuanzia miaka 18 sisi tumeshakuwa *scraper* hata ukinywa sawa. Watoto wadogo na wenyewe tuwa-*boost* kwa *energy,* kwa kweli haifai. Ninaomba tujaribu tu, sisi wote humu ndani tuna watoto, chukua *energy* moja mpe mtoto wako hata kama alikuwa anasinziasinzia utaona anaanza anakwenda kucheza kwenye *garden*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri tuangalie hatuwezi kuweka kodi kwa sababu ya kulinda, hiyo lugha kidogo inaleta mashaka kwamba tuitoe hiyo *energy* kunywewa na kila mtu kama ina madhara tukanywe watu ambao tumeshaona dunia inaendaje huko mbele.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninataka nichangie kama alivyochangia mwenzangu Mzee Sanga, tunafanya biashara ya magari, ukiweka magari kwa kumlinda mtu anayeunganisha magari Dar es Salaam, hii ni kuua ushindani kwanza, kwa sababu tunaenda kukopa kwenye benki, ukienda kukopa leo unataka Mchina mmoja, wanakupa mwaka mmoja na nusu mwaka hadi miaka miwili, ukienda kukopa *Scania used* wanakupa miaka mitatu, miaka mitano. Sasa kwa nini, wanataka kutupeleka turudi kwenda kumnyenyekea mtu mmoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hata leo tukikubali kwamba tuache kuagiza nje, huyu mtu aliyeletwa Dar es Salaam aliyekuja Dar es Salaam kuwekeza ana uwezo wa kuhudumia *demand* ya wanunuzi wa magari Tanzania? Hawezi! Tunarudi tena kwenye ukoloni unalipa gari leo unaambiwa subiri miezi mitatu na hela yako anayo na hela ni ya riba ya benki, hii haiwezekani! Kwa sababu sisi tunahamasisha watu wawekeze tunategemea magari, malori, ma-*truck* haya yabebe mizigo yasafirishe, tuache hayo mambo ya kuongezea utaratibu mwingine ambao utawakwaza wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa wote *uniform,* kila mtu amiliki gari ya *FAW* au gari za Kichina, hapana! Tuachwe huru kama tunavyonunua gari ndogo unaweza kuwa *Benz,* unaweza kuwa na *Rolls-Royce* kama uhuru wa magari mengine. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa hili ajaribu kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia mimi na wewe tumeingia pamoja kwenye Bunge hili, kwa kweli umetuonesha wewe ni mwanafunzi mzuri sana. Umefanya kazi kubwa inawezekana kila mtu wakati unaanza hata kupiga kampeni, mimi mwenyewe ulinifuata kuniomba kura nilikushangaa huyu dada atatuweza mle ndani? Wakati unaingia kwenye Unaibu Spika, lakini umeweza ku-*copy* vizuri leo tunajivuna tuna Rais wa Mabunge ya Dunia, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata sisi humu ndani nimepata bahati ya kuzungumza wa mwisho, hata sisi humu ndani tumefanya kazi kubwa sana kila mtu aliyemo humu ndani amechangia kwenye maendeleo ambayo yanasifika leo Tanzania. Katika kusifika kwa Bunge hili Wabunge wote hawa wamechangia vizuri wamekusaidia mpaka mwenzetu umeenda kuwa kule. Ninakuomba na wewe utuombee, sisi hatuna mashaka tumewaambia Wanauyole tuna kazi na wewe bado, iwe jua, iwe mvua tunaomba hata wale wanaotarajia kwenda kuchukua fomu, mtu akifanya vizuri mwacheni sisi hatushindanishi *degree,* tunashindanisha utendaji.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwako huko kuna madaktari, sisi hatuhitaji kushindanisha elimu zenu, tumeona huyu mtu anatakiwa mpaka na dunia, halafu unaenda unamwekea mtu Uyole kwa kweli! Aaah, wataniangusha sana watu wa Uyole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwombea kura sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, umefanya kazi nzuri sana, hongera sana. Najua kiti chake ni cha moto, mtu akiitwa Waziri wa Fedha tunaamini kwamba anaiba hela, lakini kwa kazi zote zilizofanyika amemshauri sana Mheshimiwa Rais na ameshauriana na Baraza lote la Mawaziri wamefanya kazi nzuri sana, tunamwombea Mungu arudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami kijana wako hapa nimesimama vizuri leo nimevaa kama Shehe hapa, hiki kiti changu Mheshimiwa ninaomba anitunzie kwa sababu nimefanya kazi nzuri kwenye Jimbo langu, ninawaomba wananchi wa Jimbo la Geita, Nkome, Kakubilo, Bugalama, Kata zote za Jimbo langu leo ndiyo namaliza hotuba yangu tukutane Jimboni. Nimefanya kazi nzuri nimeliweka Jimbo langu kwenye ramani, Wabunge wote kabisa ninaomba waniombee ili niweze kurudi tena na kulisukuma gurudumu letu la maendeleo. Wangapi wataniombea, wanyooshe mikono? Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Mohamed Suleiman Issa, ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kupata nafasi ya kuchangia mchango wangu kwa mara ya mwisho. Tunaamini kabisa Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa sana ndani ya nchi hii, tunampongeza sana, karibu kila eneo kwa Watanzania mkono wa Mheshimiwa Rais tumeuona, sekta nyingi amezigusa, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri na Wasaidizi wao kwa kazi kubwa

ambayo wameifanya ya kusimamia Wizara ambayo ni nyeti, Wizara ambayo kila mtu anategemea au anakuwa na matumaini makubwa ya kupata kutoka kwenye Wizara hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha 2025/2026, ninajikita kwenye eneo moja tu eneo la Sheria ya Mamlaka ya Msajili wa Hazina ambayo ipo Sura 370 pamoja na Sheria ya Umma 116. Kwenye eneo hili kuna mapendekezo ambayo yamependekezwa na Serikali, lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa kuja na mapendekezo mahsusi ambayo yanakuja kuiangalia, kuipa angalizo Serikali badala ya Msajili wa Hazina kukusanya 15% na mapendekezo ya Serikali yafike mpaka 60%, hapa ninaungana na Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imekuja na mapendekezo ambayo ninachukulia taasisi moja tu Taasisi ya Bandari. Kama Wabunge watakumbuka Serikali ilikuja na mapendekezo ambayo yalitikisa nchi tukaja na uwekezaji mkubwa wa *DP* World, ambao mwanzoni Watanzania wengi walikuwa hawaelewi, lakini baadaye wamekuja kuona mafanikio makubwa ambayo yamepatikana ndani ya kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kifupi Serikali imeongeza mapato kupitia Mamlaka ya Bandari. Mamlaka ya Bandari ilikuwa na uwezo wa kukusanya trilioni 1.1, leo hii Mamlaka ya Bandari baada ya uwekezaji mkubwa wana uwezo sasa wa kukusanya trilioni 1.4, ni uwekezaji mkubwa ambao ulikuwa umewekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika kipengele ambacho kimeweka Msajili wa Hazina aweze kukusanya makadirio mpaka ya 60% tunawanyima uwezo Mamlaka ya Bandari ya kufanya kazi. Kwenye eneo hili, tunaiomba Serikali iangalie kwa makini kwa sababu hata ule uwekezaji tuliouona na hata ile dhamira ambayo Mheshimiwa Rais aliiweka na kuwaaminisha Watanzania itashuka mara moja.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana kwenye eneo hili Mheshimiwa Waziri watafakari sana Serikali tusiwe tunaenda, tunapiga hatua moja halafu tunarudi tena hatua tano nyuma. Ninaomba na kuishauri Serikali kwenye eneo hili tubaki kwenye mapendekezo yaliyokuwepo ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mafanikio makubwa ambayo yamepatikana ni pamoja na kuongezeka kwa mapato ya kodi ya forodha, lakini baada ya uwekezaji kumekuwa na upunguaji wa muda wa meli wa kusubiri ambako tumesaidia sasa hivi hata baadhi ya makampuni yameanza kushusha bei za gharama ya usafirishaji, kwa sababu ule muda ambao ulikuwa unatumika kwa asilimia kubwa wa kusubiri mzigo haupo tena.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali tuangalie suala la hii 15% tuiondoe, ibaki ile ile 15% badala ya ile 60%. Tunapoweka kati ya 15% na 60% tunatengeneza wigo ambao utamfanya Msajili wa Hazina afanye maamuzi bila kufuata utaratibu, tunaomba hili wauliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya utekelezaji wa miradi ambayo Mamlaka ya Bandari imeanza kutekeleza, yapo mambo ambayo yamefanyika na yanatarajiwa kufanyika. Uwekezaji uliopo, Serikali kama tutawaachia hawa bandari wakaendelea kufanya utekelezaji wa yale ambayo tumekubaliana, kwanza Serikali watanufaika kwa kiwango kikubwa. Bandari wana uwezo sasa wa kuwekeza gati nyingine mpya ambayo itawafanya Serikali wapate kukusanya kwenye gati moja trilioni moja.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inapowanyima uwezo wa kujenga miundombinu, tukabaki na eneo lile dogo tu kuangalia ile miundombinu iliyopo, ninaona sivyo. Tuwaachie Mamlaka ili Serikali iweze kukusanya kwa kiwango kikubwa na tusione tu kwamba shilingi ya leo ni ya muhimu sana kuliko shilingi ya kesho. Uwekezaji wowote unapowekeza ndipo utakapopata mapato makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kupitia Mamlaka ya Bandari kuongeza maboresho ya kujenga gati namba nane

mpaka 11. Hawa hawawezi kujenga kama tutakuwa tumechukua fedha zao kwa asilimia kubwa kiasi kwamba sasa hata ule uwekezaji na kule kuaminiwa na benki ambazo wanaweza wakakopeshwa hawatakuwa na hiyo fursa. Kwa hiyo, tunaomba hili Serikali waliangalie kwa kina na waone umuhimu wa kuwaachia hizi fedha kwa ajili ya uwekezaji zaidi ili Serikali baadaye, baada ya miaka miwili, mitatu tutakuwa na uwezo mkubwa sana na Mamlaka ya Bandari itakuwa na nafasi ya kufanya vitu vingi.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo lipo pale bandarini, kuna *project* ya kujenga matenki pia ipo *project* ya kuhamisha ile miundombinu iweze kupelekwa sehemu nyingine ya mafuta na kupanua eneo la bandari, wakiwanyima hizo fedha hawataweza tukitegemea kwenye mfumo ule wa kutegemea ruzuku ya Serikali. Ninaomba eneo hili waweze kuwaachia ili waweze kufanya kazi itakayowasaidia na kuifanya Taasisi ama Mamlaka ya Bandari iwe na uwezo mkubwa wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo maendeleo makubwa ambayo tunayategemea kuna mkakati wa kupanua lango la kupitia meli, bila kuwaachia fedha hawana uwezo wa kuweza kufanya kazi hii ambayo wanaitegemea kuifanya. Pia tuna miradi mingine endelevu ambayo ipo inayotegemewa kufanywa na Mamlaka ya Bandari ni pamoja na kuanza kujenga Bandari ya Mbegani kule eneo la Bagamoyo. Niombe sana eneo hili walitazame kwa kiwango cha hali ya juu ili tuachie hawa waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninayasema haya? Eneo hili ni eneo muhimu na wao Serikali wanajua ndiyo chanzo cha mapato. Wanapoboresha maeneo hayo karibu kila sekta itakuwa na nafasi ya kukusanya kodi kwa sababu ni eneo lenye lango la kukusanya kodi bila shida. Kwa hiyo, ninaomba eneo hili tulifanyie kazi na tuweke mkakati wa kuacha mazingira yale ambayo yapo na ninaunga mkono hoja ya wenzangu wa Kamati ya Bajeti kile kilichopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa vyanzo vipya vya mapato ambavyo vinakuja kuwafanya Watanzania

wote tupate bima ya afya, eneo hili ninaunga mkono, lakini pamoja na kuweka Mfuko ambao utasaidia dawa za waathirika wa UKIMWI hii itatusaidia sana na kutengeneza mazingira ya Watanzania kuwa na nguvu ya kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe, kwa kazi kubwa ya kuliendesha na kulisimamia Bunge hili umetulea Wabunge ndani ya miaka mitano kwa mapenzi mazuri na umeliendesha hili Bunge bila upendeleo, umetulea kama familia moja, tukutakie kila la heri kwenye Jimbo lako uweze kushinda bila kuwa na taabu, ninaamini wananchi wa Mbeya wana uelewa na wanajua thamani yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Wabunge wenzangu wote ambao tumefanya kazi pamoja, tumekuwa na umoja, tumefanya kazi vizuri na kwa dalili ninayoiona karibu 99% tunaweza tukarejea kwa sababu Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa karibu kila eneo tumepata mkono wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi ya kipekee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Vijijini kwa sasa Tanganyika, ambao walinipa dhamana na tumefanya kazi vizuri. Pia, ninawapongeza na kuwashukuru Wabunge wenzangu wa Kamati ya Miundombinu ambao tumefanya kazi kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono, ahsanteni sana.. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said Issa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, shukrani za dhati nitoe kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametupa uhai na leo hii kuja kujadiliana kuhusiana na maslahi na uendeshaji wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi ili niweze kuchangia mchango wangu huu. Nitachangia katika hoja ambayo ameizungumzia Mheshimiwa Kakoso, ambayo ni *Treasury Register Act, Chapter* 370 ambayo inazungumzia *remittance of fifteen to sixty percent to the consolidate fund.*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu kwanza ninaunga mkono maoni ya Kamati yote ambayo wameyatoa katika sehemu hii, ambapo Kamati wameeleza kwamba hii haitakuwa sawa kuwepo hapa au kufanyika hivi na ninasema vilevile haitakuwa sawa kufanyika hili, kwa sababu ukitoka *fifteen to sixty percent* ina maana kwamba ni *four hundred percent* umeongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haidhuru kwamba tumesema *between,* sasa hatujui nani atakuwa yuko kati, nani yuko mwanzo, nani yuko mwisho na hofu yangu tukiiacha hivi tukiondoka tulishawahi kupitisha kitu hivi *in blanket,* sasa huko mbele hiyo Kanuni hatujui nani atakuja kupigwa kwenye *sixty,* nani atakwenda kwenye *fifty,* nani anatakwenda kwenye *forty*, ingawaje kwamba kuna neno limesemwa kule mwisho *as determined by Public Finance Act*. Sasa kule kwenye *Public Finance Act* sijaona kama kuna kifungu labda kimeelezea kitaendaje endaje, hilo moja.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni upi? Wasiwasi wangu ni kwamba tutazinyima kampuni hizi ukwasi na ukwasi wenyewe hapa kwa sababu imesema *monthly remittance,* kwa kuwa ni *monthly remittance* ina maana kwamba hizi kampuni zitakosa kufanya zile *short term obligation* zao. Sasa tukiwanyima ukwasi maana yake hapa hatuzungumzii mikopo mikubwa ambao wanatazama *solvency* ya *company,* lakini hapa tunazungumzia kwamba *short term obligations* zinaweza zikaja zika-*fail*. Kwa maana hiyo, ile *smooth operations* za hizi taasisi itakuja kuwa ngumu. Sasa hilo mimi nalisema ili tujaribu kuangalia na tutazame Kamati ilipotushauri ili tuende na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shamsi pia alisema hapa kwamba je, hizi kampuni zilivyowekwa kwamba ziwe zinaongozwa

ziwe *public companies*, Je, tulikuwa tunaangalia mapato au tuangalia maslahi mapana ya Taifa? Katika bidhaa kuna vitu vinaitwa *public goods, public goods* nyingine huwezi ukazipeleka katika *private sector,* ni lazima ziendeshwe na *public sector* inavyofanya zile kazi zake wakati mwingine kwamba wanaangalia maslahi mapana ya Taifa, kwamba nini kitatokezea kule, hili ninaona kwamba tuliweke katika kipaumbele ambayo yalikuwa ni maoni ya Mheshimiwa Shamsi Vuai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tujifunze Waswahili tunao msemo tunasema, ukupigao ndiyo ukufunzao, maana kama haujakupiga hauwezi kukufunza, lakini hebu tujifunze. Bunge la Kumi na Moja tulisema hapa *TANAPA,* Ngorongoro wanapata mapato makubwa wana matumizi mabaya, pesa zao ziende Mfuko Mkuu, tukapeleka malalamiko tumeona, leo sheria imekuja imefanya nini? Inapunguza.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa hapa tuna-*export levy* ya korosho tulisema yote iende Mfuko Mkuu wa Serikali, ndugu zangu hapa wa Kimakonde wakasema sana kwa korosho yao, iende Mfuko Mkuu wa Serikali, badala yake leo hii tunatoa tunasema kwa miaka minne Kamishna akikusanya apeleke wapi, katika Bodi ya Korosho. Kwa sababu umetupiga, Je, hatujifunzi huu uliotupiga? Maana ukupigao ndiyo ukufunzao.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ya leo tunayotaka kuipitisha imepunguza hayo makali, lakini imekuja kuongeza makali katika hizi kampuni nyingine. Kwa hiyo ninaomba tujifunze na hili, tusipojifunza maana yake ni kwamba tunaweza tukapata kama haya ambayo yalitutokea.

Mheshimiwa Spika, tufanye nini basi? Kama tunahisi hayo mapato yanavuja, hayapatikani ipasavyo, zipo kule bodi na bodi uteuzi wao ni Rais. Waziri, hizi bodi basi tuweke watu *competent* waweze kusimamia, watakavyosimamia haya yatakwenda vizuri kwa sababu ndiyo tayari zile bodi tumeziamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, kwa kuwa Kamati hapa sasa imeleta *schedule of amendment*, ninaomba Serikali ikubali hii

*schedule of amendment* ya Kamati kwa sababu Kamati imeona na haya kihistoria yametokezea hapa. Kuna *theory* ya pesa za mtoto kukamatwa na mzee, zote tunajua hapa. *Theory* ya pesa za mtoto kukamatwa na mzee; mzee mara nyingi sana akikamata pesa za mtoto akimwambia nitakupa kila baada ya mwisho wa mwezi, sio rahisi mzee yule kila mwisho wa mwezi zile pesa akazitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulishafanya kwenye *property tax* hapa na hazikwenda. Mzee akifika tu siku atakuja kusema hizi nisubiri kidogo, nisubiri; tutaua mashirika maana *Consolidated Fund* ndiyo mzee, lakini hii Mifuko ya huku ndiyo mtoto. Zikikamatwa pesa huku tutakuja kuua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote ninatoa shukrani; hii changamoto isingetokea bila kwamba haya makusanyo yameongezeka. Kwa hiyo, niipongeze Serikali kwamba mapato kumbe yameongezeka sasa tunatafuta njia ya kudhibiti. Sisi kama Wabunge njia ya kudhibiti tunaona sio hiyo, tupite hii njia ambayo Kamati imetushauri. Hii njia iliyotushauri Kamati itakuwa ni salama kuliko njia hii kwa sababu hapa tayari tunazo *reference* ya sheria tulizozipitisha hapa hapa kwenye *Finance Act,* lakini badala yake tukaja tuka-*review* tukarejea.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja mia kwa mia na ninashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Said Issa atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika *Finance Bill* hii ya 2025. Nianze kwa kumshukuru *Allah Subhanahu Wataalaa* na kumtakia ziada za heri Bwana Mtume Muhammad *(S.A.W)* kwa kutujalia kuwa hapa tukiwa wazima na afya kamili.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu. Kwanza nitaanza na Sura ya 196 kulingana na

Ripoti ya Kamati pale inaposema ushuru wa mbao laini utatozwa 30% mpaka 150% kulingana na ule ulaini wa ile mbao. Ninaamini hii ni katika vipimo vitakavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, hapa mchango wangu, kwanza niipongeze Serikali kwa kuja na wazo hili la kutoza kodi kwenye *export* ya mbao laini kwa sababu imekuwa viwanda vyetu vya nchini hapa vimekuwa haviwezi kulindwa, haviwezi kufanya kazi vizuri kutokana na kwamba mbao nyingi sana huwa zinasafirishwa kwenda nje kwa sababu ilikuwa hakuna tozo kama hivi. Kwa hiyo, ninaipongeza Serikali kwa kuja na tozo hizi lakini nina ushauri.

Mheshimiwa Spika, bado ninaona 30% ni ndogo kwa sababu bado ita-*encourage* watu kufanya *export* ya mbao laini; hili linakuja vipi? Hakuna *price indicator* ya hizi mbao laini, ingekuwa ipo *price indicator* kidogo ingekuwa rahisi, lakini hakuna *price indicator*. Maana yake nini? Hatuwezi kujua kwamba yule ambaye ana-*declare* kwamba thamani ya mbao zangu hizi ndiyo sahihi. Anaweza aka-*cheat* na baadaye hata kama tumeweka 30% lakini ikaonekana kwamba amelipa kodi. Ushauri wangu ni kwamba amelipa kodi. Ushauri ni kwamba kiwango hiki kiongezwe mpaka 30%, huo ni mchango wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, mchango wa pili ninajikita bado pale kwenye Ripoti ya Kamati. Kwenye kusema kwamba baada ya *return* ya ada za bandari zitalipwa kwa siku 20, imekaa vizuri kwa sababu hata sisi pale Zanzibar kwenye *ZRB* tunafanya hivyo, lakini imechanganywa kidogo katika Kiswahili hii ripoti kwamba baada ya makusanyo, siyo baada ya kufanya *return* ya mwezi uliopita. Lazima ikae wazi kwa sababu inawezekana sheria ikaja ikapita hapa baadaye tukaona kwamba makusanyo na hii *statement* inavyoeleza, makusanyo yanapokusanywa maana yake baada ya siku 20 ambayo sio hivyo, ni baada ya *return* ya mwezi uliopita. Kwa hiyo, hivi ninafikiri Kamati ilingalie lisije likatuletea ukakasi katika kutengeneza hii sheria.

Mheshimiwa Spika, nijikite pia kwenye suala la mafao ya wastaafu. Jambo hili kwa kweli nimeliona ni zuri kwa sababu Waziri atarejea *pension* zile kwa kupata idhini ya Mheshimiwa Rais. Sasa

ninafikiri jambo hili Mheshimiwa Rais ni taasisi na wanufaika wa pensheni hizi wamekuwa wakipiga kelele siku hadi siku. Sasa kutokuweka wazi kwamba wanakwenda kufaidika nini kupitia sheria hii ambayo ni utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, bado ina maana kuna ukakasi wa kujua kwamba wanakwenda kunufaika vipi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais atapelekewa na yeye atatoa ushauri wake lakini bado hawa wanufaika wanakaa na *dilemma* hawajui ni nini kinachoendelea. Kwa hiyo, sheria ingetamka wazi kwa sababu tunaenda kutekeleza sheria hii kwa bajeti hii inayokuja. Kwa hiyo, ilitakiwa itamke wazi kwamba kutoka hapa wanakwenda kunufaika hapa. Hatuwezi kujua wanaweza kuja kuongezwa kiasi hiki baadaye ikawa ni kelele tena. Kwa hiyo, ninashauri kwamba sheria ingetamka wazi kwamba hawa waongezwe kiasi hiki kutokana na hali inavyokwenda na *inflation* ilivyo na hali ya mshahara wake ulivyokuwa na vigezo vingine ambavyo vinakuja.

Mheshimiwa Spika, nijikite sehemu nyingine kwenye suala la tozo ya mafuta ya taa na *petrol*. Sipingi kwenye tozo hizi kwa sababu tumeamua kujitegemea ni jambo la kawaida na ndiyo Serikali imeona katika kukusanya mapato, lakini nilikuwa ninashauri mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza imeletwa hapa kwamba 70% zitakwenda kwenye UKIMWI na 30% itakwenda kwenye Mfuko wa Bima ya Afya. Sasa tumefikiri vizuri na Mfuko wetu wa Bima ya Afya umekuwa ukiyumba mara kwa mara. Sasa lakini kupeleka 70% kwa 30% ninaona kama hakuna uwiano kwa sababu sijui ni vipi kama kuna vyanzo vingine ambavyo vitapeleka Mfuko wa Bima ya Afya kuwa imara. Sasa kuweka Mfuko wa Bima ya Afya, 30% peke yake kwenye hii ninaona bado ni ndogo. Nilitamani kwamba iwe 50/50 ili tujue.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo, tozo hizi wananchi wamekuwa wakizilalamikia kwamba tunatoza tozo halafu hakuna mrejesho. Kwa hiyo, sheria nayo itamke hapa kwamba kila mwezi itolewe taarifa ya makusanyo ambayo yamepatikana kwenye

tozo hizi ili kujua Mfuko wetu unanenepa vipi. Sasa kunakuwa na tozo lakini hatujui Mfuko wetu unanenepa vipi, matokeo yake wananchi wanalalamika huko mwisho wa siku inakuwa Serikali inaonekana kama vile haipo sawa. Jambo hili ni sawa tu kwa sababu Serikali inafanya kazi kubwa, inatumia *sense* nyingi. Kwa hiyo, hakuna shida lakini uwazi na uwajibikaji ndiyo tunaouhitaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kilichonifanya leo nichangie ni hiki hapa. Kwa kweli nimeona kitu ambacho mimi binafsi kimenichanganya. Katika Sura ya 148, kutoza tozo katika miamala ya benki inayofanyika pamoja na malipo ya kielekroniki. Maana yake tumehama kutoka kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa ambazo unanunua, tunakwenda kwenye miamala ambayo unafanya. Sasa ni sehemu pia ya mapato, lakini hili jambo mbona limekuja kwa kasi? Maana yake tulikuwa na 20% ya *VAT* pale nayo ilikuwa shida mpaka watu wakalalamika ikashuka kwa asilimia mbili ikaja 18%.

Mheshimiwa Spika, leo mtu fedha zake mwenyewe anataka kufanya biashara au anataka kununua kitu, katika shilingi laki moja ichukuliwe shilingi 16,000; hii kwa kweli italeta mkanganyiko na niwaambie kwamba hii ikitekelezwa kwa muda huu sijui kama hizo kura mtazipata.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa muda huu, 16% itozwe kwa sababu ongezeko la thamani tunajua kwamba kule unaponunua unalipa, ukiuza unalipa, unachukua *difference* ile ndiyo ambacho umelipa. Yaani wewe ni asilimia ndogo tu lakini sasa huku kwenye miamala huku, 16% nani atakurudishia? Kwa hiyo, ni fedha nyingi sana, nilifikiri wangeanza na asilimia mbili mpaka tatu, lakini wanakwenda kuweka huku? Hakika hili litaleta *disaster*. Mungu ajalie turudi kwenye Bunge lijalo, ninajua CCM wako wengi watapitisha hapa.

Mheshimiwa Spika, kwenye Bunge lijalo tutakuja kukumbushana kwenye hili ninalolizungumza, hizo kelele ambazo zitalia huko. Kwa hiyo ushauri wangu, wauchukue waufanyie kazi, 16% hii ni kubwa sana kutoa tozo kwenye miamala ambayo tunataka kununua au kutuma fedha nje.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisafiri katika nchi za wenzetu, ipo hiyo miamala wanafanya *free* kabisa. Kwa mfano, pale China wanafanya *Alipay*, unajaza fedha kwenye *Alipay* yako na unanunua kila kitu, hutaki kushika fedha, lakini unafanya kazi vizuri. Fedha zinakuwa kwa Serikali wanazifanyia kazi wanafanya mambo yao wanayotaka kwa sababu wao wana *electronics* tu.

Mheshimiwa Spika, sasa kweli tunakwenda kutoza 16% ambayo huyu mtoaji, huyu mlipaji hana pa kulipa wala hana pa kurejeshewa. Kule kwenye zile *T* ipo sehemu ya kurejeshewa. Kwa hiyo jambo hili kama halikurekebishwa siungi mkono hoja. Hii inaenda kuua watu na haikubaliki, mimi siungi mkono hoja kama haikurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nianze kwa kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Konde kwa imani kubwa waliyonipa kwa kunichagua na kuwatumikia. Ninaamini nimefanya vizuri na nina nia tena ya kurudi tena jimboni wanichague tena, wanipime waone kwamba nini nilichofanya. Bila shaka wameridhika na utendaji wangu na ninaamini kwamba watanirudisha.

Mheshimiwa Spika, niwape siri tu, kule Jimbo la Konde wapiga kura ni 8,300, CCM ni 600 tu. Kwa hiyo *calculation* watafanya wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Said. Hebu hiyo hoja yako ya mwisho ni kifungu gani kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameleta marekebisho mengi tu hapa sijui kama ni sehemu ya hicho kifungu au namna gani? Hiyo hoja yako ya mwisho ya miamala ni kifungu cha ngapi?

*(Hapa Mhe. Mohamed Said Issa aliendelea kuzungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**SPIKA:** Kwenye sheria ipi? Sawa ahsante.

Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja ujiandae kuja kuhitimisha hoja yako.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru nami kwa kunipa nafasi nichangie Muswada wa Sheria ya Fedha. Niwapongeze sana Mawaziri, (Waziri wa Fedha, Waziri wa Mpango na Manaibu Waziri) kwa kazi kubwa ambazo wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimesikia hapa Kamati ya Bajeti imekuwa ikitoka usiku hasa jana ikiwa inashughulikia Muswada huu. Ninawapongeza sana Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa ambayo wamefanya kuhakikisha kwamba wanatufikisha hapa tulipo leo ambapo ni pazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nina eneo moja tu ambalo ninataka nichangie hapa ambalo pia limezungumzwa na Kamati. Niwapongeze sana Kamati kwa marekebisho ambayo wamekuja nayo, wamesema hapa wamepeleka *schedule of amendment* kwa Spika juu ya Sheria ya Mamlaka ya Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura Na. 370 pamoja na Sheria ya Fedha za Umma, Sura Na. 348. Niwapongeze sana kwa kuliona hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Serikali yameoneshwa hapa kwamba wamependekeza kwamba mashirika ya umma yapeleke *contribution* ya 15% mpaka 60% (hapo katikati) kulingana na namna ambavyo Waziri na Msajili wa Hazina wataona. Sijajua wametumia upembuzi yakinifu upi kuja na hii hoja.

Mheshimiwa Spika, niseme mimi ni mjumbe wa Kamati ya *PAC*, tunapitia hesabu nyingi za mashirika ya umma. Kati ya mashirika ya umma 300 *plus* kwanza ambayo yanaweza tu kulipa hii 15% iliyopo sasa hivi, sidhani hata kama 100 yanafika. Yaliyo mengi hata hii 15% iliyokuwepo bado hayawezi kulipa.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi hata ya mashirika tulikuwa tunawauliza bahati nzuri wame-*expense* lakini hawalipi. Wana-*acknowledge* kwamba tunadaiwa, Msajili wa Hazina kila mwaka anawadai, madeni yanaongezeka. Ukiwauliza kwa nini hawalipi wanasema hatuna uwezo wa kulipa, lakini kwa sababu sheria inawataka wawalipe kwa hiyo kwenye *comprehensive income statement* wanaweka kama matumizi lakini mwisho wa siku hawayalipi kwa sababu wanatengeneza vitabu *under full basics* hawawezi kulipa na mwisho wa siku yanaendelea kuwa madeni, madeni, madeni.

Mheshimiwa Spika, ukiona hata hii 15% haikuweza kulipika kwa mashirika mengi maana yake nilitamani hata leo Waziri wa Fedha au *TR* aje na pendekezo la kushusha hiyo 15% ili yaliyo mengi yaweze kulipa.

Mheshimiwa Spika, imefika sehemu walikuwa wanakaa mezani sasa kwamba shirika linadaiwa lipeleke *contribution* ya 15%, nichukulie mfano shilingi bilioni 10, sasa hawawezi kupeleka wanasema basi turuhusu tulete hata shilingi bilioni moja; wanasema basi leteni hata hiyo bila sheria yoyote. Kwa nini? Kwa sababu hayana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitamani tuyajengee kwanza uwezo wa haya mashirika kufanya vizuri kama Mheshimiwa Rais alivyosema juzi wakati anapokea gawio kwamba tuyalee mashirika, tuyatengeneze yafanye vizuri, tuyasimamie hata kwenye matumizi yao yalete tija na mwisho wa siku sasa wawekeze na wakiwekeza huko mbele kupitia uwekezaji wao tutapata kingi kingi na ikiwezekana wataona namna gani vipi haya mashirika yamewekeza yaweze kutoka hapo yalipo kwenye 15% kwenda kwenye asilimia nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa leo kwa mimi ambaye nimekaa kwenye Kamati ya *PAC* ninavyoyaona haya mashirika, ukichukua *running cost (recurrent expenditure)*, ukija kuchukua *capital expenditure (government expenditure)* ukijumlisha haya hawawezi kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo ukitoa kwenye 15% peleka 60% weka katikati labda 40%; ukitaja 40% mashirika haya tutayaua. Sasa sijui kwa nini *TR* amekuja na hii, lakini nilitamani afanye kwanza upembuzi wa kutosha kwenye mashirika yote hayo 300 *plus* ayaone ni yapi ambayo hata hii 15% hayawezi kuleta, aone namna ya kuyasaidia hata haya mengi ambayo hayawezi kuleta basi yaweze kuleta hii 15% ili apate fedha nyingi kwenye Mfuko wake, atoke kwenye hiyo shilingi *trilioni moja point* ngapi alizopata, sasa aende kwenye hata kwenye shilingi trilioni mbili ili mashirika mengi yaweze kulipa.

Mheshimiwa Spika, tunavyoenda hapa ninahisi kuna mashirika mawili, matatu au manne yaliyolengwa kulipa hizi fedha. Anayaacha yaliyo mengi ambayo yanakosa sifa kwa 15% kwa sababu hayana uwezo. Kulikuwa na uwezo wa kuyatafuta mengi wakalipa asilimia tisa lakini mwisho wa siku tukakusanya kidogo kwa mashirika mengi halafu uki-*compile* unapata kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na mapendekezo ya Kamati kwamba, waondoe hii na mwisho wa siku ibaki kama ilivyokuwa zamani, waendelee kutoza *contribution* hii ya 15%. Hii 15% inatozwa kwenye pato ghafi, yaani wewe kitendo tu cha kukusanya leo shilingi bilioni moja chukua 15%, ambayo ni shilingi milioni 150, peleka Serikalini na leo wamekuja na hoja ya kila mwezi, maana yake ni ukikusanya mwisho wa mwezi peleka, sasa unapeleka wakati wewe *recurrent expenditure* yako bado! *Capital expenditure* yako bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaona hapa niungane na Kamati, waiondoe hii ibaki kama ilivyokuwa zamani. 15% Profesa Kitila na Msajili wa Hazina waangalie hili, pamoja na Waziri wa Fedha, ili wayasaidie mashirika mengi yalipe hiyo 15% tuondokane na wao kutokushindwa kulipa kwa sababu ya zile asilimia ambazo tumeziweka. Kwa hiyo, ninaunga mkono mapendekezo ya Kamati ibaki 15%, kama ilivyokuwa awali, ili turuhusu mashirika haya yawekeze, yaweze ku-*incur* matumizi ambayo wameweka, kwa ajili ya *recurrent expenditure*.

Mheshimiwa Spika, hapohapo pia, *contribution* hii ambayo inapelekwa Serikalini kwa mujibu wa Sheria, Sheria ipo na imetaja kwamba, hili linatakiwa kupelekwa Serikalini. Hii siyo *donation,* lakini cha kushangaza ni siyo *allowable cost* kwenye *tax*. Mwisho wa siku na yenyewe tena inakuja kukatwa kodi.

Mheshimiwa Spika, yaani ninatakiwa kupeleka shilingi milioni 150 Serikalini, nimepeleka. Kwenye vitabu vyangu ninavyotengeneza *comprehensive income statement,* nimetengeneza, nimeweka kama matumizi. Mwisho wa siku ukienda kwa Mwenda, *TRA,* anakwambia aaha, mimi hii siitambui, itakuwa charged 30% kama *corporate tax*. Haiwezekani, hii siyo *donation!* Ingekuwa *donation* ningekubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wangeamua, *take an example* tuchukulie shirika gani? Tuchukue *TPA,* wamechukua shilingi milioni 500 wakaenda kulisaidia Kanisa, wakaenda kusaidia *charitable Teva;* hiyo ni sawa kwangu kwa sababu, hakuna sheria yoyote inayokufanya wewe uchukue fedha kwenda kuchangia mchango kwenye taasisi yoyote, lakini hii iko kwa mujibu wa sheria. Unatakiwa kuichukua na kuipeleka Serikalini. Kwa nini inakuwa *charged corporate tax* wakati iko kwa mujibu wa sheria?

Mheshimiwa Spika, ninadhani Mwenda pamoja na Waziri wa Fedha waangalie upya hii, haya mashirika tunayapa gharama ambazo siyo za msingi, fedha zinaenda kulekule. Hiyo *TRA* inakusanya, inapeleka Serikalini, hawa 15% wanapeleka Serikalini. Hii inatakiwa iwe *allowable expenditure* kwenye kutoza kodi, haitakiwi kutozwa kodi kwa sababu, ni takwa la kisheria na siyo maamuzi ya taasisi kuipeleka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, yangekuwa ni maamuzi ya taasisi kupeleka Serikalini, hapo ilikuwa ni sawa kuirudisha na kuwa *tax* bila ya 30% kwa maana ya kwamba ni *tax,* lakini kwa sababu ipo kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Namba 348, hii lazima iwe *allowable deduction*. Moja ya sehemu ambayo linatakiwa lifanyike kwa haraka, Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamishna wa *TRA,* ni eneo hili kwa sababu ni kitu ambacho kinajulikana *and it is allowable expenditure*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilivyoanza kuangalia vitabu vya mashirika ya umma, leo nimepitia *TCRA* nikapitia na *TPA,* pamoja na *TANESCO.* Eti inaonekana kwamba, ukishailipa, ukii-*expense* kwenye vitabu vyako vya fedha, kwa maana ya *income statement*, mwisho wa siku ukipeleka *TRA* vitabu vyako wanakwambia, hapana, sisi hii hatuitambui; sasa huitambui vipi wakati nimepeleka Serikalini! Imeenda Serikalini halafu unasema huitambui! Mheshimiwa Mwigulu, hii aitambue kwa sababu ni fedha ambazo zimekwenda Serikalini na zimepokelewa kwenye Mfuko Mkuu, lazima zitambulike, *TRA* ni lazima azijue. *This should be allowable cost* wakati tunatengeneza *comprehensive statement.*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamad Hassan Chande. Mtoa hoja, jiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na niwe mchangiaji katika hoja ambayo iko mbele yetu leo, yaani *Finance Bill*. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Rahim, Mola ambaye, kwa uwezo na rehema zake ametujalia hadi sasa tupo katika hali ya usalama, uzima na afya.

Mheshimiwa Spika, pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuwa katika Wizara ya Fedha, ni miaka kadhaa sasa. Hii ni imani kubwa sana kwangu mimi na Mheshimiwa Waziri wangu wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii leo niwashukuru sana Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndugu yetu, Mwenyekiti Oran Njeza kwa kweli, ni mtu wa hekima na busara kubwa sana. Ninawashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati hiyo. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara moja niliwahi kusema kwamba, Kamati hii haina wakati wa *kailula* wala wakati wa *daku*, wao

muda wote wako kazini tu. Kwa hiyo, tuwashukuru na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wao mkubwa na kwa kweli, kwa michango mizuri ambayo wametoa. Ushauri ambao wamependekeza hapa leo, wameishauri Serikali, ni mzuri na mkubwa sana. Ninawaahidi kwamba, Serikali imeuchukua na itaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, ninaomba nimshukuru sana sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambaye yeye ni mlezi wangu, ni *mentor* wangu. Kwa kweli, haya yote ambayo unaona ninachapa kazi msaada wake ni mkubwa sana kwangu katika kunilea na kuniendeleza katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwashukuru sana wataalam wetu wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Natu Mwamba, Naibu Makatibu Wakuu wote watatu akiwemo Elijah Mwandumbya, Ndugu yetu Bi. Amina na dada Omolo. Tunawashukuru sana Makamishna wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru na ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwa kiasi kikubwa tunavyosaidiana na kushirikiana katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, niwashukuru sana sana wananchi wangu, wapiga kura wenzangu, wa Jimbo la Kojani kwa namna wanavyonipokea na kunipa ridhaa yao kuja huku na ninategemea kabisa kwamba, nitarudi tena, *Insha Allah*. Naomba waendelee kuniombea na ninawaombea ili turudi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, wananchi wa Jimbo la Kojani, lakini siyo peke yao, hata Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, Zanzibar na Mikoa yote ya Tanzania, ukweli Viongozi wa Mikoa wa Chama na Serikali Tanzania nzima wanatupa ushirikiano mkubwa sana. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda hautoshi, siyo rafiki sana, ninaomba nijielekeze kidogo tu kwenye hoja chache ambazo zimetolewa ama wameshauri Waheshimiwa Wabunge. Ni ukweli kabisa ambayo wamezungumza na wameshauri, lakini nataka niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge kusema kwamba, tunajitahidi kukusanya mapato, ili tuepukane na utegemezi wa watu wengine kutusaidia. Kwa hiyo, Serikali ina nia njema sana ya kupendekeza vyanzo vipya ama kuongeza kidogo ili kuwa na uwezo mkubwa sana wa Mfuko wetu. Hiyo ndiyo nia ya Serikali, ili kusudi miradi yetu yote tuifanye wenyewe tuachane na kutegemea wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona mabadiliko sasa hivi ya nchi za wenzetu huko duniani, wameanza kuondoa misaada yao. Kwa hiyo, sisi wenyewe ni lazima tujifunge mkaja ili kusudi kuhakikisha kwamba, tumepata fedha kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ambayo imetolewa ni mizuri sana, lakini kuna hoja moja ambayo Waheshimiwa Wabunge wamepaza sauti sana; hii ya mashirika ya umma kuongezewa, kutoka 15% hadi 60%. Tumesikia sauti zilizotoka kwa uzito mkubwa sana kwa hisia na tumeshauriana hapa na Mheshimiwa Waziri, hili litafanyiwa kazi, lakini Mheshimiwa Waziri atakuja hapa kulizungumza vizuri sana kwa sababu, tunasema kwamba, ladha ya maji ya dafu yawe ndani ya bobo lake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ataeleza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulisema ni pongezi ambazo wametoa kwa yale marekebisho ambayo yamefanyika ikiwemo hata malipo kwa mitandao au mawasiliano. Kwamba, Serikali imeondoa kabisa lile ongezeko lililokuwepo, imebaki kama ilivyo. Tunashukuru sana kwa pongezi hizo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri tumezipokea na tutazipeleka kunakohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kumalizia kwa ndugu yangu, Mheshimiwa, *Sheikh* Mohamed Issa. Mheshimiwa Mbunge alipokuwa anatoa hoja yake hapa mwisho, kamalizia kutoa

taarifa, anasema kwamba, kule Konde ni 10% tu ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu bado anafikiria karne ya 18; tuko karne ya 21 sasa. Konde la Karne ya 18 siyo la 21, mabadiliko ni makubwa sana na hii ni kwa sababu, Marais wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar wamefanya kazi kubwa sana. Leo ukienda Konde masoko ya kisasa ambayo unayaona au shule za msingi na sekondari, kule vijana wa msingi wanasoma kwenye viyoyozi, yaani wako kwenye viyoyozi kabisa, wako kwenye ghorofa, yaani *G plus three,* huko ndiyo wanasoma watoto wa msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, karne hiyo ya 18 anayoifikiria Mheshimiwa *Sheikh* Mohamed hakukuwa na hata darasa wakati huo, ilikuwa watu wanasoma chini ya mwembe. Kwa hiyo, Mheshimiwa ninaomba ujiandae sana, maana yake ni uchaguzi ujao sijui kama hatutolamba kisahani chote; mwakilishi, Mbunge na Madiwani kwa sababu ya wanachama wengi ambao tukonao huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Hebu sema tena. Sema tena, ili iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, uje uhitimishe hoja yako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, *madame de monsieur, c'est Young African, c'est* Pakome Zouzoua, *c'est* Clement Mzize. Leo ilikuwa ni siku kubwa, nilisema ni tarehe 25 Jumatano, kulikuwa na shughuli kubwa, lakini kwa sababu

shughuli bado inaendelea nilisema *boss* wangu atasema kesho matokeo, ili niseme tu, ni Yanga tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kauli hiyo ya utangulizi, niende moja kwa moja kwenye kukushukuru wewe mwenyewe kwa kuendesha vizuri sana kikao hiki, pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Pia, nishukuru na kuwapongeza Kamati ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Ndugu yangu, Mheshimiwa Oran Njeza, Mwenyekiti wa Kamati, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Ndugu yangu Twaha Mpembenwe. Ninajua hapo alipo atakuwa na wakati mgumu kidogo, lakini niwapongeze Kamati yote ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nawasilisha, tumekuwa na kikao kizuri sana na Kamati, lakini pia tumepata maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge kuanzia wakati wanajadili Hotuba ya Bajeti ya Serikali. Kama nilivyosema, nilisema tutakapokwenda kwenye *Finance Bill* tutayazingatia maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Sitapitia hoja moja baada ya nyingine, lakini nitataja tu baadhi ya hoja kubwa ambazo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamezisemea kwa sauti kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya hoja ilikuwa ni ushuru tuliokuwa tunauweka kwenye makaa ya mawe. Tumezingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge na tumefanya marekebisho kwa kuondoa pendekezo hilo, kama ambavyo nilisema pale awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwenye pendekezo tulililoleta kuhusu Sheria ya Benki Kuu, tumeweza kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Siyo hilo tu, tulileta pendekezo pia, la kuongeza ushuru kwenye mawasiliano baada ya kikao na Kamati na mapendekezo ya pamoja na ya Bunge zima, tumezingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwa kubakiza ushuru kwenye kiwango cha 17 na kuondoa pendekezo lile la kuongeza ushuru katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa pia tumeshusha ushuru wa uagizaji wa samaki kutoka dola 2.5 hadi Shilingi za Kitanzania 1,500. Baada ya kushauriana na Kamati na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, tumezingatia na kuleta pendekezo ambalo wataliona kwenye jedwali na kushusha kwa kiwango cha dola 1.25 ikiwa ni nusu ya kiwango kilichokuwepo, ili kuweza kuzingatia uwekezaji unaofanyika kwenye sekta hiyo na wakati huohuo tukizingatia mahitaji kwenye upande wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, lilikuwepo jambo la suala la ushuru kwenye mazao ya misitu. Tumezingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na sasa pendekezo tutakaloliweka kwenye jedwali ni asilimia mbili badala ya asilimia 3.5 tuliyokuwa tumeipendekeza. Hii ni sehemu tu, lakini yapo maeneo mengine mengi ambayo tumezingatia maoni ya Bunge lako Tukufu, pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Kamati, kama ambavyo itabainika katika majedwali tutakapokuwa tunayapitia, Bunge lako litakapokaa kama Kamati.

Mheshimiwa Spika, niseme mambo machache tu ambayo ni ya kisera. Kuna maeneo tumeweka *IDL,* tumeweka ushuru ambao baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamechangia, unahusisha masuala ya kulinda viwanda vyetu. Tumetafakari sana maeneo haya ambayo tumechukua hatua hii.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wakipata fursa wapitie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Katika hotuba yake ambayo sisi tumeitumia kama moja ya nyaraka iliyotusaidia na pia, tumetumia vikao vya sekta pamoja na wadau wa sekta binafsi, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge walivyofanya Wajumbe wa Kamati, tumejiridhisha pasipo shaka kwamba, tuna bidhaa ndani ya nchi yetu ambazo sasa tunazizalisha takribani mara mbili ya mahitaji yake. Tunazalisha bidhaa kwa takribani mara mbili ya mahitaji ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa kawaida wa kiuchumi, mtu akiwa amewekeza kwenye kiwanda, mbali na kodi anayolipa kwa Serikali, mtu wa aina hiyo anatusaidia ajira kwa Watanzania.

Mbali na huduma anayoitoa, yaani bidhaa anayoiuza, kitu kimoja kikubwa ambacho ni cha kiuchumi ni kwamba, anatusaidia kutoa ajira kwa Watanzania na anatusaidia kukuza uzalishaji ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari na kufanya tathimini hiyo, tuliona maeneo ya viwanda vya aina hiyo ambavyo vinazalisha takribani mara moja na nusu, mara mbili na vingine vinaelekea mara tatu na viwanda hivyo bado havijazalisha *at its full capacity ya installment* ya kiwanda chenyewe. Tumeona viwanda vya aina hiyo ama bidhaa za aina hiyo, tukiendelea kuruhusu bidhaa zinazotoka nje na zingine, hata *standard* yake siyo ya kiwango hicho, tukaziruhusu zikaja na nyingine kwa bei ya chini, utaendelea kudumaza viwanda vyetu, tutaendelea kudumaza uchumi wetu, tutafanya Taifa letu liwe la kuagiza bidhaa kutoka nje na tutaua morali ya mtu yeyote kuwekeza ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumesema, tuanze na baadhi ya bidhaa ambazo tayari uzalishaji wake umeshavuka kiwango kinachohitajika mara moja na nusu, mara mbili na zingine zikizalisha kwa kiwango chote cha uwezo wa kiwanda, zinaweza zikazalisha hata mara tano ya bidhaa zile zinazozalishwa hapa ndani ya nchi. Tuwapatie fursa watu wa aina hii wawekeze kwa kiwango cha mwisho. Watumie uwezo wao wa mwisho wa viwanda hivyo, ili kuweza kuajiri Watanzania wengi zaidi, waweze kulipa kodi na pia, tuweze kukuza uchumi na ku-*transform* uchumi wetu kutoka kwenye uchumi ambao unazalisha bidhaa ghafi uende kwenye uchumi ambao unaongeza thamani ya bidhaa ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la kitaalam na ni jambo la kiuchumi. Popote pale ambapo unaiona nchi imeendelea, ni nchi ambayo inazalisha bidhaa na inaziongezea thamani ndani ya nchi yake na ndizo ambazo zinatumika ndani ya nchi. Nchi yoyote ambayo inategemea uagizaji wa bidhaa kuendesha nchi, ni nchi ambayo iko kwenye hatari sana na *future* yake, uendelevu wake siyo wenye uhimilivu. Kwa sababu kila siku bidhaa zile

zikipata tatizo kutoka kwenye, uko unakozalishwa ama tatizo la usafirishaji ile nchi kila wakati itakuwa iko kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na Waheshimiwa Wabunge niwaombe kwenye bidhaa zile ambazo tuna viwanda ndani ya nchi na vinazalisha takribani mara mbili ya mahitaji, tuvilinde viwanda vile. Tuvilinde viwanda hivi, bidhaa hizi zitazunguka tu zitafika kila eneo la nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kazi inaendelea kufanyika, ni vile kazi kubwa kama hiyo haiwezi ikafanyika ndani ya mara moja; lakini mimi pamoja na Waziri wa Viwanda pamoja na Waziri wa Mipango na Uwekezaji kaka yangu Profesa Kitila na kaka yangu Jafo, tuliwapa jukumu timu ya wataalam itutafutie *formular* ambayo itawezesha bidhaa inayotoka Dar es Salaam ikaenda Kigoma, bidhaa inayotoka Dar es Salaam ikaenda Kagera, iendelee kuwa na uwiano unaofanana wa bei. Mbona *Coca-Cola* huwa inauzwa bei ileile kila mahali inapokuwa ndani ya nchi? Kwa hiyo haya tutayafanyia kazi. Utofauti wa bei usitufanye tuue viwanda ambavyo tumeshawekeza ndani ya nchi na tukajivunia kuleta bidhaa kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mipaka hii ni ya kiutawala, lakini huo ndio ukweli, kwamba mipaka hii ndiyo inayotaja wapi na wapi ni nchi gani; hili halipingiki. Kila palipo na mpaka ndiyo hivyo pamekwishatajwa kwamba hapo ndipo mpaka wa nchi na sisi nchi yetu ni Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo zile bidhaa tumeziorodhesha ambazo tayari tumeshajitosheleza na tutakwenda hatua kwa hatua hata kwa bidhaa zingine. Jambo hili tungeacha uchumi pembeni, tukaacha uzalendo pembeni, sisi kama Wizara ya Fedha tungepigania uagizaji kutoka nje. Kwa sababu kuagiza bidhaa kutoka nje ni jambo rahisi sana halafu unakusanya; lakini hilo siyo jambo endelevu katika Taifa. Tunajali zaidi uchumi, kujenga uchumi na ustawi wa Watanzania kuliko kujivunia kuagiza bidhaa kutoka Mataifa mengine. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wakubaliane na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa yale ambayo yanahusiana na nchi ambazo zipo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; tulikuwa na kikao cha kina sana ndani ya vikao vya Mawaziri wa Fedha. Tumeweka wigo ule ambao tumeweka Kamishna Jenerali ili aweze kuchukua hatua ambazo zinazingatia maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nimemsikia Mheshimiwa babu yangu Veda, nimemsikia ndugu yangu Musukuma wametoa hoja za msingi sana na mpaka nikawa ninaangalia, nikawa ninataka kujiridhisha hivi kweli Musukuma huwa ni darasa la saba hizi akili mbona nyingi sana; na ndiyo maana watu wa Geita waendelee kumchagua tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli zile hoja walizozitoa, lakini na sisi tulivyokaa na Kamati; jana tumekaa mpaka saa nane usiku, tumetafakari tukaona hoja kama hizi zilitolewa pia kwenye Kamati. Tukakubaliana, kwamba wigo huu tuliouweka, dirisha lile tuliloweka ndilo ambalo tutalitumia kutekeleza mapendekezo yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa. Pia tutatekeleza maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na wakati uleule tutaendelea kutumiza lengo lile ambalo linahusu nchi yetu na malengo ambayo tumejiwekea kama nchi yetu kuweza kuyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya msingi sana, ni mambo ya msingi sana ambayo yanahusisha uzalishaji ndani ya nchi. Fikiria mkulima wa Tanzania ambaye amepata ruzuku ya Serikali akazalisha kwa kiwango cha kutosha, akishamaliza kuzalisha kwa kiwango cha kutosha eti soko lake liharibike kwa sababu tumepunguza masharti ya kuagiza bidhaa zinazotoka nje.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana na Waziri wa Viwanda; tumekubaliana na Waziri wa Mipango na tumekubaliana na Waziri wa Kilimo, kwamba kuanzia mwaka wa fedha unakuja tutaenda kuweka tena ushuru pamoja na kodi kwenye mazao yanayoagizwa kutoka nje ambayo huku ndani wakulima wetu wameendelea kuongeza uzalishaji. Mazao hayo ni alizeti, ngano, mawese, pamba, mazao yanayotokana na pamba pamoja na mazao mengine, yale ambayo uzalishaji wake umeendelea

kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na hatua ambazo Serikali inachukua.

Mheshimiwa Spika, tulisema tutoe tamko kwa mwaka huu ili mwaka unaofuata hatua hizi za uzalishaji ziwe zimeshaendana sambamba na tamko ambalo tunalitoa ili tusije tukaathiri masuala ya bei na upatikanaji wa bidhaa, tusije tukatengeneza uhaba wa upatikanaji wa bidhaa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni mengine Waheshimiwa Wabunge wamekwishatoa ambayo Serikali imechukua, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ilizochukua hasa za kuwajali Watanzania. Moja ya eneo, tumewapunguzia gharama ndugu zetu wa bodaboda, tumewapunguzia gharama ndugu zetu wa hoteli, *lodge* pamoja na maeneo mengine ya uzalishaji. Tumewapunguzia ushuru wa huduma katika maeneo mbalimbali ambayo ilikuwa ni kero kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, tumeweka kipengele cha kulinda ajira za Watanzania. Tumesema tutaje, tubainishe, tubainishe na jambo hili litasimamiwa na Wizara na Waziri wa Sekta. Tubainishe majukumu ambayo yanaweza yakafanywa, shughuli za kibishara zinazoweza kufanywa na Mtanzania na shughuli za kibiashara zinazoweza kufanywa na mgeni. Mambo haya tuliyasema siku zilizopita, lakini kwenye masharti ya utoaji wa leseni hatukuwa tumeweka kwenye sheria. Kwa hiyo, tumeona tulifunge hili kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hatuwachukii ndugu zetu ndani ya dunia hii, hatuwachukii ndugu zetu ndani ya Afrika hii; lakini huu ni ukweli usiopingika kwamba kila mtu ana Taifa lake, kila mtu ana Taifa Lake. Kwa hiyo na Watanzania acha wavune matunda ya Utanzania wao, lakini pia na matunda ya uhuru wa Taifa lao. Hatuwezi tukaruhusu hata shughuli ambayo inaweza ikafanyika na Mtanzania, tukaruhusu tu uholela. Hii tumesema tuiweke kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, tutakwenda hatua zaidi. Wapo pia wageni sitotaja mataifa yao ambao walikuwa wanakuja wanachukua hizi shughuli za Watanzania, lakini pia wanafanya kinyemela, hawalipi kodi, wanachukua shughuli lakini pia na kile walichovuna wanatorosha. Ninamuagiza Kamishna Mkuu wa Mapato ahakikishe anapitia kila mianya ya utundu wa aina hii na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, diplomasia siyo uholela, ni lazima sheria za ndani ya nchi zinazozingatia masuala ya kodi, zinayozingatia masuala ya biashara lazima tutayazingatia. Kamishna Mkuu pamoja na vyombo vyote wafanye kazi ili kuweza kuhakikisha kuwa mianya aya aina hii yote hatua zinachukuliwa kwa wale ambao wanatumia vibaya utaratibu wa mahusiano au utaratibu wa kufanya biashara kati ya Tanzania na wananchi hawa wa nchi zingine ambao wako ndani ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba tumeweka sharti la kutokufunga biashara. Nililisema mwaka jana hili, lakini kwenye utekelezaji nikaona linalegalega. Nitoe rai kwa watendaji wote wa Serikali. Lazima tuheshimu, lazima tujenge utamaduni wa kuheshimu Sekta Binafsi. Enzi ambazo Serikali ilikuwa inaweza ikafanya majukumu yote zimepita, zilikwishapitwa na wakati. Wakati tuna wanafunzi 14 Chuo Kikuu tuliweza kuwaajiri wote. Hata makusanyo ya kodi kutoka kwa waajiriwa wa Serikali tu yangetosha kuendesha Serikali. Leo hii Serikali haiwezi ikaajiri watoto wote wa Kitanzania kwenye ofisi za Serikali; hivyo ni lazima sekta binafsi ifanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, kodi ya kuendeshea nchi hii haiwezi ikatoka Serikalini pekee yake ni lazima itatoka sekta binafsi na sekta binafsi ndiyo *engine* ya kukuza uchumi huu. Kwa hiyo yeyote ambaye yuko kwenye *regulator authority* au ofisi ya Serikali tuendelee kujenga utamaduni wa kuheshimu sekta binafsi, tuheshimu biashara. Biashara ni mitaji, tuheshimu mitaji ya watu. Mtu kama kawekeza mtaji ni lazima tuheshimu mitaji hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumesema biashara zisifungwe kwa sababu yoyote ili biashara zenyewe ziendelee na uzalishaji.

Biashara haiwezi ikakosea. Kama mwenye biashara kakosea, tuchukue hatua kwa aliyekosea tuiache biashara iendelee kufanya kazi. Hata kama ni masuala mengine yanayohusiana na masuala ya kimadai, ya kikodi na mengine yoyote yale tuiache biashara yenyewe iendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, inatokea katika maeneo mengine. Anatokea mtu yuleyule anadaiwa benki. Haya benki ni mkopo, tunaweza tukasema ni mkopo wake. Inaweza ikatokea eneo lingine amefungiwa biashara na yeye anaidai Serikali, lakini biashara yake imefungwa. Kwa hiyo haya tumetafakari ndani ya Serikali na mambo kama ya aina hii ndiyo hatua ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa akizichukua za kuwezesha sekta binafsi ifanye kazi bila kusumbuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi tulitokea vijijini, wafugaji tunayajua sana haya. Wazee wetu walikuwa wanajua kutunza vitu vitatu. Kimoja, kama ng'ombe anampatia maziwa, walikuwa wanajua sana kutunza kale kandama mpaka kakue, kwa sababu anajua bila kale kandama hataweza kukamua. Sasa kama una biashara na hapo ndipo unapotoza kodi ni lazima uitunze ile uendelee kupata kodi, vinginevyo ukiifunga ndiyo umeshamaliza tena hutaweza kukusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, wazee wetu walikuwa wanapenda kutunza vyanzo vya maji. Tulikuwa tunatembea hata iwe mwendo mrefu kiasi gani, wataiweka mifugo kama kule *roundabout* ili isifike pale kwenye chanzo. Lazima watunze chanzo, wakivuruga chanzo keshokutwa hawatapata yale maji. Kwa hiyo tumesema hili tulifanye na taasisi zote za Serikali na zile zinazotoza leseni zizingatie utaratibu huu. Ni utaratibu ambao utatupa uendelevu katika masuala ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwenye nchi yetu no lazima tuendelee kujenga mazingira yatakayoongeza kodi ndani ya nchi. Hii dunia inakwenda inaharibika kila siku. Zamani kulikuwepo na misaada, misaada kabisa ya kibajeti, wanatokea nchi hii, hii na hii wanaweka kwenye kikapu, wanaweka kwenye kikapu. Kuna nchi

zilikuwa zinaendeshewa bajeti yake na misaada tu. Karne ile ilipita.

Mheshimiwa Spika, tumeshavuka huko na tunapokwenda sasa hivi kama Taifa; na ndiyo maana Dkt. Samia Suluhu Hassan akaweka mkazo kwamba, yale yote ambayo tulikuwa tunapata kwenye *partnership*, kwenye utaratibu hata wa sekta binafsi yanayohusu sekta zetu zile Serikali imeweka fedha na itaendelea kutengeneza utaratibu wa kujitegemea ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunakuwa ni Taifa linalojitegemea lina mapato ya kuweza kuendesha nchi yake, mapato ya kuweza kutekeleza miradi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania hili hata siyo jambo geni, tumekwishatekeleza baadhi ya miradi kwa fedha zetu. Miradi mikubwa ambayo kwa nchi nyingine hiyo ndiyo ingekuwa bajeti ya nchi. Mradi kama bwawa la umeme, zaidi ya trilioni sita. Kwa nchi zingine hayo ndiyo mapato ya nchi nzima, ya mwaka mzima. Sisi tumetekeleza mradi mmoja wa bwawa la umeme. Mradi kama wa reli, tena nchi nyingine kubwa tu, zaidi ya trilioni 27, dola bilioni 10 ni *reserve* ya nchi nzima hiyo, sisi tumetekelezea mradi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuendelee kujenga utaratibu wa kuikuza sekta yetu binafsi na nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na nidhamu ya matumizi ili tuweze kuhakikisha kwamba tunachokusanya kinajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ya kuongezea bajeti ni nidhamu ya matumizi. Hili tumeliweka kwenye malengo yetu ya bajeti ya mwaka huu na tuna uhakika tunakwenda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, nisiongee sana kwa sababu nina furaha nimepata michango mizuri sana kutoka kwenye Kamati na Wabunge na furaha imezidi, kwa hiyo niishie hapa. Ninakushukuru kwa nafasi, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana, hoja imeungwa mkono. Wameshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

Waheshimiwa tuketi. Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025**
***(The Finance Bill, 2025)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima mila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu iliyopitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22

*(Ibara mpya ya 22 iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 30

Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 46

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49

*(Ibara mpya ya 49 iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57

*(Hapa kuna Mheshimiwa Mbunge aligonga meza)*

**MWENYEKITI:** Nani amegonga meza. Mheshimiwa, una hoja? Hapana.

Ibara ya 58

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 64

*(Hapa kuna Mheshimiwa Mbunge aligonga meza)*

**MWENYEKITI:** Nani amegonga meza tena. Una hoja?

Waheshimiwa Wabunge, ukigonga meza nikiwa pale juu unakuwa unafurahia jambo, lakini ukigonga nikiwa hapa maana yake una hoja ya kifungu kinachoulizwa hapa. Haya tuendelee.

Katibu.

Ibara ya 64

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 65

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 66

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaleta mapendekezo ya kufuta Kifungu cha 66.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kufutwa kwa Kifungu cha 66 Serikali inapendekeza hivyo tunaafiki?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78
Ibara ya 79
Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 82

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 83
Ibara ya 84

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 85

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 89

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 90
Ibara ya 91
Ibara ya 92

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 93

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 94

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Kifungu cha 94, kina marekebisho ya Serikali na marekebisho ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho ya mwisho ya Serikali sisi tunafuta yale marekebisho yetu, kwa hiyo tunakubaliana na marekebisho ya mwisho ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, marekebisho…

Mheshimiwa Waziri kwenye kifungu hiki Kamati kwenye taarifa yake ilisema kwamba wameona haya marekebisho kwa mujibu wa Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ya kwao

yameondoka yanabaki haya ya kwako ambayo haya ya kwako yanabakisha kile kifungu yanafuta tu maneno 15% to 60% kwa hiyo linaongezeka neno *of at least 15%*. Sasa hii at least ina tofauti gani na hii? Ina tofauti gani yaani hii *at least 15%* na hii *from 15% to 60%?*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *flexibility* tu kwamba ikiwa *exactly 15%* tunakuwa tumefunga wigo wowote hata pale ambapo pana ziada, lakini ikiwa *at least* inategemea, inaweza ikawa 15%, lakini hii ni kutokana na kwamba kama pana tathmini iliyofanywa na Msajili wa Hazina pakaonekana kuna sehemu ambako tunaweza tukapata mapato bila kuathiri shughuli za msingi zile kama ambazo Waheshimiwa Wabunge walizibainisha tuwe na hiyo *flexibility* ya kuweza kutekeleza Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumekaa na Msajili wa Hazina na tumekaa na wenzetu tukaelewana, ile nyingine iliyokuwa inataja *15% to 60%* ilikuwa inakosa hayo maneno ya tathmini inayofanywa na Msajili wa Hazina kwa sababu huyo ndiye ambaye atakuwa anafuatilia hizo shughuli za kila siku.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali uzuri yupo pale. Hebu nielezee hilo neno *at least* kwa sababu maana yake afadhali hata ile yenye *60%* imeweka *Cap,* sasa hivi maana yake unaweza kwenda hata mbele ya hapo maana hapa ni *minimum* kwa hiyo *maximum* utaamua mwenyewe baada ya kutafakari sasa hebu nieleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kimahesabu ukitaja kimahesabu neno hilo *at least* kimahesabu ndiyo unalifungulia vile, lakini kiutekelezaji kitakachoamua ni kazi itakayofanywa na Msajili wa Hazina na yeye ndiyo anayesimamia hizi shughuli zote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tumeshapata changamoto huko nyuma tayari, tungekuwa hatujawahi kupata kwa sababu

hata hii ya *TANAPA* ndiyo imekuja sasa hivi baada ya miaka yote ya *TANAPA* kushindwa kufanya kazi. Sasa leo Bunge kupitisha hii *blanket* ya kusema *at least* halafu mtu mwingine akaamue huko wakati hatujui hiyo *limit* itakuwa wapi ni afadhali hata ile ya *60%* basi, kwa sababu ya *60%* tungekuwa tunajua ni kati ya hapa na hapa na hutazidi. Sasa hii uliyoweka kwamba hapa ndiyo chini, juu hatujui ukiamua kuvuta zote tutafanyaje?

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yeah* na hapa nilichokiona...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, simama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Hamna neno.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona ni kwamba tumeondoa ile *Cap* sasa, kwa hiyo inaweza kuwa sawa na 15% au zaidi. Kwa hiyo, sasa labda kutafakari vizuri ile ya *15%* mpaka *60%* au hii *at least 15%* lakini sasa maana yake *at least 15%* unaweza kwenda mpaka 80% na kadhalika, kwa sababu sasa *at least 15%.* Kwa hiyo, tujiridhishe tu kwamba tunataka nini lakini ilivyo sasa ni *15% and above*.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa hiyo *15% and above* ndiyo inaendana na haya maneno yaliyoletwa na Kamati humu kwenye taarifa yake, ambayo angalau hiyo hii ilikuwa inaweka 60%, kwa hiyo huwezi kuzidi hapo, lakini hii ya sasa ndiyo kabisa unaweza hata kuzidi 60%. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tumeshapata changamoto huko nyuma tusijiwekee wenyewe mazingira magumu wacha Serikali ikafanye hiyo tathmini.

Halafu tathmini mtakayoleta mtasema sasa tunavyoona haya mashirika kati ya 15% na 20% hapa ili angalau Bunge liwe

linajua linapotunga sheria mtaishia wapi ili zile changamoto ambazo tumezipata kutoka kwenye haya mashirika mengine zisijiree kwenye haya mashirika ambayo yanataka kuingizwa hapa kwenye *at least* halafu mwende mpaka 60%, mwende mpaka 80%, mwende mpaka 100% mkiamua kwa mwezi kwamba lete yote sasa hiyo, kidogo itakuwa mtihani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo na kwa hoja ya humu kwenye Kamati hiki walichokiandika kwa kweli Serikali ile tathmini mnayoisema sasa hivi kwenye mwaka huu kafanyeni hiyo tathmini mkishafanya mtuletee ile *Cap* kwa sababu bila *Cap* tutarudi huku kwenye *TANAPA* tena.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika haya ni ya Watanzania na Msajili wa Hazina ni Mtanzania na Serikali ni ya Watanzania hiyo hofu ambayo itakuwa imechukuliwa kutoka kwenye *experience* itakuwa kubwa sana, kwa sababu hata mashirika yanavyoendeshwa sasa hivi na miaka kadhaa ambayo tunatolea mfano ni tofauti. Umeona jinsi ambavyo *reforms* zinazofanyika kwenye mashirika yetu, *professionalism* ambayo inafanywa na Msajili wa Hazina na miiko ya uendeshaji wa mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini hivi tunavyopanga tutarudi hapa tukiwa tumeshatengeneza...

**MWENYEKITI:** Wewe tueleeshe vizuri hapa tuiweke *TANAPA,* hapa tuiweke *TPA;* haya mawili tu. *TANAPA* kwa pesa iliyokuwa inahitaji, kwa pesa inayokusanya hapa nimesikia kwenye taarifa sijui kama ni ya Kamati au ni ya wapi au ni mchango walikosema katika bilioni hamsini na ngapi ambazo walikuwa wanahitaji wamepewa tisa, ni wapi niliposikia, taarifa ama ni wapi? Nani amechangia Mheshimiwa Mbunge?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeonesha hapo kwamba mpaka sasa katika bajeti yao

waliyopaswa kupewa *49.6 billion* wamepewa *only nine billion* ambayo *is less than 20%* ya walichopokea.

**MWENYEKITI:** Haya hilo ni shirika ambalo limekuwa na hali mbaya, huku kwenye hali nzuri *TPA* nimemsikia Mwenyekiti ninadhani ametoka nje kidogo, lakini Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu nimesikia *TPA* wakizungumziwa kwamba wanafanya vizuri baada ya kurejeshewa, si ndiyo? Ama sijamsikia vizuri Mheshimiwa Mwenyekiti?

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho unachotolea mfano cha *TPA* ndiyo hasa ambacho Serikali inataka. *TPA* imeweka mpango wa utekelezaji wa uendelezaji wa bandari *then* wakapewa fedha wakatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si utaratibu mzuri kwa kweli katika nchi ambapo tuna sehemu miradi imekwama, tuna sehemu huduma za jamii zinahitajika, tuna sehemu kuna jambo linahitajika halafu tukaweka sheria tu ya kumwachia mtu mwingine fedha awe nazo tu. Ninadhani huu siyo utaratibu mzuri lakini hata hawahawa kwa sababu Msajili wa Hazina yupo kwa ajili ya kazi hiyo atafanya tathmini kama kuna uwekezaji na kuna mpango kazi unaofaa Msajili wa Hazina naye ana maslahi mapana ya Taifa na anazingatia na *actually* hiyo ndiyo shuguli yake, litazingatiwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge inawezekana kwa sababu tumebadilisha hapa na ndiyo sehemu zingine labda ukwasi umekuwa mdogo, niwakumbushe na mimi nimepata *institutional memory* nikiwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kuna kipindi tulikuwa tunakopa kulipa mishahara ya watumishi wa umma, tulikuwa tunakopa kutoka *Commercial Bank* halafu taasisi hizi (mashirika ya umma) wanafanya mkutano wa bodi Geneva Uswisi kule, wanafanya mkutano wa bodi Paris Ufaransa kule, wanafanya mkutano wa bodi Ubelgiji, wanajadili hoja zinazohusu shirika wanafanya uwekezaji ambao ni *white elephants* yaani ni kwa

sababu fedha zimewazidi zipo nyingi, basi wanafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *abuse* zilikuwa nyingi sana, ndiyo maana tunasema tufate utaratibu huu tathmini itakuwa inafanywa...

**MWENYEKITI:** Sasa hivi hayo mashirika wanawaletea bajeti au hawaleti? Wanaleta bajeti, hawaleti kwa Msajili wa Hazina; wanaleta hawaleti?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo tunapata tena kwa tathmini...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza wanaleta bajeti hawaleti, Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zinapatikana na zingine zinafanyika ndani ya Msajili wa Hazina zingine kwa taratibu zile za bodi zao. Huu ndiyo utaratibu *standard* katika maeneo yote. Hizi fedha ingekuwa tu Waziri wa Fedha ndiyo anaagiza yaani ingekuwa tu Mheshimiwa Waziri anamtuma kamishna ama zinachukuliwa kwenye *account* zinavamiwa Waheshimiwa Wabunge walitakiwa wapate hofu, lakini kwa utaratibu huu ambao ni wa tathmini, tathmini ya Msajili wa Hazina...

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa wasiwasi wa Bunge ni kwamba hiyo tathmini sisi tusipoweka mpaka ni nani anayeenda kuweka mpaka? Ndiyo maana nimesema ni afadhali hata mliyokuwa mmesema 60% ili Bunge liwe linajua kwamba jamani tumesema hawa zitatolewa kuanzia 15% mpaka 60%. Sasa hivi imeachwa wazi maana yake ni mpaka 80%. Pia inaruhusiwa lakini sasa hii ya kwamba watu wataenda sijui wapi hizo ni *controls* ambazo Serikali inapaswa kuwa nazo.

Bodi inaenda kufanya mkutano sijui wapi huko, bajeti waliomba wapi? Kwa nini waruhusiwe kwenda kufanya mkutano wa bodi Geneva wakati jengo lao lina *board room?* Sasa sijui tunataka ku-*address* jambo gani hapo kwa kweli.

Kwa upande wa mashirika kulindwa yafanye kazi yake tumeona mfano wa *TANAPA* na hapa hatuwezi kujitetea kwa sababu Kamati ndiyo zenye taarifa kwamba *TANAPA* haifanyi vizuri kwa sababu haikupata ndiyo maana tumeleta marekebisho na marekebisho umeleta mwenyewe humu kwamba sasa watapewa 51%, kwa nini 51%? Si umeona kwamba katika zile bajeti zao 51 ndiyo wataweza kujiendesha, hawa wengine wakichukuliwa 80 watawezaje kufanya kazi? Pumzika kidogo, ninaona *AG* kasimama kule.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninashauri tubaki na ile ya mwanzo ya *contribution of 15% to 60% of the gross revenue* halafu tunaendelea na ile *proviso provided that*... yaani kimsingi kwa maana ni muhimu kuweka ile *Cap* badala ya kuiacha *open ended*.

**MWENYEKITI:** Kule nilikuona umesimama Mheshimiwa Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameweka vizuri kwa sababu ukishasema tu *at least* kihesabu na kwa sababu tunazungumzia *percent* maana yake ni 100% kwamba kuanzia 15% mpaka 100% kesho atakuja *TR* Mzee Songe ata-*discuss* na wahusika akisema lipeni 90%. Kwa hiyo, lazima hapa tuwe na *margin*, ningeliweza kumshauri Mheshimiwa Waziri wakatathmini halafu *next time* wanaweza kuja na ma-*group* sasa ya mashirika kwamba mashirika yanayokusanya labda *trillion* tano walipe 20%, wanaokusanya trilioni moja walipe 17%, wakileta kwa *style* hiyo itakuwa nzuri zaidi kuliko kusema *at least*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishasema *at least* maana yake ni kuanzia 15% mpaka 100% na kesho wataleta 70%, Kwa hiyo, kwa kuwa Mwanasheria Mkuu ameiona na ameiweka vizuri basi na

mimi nikubaliane na Mwanasheria Mkuu iishie 15% kama zamani tusonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme kwa *wharfage* kidogo, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri, hivi amesema 60%? Ukishasema 60% hiyo haiwezekani kwa sababu mashirika haya tutasababisha yarudi kwenye matatizo yale za zamani. Kwa hiyo, iishie kwenye 15% lile neno *at least* liondoe kwa sababu lile neno *at least* linasabisha kuwa na *margin* ya kuanzia 15% mpaka 100% hapa katikati, kwa hiyo libaki 15% kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, alizungumza kidogo kuhusu *wharfage,* kwanza lazima tufahamu tafrisi yake. *Wharfage* ni tozo kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya sehemu husika sasa unaposema unataka 10 iwe sehemu ya mapato ya Serikali, si sawa kwa sababu *definition* ya *wharfage* ni tozo kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya sehemu husika. Kwa hiyo, *wharfage* ambayo inatozwa pale *TPA definition* yake ni kwa ajili ya kuendeleza huduma za miundombinu za bandari, nilitaka kuongeza hiyo pia.

**MWENYEKITI:** Sasa hapa pia kazi yangu pia ni kumlinda Mheshimiwa Waziri, Waziri hajaisemea hiyo *wharfage*. Kwa hiyo, lazima niiweke sawa.

Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninafikiri kwamba tujue kwamba kuna mashirika tofautitofauti sana. Mashirika yale yanayozalisha na yanayofanya biashara ni tofauti na mashirika ambayo. Yanayokusanya tozo yanatumia *asserts* za Serikali, *asserts* za nchi hii; wanakusanya kama *TCRA, EWURA* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanavyokusanya ni kama mtu anayekusanya kodi ya kawaida. Kwa hiyo, sasa *issue* hii kwamba wanaweza ukasema *at least 15%* kwamba mashirika kama hayo yanaweza yakalipa zaidi, lakini mashirika haya mengine ambayo

yanalindwa na *TR* mashirika hayo *TR* amezungumza na Kamati na yeye ndiye alituhakikishia kwamba yeye atafanya tathmini yake na atajiridhisha kwamba shirika hilo lina uwezo na lina akiba ya kutosha kulipa hiyo zaidi ya 15%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri kwamba uamuzi wako uwe umetoka wa kusema kwamba waendelee na hiyo *at least* lakini mwakani walete marekebisho ambayo yatatuambia ukomo ni wapi, baada ya kufanya hiyo tathmini sasa kwa ujumla na ku-*group* haya mashirika tofautitofauti.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waziri kabla hujazungumza, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri upo sahihi kwenye hiyo *concern* ya kwako na Kamati tuliiona hiyo ila kutokana na ile *amendment* ambayo ipo kwenye ile amendment ya mwanzo kwenye ukurasa wa 11 hayo yote ambayo yameandikwa kwenye hii *amendment* ya mwisho yanakuwa hayapo kwa vile kuna *proviso* ambayo hiyo *proviso* ndiyo sasa inatupelekea kwamba tunaamini kwamba Msajili wa Hazina atatathmini ni mashirika yapi ambayo yatachangia kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada pia ya kupata hiyo *analysis* ya *Treasury Register,* Waziri wa Fedha ataenda kuyaoredhesha ambayo yatajulikana ya kwamba hayo mashirika yatachangia kiasi gani, lakini tulilenga kwenye yale mashirika ambayo yanajishughulisha zaidi zaidi na kukusanya tozo ambayo ni kama ni *replica* ya *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri uko sahihi. Ninafikiri inabidi waiweke vizuri hiyo, kwa sababu hii ukiisoma hivi hivi hii *clause 94* ambayo unaisoma hii bila kusoma *proviso* kwa kweli inakuwa haina maana, lakini ukisoma *proviso* ni kwamba hii 15% inakuwa siyo *TRA* ila ni *TR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili wa Hazina yeye ndiye atasema mimi Shirika langu litachangia kiasi kadhaa na Waziri wa

Fedha naye atakwenda kuorodhesha ili ajue ya kwamba *liquidity* ya kwangu itakuwa namna gani kila mwezi, lakini sisi tumesisitiza kwenye *performance*. *Performance* ya mashirika tusiangalie kuyatoza kodi mashirika, *TR* yeye ahakikishe kuwa haya mashirika yanafanya kazi kwa tija, ndiyo sababu tukakubaliana hiyo *proviso*. Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mawili. Jambo la kwanza kwa nini tunaiweka hii, uchumi wetu tunatarajiwa uchangiwe na makundi matatu tunapoelekea huko mbele. Moja, Serikali kupitia makusanyo ya kodi *TRA*. Pili, mchango wa Serikali kupitia mashirika ya umma na hayo mashirika ya umma yapo katika makundi matatu. Mashirika ya umma yanayofanya biashara, mashirika ya umma ambayo ni *regulatory* hayo ambayo yanakusanya tozo na mashirika ya umma ambayo yanatoa huduma kwa niaba ya Serikali na hapa hatuzungumzii mashirika ya umma *category* ya tatu ambayo yanatoa huduma, kwa hiyo, haya mawili lazima yachangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo sasa hivi ni kwamba mashirika haya tumeyapa *very minimum,* akishachangia *15%* ame-*relax.* Sasa ili tufike tunapokwenda, tunazungumzia tutafute uchumi wa dola trilioni moja kutoka kwenye haya makundi matatu, *private sector,* Serikali kupitia *TRA* na mashirika ya umma, lazima tuya-*push.* Kwa hivyo, nadhani *compromise* nzuri ni hii ambayo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ameileta, kwamba tuwape hiyo *minimum 15%* tuwapeleke mpaka *60%*, lakini Waziri mwenye dhamana ya fedha atafanya tathmini ambacho kiwango gani Msajili wa Hazina atakuwa amekuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani ili tuweze kupata *balance* nzuri, wachangie, lakini pia tusiwaumize ili waendelee kufanya shughuli zao vizuri wasiishi tu kwenye *minimum*. Ninadhani ambayo Mwanasheria Mkuu ameileta ingeweza kuwa *a compromise* nzuri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa naona sijui kama tumechanganya mambo au ni mimi nimechanganya wakati wa kueleza. Hicho alichosema *AG* ndicho kilichoko humu, kilichopelekea Kamati kuleta hoja kwamba kwenye hili hatujaelewana na Serikali. Kamati ya Bunge ndiyo ikaleta haya mapendekezo kwamba Kifungu 94 na 116 vifutwe, sawasawa? Hiyo ni *amendment* ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri akaleta *amendment* kwamba badala ya hawa wamependekeza kufuta, aah aah, hapa tuondoe ile hoja ya Kamati kwamba iwe kati ya 15% na 60% kwa sababu Kamati ina wasiwasi. Kuliko tubaki kwenye 15% bora tuseme *at least*, sawasawa? Sasa hii *at least* hofu yake ni kwamba inaweza ikaenda mpaka wapi, 80%. Sasa wakati wa maelezo hapa, ndiyo nikasemaje, yaani kuliko hii mmeweka *at least* ni afadhali yaani hata mngekubaliana na ya tangu mwanzo, kwa sababu kama unalikubali neno *at least* kuingia hapa bila kuweka *cap,* maana yake sasa hujatengeneza sheria ambayo, umeitunga sheria.

Waheshimiwa Wabunge, hapana siyo hoja ya kwenda nayo kwa sababu hiyo ndiyo inayoua mashirika, ndiyo maana inakuja hoja ya kufanya tathmini ili ninyi mjiambie ni asilimia ngapi unaweza kuchukua *TCRA*, asilimia ngapi unaweza kuchukua *EWURA*, asilimia ngapi unaweza kuchukua kwenye shirika ambalo hapa wameliwekea kwamba lile ambalo linakusanya kama *min TRA,* ndiyo hoja ya tathmini inapokuja, lakini ukiweka tu hapa kwamba hapa mpaka pale maana yake utaenda kuchukua *60%* halafu hawa watu hawawezi kujiendesha, ndiyo hoja ya tathmini ilipotokea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuwe pia tunaenda vizuri, maana Mwenyekiti alisimama mwanzo akasema wameondoa ya Kamati kwa sababu wamemwelewa Waziri baada ya kuandika neno *at least*. Kama sisi tumelielewa neno *at least* tupite nayo, lakini tukumbuke kilichotupata wakati wa *TANAPA*. Ninatolea mfano *TANAPA* kwa sababu ndiyo imetolewa mfano hapa na Wabunge.

Kwa hiyo, kupitisha tunaweza kupitisha na neno *at least,* lakini huko kwenye Kamati mtakuja tena, wamekuja wamesema nini, wamefanya nini, kwa nini, kwa sababu sisi ni kama tume-*delegate* ile kazi yetu ya kutunga hiki kifungu, kwamba aende mtu mwingine huko akatunge yeye kwamba anataka afike wapi. Kwa nini, Kamati haijatuambia kwamba sasa yenyewe imefanya tathmini inataka mpaka ngapi, 20, 30, 40 au ngapi, haijasema.

Waheshimiwa Wabunge, upande wa Serikali ndiyo hawakwenda kwenye Kamati kwenda kusema kwamba jamani sisi, kujieleza na nini, ndiyo Kamati inavyosema. Kwa hiyo, hoja hii ilivyo hapa, pendekezo lililopo mezani ni la Wizara kwamba tutaondoa hili neno *60%* kwa sababu limewatisha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati, tutaweka *at least* tutaenda sasa pale 20, 40, 50, 60, 80 kulingana na tathmini aliyofanya *TR*. Tumeelewana vizuri Wabunge? Sawa, tusonge.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaelewana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatujaelewana tena? Haya Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Deo Mwanyika. *(Kicheko)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatujaelewana, kwa sababu kama Kamati ili-*intend* kwamba imekubaliana na hoja ya Serikali ambayo kwa kiasi kikubwa ukiisoma hoja ya Serikali au *amendment* ya Serikali inazungumzia kitu ambacho ni *worse than* kile ambacho kipo kwenye sheria. Kwa hiyo, ni vizuri basi tukiwa hapa hapa tuka-*phrase* kidogo angalau tujipe nafasi, kuliko tukaiacha tena, yaani kinachokuja ni *worse than* kilichokuwepo halafu Bunge likasema kwamba tunakubaliana nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani ni vizuri Kamati na yenyewe ika-*recap,* ikapewa nafasi ya kuongea kama kweli ili-*intend* hivyo, kwamba *at least* baada ya maelezo hayo kwamba ili-*intend* kwamba hiyo *at least* ni *okay, but at least is an open check, that is the reality.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo, ndiyo hoja iliyopo kwamba Bunge linatunga sheria ambayo inaweka *at least*, yaani mtu mwingine ndiyo akalisaidie kufanya kazi *literary.* Sasa kwa sababu tathmini hatujafanya, sisi hapa ndani hatuna uwezo wa kusema jamani basi kuliko ile 15% tupeleke 20% hatuwezi kusema hivyo kwa sababu tathmini haijafanyika pia hatuwezi kusema 60% kwa nini kwa sababu si tumeona mifano huko? Kuna watu wamepata hali mbaya. Mheshimiwa Waziri, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba Serikali haijafanya tathmini. Chimbuko la lile pendekezo la Serikali ni kutokana na mwenendo wa takribani miaka mitatu ambayo umeshuhudia Mheshimiwa Rais amekuwa akipokea gawio kitaifa na hicho ndicho Waziri wa sekta alichosema kwamba kwa kweli kumwekea tu yeyote anayefanya vizuri 15%, ambaye anasuasua 15%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi *equal is not equality,* tunavyoweka hii *range* tulikuwa tunamaanisha kwamba tathmini ambayo hii *range* imezaliwa na mwenendo wa miaka takribani miwili, mitatu ambayo tumeona kwenye *performance* ya mashirika yetu na usimamizi uliyofanyika. Kwa maana hiyo, sisi tungeomba na tunaji-*commit* mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba sisi ni Serikali inayowajibika, tunaomba turejee lile pendekezo la kwanza ambalo na Mwanasheria Mkuu amelishauri Bunge lako Tukufu inayoanzia 15% mpaka 60%, lakini kwa tathmini ya usimamizi wa mashirika ya umma unaofanywa na *TR* ili tuweze kuvuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, duniani kule kunaendelea kuharibika kama nilivyosema, nchi yetu inatekeleza miradi mikubwa kuliko nchi yoyote ya *EAC,* wala *SADC,* wala hapa Afrika. Kwa hiyo, itasaidia pale ambapo kuna shughuli ambazo zinaweza zikawa *financed* na fedha hizo, kama ambavyo Waziri wa Sekta ametoka kutuelezea. Twende na pendekezo lililokuwa la kwanza, pia tumeweka msisitizo wa tathmini ambayo itakuwa inafanywa ambayo imetokana na mwenendo ambao umepatikana katika miaka hii mitatu miwili ya usimamizi wa mashirika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nani anataka kuongea? Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kazi ya Bunge ni kutunga sheria na sheria ikitungwa halafu ikaja ika-*backfire* baadaye sidhani kama Bunge lako Tukufu litakuwa limefanya kitu cha busara. Sasa ili kuondoa hiyo *fantasy* iliyopo tu-*maintain status quo*. Serikali ifanye *review, mid-year* basi tutakuja hapa tutapitisha hicho Serikali ambacho itakuwa imekifanya na tukifanya hivyo ninafikiri tutakuwa tumefanya kitu cha busara, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sijui nielezeje vizuri, yaani kuna hoja ya msingi. Hoja ya msingi iko hivi, wale waliokuwa wameweka ile asilimia yaani hamna kushuka, hamna kupanda walikuwa na sababu. Kwamba hapa ndipo ambapo Serikali ifanye nini, iishie. Baada ya tathmini kama Serikali inaona kwamba tufike 20, Serikali inapaswa kuja na kusema sasa tupande tufike wapi, 20. Ukisema kuanzia hapa mpaka hapa, yaani mamlaka yetu siye tumkabidhi mtu mwingine? Inakuwa ngumu kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge limkabidhi mtu *blank cheque* kwamba wewe nenda ukajaze mwenyewe humo ndani, hiyo ndiyo inayotupa shida, kama ingekuwa ni hoja ya Kanuni tungeshatunga hapa, kwani Kanuni si anatengeneza Waziri, lakini hiki ni Kifungu cha sheria tunatunga Bunge. Hatuwezi sisi ku-*delegate our obligation to a TR,* hiyo itakuwa ngumu na ndiyo hoja ya tathmini inapokuja. Ikiwa Serikali imeshafanya tathmini isiseme kati ya hapa na hapa, turudi pale kama wanasema 30, 30 hiyo, kama wanasema 60, 60 hiyo, kama mnasema 80, 80 hiyo kwa tathmini mliyofanya.

Waheshimiwa Wabunge, sasa mkisema kwamba, hiyo tathmini kama ingekuwepo kama Mheshimiwa Waziri anavyosema Kamati ingekuwa imesema, taarifa ya Kamati sijui mmeisikia wote humu ndani, Kamati haina hiyo taarifa.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina, kwa maana ya Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, walifanya tathmini na kuya-*profile* haya mashirika hayafanani, lakini kubwa walilojiridhisha baada ya tathmini ni kwamba kuna mashirika ambayo yenyewe *by their very nature*, yaani wao hawahitaji kufanya *project* hela zinakuja tu, yaani kama ni mbuga za wanyama zipo, wanyama wapo, yaani yeye hahitaji kwenda kufanya mradi wowote ule, ni kwamba fedha zinaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, shirika ni kwamba kutokana na shughuli zake fedha zinaingia, linakusanya labda *let's say* mpaka shilingi bilioni kadhaa, sasa mashirika ya namna hiyo yalikuwa unaya-*limit* tu na *fifteen percent*. Kwa hiyo, utafiti wao ukawapelekea kwamba waje na hiyo *range* halafu kwenye hiyo *range* kwa sababu yako tofauti tofauti kuna mwingine anaweza kuwa atalipa *around 20%*, mwingine 25%, mwingine *30%* lakini ni *15% to 60%* isizidi hapo wakaweka hiyo *cap*. Sasa anavyokwenda ku-*implement* kule ndiyo atafanya *analysis* ajue huyu ana-*follow* kwenye 20%, ana-*follow* kwenye 25%, ana-*follow* kwenye 40% au ana-*follow* kwenye 60%. Kwa hiyo ndiyo maana ikaweka ile *15%* to 60%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ilivyokuja kuwa *improved* hapa sasa hivi, ukisema *at least 15%* ina maana ile *cap* umeiondoa. Sasa inaweza ikaenda mpaka juu zaidi, ndiyo maana nikawa nashauri kwamba tubaki na ile ya mwanzo *contribution of 15% to 60% of the gross revenue* halafu ile *proviso* inaendelea, *provided that this section shall come into effect upon analysis,* zile ambazo zitafanyika ili akajue huyu ana m-*place* wapi.

**MWENYEKITI:** *Analysis* italetwa Bungeni, *analysis* ya *TR* italetwa kwenye Kamati.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezi kuletwa Bungeni.

**MWENYEKITI:** Haiwezi kuletwa kwa sababu ni jambo la utekelezaji wa sheria.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sahihi kabisa.

**MWENYEKITI:** Sasa sisi tusipotunga hiyo sheria hapa, hii siyo adhabu, zile adhabu ndizo tunasema Jaji ataangalia, si ndiyo, ndiyo huwa tunaweka a *minimum of*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sahihi kabisa. Sisi tunawapa hiyo *Cap* ndani ya *15% to 60%* waende.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*, hiyo ndiyo iliyokataliwa na Kamati.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tunawashauri Kamati, *it is better* kuwe na *Cap*, bila *Cap* italeta shida.

**MWENYEKITI:** Sasa hayo mlipaswa mshauriane kwenye Kamati, *unless* mnahitaji muda sasa hivi mpeleke huo ufafanuzi kwa Kamati halafu sisi tuwasubiri hapa, kwa sababu vinginevyo Kamati haijapata huu ufafanuzi, *at least* kwa hii taarifa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo. Mheshimiwa Makamu.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo ndiye nimesoma taarifa kwa niaba ya Kamati, moja ya changamoto tulisema kwamba Kamati haijapata *technical analysis* iliyokuwa imepelekea kufika tulikofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kuwawakilisha wananchi, sasa hatuwezi tukameza mate yetu wenyewe ambayo tunakuwa tunayatoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa umesimama. *(Kicheko)*

**MHE. ORAN M. NJEZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tunaenda vizuri. Ukiangalia *amendment* ya Kamati tulikuwa tunaondoa hiyo *ambiguity* ya *15% to 60%,* tulitaka tuiondoe ndiyo akaja na hiyo *proviso*. Ninaomba tubaki na ile *fifteen* hiyo *at least* iondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hata ukisema *15% to 60%* nayo bado inatuletea shida. Kwa hiyo, baada ya miezi Sita watakuja tena, kwa vile sheria siyo msahafu tutakuja tuibadilishe ila *proviso* hii waliyoiweka ibaki kwenye *amendment*, *proviso* ibaki, *at least* iondoke, ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, haya kuna Wabunge, ninyi Wabunge mtakuwa wa mwisho, tumalize hoja hii tupige hatua. Mheshimiwa Ali King alitangulia. Mheshimiwa Ali King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mkwamo kama huu ambapo tulihisi kwamba tungelifikia mahali tukaokoa mashirika yetu, lakini tukaona kwamba tunaenda kubaya zaidi. Maana tulikuwa tuko kubaya ndivyo tulivyosema mwanzo, lakini tunaenda kubaya zaidi, basi ni bora tukabakia pale tulipokuwepo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti anasema ibakie 15% ile *at least* iondoke na hii *experience* ambayo tumeipata katika Bunge hili, tukiacha hili *gap* kitakachokuja kutokea hapa tutajilaumu sisi Bunge kama tutatoa mamlaka hayo. Kwa maana hiyo, hayo mamlaka tusiyatoe hili *gap* likabaki wazi, kwa sababu kitakachokuja kutekelezwa kitakuwa bado ni cha Bunge kwa sababu tumeacha wazi. Sasa bora tuishie kwenye ile 15% kama ilivyokuwa mwanzo.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante, Mheshimiwa Keisha, samahani Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu mdogo wa sheria au masuala haya, ninatamani nishauri jambo. Nilimsikia Mheshimiwa Waziri pale mwanzo akisema kwamba tathmini imefanyika na ndiyo maana wameweza kuweka katika mlengo huo. Kama tathmini imefanyika na inaonesha kabisa mashirika fulani yana uwezo kiasi gani na shirika fulani lina uwezo kiasi gani na mashirika fulani yana uwezo kiasi gani. Bunge ndiyo tunatunga sheria, kwa nini tusitunge sheria kutokana na aina ya mashirika ambayo tuko nayo? Kama mashirika yale ambayo hayaingizi kiwango kikubwa cha pesa, basi tuyatengenezee sheria ya kwamba asilimia kadhaa hiki ndiyo wanaweza wakaingiza *exactly* asilimia ambayo sisi tunahitaji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ulikuwa ni huo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mansoor.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa kushauri, kama nimemwelewa Waziri wa Mipango alisema kwamba tunazo taasisi za aina tatu. Ningeshauri Serikali inge-*profile* ingeleta hiyo *Cap* ya aina tatu, kwa sababu kuna mashirika yanayofanya biashara, unaweza mfano ukawa-*charge* *30%*, ukaenda kwenye mashirika yanayotoa tozo tu ukaongeza ukaenda kwenye *50%,* ukawa na *bracket* huwezi kuwa na *one bracket* kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa wa-*profile* kwanza kuna zingine zinatoa *service* kama *TPA,* maana yake wale wanatoa *wharfage* ili waweze kuendeleza pia miundombinu wanayoitumia. Kwa hiyo, ningeshauri Serikali ingefanya *profiling* ya hizi taasisi zake halafu ikaziweka kwenye hiyo *bracket*. Sisi tumepitisha sheria ya kwamba taasisi ambazo zinafanya biashara tunawapa *minimum of this percentage*, zile taasisi ambazo zinafanya *service* na ambazo zinatakiwa zinatoa tozo kama *TRA* tunaziwekea *bracket.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mansoor, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni kwamba hata ndani ya *category* moja hazifanani. Kwa hivyo, hata kama shirika linafanya biashara, biashara hazifanani ndiyo maana Msajili wa Hazina lazima kila mwaka afanye tathmini aweze ku-*determine* shirika lichangie shilingi ngapi. Kwa hiyo, nadhani suala la tathmini haliepukiki ni vigumu sana kusema kwamba wachangie hii kwa mwaka huu, lazima tathmini ifanyike kwa sababu yanatofautiana kwa kila mwaka.

**MWENYEKITI:** Kwa sasa hivi kwa kuwa kuna hii 15%, tathmini inafanyika au haifanyiki? Nitakupa au unataka kujibu hiki tu nilichouliza, kwa sababu nitakupa nafasi wakimaliza Waheshimiwa Wabunge.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, hicho hicho tu.

**MWENYEKITI:** Haya sawa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tathmini ndiyo iliyoleta *range* hii.

**MWENYEKITI:** Hapana, acha hii *range*, sasa hivi ambapo sheria inasema *15%. TR* anafanya tathmini ya nini kilipwe na shirika fulani au ni shirika linapaswa katika yale mapato yake lijue kwamba *15%* lazima nipeleke Serikalini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima *TR* afanye tathmini, siyo *automatic*. Lazima afanye tathmini kwa sababu kuna kipindi shirika kwa kweli hata kulipa hiyo *15%* haiwezekani, ukichukua unali-*collapse*. Kwa hiyo, anafanya tathmini anaona kweli lichangie ama tumwache. Kwa hiyo, tathmini inafanyika hata sasa.

**MWENYEKITI:** Sawa, kwa hiyo huku kwenye sheria tumeweka *15%* lakini kuna mahali mna-*charge* saba? Si ndiyo saba, sita au 10?

Mheshimiwa Waziri kuna mahali ambako sheria imesema 15% na tunashuka chini kwa sababu ya mapato?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ilipowekwa inatekelezwa, lakini kwa yule ambaye hana, kwa shirika ambalo halina ndiyo *essence* ya tathmini haliwezi likachangia kwa lile ambalo halina. Sasa hivi hapa tunatunga sheria na kama nilivyotangulia kusema hii wala siyo kwa nia mbaya wala siyo kwa ajili ya kuya-*target* mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mabadiliko madogo ya uendeshaji ambayo yameleta manufaa na yameshatoa ishara kwamba hili ni jambo linaloweza kufanyika na *in fact* inatolea miaka mitatu au minne; siyo miaka mitatu, minne tu imeanza kuanzia Serikali ya Awamu ya Tano hapo nyuma utaratibu wa kuya-*task* haya mashirika yatengeneze *discipline* ya mipango yao na matumizi ili yaweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kuwa mashirika hayafanani, tukipitisha tu kwamba lile lenye uwezo mdogo litoe 15% na lile ambalo lina uwezo mkubwa litoe 15% tutakuwa tunayaumiza baadhi na mengine tutakuwa tunapendelea. Baadhi yatakuwa na kiwango kikubwa sana cha fedha. Hii ndiyo *essence* ya tathmini ili iweze ku- *capture a range of* mashirika pamoja na shughuli hizo zinazofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa zaidi ni kwamba sasa hivi hamasa iliyopo ya kuyafufua mashirika yetu haya ni kubwa. Tumetunga mpaka sheria hizi na tunapiga hatua hii. Kwa hiyo niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge twendeni turudi kwenye ile ya 15% mpaka 60%.

**MWENYEKITI:** Sawa, wakati ukiketi kuna Mbunge anataka kusema na nitakupa fursa. Wakati ukiketi hapo hebu fanya hesabu ile ya *TANAPA* halafu tuone hapa tunaweza kuwekaje ili

shirika lisijikute limerudi kule ambako wengine wameenda lakini kwamba hapa tutaacha *blank* itakuwa ngumu. Yaani kwamba hapa tutaacha *blank* na hii "*at least*" mliyoleta itakuwa kidogo ngumu, lakini anzeni kutafakari kwa zile changamoto za *TANAPA* na pale ilipofika, hii *60%* itakuwa mmeenda mbali sana. Kwa hiyo fanyeni hiyo ili tuweke *Cap*.

Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa hii hoja. Kusema kweli hii hoja tukiiacha kama ilivyo huko tunakokwenda huko sasa mashirika kama *TANAPA* na *TAWA* tembo watatuua kwenye maisha yetu mjini hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya sana. Ninaona yaani sijui kama ni sheria, ingekuwa mimi ni uwezo wangu labda niseme kwangu wala hoja sioni kama ni sheria. Hoja kungetokea kwamba kama *TANAPA* anatoa 15% hela yoyote ya *TANAPA* ikiingia benki, 15% iende Serikalini, asilimia inayobaki iende *TANAPA* ili wasije kuomba hela Serikalini. Hiyo ingefaa sana, lakini kama hela yote inaenda Serikalini kurudi kazi; tutakufa huku na tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* wana mashirika ya hifadhi 22. Mashirika yanayotoa faida matano, hela yote inaenda inaishia huko; tutafanyaje? Ninadhani hii hoja kama inashindikana tuirudishe kwenye Kamati, lakini watusaidie Mashirika ya Umma yale yanayotoa huduma. Mengine yote hata yangetoa 60% sawa lakini haya yanayotoa huduma *please* hayo tuyawekee ili watusaidie.

**MWENYEKITI:** Ngoja nikutoe wasiwasi kwanza hili la *TANAPA* Mheshimiwa Waziri na Serikali wameshalifanyia kazi yaani humu yamo marekebisho yanayoihusu *TANAPA*. Yamo marekebisho ambayo *TANAPA* watakuwa wanapewa 51% ninafikiri. Siyo 51?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tusichanganye mambo mawili. Moja, kwenye upande wa *TANAPA* tunaongelea utaratibu wa kibajeti yaani kule kwenye *TANAPA* kuna wakati

bajeti yao ilikuwa inajitegemea, tukaona hawajitoshelezi. Ikatokea wakawa wanapata bajeti kutoka Mfuko Mkuu, kukatokea ucheleweshaji ambao ulikuwa unasababisha miundombinu isiwe vizuri. Kwa hiyo, tukasema kwa ile ya *TANAPA* wapate kiwango ili waweze kutekeleza miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kwingine tunachoongelea hii *15% to 60%* si masuala ya kibajeti, haya ni magawio ambayo inatakiwa wa-*remit* Serikalini. Kwa maana hiyo kwenye bajeti ndiyo unaweza ukampatia kiwango kwamba *TANAPA* yeye atachukua hii hapa, Ngorongoro yeye atachukua hii hapa, *TAWA* atachukua hii hapa kama ni mgawanyo wa bajeti, lakini kwenye magawio hii inatakiwa ifuatane na uwezo wa shirika na hii inatakiwa ifanye tathmini na hii itakuwa *range* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni r*ealistic* kuweka kiwango kimoja na hata kama tuliweka hii iliyopo ilikuwa ni kwa kuanzia kule tulikotoka ambako *governance* ya mashirika yetu ilikuwa *TR* yenyewe ilikuwa *department* ambayo inashughulika tu hivi, sasa hivi imesimama na tumerekebisha sheria yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tukubaliane twende na *range* hiyo na hili litaleta manufaa *between 15% to 60%.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *60%* hapana. Ilikataliwa na Kamati kwa hiyo sitaki kuingia huko turejee. Ninyi tafuteni huko, si mmesema mnayo tathmini *already?* Itafuteni ili tuiweke hapa tusiache goli wazi.

Waheshimiwa Wabunge inabidi tupige hatua sasa, inabidi tupige hatua. Mheshimiwa Condester halafu Mheshimiwa Dkt. Chamuriho utakuwa wa mwisho.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi. Pamoja na kwamba sina uelewa mkubwa sana kwenye mambo ya sheria, kama suala ni neno *"at least"* halipaswi kuwepo, lakini pia tukiwaacha hivi hivi *TR* ataenda kutengeneza sheria kwa niaba yetu. Ushauri wangu na kuzingatia maoni ya Kamati kwamba tuseme *"at least" 15% but not*

*exceeding 40%* au *50%* ili wale ambao Mheshimiwa Waziri anayaongelea yale mashirika ambayo yanapaswa kucheza hapo basi yaogelee kwenye hizo asilimia. Sisi hii sheria tuwe tumeitunga kwa sura hiyo, ni ushauri wangu.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Daktari karibu.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa tatizo ninaliona kwa pande zote mbili kwa sababu nilikuwa huko na nilipata uzoefu kidogo. Yaani pande zote mbili wana hoja kwamba unaweza kuwa na mashirika ambayo kweli yana pesa zaidi ya wanayohitaji na unaweza kuwa una mashirika ambayo yanashindwa kujiendesha kwa sababu yamechukuliwa pesa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo *scenario* zote zipo na nikiangalia hizo hofu mbili ambazo zote ni za ukweli. Nikiangalia hizi *proviso* ninasema kwa nini tusiongeze *proviso* ya tatu pale A, B, na C kwamba *provided date the institution shall be able to run itself*? Maana *issue* ni kwamba hofu ni shirika lisishindwe kujiendesha ndiyo hofu kubwa hiyo, lakini ni kweli kwamba kuna mashirika ambayo huwa pesa zinakwenda zinabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapendekeza hapo kama watakubali na hao *drafter* wairekebishe "*at least 15*" ibaki lakini *proviso* iwekwe pale kwamba wasichukue kiasi kwamba mpaka shirika likashindwa kujiendesha. Kwa hiyo, hiyo itakuwa ni *automatic* sheria imeweka hitaji la kufanya tathmini palepale asichukuliwe zaidi ya kushindwa kujiendesha.

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa Wajumbe hii ilikuwa ni kifungu cha 94. Wakati wanasubiriwa wataalamu hapa walete hiyo tathmini tusonge na vifungu vingine halafu tutakirejea kifungu namba 94.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 95
Ibara ya 96
Ibara ya 97

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 98

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 99

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuko kwenye kutunga sheria na lazima Bunge tuwe tunatunga wote kwa pamoja.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 100

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 101

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 102

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 103
Ibara ya 104

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 105

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 109

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 110
Ibara ya 111
Ibara ya 112
Ibara ya 113
Ibara ya 114
Ibara ya 115

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 116

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 116 ninadhani ni hiki ambacho kinafanana na kile kingine cha 94. Kwa hiyo, tutakachokubaliana hapa kitakuja na kwenye 116, kwa hiyo tutakirejea.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 117
Ibara ya 118
Ibara ya 119

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 120

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 121

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 122

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 123
Ibara ya 124

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 125

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 126

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 127

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 128
Ibara ya 129

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 130

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 131
Ibara ya 132
Ibara ya 133

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 134

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 135
Ibara ya 136

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 137

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 138
Ibara ya 139

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Haya, tunarejea. Tumepata muafaka wa tathmini? Hatujapata bado tunahitaji muda? Hatujapata, haya Mheshimiwa Waziri wa viwanda.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashauri katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza Wabunge tutafakari kidogo kwanza hizi taasisi maana yake ni taasisi za Serikali; hili ni jambo la kwanza. Pia, *TR* ndiyo msimamizi wa hizi taasisi tumempa *mandate* hiyo ya kuweza kuzisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuangalie, hizi taasisi zinatofautiana kiukwasi, taasisi moja na taasisi nyingine, lakini vilevile kutokana na hilo jicho la tathmini imeonekana kwamba vilevile Wabunge tutafakari ongezeko la bajeti ya mwaka huu lazima tuangalie baadhi ya fursa ambazo tunaweza kuzitumia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yale tuliyoyapanga katika bajeti ya Serikali lazima yaende. Kwa hiyo, haya ni mambo matatu ambayo ni ya msingi tuweze kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ninapendekeza tungebakia katika *status quo* ile ya pendekezo la Serikali la kwanza kutoka 15% mpaka 60% halafu *TR* pale kwa sababu hiyo tumempa range hizi taasisi zinatofautiana kutokana na ukwasi. Kwa hiyo, tathmini ikifanyika taasisi nyingine zitatozwa kwa 17%

nyingine 18%, nyingine 20% nyingine 23% kutokana na ukwasi uliokuwepo katika taasisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama itakupendeza tukibaki katika ile *original version* ya Serikali tutakuwa tumebaki mahali pazuri zaidi, lakini tukaongeza ile *provision* ambayo *AG* amependekeza kwamba *upon* hiyo *evaluation* ambayo imefanywa na *TR*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge uhalisia ni kwamba sisi hatuna nafasi ya kutazama hiyo tathmini inayokuwa imefanywa. Kifungu tukikitunga kwa maana ya kwamba mtu ataenda yeye aji-*fit* pale anapoona yeye inafaa yaani tutakuwa jukumu letu la kutunga sheria tumemkabidhi mtu mwingine. Yaani tukisema yeye ataamua hapa 17, hapa 12, hapa saba; hapana.

Tukiamua kufanya hivyo tuweke *cap* na kama hatuweki *cap* na nyie mmefanya tathmini tupandishe tuseme 40% kama ilivyokuwa 15% tuweke tu 40%, *full stop*. Nendeni mkafanye anayepaswa kulipa 40% kama ambavyo mmesema mkifanya tathmini wengine wanalipa saba, kwa hiyo kuna wengine watabaki 15% kama ambavyo ni jambo la kiutendaji wengine watapanda mpaka 40% ili Bunge liwe limetunga sheria kwamba mashirika ambayo yatakuwa yamefanya tathmini yakaona yanaweza kulipa mpaka 40% tunaweka 40%, lakini sasa kwamba sisi tuseme yaani hiyo tathmini itakuwa inaamua hapa 12, hapa tatu hapana jamani.

Ndiyo maana kulikuwa na sijui inaitwa hekima au busara? Kulikuwa na *wisdom* kwenye kutengeneza ile 15 kama wakati wake umepita na ni ya muda mrefu tunabadilisha tu kile kiwango kwamba kwa tathmini tuliyofanya Serikali, mashirika yetu sasa hivi yanao uwezo wa kulipa zaidi ya hii 15%, yanao uwezo wa kulipa 40% tunaweka pale 40%. Hata hivyo, kwamba tuweke *margin* ya kutoka 15% mpaka 60%, jamani yaani hapo ni parefu sana kwa kweli. Haya ninaona Mawaziri wawili mmesimama sasa sijui aongee kwanza wa nyuma halafu ufuate *Chief Whip*.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza kwa makini sana mjadala wa kifungu hiki na ninakuelewa vizuri sana hoja yako ya kifungu hiki ambacho Serikali imeomba Bunge kukitunga na hoja ya maneno "*at least 15%*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa utungaji sheria nimekusikiliza na umeelezea vizuri maeneo ambayo Bunge linatunga sheria inayoenda kutekelezwa kwenye hukumu ya adhabu, Bunge linaweza likaweka "*at least*" na "*at most*" kwa sababu Jaji ataenda kutumia busara na kuangalia mazingira katika ku-*implement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki ninaomba na mimi kuweka mchango wangu kwenye hoja ya Serikali. Serikali inapoomba kuweka "*at least 15%*", asilimia ambayo Msajili wa Hazina ataenda ku-*determine* anapoenda kufanya *analysis* ninaomba Bunge lako litambue shirika la umma ni shirika ambalo linamilikiwa na Watanzania. Ingelikuwa ni kampuni binafsi wanahisa ndiyo wanamiliki shirika, lakini katika utaratibu wa shirika la umma, Msajili wa Hazina *(Treasury Registrar)* ndiye anashika hisa kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Msajili wa Hazina kazi anayofanya kwenye mashirika haya anafanya kazi sawasawa ambayo ingeweza kufanywa na *annual general meeting* ya *shareholders*. Kwa hiyo, Msajili wa Hazina ana maslahi kwenye mashirika haya, angependa kuyaona yakifanya vizuri, angependa kuyaona yakipata faida na wakati mwingine ndiye anayeombea hata fedha Serikalini ya *capitalization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachokuomba ni Bunge hii kuamini kwamba kifungu hiki hakiendi kutengeneza mwanya kwamba Bunge limetunga sheria ambayo imempa nafasi mtu mwingine kwenda ku *implement* bali ni kifungu ambacho kimeletwa ataenda kusimamia ni mtu ambaye amepewa mamlaka na Sheria ya Bunge hili kwenda kuwa msimamizi wa *share* za umma kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana uamini kwamba ataenda kufanya kazi hii kwa maslahi mapana ya Taifa na kifungu hiki kibaki kama kilivyopendekezwa kwamba *"at least 15%"* na Waziri wa Fedha amesema vizuri kwamba hata kilivyo sasa siyo wote wanafika 15, wako wanafika chini, wako wasiopeleka na hakuna mtu yeyote anachukuliwa hatua kwa sababu hali ya mashirika inafahamika na Msajili wa Hazina anaishi na mashirika haya kila siku. Kifungu hiki kikitungwa kama kilivyopendekezwa kitasaidia tutasonga mbele na niwahakikishie kitatumika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa Wabunge nadhani tumeshakaa hapa muda mrefu. Hii "*at least*" kwa sababu, inaweka *minimum* kwamba, atapanda mpaka wapi sasa. Nadhani Serikali kama mtaona inafaa ni bora kuweka *cap, then* yeye huku chini aogelee, akitaka mmoja atoe *zero*, mwingine atoe 15, mwingine atoe 20, lakini tuweke *cap,* yaani Bunge liweke *cap.* Halafu Serikali yenyewe hiyo tathmini itajiambia huyu atoe 15, huyu atoe 20 na huyu atoe ngapi, lakini ni lazima tuweke *cap.*

Sasa *Cap.* ya 60 tumeshasikia kutoka kwenye Kamati kwamba, ile iko juu, ndiyo maana imeleta hii hoja hapa. Sasa ninaangalia kwenye hizi *objects and reasons* kwenye upande wa pale tulipofanya marekebisho kwenye *Part 20 of the bill* ambayo inahusu *TANAPA.* Pale nimeona hesabu imepigwa, imeandikwa kwa sura ambayo *TANAPA 40%* wao wanapata 51 halafu hiyo tisa, ninadhani iko na Sheria ina mahali imeweka kwamba, inaenda huko.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hawa *for now* kwa sababu, tumeshaona kuna mashirika ambayo yamekuwa sana kutoka kwenye ile 15%, kwa nini tusichukue uzoefu huu wa *TANAPA?* Wa kuweka *Cap.?*

Huko ndiyo aende sasa yeye akaogelee chini, siyo akaogelee juu kwa kutupita juu hivi Serikali kwa sababu, tathmini ile ya *sixty* Kamati imepata wasiwasi. Kwa hiyo, ninafikiri tunaweza kwenda

pale katikati kwa kuangalia mapendekezo mliyoletewa kwa *TANAPA,* tuweke *Cap.*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuelewa na ninadhani tunaenda vizuri. Nia ilikuwa hiyohiyo kwamba, hata hiyo *Cap.* itategemea mashirika yenye uwezo kwa sababu, siku zote Serikali ina nia njema, haiwezi kuua watoto wake. Kwa hiyo, ninadhani kwa sababu, tumepata uzoefu wa *TANAPA* tumefika *49, I think*.

**MWENYEKITI:** *TANAPA* ni *51 to 40,* halafu ile tisa ninadhani ina mahali ambapo huwa zinaenda. Sasa twende, kwa sasa hivi kwa sababu, ile tathmini hatuko nayo hapa, ya mashirika, vinginevyo tungetaka tutaje kwenye *schedule*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, twende hiyo hiyo *40*.

**MWENYEKITI:** Twende *40* waachiwe hiyo *60,* kwa namna anavyofanya yeye nini ile? Sijui tathmini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na ile itaenda kwa kufanya utafiti. Siyo lazima kuwe na *40,* ile ni *maximum.*

**MWENYEKITI:** Kwa sababu, hapa kwenye hiki Kifungu sasa kinasema, *"An executive agency public operation, public institution which charges or imposes and collect fees for services rendered shall remit to the consolidated fund. Monthly contribution of 15 to 60% of the gross revenue."* Sasa badala ya hii ya *from to, 15* hivi ilitungwa mwaka gani? Ile Sheria tuliyoweka *15%?* Hiyo hapo sheria ni ya mwaka gani? Angalia huko mbele ni ya mwaka gani hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *at least 15...*

**MBUNGE FULANI:** *No,* isizidi 40.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, isizidi 40.

**MWENYEKITI:** Hatuweki *at least*.

**MBUNGE FULANI:** Isizidi 40.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, isizidi 40, *yes*. Tumekubaliana na kiwango kile cha *TANAPA*.

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ninafikiri inawezekana hiyo ikawa ni zaidi ya mara mbili ya hiki wanacholipa sasa, lakini hapa kwenye hiki Kifungu kuondoa ile hofu ya Kamati kuna ile aliyokuwa anasema Mwenyekiti, *provision.* Sasa tukishamaliza hii hoja inakuja hoja ya pili ambayo, hapa imeandikwa hizi *publications* zitafanyika *monthly* na hawa mmesema walipe pia, *monthly*. Kwa hiyo sasa, kidogo inaweza ikawa mtihani, yaani ni *month* ipi? Kwa sababu, kama ni *month* ile aliyo-*collect* na wewe utakuwa ume-*publish* saa ngapi ili yeye aweze kuileta *within that time?* Kwa hiyo, ile *timing* ndiyo inaweza ikawa kidogo ngumu.

Waheshimiwa Wabunge, hapa maana yake itasomeka kwamba, *"Monthly contribution not exceeding 40% of the gross revenue",* unaondoka kwenye mtu mwingine kwenda kuzidi kule, anakuwa huku chini wenye *15,* watatoa *15* na wenye sijui asilimia mbili watoe mbili. Si ndiyo uhalisia tulioambiwa hapa kwamba, kuna wengine hawawezi hata kutoa?

Sawa, sasa hapa imesema *monthly contribution* na hapa kwenye *provision,* Mheshimiwa Waziri inasema, *"provided that this section shall come into operation upon issuance by the minister of an order published in the gazette specifying the amount of monthly contribution to be remitted by each executive agency public cooperation or public institution"* ambazo zimeshatajwa huku mwanzo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hiyo *timing* kidogo ndiyo sioni uhalisia. Yaani kwamba, tathmini itakuwa inafanyika kila mwezi au mnafanyaje, kwa namna kifungu kinavyosomeka? Ama inamaanisha kwamba, mna-*publish* mwezi huu, itaendelea *for some time?* Inawezekana mimi ndiyo sija...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inahusu utaratibu wa kawaida wa kisheria. Hizi Sheria zote tunazozipitisha zinaanza kutumika baada ya Waziri wa Fedha ku, Sheria inasainiwa na Mheshimiwa Rais halafu huko kwenye utekelezaji wa *regulations* na taratibu zile zinazohusu maeneo mahususi inatoka kwa Waziri wa Fedha.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hii *publication in the gazette* itakuwa ni ya kudumu? Siyo kwamba inafanyika ni moja kwa moja yaani, *ok?* Sawa, kwa hiyo, jamani mashirika yatakayojikuta yametajwa kwenye *order* ya Waziri ndiyo yatakuwa yanajijua hapa, sawa jamani eeh? Mimi ninafikiri tunaweza kupiga hatua, si ndiyo Waheshimiwa Wabunge au kuna?

Ninafikiri tunaweza kupiga hatua. Sasa Kifungu hiki.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Ni wapi huko tena?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa.

**MWENYEKITI:** Ahaa, Mheshimiwa Kwagilwa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri tunakwenda vizuri, lakini nilitaka utupe Mwongozo kwa yale mashirika ambayo tayari tumeshayatungia Sheria, kama vile Bandari, *TANAPA*...

**MWENYEKITI:** Tumesha...

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema nilitaka tupate Mwongozo, hii Sheria tunayoipitisha hapa kwa yale mashirika ambayo tayari *specifically* tumeshayatungia Sheria mahususi, kama ilivyo Bandari, *TANAPA* na Ngorongoro, tunayoenda kupitisha.

**MWENYEKITI:** Hebu, hiyo *principal legislation, public finance acts;* ngoja kwanza, ninataka niangalie maana hii iko *very specific,* ina-*amend* Kifungu cha 13 cha *Public Finance by deleting sub-section three, an executive agency public*...

*No,* kwa sababu, hizo Sheria tulivyotunga hii Sheria nyingine si ilikuwepo? *AG,* hii, *The Public Finance Act,* wakati tukitunga ile inayohusu *wharfage* ya *TPA,* si ilikuwepo na haikuathiriwa? Kwa hiyo, sidhani kama zinaathiriana, ndiyo maana ninataka kuangalia hii *principal legislation* ambayo inakuwa *amended* hapa, naam?

Waheshimiwa Wabunge, haiathiriki, kwani sasa hivi bandari haitoi gawio? Inatoa, hoja ni kwamba, ile *wharfage* ndiyo itakuwa haikuwa *affected,* lakini na yenyewe humu inaingia kwenye *not exceeding* endapo? Sasa hilo si ni shirika mojawapo ambalo linaleta hela, kweli utatoa ile orodha halafu *TPA* isiwemo?

Haya Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *wharfage* ni mahususi, kwa ajili ya uendelezaji na hata kwenye mashirika haya mengine, kama shirika lina mradi wa kutekeleza, wa kuendeleza jambo fulani, litaruhusiwa kuendelea na uendelezaji wake; yaani zile *core function* ambazo ziko kwenye mpango kazi hazitaathiriwa. Hii ni yale mapato ambayo yanakuwepo yanatakiwa kuwa *remitted.* Kwa hiyo, tunaongelea hayo tu, kwenye yale ambayo yana sheria mahususi niwatoe hofu hayataathirika.

**MWENYEKITI:** Sawa, mimi kwa kweli, siyo mtaalam wa haya mambo, lakini hapa inasema, *gross revenue.* Kwani *gross revenue* ni nini? Si ni makusanyo yote? Ni makusanyo yote, yaani mradi

umekusanya lazima unaingia hapa kwenye kifungu, maadam uko kwenye ile orodha ya Waziri huku nyuma, si ndiyo? Ili tuondoke hapa tusije tukaanza tena, lakini Waziri ile alisema, hapana.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo *wharfage* na yenyewe, kama inaingia kwenye *gross revenue* inaweza ikajikuta au haijikuti? Jamani Wanasheria wengine mlioko humu ndani, hebu mseme?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Wharfage* ni chanzo cha mapato, kwa hiyo, bandari ana vyanzo vyake mbalimbali, atakusanya baadaye. Sasa ndiyo tunapiga hiyo tuliyosema *not exceeding 40%,* kwa hiyo, watam-*profile* humo, lakini *wharfage* ni *just* chanzo cha mapato. Tulichokifanya wakati ule tulitaka akusanye yeye mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Sawa, ambacho na hapa kinaingia?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ndiyo. Kwa hiyo, tusiseme hii haipo? Haihusiki? Inahusika kwa sababu, si ni *gross revenue?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sahihi kabisa.

**MWENYEKITI:** Wakati anapiga hesabu ya *gross* hawezi kuacha hii pembeni, anapiga zote, lakini sasa ile tathmini iliyosemwa hapo, naam. Hiyo tathmini itakayofanywa, maana yake inaangalia mapato yote ya shirika au taasisi fulani kwa hiyo, yeye kwa sababu ya aina ya matumizi yake labda atachajiwa *(charge) 15* sasa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninadhani tunaweza kwenda vizuri kwa hiyo, ile *provision* inabaki pale. Si tumeelewana jamani eeh?

Haya Kifungu Namba 94 sasa na 116, tulikuwa hatujahoji bado.

Ibara ya 94

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 116, ngoja niangalie kinasomekaje sasa. Ahaa, 116 ni ile Sheria ya *Treasury Registrar* inabadilishwa, ili kufuta kifungu fulani na kuweka kifungu vizuri, ili kiendane na hiki tulichobadilisha hapa awali. Sawa jamani ee?

Kwa hiyo, hapa napo kulikuwa na hayo ya *monthly contribution between 15 and 60%.* Hapa napo itakuwa *not exceeding of its annual gross revenue,* sawa? Sasa ripoti ya haya, *insha Allah,* wale tunaoombeana kurejea basi tutakutana nayo.

Ibara ya 116

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho Serikali inapendekeza kupanga upya Kifungu cha 19 hadi 139. Sasa visomeke, Kifungu cha 18 hadi 137.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hizi namba zinabadilika kwa sababu, kuna vifungu ambavyo Serikali imeviongeza na kuna vifungu imevipunguza kwa hiyo, lazima namba zibadilike. Mabadiliko hayo ya namba za vifungu yanaafikiwa?

*(Mabadiliko ya namba za vifungu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na limeupitia Muswada wa Sheria ya Fedha kwa Mwaka 2025 pamoja na marekebisho yake. Sasa ninaomba ukubaliwe kama Taarifa Rasmi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inayohusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 *(The Finance Bill)*. Wote mmeafiki, ahsanteni sana.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kutunga Sheria Itakayotoza au Kubadili baadhi ya Kodi, Ushuru, Tozo au Ada mbalimbali na kufanya Marekebisho kwenye Sheria mbalimbali Zinazohusu Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato ya Umma *(A Bill for an Act to Impose and Alter Certain Taxes, Duties, Levies, Fees and to Amend Certain Written Laws Relating to the Collections and Management of Public Revenue)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa mara ya tatu na hiyo inaashiria kukamilika kwa kazi yetu ya kutunga Sheria. Sasa Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 *(The Finance Bill 2025)* umepitishwa rasmi na Bunge.

*(Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025*
*(The Finance Bill, 2025 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufanya kazi hiyo sasa Muswada huu atapelekewa Mheshimiwa Rais, ili na yeye kwa mujibu wa Katiba aweze kufanya kwa sehemu yake. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwashukuru sana kwa kazi nzuri. Kamati yetu ahsanteni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya, lakini pia, niwashukuru Serikali kwa usikivu ambao mmekuwanao kwa maoni ya Kamati. Mmeleta marekebisho mengi kabisa, mengine hata vifungu mmevifuta. Tunawashukuru sana kwa ushirikiano mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hivyo basi tunawatakia kila la heri katika kwenda kukusanya hizi fedha ambazo zimetungiwa sheria tayari. Hatuna wasiwasi kwamba, fedha hizi zikishakusanywa zitaenda kwenye miradi, kama ambavyo mmekuwa mkifanya siku zote. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa sheria hii ambayo imetungwa na Bunge sasa.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa uvumilivu. Muda umeenda kidogo, lakini ni shughuli ambayo ilikuwa ni muhimu kuifanya.

Baada ya kusema hayo, kuna tangazo moja. Kamati ya Uongozi tuonane kwa dakika chache hapa *lounge,* mara baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge, mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.37 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 26 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*